# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Saba – Tarehe 14 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. – EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI.**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki Mbunge wa Tarime Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 80

### Chumba cha kuhifadhi maiti – Tarime kuanza kufanya kazi

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, ni lini chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Wilaya ya *Tarime TC* kitaanza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Magena kilichopo Halmashauri ya Mji wa Tarime kimekwishakamilisha ujenzi wa Jengo la kuhifadhia maiti. Aidha, Halmashauri inaendelea na taratibu za ununuzi wa jokofu la kuhifadhia maiti baada ya kupokea fedha za ununuzi wa vifaatiba shilingi milioni 150 kutoka Serikali Kuu katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningependa kujua maana katika Hospitali yetu Kuu ya Wilaya Bomani, jokofu lake limekuwa likiharibika mara kwa mara.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba Jokofu lile linafanya kazi ili watu wapate huduma ambayo inastahili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli jokofu la Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime ni la siku nyingi ni chakavu na linaleta usumbufu wa kuharibika mara kwa mara, lakini Serikali imeshatenga fedha katika mwaka wa fedha ujao

2023/2024 kwa ajili ya kununua jokofu lingine kwa ajili ya Hospitali ya Mji wa Tarime. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, Swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Vituo vya Afya vitatu kwa maana ya Kinesi, Changunge na Kituo cha Nyamagaro havina chumba cha kuhifadhia maiti. Nataka nijue mpango wa Serikali wa ujenzi wa vyumba hivi kwa ajili ya kunusuru na kusaidia wananchi maeneo haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vituo hivi ambavyo vingine ni vipya havina majengo ya kuhifadhia maiti, lakini mpango wa Serikali ni kuendelea kujenga vituo hivi kwa awamu. Tumejenga majengo awamu ya kwanza, tumejenga awamu ya pili na sasa tunakwenda awamu ya tatu kwa ajili ya kujenga majengo mengine yakiwemo majengo haya ya kuhifadhia miili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Na. 81

**Ahadi ya ujenzi wa shule za sekondari katika kata ambazo hazina sekondari**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, ni shule ngapi za sekondari zimejengwa katika Mkoa wa Mtwara ambao una zaidi ya kata 50 ambazo hazina shule?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari imejenga shule 231 za kata na shule 10 za wasichana za kitaifa katika mikoa 10. Hii ikiwa ni awamu ya kwanza ya ujenzi kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, katika awamu hii ya kwanza Mkoa wa Mtwara umeshajengewa shule 10 za kata katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa wanafunzi na kata ambazo zilikuwa hazina shule.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itajenga shule za sekondari katika kata ambazo wanafunzi

wake wanatembea umbali mrefu kwa mfano Chilangala, Mkomatuu ambazo ziko katika Jimbo la Newala Vijijini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tunafahamu na kutambua kwamba shule hizo zimejengwa tunashukuru, lakini mkakati wa kupeleka walimu ukoje kwa sababu shule hizo mpaka sasa haijapelekewa Walimu wa kufundisha? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Wambura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza la je, ni lini Serikali itajenga shule hizi kwenye kata zilizosalia? Dhamira ya Serikali ni kujenga shule katika kila kata ya nchi yetu na hii ilikuwa ni awamu ya kwanza tu. Hata hivyo, niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kwenda kwenye awamu ya pili ya kujenga shule hizi za kata na muda si mrefu wataanza kuona shule hizi zikijengwa katika halmashauri zote 184 katika nchi yetu. Kila halmashauri itapata walau shule moja kwenye awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, Mkakati wa Serikali. Wabunge ni mashahidi, wameona namna gani Serikali hii ya Awamu ya Sita imetangaza ajira zaidi ya 21,000 kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Angela Kairuki ya kuajiri Walimu na watumishi katika Sekta ya Afya. Hii yote ni kwenda kuhakikisha kwamba Serikali inaziba mapengo haya ya Walimu ambao wanahitajika kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, swali la Nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na idadi ndogo sana ya wanafunzi wanaosoma katika *A-level* Mkoani Mtwara. Je, Serikali haioni sababu ya kutoa motisha kwa kutenga kiasi kikubwa cha wanafunzi wanaotakiwa kusoma sekondari za *A-level* ambazo ziko katika Mkoa wa Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungahela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati huo anaouzungumza yeye na ndio maana tayari imetengwa fedha ya kujenga shule za sekondari za mikoa kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaotoka kwenye maeneo husika wanabaki katika maeneo hayo hasa wasichana. Pia tayari Serikali imekwishatenga Shingi Bilioni tatu kwa mikoa 10 ya mwanzo na sasa itakwenda tena kwenye awamu ya pili kwenye mikoa mitano, halafu itakuja kumalizika katika mikoa mingine, hii ni kuwabakiza.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna shule zile za *A - level* ambazo zilijengwa na wananchi kule na Serikali ikaja kumalizia, huwa zile zinatoa kipaumbele kwa wanafunzi wa maeneo yale kasoro zile shule maalumu tu za kitaifa ndio zinachukua wanafunzi kutoka katika kila eneo la Taifa letu. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 82

**Ajira kwa walinzi, wapishi na makatibu muhtasi shule za sekondari za kata**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaajiri watumishi wa kada ya ulinzi, upishi na makatibu muhtasi katika shule za sekondari za kata nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, naomba kujibu swali namba 82 lillliloulizwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ajira kila mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga nafasi 201 za Makatibu Muhtasi na tano za Wapishi. Watumishi husika wataajiriwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Aidha, kwa katika Kifungu cha 6(1) cha Sura ya 298 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Toleo la 2019, Waajiri mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa hutenga bajeti kwa kuzingatia kada na maeneo yote ya vipaumbele ikiwemo Walinzi, Wapishi na Makatibu Muhtasi na kuwapanga katika maeneo yenye uhitaji ikiwemo shule za sekondari za kata nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la Nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Samahani sana, naona hata majibu yaliyotolewa hayana uhalisia kabisa. Nafasi tano kwa wapishi nchi nzima na nafasi 200 za makatibu muhtasi kwa ajili ya shule ya sekondari. Katika maelezo yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema pia eneo hili la ajira kwa halmashauri zimepewa nafasi. Hakuna Halmashauri hata moja nchini inaajiri kada hizo.

Mheshimiwa Spika, maswali yangu madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa sasa wazazi wengi nchini wamebeba mzigo mkubwa wa kulipa michango kupitia watumishi hawa ambao wanalipwa kwa michango ya wananchi; na kwa kuwa katika shule zetu familia moja inaweza kuwa na watoto wawili, watatu mpaka wanne, Serikali haioni kuwa ni wakati muhimu na muafaka wa kuweza kuongeza ikama ya ajira hii kwa ajili ya watumishi hawa ili kupunguza mzigo kwa wazazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika kibali cha ajira kilichotolewa juzi Serikali haikutoa kipaumbele kwa ajili ya Walimu wa kada ya kilimo…

**SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, je, ni kwa nini Serikali haiweki kipaumbele kutoa kibali kwa Walimu wa mchepuo wa kilimo ili vijana wetu waweze kupata stadi za klimo kutoka shule za sekondari nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza

nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba takwimu tulizotoa ni takwimu sahihi na usahihi wake unakuja kutokana na ukweli kwamba, Mheshimiwa Mbunge ajira hizi zinatokea kwenye halmashauri zetu. Halmashauri ndizo zinazoomba na sisi kama Ofisi ya Rais, Utumishi, tunapokwenda kuomba Kibali tunaomba kwa ikama iliyoombwa tukiangalia na Bajeti ambayo imepitishwa na Bunge lako. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwanza apate kufahamu kwamba kilichoelezwa hapa ni kutokana na taarifa zilizoombwa kutoka katika maeneo yetu ya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, pia pamoja na hilo tunakubaliana kiukweli kwamba hitajio la kuongeza ikama kwa ajili ya ajira hizi ambazo zimeelezwa ni jambo la msingi na sisi kama Serikali tumelisikia.  Pia nimwombe tena Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako, tunapokwenda kutaja vipaumbele vya maeneo yetu ya kiutawala kwa maana ya halmashauri, basi tuangalie kwamba hii ni sehemu moja wapo ya eneo muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili, juu ya walimu wa mchepuo wa kilimo. Ameeleza hapa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, wakati anatoa taarifa juu ya idadi ya nafasi za ajira zilizotolewa, iko nafasi ya ajira za Walimu, ziko nafasi za eneo la afya. Katika eneo hili la elimu naamini kabisa kama kipaumbele ndani ya halmashauri zetu kitaainishwa wazi, kwamba tunahitaji Walimu watakaokwenda kusaidia kusimamia eneo la kilimo, basi sisi kama Serikali sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tuko tayari kwenda kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba malengo ya kuhudumia wananchi wetu yanakamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali kwa kifupi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Tuna walinzi katika shule zetu za msingi, sekondari, vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya lakini hakuna…

**SPIKA:** Swali, swali, swali.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, hakuna...

**SPIKA:** Swali, swali, swali, ukianza na hakuna hamna swali hapo. Uliza swali.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, je, kada hizi zinalipwa na Mamlaka ipi hasa kwa sababu kuna mkanganyiko mkubwa?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juu ya ajira hizi za walinzi na kada mbalimbali kama ulivozitaja walipaji ni halmashauri kutokana na ikama ambayo wamejipangia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itaweka kipaumbele kuajiri Maafisa Mipango na Maendeleo ya Jamii ili kupanga na kuchechemua maendeleo katika halmashauri zetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Hokororo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Mipango na kada mbalimbali katika Serikali kama ambavyo imekuwa inaombwa vibali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Vile vile, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imetoa vibali 30,000 vya kuajiri kada mbalimbali. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama eneo hilo alilolieleza na uhitaji ambao tunaufahamu, nataka nimhakikishie kabla ya mwisho wa mwaka jambo hilo tutalifanyia kazi tuweze kuhakikisha kwamba hiyo kada imeenea kama ambavyo imeombwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, sasa aulize swali lake.

Na. 83

**Ahadi ya kuwapatia wananchi eneo kutoka Mbuga ya Ipembampazi – Sikonge**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Wananchi wa Sikonge watapatiwa eneo la hekta 33,000 kwenye Mbuga ya Ipembampazi litumike kwa kilimo na ufugaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Msitu wa Ipembampazi ina umuhimu katika kuimarisha mfumo wa ikolojia wa Ugalla - Moyowosi unaojumuisha maeneo ya hifadhi yaliyopo katika Mikoa ya Tabora na Kigoma ambapo eneo la msitu huo linatumika kama mtawanyiko na mapito ya wanyamapori hususan tembo. Eneo hilo lina wanyamapori wa aina mbalimbali na limetengwa kuwa kitalu cha uwindaji wa wenyeji.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Bwawa la Olua ambalo lilizinduliwa na Mwalimu Nyerere tarehe 15 Julai, 1977, yeye mwenyewe aliahidi kwamba atatoa eneo kwa ajili ya *scheme* ya umwagiliaji kwa kutumia maji ya bwawa hilo.

Je, ahadi ya Rais tangu lini ilifutwa?

Swali la Pili; kwa kuwa Mawaziri sita wa Maliasili wameshalitembelea eneo hilo tangu mwaka 2010 na Waziri wa mwisho alikuwa Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla mwaka 1929, Je,…

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, swali sasa; ahadi ile ya Mheshimiwa Rais na ahadi ya Waziri wa Maliasili lini itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nirejee tu kwenye jibu langu la msingi kwamba maeneo haya yanapokuwa yameombwa mara nyingi wataalam wanaenda kuhakiki na wanaangalia kama kuna maeneo ambayo ndani yake kuna wanyama wakali na waharibifu hususani tembo, pia tunaangalia vitu mbalimbali ikiwemo masuala ya ikolojia wataalam walipoenda kuangalia walikuta umuhimu wa maeneo haya kuendelea kuhifadhiwa, na hii ahadi iliyotolewa ilikuwa ya mwaka 1977, tunatambua kabisa hifadhi hizi zinasimamiwa na Halmashauri lakini pale ambapo kunakuwa na umuhimu wa kuwaachia wananchi basi Serikali inafanya tathmini na inarejea na kuwarudishia wananchi waendelee kuyatumia kwa ajili ya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumuomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi bado ipo, tathmini itaendelea kufanyika na pale ambapo tutaona kuna umuhimu wa kuyarejesha haya maeneo basi tutafanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini mwaka 2021/2022 ambao mashamba yao yaliliwa mashamba yao hawajalipwa fidia yao. Je, Serikali itawalipa lini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Maboto Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi sana kupunguza madai ya kifuta machozi na kifuta jasho, kwa upande wa Mkoa wa Mara ninaahidi tu kupitia Bunge lako hili ndani ya kipindi hiki tunachoendelea na bajeti tutaenda kumalizia madai haya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Michael Mwakamo.

Na. 84

**Hitaji la Mahakama ya Wilaya - Kibiti**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO K.n.y. MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kuendelea kuniamini naahidi kwamba nitaendelea kufanya kazi kwa unyenyekevu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria sasa naomba kujibu swali Mheshimiwa Twaha Ally kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama inaendelea kutekeleza mpango wake wa ujenzi na ukarabati wa majengo katika ngazi zote. Katika mpango huo, Mahakama ya Wilaya ya Kibiti imepangwa kujengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, maandalizi ya awali yameshaanza kufanyiwa kazi na kukamilika, ikiwemo usanifu wa mradi, pamoja na maandalizi ya kabrasha za zabuni. Hivyo, mara baada ya bajeti kuanza, utekelezaji wa mradi huu utaanza mara moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru Serikali kwa majibu mazuri ya kuihakikishia Halmashauri au Wilaya ya Kibiti kupata Mahakama ya Wilaya. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa sasa hivi Mahakama hiyo iko kwenye jengo la Mahakama ya Mwanzo ambalo limechakaa. Je, Serikali ina mpango gani kulitumia au kulifanya ukarabati jengo hilo ambalo litabaki kutumika kama Mahakama ya mwanzo?

Swali la pili; Mkoa wa Pwani una Mahakama za Mwanzo 21, kati ya hizo zipo ambazo zimechakaa na nyingine zimebomoka babisa ikiwemo ya Kibaha Vijijini pale Kata ya Ruvu na Kata ya Magindu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzijenga hizi zilizobomoka na kuzifanyia ukarabati zile ambazo zimechakaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Mbunge wa Kibaha Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kufahamu endapo tutajenga Mahakama hii ya Kibiti hilo jengo ambalo sasa linatumika kama tutalikarabati. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jengo hilo litaendelea kutumika na Mahakama ya Mwanzo kwa kuwa saa hizi wametuhifadhi Mahakama ya Wilaya, kwa hiyo tutalikarabati.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anapenda kufahamu katika Mkoa wa Pwani Mahakama ya Mwanzo hizi mbili ambazo amezitaja. Mahakama yetu imeweka mpango kabambe wa kuhakikisha tunakarabati Mahakama zote ambazo zimechakaa, katika Mkoa wake wa Pwani tunakwenda kukarabati Mahakama 19 pamoja na hizi mbili ambazo amezitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana. Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuzijenga Mahakama za Mwanzo za West Meru Mkwaranga na Ngerenanyuki ambazo ziliachwa tu zikaharibika kabisa sasa hivi yamebaki magofu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, naomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wetu wa ujenzi na ikarabati wa mahakama katika mwaka huu wa fedha tunategemea kukarabati na kujenga Mahakama 60 za mwanzo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika Mkoa wake pia Arumeru tumeweka Mahakama za kukarabati tutampatia *list* ataona Mahakama zake kama zinahitaji kukarabatiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, sasa aulize swali lake.

Na. 85

**Idadi ya *Diaspora* wetu na mchango wao katika uchumi wa nchi - Tanzania**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza: -

Je! Tanzania ina *Diaspora* wangapi na ni upi mchango wao katika uchumi wa nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki naomba

kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa kutoka ofisi zetu za uwakilishi wa Kibalozi, idadi ya *diaspora* wa Tanzania ni milioni 1.5. Aidha, Wizara inakamilisha mfumo wa kidigitali wa uandikishaji wa *diaspora (Diaspora Digital hub)*, ambao unaotarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023. Mfumo huu utawezesha ukusanyaji endelevu wa takwimu za *diaspora*.

Mheshimiwa Spika, *diaspora* huchangia katika maendeleo ya nchi kwa kutuma fedha za kigeni nchini *(remittances)*, kuwekeza, kuleta mitaji, utaalam na teknolojia inayoweza kuchangia kukuza uzalishaji wa mazao, bidhaa na huduma mbalimbali zenye tija kiuchumi. Aidha, *diaspora* hutangaza fursa za kiuchumi, biashara, utalii na uwekezaji zinazopatikana nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2022, *diaspora* wa Tanzania walituma nchini kiasi cha dola za Marekani bilioni 1.1 sawa na shilingi trilioni 2.6. Vilevile, katika kipindi hicho *diaspora* walifanya uwekezaji kupitia ununuzi wa nyumba na viwanja wenye thamani ya shilingi bilioni 4.4 na ununuzi wa hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 2.5. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, idadi ya watanzania ambao wako *diaspora* milioni 1.5 ni sawasawa na idani ya wananchi wote ambao wanaoishi katika Mkoa wa Mtwara. Pia ni zaidi ya wananchi ya wananchi wote ambao wanaishi katika Mkoa wa Pwani, Songwe, Iringa, Lindi, Njombe na Katavi.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa ukubwa wa idadi ya wananchi hawa; je, Serikali haioni wakati umefika sasa

kushirikiana nao kuwa na uongozi rasmi ambao utakuwa daraja kati ya *diaspora* na Serikali yetu hapa nyumbani?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali imekiri mchango mkubwa wa *diaspora,* sasa Serikali haioni kwamba wakati umefika wa kuondoa vikwazo na kulieleza Bunge hili mchakato wa uraia ama hadhi maalum umefikia wapi? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu,

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu uongozi Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na *diaspora* ambazo ziko *organized* katika nchi mbalimbali, kwa kutambua hilo Mabalozi wetu wote katika nchi wanazotuwakilisha ndio Walezi wa Jumuiya hizi za *diaspora* na wamekuwa wakipata ushirikiano mkubwa sana katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la kuondoa vikwazo, hili ni kweli kwa kutambua mchango mkubwa wa *diaspora* katika maendeleo ya nchi yetu, tayari Serikali imeamua kutoa hadhi maalum kwa diaspora, hivi sasa Serikali inakamilisha taratibu za kuwapa hadhi maalum na muda si mrefu *diaspora* watapatiwa hadhi maalum. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Kassim Hassan Haji Mbunge wa Mwanakwerekwe, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa.

Na. 86

**Kutengeneza kitambulisho kimoja chenye taarifa zote muhimu**

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA K.n.y. MHE. HASSAN HAJI KASSIM** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kuwa na kitambulisho kimoja chenye taarifa zote za huduma ndani ya kadi moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Haji Kassim, Mbunge wa Jimbo la Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* inatengeneza vitambulisho vya Taifa kwa kutumia teknolojia ya *smart card* ambapo kitambulisho kinakuwa na *chip* inayokiwezesha kutumika kwa matumizi mbalimbali. Kitambulisho hiki kinaweza kutumika kama pochi ya fedha ya kielektroniki *(E-Wallet)*, *Atm card* kwa ajili ya kutoa fedha kutoka mashine ya *ATM*, huduma za Bima ya Afya, Kitambulisho cha Mpiga Kura na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia *NIDA* inaendelea kufanya mawasiliano na taasisi nyingine zenye vitambulisho ili kuona uwezekano wa kuoainisha taarifa zilizomo katika vitambulisho tofauti kwa madhumuni ya kuwa na kitambulisho kimoja. Mara muafaka

utakapofikia wananchi watajulishwa rasmi lini utaratibu huo utaanza kutekelezwa. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul-hafar Idrissa, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Kwa niaba ya Mheshimiwa Kassim sasa mawasiliano haya ya Serikali yatakwisha lini, ikizingatiwa Serikali yote ipo Dodoma, ili mchakato huu uanze kufanya kazi. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdul-hafar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ipo Dodoma lakini taasisi zenye kutoa vitambulisho siyo zote ziko Dodoma, ambacho tunaweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mazungumzo yanaendelea Wizara itafuatilia na ple ambapo kutakuwa na mkwamo basi ngazi za Wizara tutazungumza kwa sababu imeonekana nia ya Watanzania ni kupunguza idadi ya vitambulisho ambavyo mtu anabeba ili kuwa na kitambulisho kimoja chenye taarifa zote. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simai, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, haki ya Kitambulisho cha Mtanzania ni haki ya kila raia wa nchi hii.

Je, Serikali haioni haja ya kuambatanisha kitambulisho cha Mtanzania na cheti cha kuzaliwa mara tu baada ya mtoto kuzaliwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi tumesema umuhimu huo upo lakini kuhusu cheti cha kuzaliwa hili litakuwa la kisheria lazima sheria yetu ya *NIDA* irekebishwe Sheria ya Kitambulisho cha Taifa kwa sababu sheria ile inatambua mtu anayestahili kupewa kitambulisho ni yule aliyefikisha miaka 18 na kuendelea, lakini anayezaliwa leo anastahili kupata kitambulisho cha kuzaliwa. Kwa hivyo tutajitahidi katika marekebisho hayo kuweza kulijumuisha suala ambalo Mheshimiwa Mbunge amelihoji. Nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali haioni haja ya kuondoa matumizi ya Kitambulisho cha Taifa wakati Serikali haijajipanga kuwapa wananchi wake vitambulisho na kuondoa usumbufu unaowapata wananchi wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant Daud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja anayojaribu kuihoji inatokana tu na changamoto tulizozipata. Jambo linalotia faraja ni

kwamba katika bajeti hii tunayoendelea kuitekeleza, Serikali imeweza kutoa fedha zote zaidi ya Bilioni 40 zilizokuwa zinahitajika ili kumlipa Mkandarasi na hatimaye aweze kuzalisha vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, nimpe *assurance* Mheshimiwa Mbunge kwamba mara vitambulisho vitakapozalishwa Watanzania wote ambao walikuwa wako kwenye *backlog* hawajapata vitambulisho watapata vitambulisho vyao. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migila, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Ulyankulu ambao walipatiwa uraia wana cheti cha *NIDA*, mara kwa mara wamekuwa wakiambiwa watanyang'anywa vitambulisho vyao vya *NIDA*.

Je, ni sababu zipi ambazo zinapelekea wananchi hawa kutishiwa kunyang'anywa vitambulisho vyao vya uraia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Migilla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatuna utaratibu wa kumnyang'anya kitambulisho mtu aliye na sifa za kupata kitambulisho hicho, sasa kama pana mamlaka au Afisa yeyote wa Serikali anawatishia kwamba atawanyang'anya, tuombe tu Mheshimiwa Mbunge atupatie hizo taarifa ili tuweze kuzifuatilia kwa umakini kuona sababu na nini kilizosababisha watishiwe hivyo, lakini utaratibu huo haupo. Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas Mbunge wa Kinondoni sasa aulize swali lake.

Na. 87

**Kufanya tathmini upya kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kufanya mapitio ya tathmini kwa wananchi wanaopisha mradi wa kuboresha Bonde la Mto Msimbazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angeline Mabula, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko ya wananchi yaliyojitokeza kuhusu uthamini wa mali katika eneo la Bonde la Mto Msimbazi, Serikali kupitia Wizara yangu na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kufanyia kazi malalamiko hayo kabla ya kuidhinishwa kwa taarifa za uthamini. Aidha, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi litafanyika baada ya malalamiko hayo kupatiwa ufumbuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mradi huu unapita katika Kata za Kigogo, Mzimuni, Magomeni, na Hananasifu. Je, Serikali sasa iko tayari kutoa Tarehe au muda lini mapitio hayo yataenda kufanyika ili wananchi wa maeneo yale waweze kufahamu?

Swali langu la pili, ningependa kama ikiwezekana Serikali itoe tangazo mapema ili wananchi wale wote waweze kuwepo wakati tathmini hizo zikifanyika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Tarimba Abbas kwa maswali yake mawili.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimfahamishe kwamba katika mradi ambao unaendelea sasa pamoja na Kata alizozitaja mpaka sasa wananchi waliofikiwa ni 2,217 kati ya 2,432 ambao watafikiwa. Katika hao ambao wamefikiwa sasa katika ule mradi, asilimia 92 ni wananchi 2,057 wameshakubali wamefanyiwa uhakiki na kati yao ni 160 tu ambao hawajafikiwa. Kwa hiyo, kaya ambazo hazijafikiwa ni 215 na nadhani zipo katika yale maeneo ambayo umeyasema, hivyo wakifikiwa nadhani nao pia watapata huduma ile ile ambayo wamepatiwa wengine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu kutoa tangazo, inawezekana likatoka, lakini huwezi ukalitoa kwa sasa kwa sababu *procedure* hiyo bado inaendelea. Kampuni iliyopewa kufanya kazi hiyo bado ipo uwandani inafanya

kazi. Kwa hiyo, pale itakapokuwa imefikia kwenye hatua ambayo ni ya mwisho, kwa sababu maeneo yanayotwaliwa yote yanafahamika, basi wataambiwa wananchi, lakini kwa sasa huwezi kutoa tangazo kwa sababu bado pia tupo kwenye utaratibu wa kukamilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

Na. 88

**Kuondoa kodi kwenye vifaa tiba**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuondoa kodi kwenye vifaa tiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vifaa tiba, kinga, dawa na vitendanishi ni miongoni mwa bidhaa zenye sifa za kupata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kupitia Jedwali la II la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148. Jedwali hilo hufanyiwa maboresho mara kwa mara ili

kuhakikisha huduma zitokanazo na bidhaa hizi zinapatikana kwa gharama nafuu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika Hospitali ya *Ocean Road* kuna changamoto ya baadhi ya mashine za mionzi kukaa muda mrefu bandarani kutokana na kutokamilika kwa taratibu za kikodi; je, Serikali ina mpango gani wa kuweka utaratibu mzuri wa vifaa tiba hivyo kuondolewa mlolongo wa taratibu hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali sasa haioni haja ya kuondoa kodi zote kabisa ya vifaa tiba vyote vya wagonjwa wa kansa, figo na kadhalika ili hospitali nyingi ziweze kutibu hayo magonjwa na kutibu Watanzania walio wengi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo sasa ni mzuri, kwani Mheshimiwa Waziri wa Afya akisharidhia tu, basi vifaa hivyo vinapatiwa msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, ni kwamba vifaa tiba vyote vikiwa vya kansa, figo na kadhalika vinapatiwa msamaha wa kodi baada ya kupata ridhaa tu ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, ahsante.

**SPIKA:** Kwa hiyo, tutakuwa sahihi kwamba anayecheleweshа vifaa ni Wizara ya Afya na siyo Wizara ya Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, sisi tukipata tu barua ya Mheshimiwa Waziri wa Afya kuhusu vifaa tiba, basi tunatoa msamaha bila pingamizi yoyote.

**SPIKA:** Waziri wa Nchi, naona Waziri wa Afya hayupo wala Naibu wake. Huu ndiyo uhalisia? Kwa sababu haya maneno ya Mheshimiwa Mariam Kisangi, maana yake atakuwa kayatowa *Ocean Road*, wanasubiria vifaa viko bandarini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba suala hili tulichukue, tutalifanyia kazi vizuri Serikalini ili tuwe na majibu ambayo yana uhakika na tuweze kumkabidhi Mheshimiwa Mbunge na kuona tatizo hilo linaweza likahitimishwa namna gani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hilo litatusaidia ili tuwe na uelewa wa pamoja. Kama hivyo vifaa havidaiwi kodi, kikishafika na kimeandikwa jina la hospitali kinakoenda, kielekee huko.

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti, sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Ujenzi wa Barabara ya Kilosa – Mikumi**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, ni lini Barabara ya Kilosa hadi Mikumi itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imeanza kujenga barabara ya Kilosa – Ulaya hadi Mikumi kilometa 77 kwa awamu kulingana na kiasi cha fedha kilichotengwa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha shilingi milioni 1,300.00 zimetengwa. Mkataba wa ujenzi umesainiwa kujenga kipande cha kilometa moja katika eneo la Ulaya, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nashukuru sana kwa majibu ya Serikali kusikia kuwa barabara ya Mikumi – Kilosa imeanza kufikiriwa na itaanzwa kujengwa, lakini naomba ipewe kipaumbele kwa sababu ni barabara muhimu.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza: Kutokana na msongomano wa pale Msamvu, Morogoro Manispaa, naomba kujua barabara ya *bypass* ni lini itajengwa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: Ni lini itajengwa Barabara ya Ubena – Ngerengere mpaka Mvuha kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya *bypass* katika Mji wa Morogoro ni sehemu ya Mpango wa *Express Way* ambayo itajengwa kutoka Chalinze hadi Morogoro na iko tayari kwenye usanifu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba itatokea Kingorowira – Makunganya hadi Sanganga eneo la Mzumbe. Kwa hiyo, hilo litaondoa changamoto ambayo ipo katika Mji wa Morogoro kwa maana ya msongamano. Kwa hiyo, tayari Serikali imelifanyia kazi na limeingizwa kwenye huo mpango.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la barabara ya Ubena – Zomozi kwenda Ngerengere, barabara hii ilitangazwa kwanza kwa awamu kilometa 11.6 lakini haikupata Mkandarasi, imetangazwa tena kuijenga kwa kiwango cha lami, na hivi tunavyoongea sasa hivi, tathmini ya zabuni inaendelea kwa barabara hiyo kwa kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini barabara ya Katoke – Nyamirembe itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, kwani ipo kwenye bajeti ya mwaka huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja tumeitengea bajeti kwa ajili ya kuanza maandalizi kuijenga kwa kiwango cha lami na tuna hakika kwamba hata katika bajeti itakayokuja tumependekeza hiyo barabara ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wakati Barabara ya Namtumbo – Songea au Songea – Namtumbo inajengwa, Serikali ilifanya tathmini kwa nyumba zilizokuwa karibu na barabara na kuwalipa fedha wenye nyumba hizo zilizobomolewa, lakini leo hii kumejitokeza nyumba zilizokuwa nyuma ya upanuzi wa barabara hiyo zimeenda kuwekewa *X* na kutakiwa zivunjwe Namtumbo Mjini.

**SPIKA:** Swali.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Je, Serikali inaweza kusitisha zoezi hilo mpaka ije ifanye tathmini, nyumba hizo zisibomolewe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nimemwelewa vizuri, baada ya mabadiliko ya sheria, tuliongeza upana wa barabara kutoka meta 45 kwenda 60. Kwa hiyo, kila upande

tumeongeza kilometa 7.5 kila upande. Sasa kama suala ni hilo, Serikali inafanya tathmini kwa maeneo yote ili kujua gharama halisi ya wale ambao barabara imewafuata. Kwa sababu walikuwa wamejenga maeneo hayo kisheria, lakini kwa sababu tumeamua tupanue barabara zetu kutokana kuongezeka na kuboresha miundombinu yetu, tunalazimika, na hao watu watalipwa fidia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini sasa Serikali itamaliza kutujengea barabara inayotoka Mayanga kuelekea Mkunwa kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja itajengwa kwa kiwango cha lami, na kwa kweli itategemea na upatikanaji wa fedha na kwa kweli sina uhakika kama kwenye bajeti hii imo. Tusubiri hiyo bajeti tuone kama itakuwa ipo kwenye mapendekezo kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Barabara ya kutoka Uvinza mpaka Kasulu itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Uvinza – Kasulu ni sehemu ya barabara kuu ya kutoka Mpanda – Kasulu hadi Nyakanazi na tayari Serikali imeshaanza kuijenga kipande cha Uvinza kwenda Mpanda, na sasa hivi Serikali inatafuta fedha ili kukamilisha kipande hicho ambacho kimebaki takribani kama kilometa 57. Kwa hiyo, tutaikamilisha yote, na tumefunga upande ule wote kuwa barabara ya lami kutoka Nyakanazi – Mpanda hadi Tunduma, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Mloo – Kilyamatundu – Ilemba – Mtowisa hadi Majimoto kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kipande cha Mloo hadi Kamsamba imewekwa kwenye mapendekezo ya bajeti. Pia ilikuwa ni ahadi ya Waziri Mkuu, aliaagiza, lakini upande wa Kilyamatundu hadi Muze tumeshaanza barabara hiyo kutoka Ntendwa hadi Muze kwenda Kilyamatundu. Kwa hiyo, barabara hiyo tumeshaianza na ni matumaini yetu kwamba tutaendelea kuikamilisha. Ni barabara ndefu yenye kilometa zisizopungua 300, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya muda mrefu ya kujenga barabara ya kutoka Rujewa – Madibira mpaka Mafinga yenye kilometa 151? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilitengewa fedha kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Tunaamini pia tutaiweka kwenye mapendekezo ili iweze kuanza kwa ajili ya uzalishaji mkubwa sana wa mpunga katika eneo ambalo hii barabara inapita, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Barabara ya Kolandoto kwenda Kishapu - Mwangongo yenye kilometa 63 ni barabara ambayo sasa imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Kishapu; na barabara hii iko kwenye Mpango wa Bajeti 2022/2023; na iko

kwenye Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi; ni lini sasa barabara hii itaanza kutekelezwa rasmi?

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye, lakini hii barabara ni sehemu ya barabara ndefu ambayo tumeitengea bajeti na atakubaliana nami, kwa ajili ya kuanza maandalizi kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, tuna uhakika barabara hii kwa kuwa iko kwenye mpango na pia ni barabara kuu, Serikali itaijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 90

**Taa za barabarani Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka taa za barabarani katika Mji wa Mpwapwa ili kuongeza usalama nyakati za usiku?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi milioni 350 kwa ajili ya kuweka taa za barabarani katika Mji wa Mpwapwa kwa urefu wa kilometa 2.5. Kazi za uwekaji wa taa umeanza na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Katika Mji wa Mpwapwa kuna eneo dogo sana ambalo liliwekwa taa zamani, lakini taa hizi muda mwingi hazifanyi kazi: Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati taa hizi ili ziweze kufanya kazi angalau katika eneo hilo dogo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Mheshimiwa Rais amejenga daraja kubwa la *TANESCO* katika Mji wa Mpwapwa; daraja hili limejengwa katika eneo lenye miti mingi, kwa hiyo, husababisha giza nene wakati wa usiku. Mazingira hayo yanahatarisha usalama wa watumiaji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba jambo la kuweka taa katika eneo hili ni la dharura lisilohitaji kusubiri taratibu za manunuzi? Kama jibu ni ndiyo…

**SPIKA:** Mheshimiwa umeshauliza maswali mawili.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, lini wataweka taa katika daraja hilo?

**SPIKA:** Umeshauliza maswali mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taa tunazoweka ni kwenye Barabara ambazo ni za *TANROADS* na kilometa 2.5 naamini tutakuwa tumepita pia kwenye maeneo hayo anayoyasema na hata tutayawekea lami na kuweka taa. Kwa hiyo, nina hakika kwa kilometa mbili na nusu tutakuwa tumekamilisha taa katika Mji wa Mpwapwa. Kama kutakuwa na changamoto ya hizo taa, nitaomba Mheshimiwa Mbunge tuweze kuonana ili tulichukue kama ni jambo la namna yake ili tuweze kuangalia kama hizo taa zinarekebishika ama tutaweka taa nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili, kama nimemsikia kuhusu daraja ambalo liko katika Mji wa Mpwapwa; limeshakamilika na tunatambua kwamba kuna mmomonyoko mkubwa ambao unaendelea. Sisi kama *TANROADS* kwa maana ya ujenzi, linahusisha watu wengi; watu wa mazingira, watu wa bonde la maji, na pia TAMISEMI kwa maana ya kwamba ni wadau. Sisi tunaweza tukajenga lakini kwa kushirikiana na hao wadau, na Mheshimiwa Mbunge tulishaongea naye kwamba Serikali imelichukua kwa wadau wote, tuone namna ya kuweza kudhibiti mmomonyoko ambao unaendelea ambao pia utahatarisha hilo daraja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba liko, linafanyiwa kazi na Wizara zinazohusika kuweza kulijenga hilo daraja, kwa maana ya kurekebisha hizo kingo za daraja la huo Mto Mpwapwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba sasa aulize swali lake.

Na. 91

**Mradi wa Chumvi Ivuna Humbula – Momba**

**MHE.CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafufua Mradi wa Chumvi Ivuna – Itumbula Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Chumvi cha Itumbula kilichopo Kata ya Ivuna Wilaya ya Momba kilianzishwa na wananchi ambao wameungana pamoja kutoka Kijiji cha Ivuna na Itumbula ili kuanzisha mradi wa kuzalisha chumvi kwenye bwawa la maji ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua juhudi na jitihada za Wananchi wa Kijiji cha Itumbula na itahakikisha kuwa kiwanda hicho kinaanza uzalishaji. Serikali imeshatoa Shilingi milioni 120 kwa kuelewa kuwa ni mradi wa kimkakati lakini pia Halmashauri ya Wilaya ya Momba imetoa shilingi milioni 50 ili kusaidia katika kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Spika, aidha mikakati ya Serikali ni kuhakikisha tunahamasisha wawekezaji wengine kuwekeza katika kiwanda hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza maswali mengine mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo Serikali imetoa, majibu haya hayaendani na uhalisia wa sasa kwa namna ambavyo kiwanda kinaendelea. Haya ni majibu ya zamani kabisa. Pamoja na hivyo ninaomba niongeze maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mradi huu ni mradi wa kimkakati, tunauliza ni lini Serikali itaanza kutupatia fedha kuendeleza mradi huu kuliko kuanza kutafuta wawekezaji wa kuanza kuwekeza maana yake tulikuwa tumesha ahidiwa kupewa fedha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kupitia Wizara ya Madini, Waziri mwenye dhamana husika alipotembelea Momba alisema angetuma wataalamu wake waje kutuandikia andiko na kufanya utafiti ni kwa namna gani tuweze kuzalisha kiwango kingi cha chumvi na tuweze kuongezea fedha. Je, Serikali mmeshapata andiko hili la wataalam ili tuweze kuombea fedha ya ziada kutoka kile kiwango ambacho tulikuwa tumepewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshsimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajua changamoto ya kiwanda hiki na tathmini inaonyesha tunahitaji takribani shilingi milioni 535 ili kukamilisha ujenzi au uendelezaji wa kiwanda hicho lakini Waheshimiwa Wabunge tunajua kwamba Serikali haifanyi biashara tunachokifanya ni kuwawezesha kama hii mradi maalum wa wale wananchi ili waweze kuendeleza mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tunahamasisha pia wawekezaji wengine ambao wanaweza kuingia na kushirikiana nao wananchi ambao wameanzisha mradi huu wa chumvi ili uweze kuwa na faida kwa wananchi. Kwa hiyo, Serikali kimsingi haiwezi kufanya biashara lakini inawawezesha wananchi ili waweze kuendeleza shughuli zao za kiuchumi kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la andiko ambalo linaweza kuonesha umuhimu wa kupata fedha kupitia Wizara ya Madini. Hili tutalifanyia kazi na tutawasiliana na Wizara ya Madini ili tuone tumefikia wapi na kumpa jibu kamili Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini unalifahamu jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, samahani naomba arudie swali lake sikulipata vizuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Atakupa Mheshimiwa Naibu Waziri hapo atakapokuja halafu mtaleta majibu ya swali la Mheshimiwa Mbunge wa Momba.

Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 92

## *Mazava Winds Group* kuongezewa eneo kwa ajili ya uwekezaji – Morogoro

**MHE. NORAH W. MZERU** aliauliza:-

Je, ni lini Kiwanda cha *Mazava Winds Group* – Morogoro kitapatiwa eneo kubwa la uwekezaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *Mazava Fabrics and Production East Africa Limited* kinajishughulisha na uzalishaji wa nguo. Kiwanda hiki kipo chini ya mamlaka ya *EPZ* na kinafuata taratibu za uwekezaji zilizowekwa na Mamlaka hiyo. Kiwanda hiki kinatumia majengo ya kupanga kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya *EPZ* kwa kushirikiana na Mkoa wa Morogoro waliwezesha kupatikana kwa eneo la uwekezaji linalofahamika kwa jina la *Star City* lililopo Manispaa ya Morogoro, lenye ukubwa wa mita za mraba 20,000. Mwekezaji alikubaliana na eneo hili kuwa linafaa kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mkoa wa Morogoro umetenga eneo la uwekezaji ambalo pia linafaa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda liitwalo Kiyegera. Eneo hili linafaa kwa uwekezaji Mkubwa na Mdogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, swali la nyongeza.

**MHE. NORA W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu mkubwa wa kutenga maeneo ambayo hayana migogoro na ardhi ili kuwaruhusu wawekezaji waweze kuwekeza kwenye maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilitaka kujibu swali ambalo ameliuliza Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na masuala ya utengaji maeneo ya uwekezaji. Maelekezo ya Serikali katika mikoa yote na katika halmashauri zote ni kuhakikisha kwamba wanatenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji na maeneo yale lazima yatambuliwe ili yaweze kuwa tayari kwa ajili ya uwekezaji na kama kuna suala pengine la wananchi katika maeneo yale wanatakiwa waongee nao na waweze kuyamiliki kama ni halmashauri yenyewe au ni Serikali ya Kijiji ili muwekezaji anapopatikana kusiwe na mgogoro.

Mheshimiwa Spika, pia tunayo yale maeneo ya *EPZ* ambayo yapo yalikuwa yametengwa nayo yamewekwa kwa ajili ya uwekezaji. Kwa hiyo kwa maana ya Serikali tayari tunalitambua hilo katika kuepusha migogoro na wananchi. Na niombe Mbunge anione kama kuna eneo maalum ambalo pengine linahitaji maelezo ya ziada.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge nadhani umesikia majibu. Utaenda uonane na Waziri kwa ajili ya jambo hilo, ahsante sana.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nimeridhika na majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* Serikali imewekeza fedha nyingi na tayari *Found Machine* imeshakamilika wameshaanza kufanya kazi.

Swali langu; je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kuelekeza taasisi zake kama vile *TANESCO, TANROADS* na taasisi nyingine waweze sasa kuanza kutumia kiwanda hiki kwa kununua vipuri na chuma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha umesoma swali la msingi? Peleka swali lako kama la msingi. Hii ni mara ya pili nazungumza au wewe hauna kishikwambi hapo Mheshimiwa? Hebu liandike hilo swali lako lije lijibiwe hapa kikamilifu na Serikali. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 93

**Mkoa wa Mtwara kunufaika na uchumi wa bluu**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani Mkoa wa Mtwara umewekeza na unanufaika na uchumi wa Bluu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuufanya Mkoa wa Mtwara kunufaika na uchumi wa bluu, Serikali imeimarisha miundombinu ya Bandari ya Mtwara na kuifanya kuwa ndiyo kituo kikuu cha usafirishaji wa bidhaa na malighafi mbalimbali. Serikali pia imejenga Kituo cha uzalishaji wa mbegu za mazao ya baharini (majongoo bahari, pweza, kamba na kadhalika) ili kuwasaidia wananchi wa mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mamlaka ya Ufundi Stadi *(VETA)* inatoa mafunzo ya ufugaji wa majongoo bahari na kujenga vizimba vya ufugaji. Aidha, Serikali ya Mkoa wa Mtwara imeelekeza nguvu zake kwenye kilimo cha Mwani katika eneo la Naumo Wilayani Mtwara bila kusahau kilimo cha chumvi ya Bahari.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuvutia wawekezaji katika uchumi wa Bluu nchini hasa katika sekta za usafirishaji baharini, kilimo, uvuvi, na utalii kwa ajili ya mikoa ya pwani ukiwemo Mkoa wa Mtwara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza; miongoni mwa watu wanaolima chumvi kwa wingi ni wakazi wa Mkoa wa Mtwara, changamoto kubwa wanayoipata ni soko la uhakika. Nataka kujua mkakati wa Serikali ni upi kuhakikisha wakulima wale wa chumvi wanapato soko la uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ili kuchochea uchumi wa bluu; uwepo wa dhana bora za uvuvi ikiwemo meli ya uvuvi ya kisasa ni jambo la muhimu. Je, Serikali ina

mkakati gani wa kuleta meli ya kisasa ya uvuvi katika Bahari ya Hindi iliyopo Mkoa wa Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli moja ya changamoto kubwa tuliyonayo kwa wazalishaji wa chumvi hasa wadogo ni changamoto ya soko la uhakika kwa chumvi yao na hasa ambayo ni malighafi kwa maana ya kuwa siyo *finished product.*

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ya Serikali tumeshaanza kutekeleza na kuzuia uingizaji wa malighafichumvi au chumvi ambayo inatumika kuzalisha chumvi ya kula kutoka nje. Hili tumeshalisema na tunaamini viwanda vya ndani vinavyozalisha chumvi vitatumia malighafi zilizopo kwa maana ya chumvi inayozalishwa na wakulima wadogo wadogo wakiwemo wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, zaidi tunahamasisha katika masoko ya kikanda kwa maana ya Afrika Mashariki na *SADC* ili tuone nchi ambazo zinakosa au hazina malighafi ya chumvi zinatumia malighafi ya chumvi yetu ikiwemo inayotoka katika Mkoa wa Mtwara ambao tunaamini itakuwa ni chumvi ambayo inapelekwa kwenye masoko hayo ili waweze kunufaika zaidi na uzalishaji wa chumvi katika maeneo haya ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa meli ya kisasa ya uvuvi kama nilivyosema Serikali tunaedelea kuhamasisha uwekezaji katika maeneo yote ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha uchumi wa bluu ambayo nayo inahusisha kuwa

na meli za kisasa ambazo zingeweza kusaidia kuwa na uvuvi wa kisasa zaidi wenye tija. Serikali pia kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea na mikakati mbalimbali ambayo mojawapo ni kuona namna gani ya kutafuta wawekezaji wengi ambao wanaweza kuvua kwa tija katika bahari yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Wananchi wa Jimbo la Makambako Serikali kupitia Wizara ya Viwanda walilipa fidia ya shilingi bilioni tatu na ushee. Kuna wananchi 19 walibaki, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga inabidi swali lako upeleke kama swali la msingi kwa sababu swali la msingi lililoko hapa ambalo unauliza swali hilo la nyongeza linahusu uwekezaji kwenye uchumi wa bluu na mambo ya chumvi sasa hili swali lingine litamuweka Naibu Waziri mazingira magumu kidogo. Kwa hiyo, peleka kama swali la msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nilete matangazo niliyonayo kwenu halafu tuendelee na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tutaanza na tangazo la wageni; tutaanza na wageni walio Jukwaa la Spika, na tutaanza na wageni wangu kutoka Benki ya NMB ambao ni Dkt. Edwin Mhede, Mwenyekiti wa Bodi ya *NMB,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Aziz Dachi ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya NMB; yupo pia Ndugu

Clement Mwinuka, Mjumbe wa Bodi ya NMB; yupo Ndugu Ramadhani Mwikalo, Mjumbe wa Bodi ya NMB; yupo Ndugu Juma Kimori, Afisa Mkuu wa Fedha NMB; yupo pia Ndugu Vicky Bishubo ambaye ni Mkuu wa Idara ya Biashara ya Serikali NMB; yupo pia Ndugu Vicent Mnyanyika ambaye ni Kaimu Mkuu wa Idara ya Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma NMB; yupo Ndugu Ally Ngingite ambaye ni Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi NMB; yupo pia Ndugu Lilian Kisamba, Meneja Mawasiliano na Uhusiano NMB, yupo pia Ndugu Nsollo Mlozi, Meneja wa Kanda ya Kati (Dodoma, Singida na Morogoro) NMB. Sasa inabidi uwe umesimama mpaka makofi yaishe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana. Yupo pia Ndugu Grace Matemu, Meneja wa Tawi la Bunge NMB. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, naamini Mwenyekiti wa Bodi ameyasikia makofi hayo naamini atafanya jambo. Haya ahsante sana, sasa jambo zuri siyo kwamba ndiyo ahame hapa, lakini jambo tu la kujua kwamba yeye na Wabunge wako vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Angellah Kairuki ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao ni viongozi wakuu kutoka Wizara ya TAMISEMI na hawa wanaongozwa na Ndugu Adolf Ndunguru ambaye ni Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Sospeter Mtwale, Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI; yupo pia Dkt. Wilson Mahera, Naibu Katibu Mkuu – Afya; yupo pia Dkt. Charles Msonde, Naibu Katibu Mkuu - Elimu. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Angellah Kairuki ambao ni Wakuu wa Mikoa kutoka Tanzania Bara; tunaanza na Mheshimiwa John Vianney Mongella ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha; yupo pia Mheshimiwa Rosemary Staki Senyamule ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; yupo pia Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; yupo pia Mheshimiwa Martin Reuben Shigella, Mkuu wa Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana, yupo pia Mheshimiwa Halima Omari Dendego ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa; yupo pia Mheshimiwa Albert John Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Kagera; yupo Mheshimiwa Mwanamvua Hoza Mrindoko, Mkuu wa Mkoa wa Katavi; yupo pia Mheshimiwa Kamishna Jenerali Mstaafu Thobias Emiri Andengenye ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma; yupo pia Mheshimiwa Nurdin Hassan Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro; yupo pia Mheshimiwa Zainab Rajab Telack, Mkuu wa Mkoa wa Lindi; yupo pia Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Meja Jenerali Suleiman Mugiya Mzee, Mkuu wa Mkoa wa Mara; yupo pia Mheshimiwa Juma Zuberi Homera, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya; haya ahsanteni sana naambiwa huku kwamba yamepigwa na yale ambayo ni kwa niaba yangu kwa hiyo, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mheshimiwa Fatma Abubakar Mwasa, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro; yupo pia Mheshimiwa Kanali Ahmed Abbas Ahmed, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara; yupo Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza; ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mheshimiwa Anthony John Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, yupo pia

Mheshimiwa Abubakar Mussa Kunenge, Mkuu wa Mko wa Pwani; yupo pia Mheshimiwa Queen Cathbert Sendiga, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa; yupo pia Mheshimiwa Kanali Laban Elias Thomas, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma; yupo pia Mheshimiwa Christina Solomoni Mndeme, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mheshimiwa Dkt. Yahya Ismail Nawanda, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu; yupo pia Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mkuu wa Mkoa wa Singida; yupo pia Mheshimiwa Dkt. Francis Michael Kasabubu, Mkuu wa Mkoa wa Songwe; yupo pia Mheshimiwa Balozi Dkt. Batilda Salha Burian; Mkuu wa Mkoa wa Tabora, yupo pia Mheshimiwa Waziri Kindamba ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wadau mbalimbali ambao Mheshimiwa Angellah Kairuki amewaalika na hawa ni Ndugu Suzana Chuma, Meneja Mwandamizi Serikali za Mitaa CRDB Makao Makuu, karibuni sana; yupo pia Ndugu Andrew Mheziwa ambaye ni Meneja Mahusiano Huduma za Kibenki kwa Serikali CRDB, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Ara Hitoshi ambaye ni Mwakilishi Mkuu wa *JAICA*, karibu sana, yupo pia Ndugu Mbonisewa Mtambalike, Afisa Programu *JAICA*, Ndugu Suzuki Yoji Mshauri wa Miradi ya *O & OD-JAICA,* Ndugu Joseph Sayi ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Kanda ya Kati-Vodacom, Ndugu Dkt. Florence Turuka, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri- *DART,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni mbaliambali ambao ni wageni wenu pia wapo wageni 14 wa Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 33 wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao ni Wenyeviti wa CCM Wilaya, Wenyeviti wa Jumuiya Wilaya, Wenyeviti wa Kata na Makatibu Kata kutoka Jimboni kwake Chamwino Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Nusrat Hanje ambao ni marafiki zake kutoka Taasisi ya Fahari ya Mama Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Asia Halamga ambaye ni Kada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Kavejuru Felix ambaye ni Mpiga kura wake kutoka Buhigwe Mkoa wa Kigoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Abdallah Chikota kutoka Taasisi ya *Cari Vission Study Abroad* ambayo inashughulika na kuwatafutia watu vyuo vikuu vya nje nchini wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Jacqueline Mbise, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni. Ninalo tangazo lingine ambalo linatoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa na pia mnakumbushwa kwamba siku ya leo Benki ya NMB imeandaa *Iftar* Maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge wote. *Iftar* hii itafanyika katika viwanja vya Bunge leo siku ya Ijumaa kuanzia saa 12.30 jioni. Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote mnaalikwa kwenye *Iftar* hii ambayo NMB wametuletea. Karibuni sana wageni wetu tunaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Angela Jasmin Kairuki aje awasilishe hoja ya TAMISEMI. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyochambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais (Fungu Namba 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 2) na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI (Fungu Namba 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 2) na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumisha Halmashauri 184 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru kipekee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kuniteua katika wadhifa wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Nikiri kwamba nimeelemewa na imani yake kubwa kwangu. Ninamuahidi kwamba nitatekeleza wajibu wangu na kufanya kazi kwa uaminifu, ufanisi, weledi na uadilifu mkubwa ili kutimiza matarajio yake aliyonayo kwangu na kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia kipekee wanachama wenzangu wote wa Chama cha Mapinduzi kwa namna tunavyoendelea kushirikiana katika kukiimarisha chama chetu ili kiendelee kushika dola.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee pia naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake wa miaka miwili tangu alipoingia madarakani. Tumeshuhudia miaka miwili yenye ushindi mkubwa, heshima na ushawishi mkubwa wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake mahiri wenye kuzingatia uadilifu, uwajibikaji, utendaji wenye malengo na unaozingatia matokeo chanya kwa manufaa ya wananchi anaowaongoza. Hii inathibitisha kiu na utashi mkubwa alionao wa kuwaletea maendeleo wananchi na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Tumeshuhudia mafanikio makubwa ya nchi nzima na kwa Ofisi ya Rais

TAMISEMI tumeshuhudia maboresho makubwa na miradi mingi ya maendeleo katika mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa hakika ni miaka miwili ya mafanikio makubwa na yenye kishindo kikubwa na cha kuacha alama.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais, katika utekelezaji wa majukumu ili kuleta mabadiliko ya kweli na maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ya bajeti, tunamshukuru pia kwa ufatiliaji wake wa karibu na ziara zake za mara kwa mara katika mikoa na wilaya zetu. Vilevile nampongeza kwa kutekeleza madaraka yake ya kikatiba ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika usimamizi na utekelezaji wa siku kwa siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi, busara na hekima. Nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azan Zungu Naibu Spika, kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge waliochaguliwa kwa umakini wao wa kuliongoza Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa George Simbachawene Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais kwa ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee pia kutumia nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote kwa kuendelea kuaminiwa

na Mheshimiwa Rais ili kumsaidia katika kuwaletea Watanzania maendeleo kwa kasi kubwa zaidi chini ya kauli mbiu ya kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo Mbunge wa Jimbo la Mikumi, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga Mbunge wa Kilolo na Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi, ushauri na miongozo yao kuhusu utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu yote 26 ya Mikoa ikujumuisha Halmashauri 184 Kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Naishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yote 28, kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 na kuyapitisha kwa kauli moja. Maadam imani huzaa imani, nawaahidi mimi na wenzangu wizarani, hatutawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile, nisingeweza kuandaa hotuba hii ya bajeti peke yangu. Uungwana unanitaka kutambua mchango mkubwa wa wenzangu wakioongozwa na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, na Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Naibu Mawaziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote na Makatibu Tawala wote Tanzania Bara. Aidha, natambua mchango mkubwa wa wataalam wakiongozwa na Ndugu Adolf Ndunguru Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Charles Enock Msonde, Dkt. Wilson Charles Mahera na Ndugu Sospeter Mambile Mtwale, Makamishna, Wenyeviti wa Bodi, Watendaji wote Wakuu wa Tume na Taasisi, Wakurugenzi na Watumishi wote wa TAMISEMI kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha ofisi yetu kufikia malengo ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa

wakati. Nasimama hapa kwa kujiamini kwa sababu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Aman Zanzibar, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa. Aidha, nitoe pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, majukumu haya makubwa, na wajibu mkubwa unaoambatana nayo, vinahimilika tu pale panapokuwa na amani ya moyo. Kipekee, niwashukuru sana wanaonipa amani ya moyo, kunitia moyo kuyakabili na kuyahimili majukumu yangu. Namshukuru sana mume wangu mpenzi, Balozi Mbelwa Kairuki, wanangu Kemilembe, Esther na Mwesigwa kwa kunifariji, kunitia moyo na kunipa tumaini. Hali kadhalika, ndugu, jamaa na marafiki kwa kunivumilia pale ninapokosekana miongoni mwao sababu ya kutekeleza majukumu yangu ya uwaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake wakati akihutubia Bunge lako la 12, tarehe 22 Aprili, 2021 yaliyohusu Kuendelea na jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi, hususani Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kutoa mikopo ya asilimia kumi kupitia mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, Ofisi ya Rais -TAMISEMI inafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati akipokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 tarehe 29 Machi, 2023, ambapo alielekeza; Kufanya marekebisho makubwa kwa kuingiza mfumo wa kibenki katika utoaji na urejeshaji wa mikopo ya asilimia kumi

ya mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuondoa vikundi hewa na upendeleo wakati wa utoaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita dhidi ya rushwa, ubadhilifu, uzembe, ukiukwaji wa maadili, urasimu na kuwawajibisha wale wote wanaodhibitika na kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazochukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinazowahudumia wananchi wake vyema na dhamira hii itatimia tu endapo Watumishi wote na Viongozi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa watafanya kazi kwa juhudi, maarifa, na uadilifu mkubwa. Pia, inasisitizwa utoaji wa huduma bora na wa haraka, wenye staha na wenye ufanisi ili kuondokana na kuwasumbua na kuwazungusha wananchi; kukusanya mapato kwa ufanisi na kudhibiti mianya ya makusanyo na matumizi yenye kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka wa fedha wa 2022/2023 pamoja na Mpango na Bajeti na Maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli na mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi trilioni 1.07. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 59.19 ni kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, shilingi milioni 249.28 ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.01 ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari, 2023 fedha zilizotarajiwa kukusanywa ni shilingi bilioni 714.48 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 647.88

kimekusanywa, sawa na asilimia 90.68 ya fedha zilizotarajiwa kukusanywa kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu Namba 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) na Mafungu 26 ya Mikoa yakijumuisha Halmashauri 184 iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 9.04. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 3.53 ni fedha za maendeleo na shilingi trilioni 5.51 ni za matumizi ya kawaida, yakijumuisha mishahara shilingi trilioni 4.63 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 885.59 kama inavyooneka katika kiambatisho namba 2.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2023, Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yalitarajia kupokea na kukusanya shilingi trilioni 6.05. Kati ya fedha hizi, shilingi trilioni 5.54 zimepokelewa sawa na asilimia 91.63 ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 1.95 ni fedha za Miradi ya Maendeleo na shilingi trilioni 3.59 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, yakijumuisha mishahara shilingi trilioni 2.94 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 644.41 kama katika (kiambatisho Namba 2). Pia Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopokelewa kwa Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI mchanganuo wake ni kama unavyoonekana katika aya ya 23 – 33 ya Hotuba ya yangu hii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa kina wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa hadi Februari 2023 ni kama unavyo onekana katika aya ya 34 – 197 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yaliyotekelezwa kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, ziliidhinishwa shilingi bilioni 143.15 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Afya ya Msingi. Hadi Februari, 2023, shilingi bilioni 124.10 zimepokelewa ambazo ni sawa na asilimia 86.69 ya fedha iliyoidhinishwa ya utekelezaji na kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza ujenzi wa hospitali 31 za halmashauri zilizoanza ujenzi katika mwaka wa fedha wa 2020/2021;

(ii) Kuendeleza ujenzi wa hospitali 28 za halmashauri zilizoanza ujenzi katika mwaka wa fedha wa 2021/2022;

(iii) Ukarabati wa hospitali kongwe 19 za halmashauri.;

(iv) Ukamilishaji wa maboma 300 na zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi; na

(v) Ununuzi wa vifaa na vifaa tiba ambapo shilingi bilioni 54.55 zimepokelewa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 11.95 ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaatiba kwa zahanati, shilingi bilioni 36.75 ni kwa ajili ya vituo vya afya na shilingi bilioni 5.85 ni kwa ajili ya vifaatiba vya kinywa na macho kwa hospitali za halmashauri 71.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Elimu Msingi na Sekondari hadi Februari, 2023, shilingi bilioni 607.56 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya shule na utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea na Utekelezaji wa Sera Elimu bila malipo, ambapo shilingi bilioni 235.75 zimetumika;

(ii) Shilingi bilioni 160 zimetumika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa 8000 katika shule za sekondari na ujenzi umekamilika;

(iii) Shilingi bilioni 12.41 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 170 za Walimu na shule za msingi zenye uwezo wa kuchukua kaya 510 wa ujenzi wa nyumba hizi uko katika hatua mbalimbali;

(iv) Shilingi bilioni 5.45 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 4,954 na ujenzi uko katika hatua mbalimbali;

(v) Shilingi bilioni 21.44 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 1,072 vya madarasa katika shule kongwe za msingi ambapo ujenzi pia uko katika hatua mbalimbali;

(vi) Bilioni 2.40 kwa ajili ya ujenzi wa shule tano mpya za msingi;

(vii) Bilioni 1.37 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa bweni 45 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi;

(viii) Bilioni 10.11 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 809 ya madarasa katika shule za msingi;

(ix) Bilioni 8.13 zimepokelewa kwa kukamilisha vyumba 271 ya maabara katika shule za sekondari;

(x) Shilingi bilioni 3.89 kwa ajili ya ukamilishwaji wa mabwalo 78 katika shule za msingi na sekondari;

(xi) Shilingi bilioni 8.20 kwa ajili ya mabweni 410 katika shule za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum; na

(xii) Shilingi bilioni 138.72 kwa ajili ya kuwezesha kufanyika kwa Mitihani ya Taifa ya darasa la nne, darasa la saba, kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023 tumeshuhudia wanafunzi 1,500,227 wa elimu ya awali wameandikishwa sawa na asilimia 109.37 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,371,690 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,411 ambapo wasichana ni 1,211 na wavulana ni wanafunzi 1,200. Katika Mwaka 2023 wanafunzi 1, 786,485 waliandikishwa na ni sawa na asilimia 109.07 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1, 637,897.

Mheshimiwa Spika, jumla ya wanafunzi milioni 1.076 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 na hadi Februari, mwaka huu wanafunzi 1,003,982 wameandikishwa ambao ni sawa na asilimia 93.3 ya wanafunzi waliochaguliwa na wanafunzi 90,898 sawa na asilimia 52.41 ya wanafunzi 173,422 wenye sifa walichaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule 508 za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu ya barabara hadi Februari, 2023 shilingi bilioni 577.8 zimepokewa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara na utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia fedha za ndani za Mfuko wa Barabra tozo ya shilingi mia moja kwa lita na fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali *(TARURA)* Ilitekeleza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 163.83;

(ii) Matengenezo ya barabara za lami zenye urefu wa kilometa 14,000,826.35;

(iii) Ukarabati wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilometa 4,724.15;

(iv) Mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 5,267.85; na

(v) Ujenzi wa madaraja 75 na makalvati 95.

Mheshimiwa Spika, Wakala unaendelea kujifunza kutoka Zanzibar na kufanya majaribio ya teknolojia mbalimbali ili kutumia udongo uliopo katika eneo la kazi badala ya kusomba kutoka maeneo mengine ya mbali. Teknolojia hizo ni pamoja na *ECOROADS, Ecozyme* pamoja na *geopolymer* na hadi sasa majaribio ya kutumia teknolojia ya *ECOROADS* yameshafanyika katika Jiji la Dodoma kwa upande wa Ilazo ambapo kilomita moja imejengwa na kukamilika. Faida zinazoelezwa na kuwekwa kwenye machapisho mbalimbali za teknolojia mbadala kwa wadau ni pamoja na uhifadhi wa mazingira, kupunguza muda wa ujenzi wa barabara kulinganishwa na ujenzi unaofanywa sasa kwa zaidi ya asilimia 40 na kupunguza pia gharama za matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Watumishi Walimu imepokea Shilingi Bilioni 7.83 na imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Imesajili Walimu 9,800;

(ii) Kupandishwa vyeo Walimu 1,003;

(iii) Imethibitisha kazini Walimu 3,347;

(iv) Pia Walimu 3,388 wamebadilishiwa vyeo;

(v) Pia TANGE za Walimu nchi nzima katika Wilaya zote 139 zimeweza kuhuishwa;

(vi) Pia tumeona vikao zaidi ya 300 vya Halmashauri ya Nidhamu kwa Walimu za kisheria vimefanyika;

(vii) Mashauri 273 ya nidhamu ya Walimu yamefanyiwa uchunguzi na kuwasilishwa katika Kamati za Wilaya kwa ajili ya kutolewa uamuzi; na

(viii) Rufaa 144 zilitolewa uamuzi ambapo Walimu 15 wamerejeshwa kazini, walimu 74 walifukuzwa kazi, mwalimu mmoja alishushwa cheo na walimu sita walipunguziwa asilimia 15 ya mishahara. Mashauri 33 yamerudishwa kwenye Kamati za Wilaya ili kuanza upya na rufaa zilizokatwa nje ya muda ni 15.

Mheshimiwa Spika, watumishi 133 wa Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya kutoka katika Mikoa 14 walipatiwa mafunzo, kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu au *Teacher's Service Commission Management Information's System*.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 yamezingatia mpango mkakati wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI wa miaka mitano kati ya 2021 – 2026. Mipango Mikakati ya Taasisi, Mikoa na Halmashauri, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa 2020, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 22 Aprili, 2021 hapa Bungeni, Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, Sera za Kisekta, Maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo yaliomo katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano 2021 – 2026, Ajenda ya Afrika ya 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2030.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kutekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:-

(i) Kusimamia masuala ya Utawala Bora;

(ii) Kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma *(D by D)*;

(iii) Kuratibu maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwenye vijiji 12,318, mitaa 4,263, vitongoji 64,361 katika halmashauri 184 utakaofanyika Mwaka 2024;

(vi) Kuratibu suala la ulinzi na usalama katika mikoa na wilaya;

(vii) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya jamii katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(viii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji za huduma za afya msingi, ustawi wa jamii na lishe katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ix) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu msingi na sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijimuishwa utekelezaji wa elimu msingi na sekondari bila ada;

(x) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongezwa ukusanywaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xi) Kuratibu ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara, usafirishaji, afya ya msingi,

elimu msingi na sekondari na majengo ya utawala katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Mitaa;

(xii) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

(xiii) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi shindani kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xiv) Kuweka mazingira mazuri ya uanzishwaji wa viwanda, biashara na uwekezaji hasa katika kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, nyuki, wanyamapori na utalii;

(xv) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

(xvi) Kuratibu utaratibu mpya wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo ya asilimia 10 ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

(xvii) Kuratibu masuala ya michezo na utamaduni katika ngazi zote za Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xviii) Kuratibu usimamizi wa masuala ya uhifadhi na utunzaji wa misitu, wanyamapori, nyuki, vyanzo vya maji, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na fursa za mabadiliko hayo kupitia biashara ya kaboni au vyoukaa na udhibiti wa uzalishaji taka katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xix) Kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Mitaa na Taasisi zilizo chini yake;

(xx) Kuendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kusajili vikundi vya ujasiriamali na vikundi vya huduma ndogo za kifedha;

(xxi) Kuboresha miundombinu ya Masoko, Ujenzi wa Ofisi za Machinga na Bodaboda pamoja na kuandaa na kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia utaratibu mpya wa mfumo wa kibenki kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais;

(xxii) Kuratibu uendelezaji wa vijiji na miji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuzisimamia Mamlaka za Upangaji katika kupanga na kuendeleza Mipango Miji na matumizi endelevu ya ardhi vijijini, ujenzi wa nyumba bora na kudhibiti ujenzi holela;

(xxiii) Kutunza mipaka ya maeneo ya utawala na kuzuia na kutatua migogoro inayohusu ardhi; na

(xxiv) Kuratibu uendelezaji wa Vijiji na Miji kwa utangamano na shughuli za kilimo, uvuvi, mifugo, huduma za maji, umeme, barabara na sekta nyingine za uzalishaji na masuala mengine mtambuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 199.19 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zinazoombwa shilingi bilioni 38.65 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi bilioni 10.53 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 28.11. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 160.53 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na kati ya fedha hizo shilingi

bilioni 112.12 ni fedha za nje na shilingi bilioni 48.41 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, shughuli zinazopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Programu ya kuimarisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 7.86;

(ii) Mradi wa ufuatiliaji na tathimini shilingi bilioni 4.40;

(iii) Mradi wa Usafi wa Mazingira shilingi bilioni 1.07;

(iv) Programu ya Uhamasishaji na Uchambuzi wa Sera kupitia *UNICEF* shilingi bilioni 3.660;

(v) Mradi wa kuboresha Elimu ya Awali na Msingi *(Primary Students Learning Boost)* shilingi bilioni 20.25;

(vi) Mradi wa Uimarishaji wa Ufundishaji na Ujifunzaji kupitia *GP learning phase two* shilingi bilioni moja;

(vii) Programu ya Elimu Msingi bila malipo, ununuzi wa vitabu shule ya msingi na sekondari shilingi bilioni 34.40;

(viii) Programu ya kuboresha elimu katika shule za sekondari *SEQUIP* shilingi bilioni 25.34;

(ix) Mradi wa kuhimarisha huduma za vifaa na ubora wa huduma za afya msingi shilingi bilioni 44.89;

(x) Mradi wa Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko na Matukio yenye athari ya Usalama wa Afya ya Jamii shilingi bilioni 3.75; na

(xi) Programu ya Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria kupitia *Global Fund* shilingi bilioni 8.70.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Maendeleo zitakazotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, ni kama zilivyoainishwa katika aya ya 201 – 229 inayopatikana katika Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inasimamia Taasisi saba ambazo ni Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA)*; Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam *(DART);* Shirika la Elimu Kibaha; Chuo cha Serikali za Mitaa; Shirika la Masoko ya Kariakoo; Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Tume ya Watumishi wa Walimu *(TSC)*.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Taasisi zimepanga kutekeleza malengo mbalimbali na malengo hayo yanajumuisha shughuli za maendeleo zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TARURA* kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 21,109.7, ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 300.61 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 8,649.97 kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa madaraja 168, ujenzi wa makalavati 317, ujenzi wa mistari ya makalavati 949, mifereji ya maji ya mvua kilomita 28.13 na ujenzi wa *drift* mbili. Ujenzi wa barabara kupitia mradi wa barabara wa *RISE*, ambapo barabara zenye urefu wa kilometa 33 zitajengwa kwa kiwango cha lami na usanifu wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 159.05. Kusimamia mradi wa uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi, kuanza ujenzi wa miundomnibu ya msingi ya Miji 12 kati ya 45 kupitia mradi wa kuboresha miundombinu shindanishi katika Miji Tanzania *TACTIC*. Ujenzi wa barabara za kiwango cha lami zenye jumla ya urefu wa

kilomita 43.82 ambazo zitajengwa kupitia mradi wa *Agri-connect*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala wetu wa *DART,* tutaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Awamu ya Tatu itakayohusisha barabara zenye urefu wa kilomita 20.6. Itakamilisha taratibu za ununuzi wa mtoaji wa huduma za mabasi ya awamu ya kwanza na ya pili. Itafanya ukarabati wa mara kwa mara wa miundombinu ya mradi. Itaboresha usafi wa mzingira katika mtandao wa wakala wa mabasi yaendayo haraka. Itadumisha usalama kwa kuimarisha ulinzi katika mtandao wa wakala la *DART*. Kubadilisha mfumo wa uendeshaji na ulipaji wa watoa huduma kutoka kupokea tozo kupita katika mfumo wa *DART* au *access fee* na kuanza kutumia utaratibu wa malipo ya umbali wa mabasi yatayokuwa yanatembea *per kilometer mode* na kukamilisha mapitio ya sheria ya wakala wetu wa *DART.*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya Utumishi wa Waalimu. Nitaendelea kusimamia utumishi huu na maendeleo ya Waalimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo katika Utumishi wa Umma. Kuendesha mashauri ya nidhamu kwa Walimu katika ngazi ya Wilaya. Kuendesha rufaa za Walimu waliokata rufaa ngazi ya Tume katika Makao Makuu. Kuwapandisha vyeo Walimu wenye sifa kwa wakati baada ya kupata vibali kutoka katika Mamlaka husika. Kuwabadilisha vyeo Walimu baada ya kujiendeleza, kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume Makao Makuu, Kuimarisha mfumo wa Kielektroniki wa *Teachers Service Commission Management Information System* na Kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wetu wa Tume ya *TSC*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo. Kitadahili wanafunzi wapya 9,500 kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Shahada ya Kwanza, Kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala mbalimbali yanayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kuendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Watumishi na Viongozi

waliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau kutoka maeneo mbalimbali, Kuhuisha na kuandaa mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa na mahitaji ya baadaye, Kuanzisha Kampasi ya Shinyanga, na kuanza ujenzi wa jengo la Utawala Awamu ya Kwanza katika Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shirika la Elimu Kibaha. Tutaendelea kutoa elimu ya msingi kwa wanafunzi 2,703 na elimu Sekondari wanafunzi 357. Tutaandaa na kusimamia mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao (*e-learning management system*) na kutoa Elimu ya Sekondari. Kuboresha utoaji wa elimu kwa wahudumu wa afya 572 katika fani ya utabibu na uuguzi kupitia Chuo cha Sayansi Shirikishi Kibaha, sambamba na kutoa elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi 500.

Mheshimiwa Spika, tutatoa elimu na mafunzo ya stadi mbalimbali za ujuzi na ubunifu katika fani kwa vijana 400 kwa kozi za muda mrefu lakini pia kwa wananchi 1,000 kwa kozi za muda mfupi kwa mafunzo ya ana kwa ana lakini pia kwa mfumo wa mtandao *(e-learning)*. Tutaendelea na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha sambamba na kuboresha miundombinu ya mashamba darasa ya kilimo pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shirika la Masoko ya Kariakoo; kwa mwaka 2023/2024 tutaendelea na ujenzi wa soko jipya na ukarabati wa soko lililoungua ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Oktoba, mwaka huu 2023. Aidha, Shirika la Kariakoo litaandaa Mpango wa Uwekezaji katika maeneo yanayomilikiwa na Shirika yaliyoko Mbezi Beach Makonde katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na Tabata Bima katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Tutakusanya marejesho ya mikopo, makusanyo na michango kutoka katika Halmashauri na mapato mengine ya ndani ambapo kiasi cha shilingi bilioni 4.13 kinatarajiwa kukusanywa. Tutatoa Mikopo kwa Halmashauri yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 3.96 ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Tutakamilisha maboresho ya muundo wa Bodi yetu ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ili kuiwezesha Bodi hii kutekeleza majukumu yake ya msingi na kwa mujibu wa Sheria. Tutakamilisha marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Bodi ili iweze kuendana na mabadiliko ya kisera na kiuchumi lakini pia mahitaji ya Halmashauri zetu. Tutaendelea kutoa huduma za kitaalam ya kuandaa maandiko ya miradi katika Halmashauri na kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wetu wa Bodi kuhusu namna ya kuchambua maandiko ya miradi, utoaji, usimamizi lakini pia ufuatiliaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, malengo ya yatakayotekelezwa na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ilivyoainishwa katika aya ya 230 mpaka aya ya 241 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itazingatia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maduhuli na mapato ya ndani. Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Halmashauri na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI zimepanga kukusanya maduhuli na mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi trilioni 1.19. Kati ya fedha hizo, bilioni 55.14 zimepangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, shilingi milioni 261.89 zitakusanywa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na shilingi trilioni 1.14 zitakusanywa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa makusanyo ya Halmashauri, shilingi bilioni 689.46 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 454.41 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mgawanyo huu unatokana na madaraja ya Halmashauri ya kuchangia shughuli za maendeleo kutokana na mapato ya ndani kwa asilimia 70, 60, 40 na 20 kama inavyoonekana katika Kiambatisho Namba 11.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya elimu; tutaendelea kugharamia elimu bila ada kwa shule za msingi na sekondari ambapo bilioni 399.64 zimetengwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 157.79 zimetengwa kwa ajili ya shule ya msingi na shilingi bilioni 241.85 zimetengwa kwa ajili ya shule za sekondari. Bajeti hii ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 53.15 sawa na asilimia 15.34 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka jana. Ongezeko hili linatokana na wanafunzi wa kidato cha tano na sita kujumuishwa katika Mpango wa Elimu Msingi na Sekondari bila ada.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea na mpango wa ujenzi wa matundu ya vyoo katika vituo shikizi ambapo shilingi bilioni 5.74 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa matundu 5,218 ya vyoo. Pia tumetenga shilingi bilioni 5.52 kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 5,020 kwa kidato cha tano na sita kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, tutajenga mabweni 61 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo tutatumia shilingi bilioni 7.86. Aidha, tumetenga Shilingi Bilioni 2.58 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa uzio wa mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kujenga vyumba vya madarasa kwa Kidato cha Tano na cha Sita kwa sekondari ambapo shilingi bilioni 47.89 zimetengwa. Tutaendelea na mpango wa ukarabati wa shule kongwe za msingi na sekondari ambapo shilingi bilioni 37.49 zimetengwa, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 33.12 ni ukarabati wa shule kongwe 184 za msingina shilingi bilioni 4.37 ni kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za

sekondari. Pia tutasimamia mitihani na tumetenga shilingi bilioni 243.61.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya; tutaendelea na ujenzi wa hospitali 41 za Halmashauri ambapo shilingi bilioni 30.29 zimetengwa. Tutaendelea na mpango wa ukarabati wa hospitali kongwe za Halmashauri 31, ambapo Bilioni 27.9 pia zimetengwa. Tutajenga vituo vya afya 16 na kukamilisha vituo vya afya vingine Sita ambapo shilingi bilioni 9.54 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea na mpango wa ukamilishaji wa zahanati 376 katika Halmashauri, ambapo shilingi bilioni 18.80 zimetengwa. Tutanunua vifaa na vifaatiba katika hospitali za Halmashauri, vituo vya afya na zahanati, ambapo shilingi bilioni 116.92 zimetengwa na kati ya fedha hizo bilioni 15.50 zitatumika kununulia vifaa na vifaatiba katika hospitali 31, shilingi bilioni 83.07 kwa ajili ya vituo vya afya 278 na shilingi bilioni 18.35 kwa ajili ya zahanati 364.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa majengo ya utawala na nyumba za viongozi; tutajenga na kukamilisha na kukarabati Ofisi za Wakuu wa Mikoa 16 ambapo shilingi bilioni 7.84 zimetengwa. Tutajenga na kukamilisha na kukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya 28 na tumetenga shilingi bilioni 8.93. Tutajenga, kukamilisha na kukarabati Ikulu Ndogo nane na tumetenga shilingi bilioni 1.61 kwa ajili hiyo. Tutajenga na kukamilisha na kukarabati nyumba 11 za Wakuu wa Mikoa na tumetenga shilingi bilioni 1.52 kwa ajili hiyo. Tutajenga na kukamilisha na kukarabati nyumba Nne za Makatibu Tawala wa Mikoa na tumetenga shilingi milioni 723.72. Tutajenga na kukamilisha na kukarabati nyumba za Maafisa Tarafa saba kwa gharama ya shilingi milioni 560. Tutajenga na kukamilisha na kukarabati nyumba za Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa 13 kwa shilingi bilioni 1.44. Tutajenga, kukamilisha na kukarabati nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya nne kwa shilingi milioni 435.

Mheshimiwa Spika, pia utajenga, kukamilisha na ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Wilaya 16 ambapo tumetenga shilingi bilioni 2.56, kwa hitimisho tutajenga kukamilisha na kukarabati Ofisi za Maafisa Tarafa 31 ambapo tumewatengea shilingi bilioni 3.24.

Mheshimiwa Spika, kwa upande *wa* Majengo ya Utawala ya Halmashauri. Kwa Mwaka ujao wa fedha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI tumetengewa shilingi bilioni 49.32 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri *71*. Aidha, shilingi bilioni 14.70 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika Halmashauri 50 kama mnavyoona katika kiambatisho Na. 19.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nyumba za Wakurugenzi na nyumba za Wakuu wa Idara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi ya Rais -TAMISEMI tumetengewa shilingi bilioni 15.25 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya Wakurugenzi wetu Watendaji wa Halmashauri na Wakuu wa Idara na kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 6.63 ni kwa ajili ya nyumba 35 za Wakurugenzi wa Halmashauri na shilingi bilioni 8.62 ni kwa ajili ya nyumba 25 za Wakuu wa Idara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya kimkakati. Ofisi ya Rais -TAMISEMI katika mwaka ujao wa Fedha imetengewa shilingi bilioni 26.98 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi 18 ya kimkakati katika Halmashauri. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, inaboresha vigezo vya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo ya Halmashauri kama inavyoonekana katika Kiambatisho Namba 20.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua boti Nne katika Halmashauri za

Wilaya za Ludewa, Buchosa, Nyasa pamoja na Sumbawanga ili kuimarisha doria, ulinzi na ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imetengewa shilingi bilioni 16.58 kwa ajili ya ununuzi wa magari 81 katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Kati ya magari hayo, Matano ni ya Wakuu wa Mikoa, magari Mawili ni ya Makatibu Tawala wa Mikoa na magari 74 ni kwa ajili ya Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa shilingi bilioni 15.99 kwa ajili ya kuchochea maendeleo katika Majimbo 214 ya Tanzania Bara au Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha ujao, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali itaziimarisha taasisi za kijamii kwenye ngazi za msingi ili ziwe utangamano na ziweze kuleta tija na kuinua ustawi wa jamii kwa utaratibu maalum utakaokuwa jumuishi. Lengo letu ni kuleta mageuzi *(transformation)* yatakayokuwa na tija katika uendelezaji wa Vijiji nchini. Mambo yatayozingatiwa ni pamoja na utangamano katika maendeleo ya Vijiji na Miji ikiwemo Miji Midogo inayochipukia, kuimarisha taasisi za kijamii kwenye ngazi za msingi na kujenga uchumi mahalia. Aidha, kuimarisha ufikishaji sawia wa huduma za umma kwa wananchi walio wengi, Utunzaji wa mazingira na kuendeleza biashara ya Hewa Ukaa kwenye Vijiji na kujenga uwezo na kuratibu utunzaji na matumizi ya raslimali, utalii na mila na kuimarisha Hatimiliki kwa usawa wa kijinsia kuendeleza mipango kabambe na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Vijijini na kusimamia vyema mipango ya uchumi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha tutaendelea na utekelezaji wa uanzishwaji, upangaji na uendelezaji wa Jiji la Kibiashara la Kwala, kwa kushirikiana na

Ofisi ya Rais – Ikulu, Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uendelezaji wa Ardhi. Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kisekta, Taasisi na wadau wengine tunatekeleza Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambapo Halmashauri 55 zilipata mkopo wa shilingi bilioni 49.47 na umetekeleza Mradi huu wa KKK ili kuboresha utoaji wa huduma za ardhi ambao umeleta mafanikio makubwa ya kuwezesha kupima ya viwanja 232,537 na umefikia lengo la asilimia 91.73.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaimarisha shughuli za ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji pamoja na ukaguzi na ufuatiliaji wa fedha katika Mikoa na Serikali za Mitaa na hii ni kutokana na uundwaji wa idara mahsusi ya usimamizi ufuatiliaji na ukaguzi katika Ofisi ya Mikoa, ikiwa ni pamoja na ongezeko la fedha za ufatiliaji na tathmini kutoka shilingi bilioni tatu hadi shilingi bilioni 9.46 zilizotengwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, napende kutoa maelekezo yafuatayo:-

(a) Wakuu wa Mikoa ni vyema wasimamie miradi inayotekelezwa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili iweze kukamilika kwa wakati baada ya ofisi hizi kuongezewa bajeti pamoja na magari 26 kwa ajili ya ufuatuliaji, usimamizi na ujifunzaji katika Mikoa yote.

(b) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwezeshe Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani kwa kuvipatia vitendea kazi na bajeti kupitia mapato ya ndani na Halmashauri zenye mapato makubwa yasiyolindwa kuanzia Shilingi Bilioni Tano na kuendelea wahakikishe wananunua magari kwa ajili ya vitengo hivyo.

(c) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziendelee kuziwezesha Ofisi za Kata kwa kuziwekea bajeti ili ziweze kusimamia ngazi za msingi za Halmashauri katika kusimamia shughuli za Serikali katika maeneo yao. *(Makofi)*

(d) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zifanye usimamizi maalum wa miradi inayokamilishwa na fedha zilizovuka mwaka kwa kuzingatia muda uliowekwa kisheria na Sheria ya Bajeti kwa kuzingatia Kanuni 21(1)(4).

(e) Uidhinishwaji wa Mpango wa Miradi inayotekelezwa na fedha za uwajibikaji wa makampuni *(CSR)* utafanywa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushauriana na Wizara ya Fedha kabla ya miradi hiyo kuanza kutekelezwa.

(f) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaelekezwa kusimamia na kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza miradi ya maendeleo kupitia mapato ya ndani kulingana na ngazi ya asilimia 70,60,40 na 20 kama ambavyo imeelekezwa katika mwongozo wa mpango na Bajeti.

(g) Halmashauri zote zilizopewa mkopo kupitia mradi wa KKK zirejeshe fedha hizo kabla au ifikapo Tarehe 31 Oktoba, 2023. Pia fedha zote zinazopatikana kupitia Mradi wa Kupanga Kupima na Kumilikisha zisiwe sehemu ya mapato ya ndani ya Halmashauri, bali ziwe ni miradi inayojitegemea na zirejeshwe katika utekelezaji na uendelezaji wa mradi hiyo. *(Makofi)*

(h) Mamlaka za Serikali za Mitaa zisifanye mabadiliko ya miradi iliyopangwa kutekelezwa bila ya kupewa idhini na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa.

(i) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zihakikishe zinaratibu uombaji wa fedha za utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Halmashauri kwa mara moja kulingana na Waraka wa

utekelezaji wa Bajeti unaotolewa kila mwaka ili kuwa na muda wa kutosha wa kutekeleza miradi ya maendeleo.

(j) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Chama katika maeneo yao ya utawala, hususan maelekezo ya Rais, Makamu wa Rais, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Aidha, natoa msisitizo kwa kila mkoa na Halmashauri ziwe na Kanzidata ya Maelekezo yaliyotolewa katika kipindi cha mwaka 2020, 2021, 2022 na 2023 katika mikoa yao pamoja na taarifa za utekelezaji;

(k) Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziratibu na kusimamia ujibuji wa Hoja za Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Halmashauri na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alizozitoa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(l) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zifanye tathmini na msawazo wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuleta uwiano katika utoaji wa huduma za jamii katika Halmashauri Moja na nyingine. Hivyo, Maofisa Wakuu wa Mikoa wakasimamie Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuendeleza na kuendesha Miji midogo inayochipukia sambamba na maendeleo ya Vijiji; na

(m) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zisimamie ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kuhimiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato na utoaji wa taarifa ili kufikia mipango na malengo yaliyowekwa katika Mpango na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea

kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI. Namwahidi nitaendelea kutimiza wajibu wangu kwa weledi katika kuisimamia Ofisi hii kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wetu wa Bunge na Wabunge wote kwa namna ambavyo mmendelea kusimamia masuala haya ya Bunge letu. Aidha, naishukuru sana Kamati yetu ya TAMISEMI inayoongozwa na Mheshimiwa Londo na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Nyamoga, kwa kazi nzuri na Wajumbe wote wa Kamati wanavyoisimamia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika maoni na ushauri wa Kamati umesaidia sana kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika ndani ya muda mfupi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma bora katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Kigua na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa maoni, maagizo na maelekezo mengine ambayo wameendelea kutuelekeza kuhusu utekelezaji wa Mipango na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya *LAAC* inayoongozwa na Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Wajumbe wote wa Kamati ya *LAAC* kwa maoni, maelekezo na maagizo yao katika kuboresha usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia, Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, wa Jimbo la Kigoma Mjini na Wajumbe wote wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa ushauri wao, maelekezo na maoni yao katika utungaji wa sheria ndogo za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa sana wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa programu, miradi na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Afya Duniani, Shirika la Ushirikiano la Kimataifa la Japan *(JAICA)*, Jumuiya ya Ulaya, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Shirika la Maendeleo la Uingereza, *Commonwealth and Development Office*, Shirika la Maendeleo la Marekani, Shirika la Maendeleo la Ujerumani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto, Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu *(UNFPA)*, Shirika la Kuleta Mapinduzi ya Kijani Afrika *(AGRF)* na nchi zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya ikiwemo Denmark, Ireland, Jamhuri ya Korea kupitia *KOICA*, Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)*, *Global Partnership for Education (GPE)*, Switzerland na Shirika la Umoja wa Mataifa la Miradi ya Maendeleo *(UNCDF)*, Makampuni ya Migodi ya *Geita Gold Mines*, *Twiga - Barrick Tanzania*, Benki ya *NMB, CRDB, DCB* na benki nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Taasisi za Kidini, Taasisi za Kifedha, Asasi za Kiraia, wananchi wote, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na makampuni mbalimbali kwa michango yao ambayo wamekuwa wakiitoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo katika kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza umaslkini. Aidha, ninawashukuru sana kipekee wananchi wote kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nawashukuru Wabunge na Madiwani pia, na viongozi wengine wote kule chini kwa namna ambavyo mmendelea kusimamia na kushirikiana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua mchango wa viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kipekee, nawashukuru tena Manaibu Waziri; Mheshimiwa Dkt. Dugange, pamoja na Mheshimiwa Ndejembi, kwa usaidizi na ushirikiano wao mkubwa wanautoa kwangu katika kutekeleza majukumu haya ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nawashukuru Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya, na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Katibu Mkuu, Ndg. Ndunguru na Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Msonde, Dkt. Mahera na Dkt. Mtwale kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha Mpango na Bajeti na usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Namshukuru pia, Bi. Paulina Mbena Nkwama, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu na watendaji wakuu wote wa taasisi zilizoko chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa mara nyingine tena Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala Wasidizi wa Mikoa, Wastahiki Mameya wote. Wenyeviti wa Halmashauri Waheshimiwa Madiwani, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wakurugenzi wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Timu zetu za Menejimenti za Halmashauri *(CMT's)*,

pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zake mpaka ngazi ya chini kabisa ya msingi, ikiwemo Tarafa, Kata, Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa kuhitimisha, Bajeti ya Mafungu yote 28 yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inatarajia kuongeza kasi ya kuwahudumia na kuwafikia wananchi kwa uharaka kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kufungua barabara mahali kusikofikika na kulinda uwekezaji ambao ulishafanyika katika miundombinu ya barabara;

(b) Kutumia teknolojia mbadala ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ili kuongeza ufanisi;

(c) Kutoa huduma bora za afya ya msingi kwa kuongeza vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya;

(d) Kuboresha huduma jumuishi za wazee ikiwemo uwepo wa dirisha la kuwahudumia;

(e) Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo ili kuwapunguzia gharama wananchi na kuongeza uandikishaji wa wanafunzi; na

(f) Kuongeza miundombinu ya elimu ili kuboresha na kusogeza mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni:-

(a) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Halmashauri zetu;

(b) Kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(c) Kuimarishaji Utawala Bora kwa kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa ili kuimarisha utoaji wa huduma na usimamizi wa shughuli za Serikali katika ngazi ya msingi;

(d) Kuimarisha kituo cha huduma kwa wateja;

(e) Kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi za Kata kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi;

(f) Kuendeleza Vijiji na Miji na kuwezesha wananchi wetu kiuchumi; na kubwa zaidi,

(g) Kufanya maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 184...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kengele ya pili imeshagonga. Dakika tatu, malizia kutoa hoja na kuomba fedha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tunaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani ya jumla ya shilingi 1,199,287,592,146. Makusanyo hayo yatatokana na maduhuli, ada za wanafunzi za Chuo cha Serikali za Mitaa, ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha. Mchanganuo ni kama inavyoonekana katika jedwali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha ujao wenye jumla ya shilingi 9,144,021,699,000 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 184.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zinazoombwa, shilingi 5,658,022,058,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara, shilingi 4,597,632,183,000 na Matumizi Mengineyo; na shilingi 1,060,389,875,000.

Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi 3,485,999,641,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, na kati ya fedha hizo shilingi 2,362,700,487,000 ni fedha za ndani na shilingi 1,123,299,154,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali yanafafanua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 02 na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 ambayo pia ni sehemu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana pia katika Tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iliyochambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) (Fungu Namba 56); Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) na Mafungu 26 ya Mikoa, ikijumuisha Halmashauri 184, kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23; Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu Namba 56); Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) na Mafungu 26 ya Mikoa, ikijumuisha Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa, ikijumuisha Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuniteua katika Wadhifa wa Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Nikiri kuwa nimeelemewa na imani yake kubwa kwangu. Ninamuahidi kwamba, nitatekeleza wajibu wangu na kufanya kazi kwa uaminifu, ufanisi, weledi na uadilifu mkubwa ili kutimiza matarajio yake aliyonayo kwangu na kwa Ofisi ya Rais – TAMSIEMI. Nawashukuru pia, wanachama wenzangu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa namna tunavyoendelea kushirikiana katika kukiimarisha zaidi Chama chetu ili kiendelee kushika Dola.

3. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee pia, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa Miaka 2 tangu alipoingia madarakani. Tumeshuhudia Miaka 2 yenye Ushindi mkubwa, Heshima na

Ushawishi mkubwa wa Kimataifa. Ninampongeza sana kwa uongozi wake mahiri wenye kuzingatia uadilifu, uwajibikaji na utendaji wenye malengo na unaozingatia matokeo chanya kwa manufaa ya wananchi anaowaongoza. Hii, inathibitisha kiu na utashi mkubwa alionao wa kuwaeletea maendeleo wananchi na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali Nchi nzima na kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI tumeshuhudia maboresho makubwa na miradi mingi ya Maendeleo. Kwa hakika ni Miaka 2 ya mafanikio na yenye kishindo kikubwa na alama.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ili kuleta mabadiliko ya kweli na maendeleo kwa wananchi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ya Bajeti. Tunamshukuru kwa ufuatiliaji wake wa karibu na ziara zake za mara kwa mara katika Mikoa na Wilaya zetu. Vile vile, ninampongeza kwa kutekeleza madaraka yake ya Kikatiba ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika udhibiti, usimamizi na utekelezaji wa siku kwa siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi, busara na hekima. Nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.); Naibu Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge waliochaguliwa kwa umakini wao wa kuliongoza Bunge lako Tukufu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb.), Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na Mheshimiwa George Mkuchika (Mb.), Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais kwa Ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi ya Rais.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mawaziri wote kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia katika kuwaletea Watanzania Maendeleo kwa kasi kubwa zaidi chini ya Kauli Mbiu ya KAZI IENDELEE!

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, na wajumbe wa Kamati kwa uchambuzi, ushauri na miongozo yao kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu Namba 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Naishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yote 28, kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24 na kuyapitisha kwa kauli moja. Maadam 'imani huzaa imani', nawaahidi mimi na wenzangu wizarani, hatutawaangusha.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** dhima hii niliyokabidhiwa ni kubwa. Kwa vyovyote vile, nisingeweza kuandaa bajeti hii peke yangu. Uungwana unanitaka kutambua mchango mkubwa wa wenzangu wakioongozwa na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge wa Jimbo la Chamwino kuwa Naibu Mawaziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote Tanzania Bara. Aidha,

natambua mchango mkubwa wa wataalam wakiongozwa na Ndg. Adolf Hyasinth Ndunguru Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Charles Enock Msonde (Elimu), Dkt. Wilson Charles Mahera (Afya) na Ndg. Sospeter Mambile Mtwale (TAMISEMI); Makamishna, Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi, Wakurugenzi na Watumishi Wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufikia malengo ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Nasimama hapa kwa kujiamini kwa sababu yao.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu haya makubwa, na wajibu mkubwa unaoambatana nayo, vinahimilika tu pale panapokuwa na amani ya moyo na afya ya akili. Kipekee, niwashukuru wanaonipa amani ya moyo, afya ya akili na kunitia moyo kuyakabili na kuyahimili majukumu yangu. Namshukuru mume wangu mpenzi, Balozi Mbelwa Kairuki, wanangu Kemi, Esther na Mwesi kwa kunifariji, kunitia moyo na kunipa tumaini. Hali kadhalika, ndugu, jamaa na marafiki kwa kunivumilia pale ninapokosekana miongoni mwao sababu ya kutekeleza majukumu yangu ya uwaziri.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake wakati akihutubia Bunge lako la 12, tarehe 22 Aprili, 2021 yaliyohusu: Kuendelea na jitihada za

kuwawezesha wananchi kiuchumi, hususani Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kutoa mikopo ya asilimia kumi kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri. Aidha, Ofisi ya Rais -TAMISEMI inafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati akipokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mwaka wa Fedha wa 2021/22 tarehe 29 Machi, 2023 ambapo alielekeza; Kufanya marekebisho makubwa kwa kuingiza mfumo wa kibenki katika uratibu wa utoaji na urejeshaji wa mikopo ya asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuondoa vikundi hewa na upendeleo wakati wa utoaji wa mikopo hiyo.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile, tunamuunga mkono katika vita dhidi ya rushwa, ubadhilifu, uzembe, ukiukwaji wa maadili, urasimu na kuwawajibisha wanaodhihirika na kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazochukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinazowahudumia wananchi wake vyema na itatimia tu endapo Watumishi wote na Viongozi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa watafanya kazi kwa juhudi, maarifa, na uadilifu mkubwa. Pia, inasisitizwa utoaji wa huduma bora na wa haraka, wenye staha na wenye ufanisi ili kuondokana na kuwasumbua na kuwazungusha wananchi; kukusanya mapato kwa ufanisi na kudhibiti mianya ya makusanyo na matumizi yenye kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 pamoja na Mpango na Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

## B. MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE, MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** maelekezo ya mgawanyo wa majukumu yaliyotolewa na Hati Idhini ya Rais (Presidential Instrument) ya Mei, 2021 yanaainisha majukumu makuu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ifuatavyo: -

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D), Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maendeleo Vijijini na Mijini;

(ii) Kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;

(iii) Kuratibu shughuli za utoaji wa huduma mijini kama vile usafiri na usafirishaji na usafi wa mazingira;

(iv) Kusimamia shughuli za Tume ya Utumishi wa Walimu;

(v) Kusimamia shughuli za ElimuMsingi na Sekondari;

(vi) Kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji wa huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe;

(vii) Kuratibu na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi;

(viii) Kuratibu shughuli za wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo;

(ix) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi; na

(x) Kusimamia utendaji wa Mashirika, Taasisi, Programu na Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi za Wakuu wa Mikoa zina majukumu yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi;

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa ElimuMsingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kuratibu uendeshaji wa Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(vii) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu katika maeneo yao ya Utawala;

(ii) Kuzingatia misingi ya Utawala Bora katika kutekeleza majukumu yao;

(iii) Kutoa huduma bora kwa wananchi kulingana na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali;

(iv) Kusimamia ukusanyaji wa mapato, matumizi ya fedha pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(v) Kuratibu wadau wa maendeleo wanaotekeleza majukumu yao katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(vi) Kuzingatia makundi maalum na masuala mtambuka katika utoaji wa huduma.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/23

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipanga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

(i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

(ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa ElimuMsingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa ElimuMsingi na Sekondari Bila Ada;

(iii) Kuratibu na kusimamia Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iv) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kushughulikia malalamiko ya walimu ikiwemo kutopandishwa vyeo kwa wakati; na wastaafu kucheleweshewa kulipwa stahiki na mafao yao baada ya kustaafu na kero zinazowakabili walimu waliostaafu;

(vi) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi shindani kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, hasa katika Kilimo, Mifugo na Viwanda. Utekelezaji wa jambo hili umehusisha uimarishaji wa Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji na Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuhakikisha kuna rasilimali watu wenye weledi pamoja na uwepo wa fedha na vitendea kazi;

(vii) Kufanya Ukaguzi, Ufuatiliaji na Tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Taasisi, Programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(viii) Kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(ix) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi;

(x) Kuratibu shughuli na utendaji kazi kwa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(xi) Kuratibu shughuli za ujenzi, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya barabara, usafirishaji, maeneo ya utawala na maeneo ya kutolea huduma za jamii kwenye Taasisi, Mikoa, Wilaya na Halmashauri;

(xii) Kusimamia matumizi ya rasilimali fedha katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(xiii) Kuratibu uendelezaji wa Vijiji na Miji, na

(xiv) Kuratibu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli na mapato ya ndani yenye jumla ya Shilingi Trilioni 1.07. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 59.19 ni kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Shilingi Milioni 249.28 ni maduhuli ya Mikoa na Shilingi Trilioni 1.01 ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari, 2023 fedha zilizotarajiwa kukusanywa ni Shilingi Bilioni 714.48 ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 647.88 kimekusanywa, sawa na asilimia 90.68 ya fedha zilizotarajiwa kukusanywa kwa kipindi hicho (*Kiambatisho Namba 1).*

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu Namba 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) na Mafungu 26 ya Mikoa yakijumuisha Halmashauri 184 iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi Trilioni 9.04. Kati ya fedha hizo, Shilingi Trilioni 3.53 ni fedha za Maendeleo na Shilingi Trilioni 5.51 ni za Matumizi ya Kawaida, yakijumuisha Mishahara Shilingi Trilioni 4.63 na Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni 885.59 (*Kiambatisho Namba 2)*.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI yalitarajia kupokea na kukusanya Shilingi Trilioni 6.05. Kati ya fedha hizi, Shilingi Trilioni 5.54 zimepokelewa sawa na asilimia 91.63 ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, Shilingi Trilioni 1.95 ni fedha za miradi ya maendeleo na Shilingi Trilioni 3.59 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yakijumuisha

Mishahara Shilingi Trilioni 2.94 na Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni 644.41 *(Kiambatisho Namba 2)*. Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopokelewa kwa Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni kama ifuatavyo: -

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Namba 56)**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Namba 56) iliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani jumla ya Shilingi Bilioni 59.19. Hadi Februari, 2023 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imekusanya Shilingi Bilioni 22.47, sawa na asilimia 56.94 ya Shilingi Bilioni 39.46 ya fedha zilizotarajiwa kukusanywa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Namba 56) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Trilioni 1.22. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 78.51 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi Trilioni 1.14 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha Shilingi Bilioni 63.38 kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni 15.13 Matumizi Mengineyo. Aidha, Miradi ya Maendeleo inajumuisha Shilingi Bilioni 758.72 fedha za ndani na Shilingi Bilioni 386.86 fedha za nje.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Namba 56) imepokea jumla ya Shilingi Bilioni 854.07, sawa na asilimia 101.7 ya Shilingi Bilioni 839.38 ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, Shilingi Bilioni 50.03 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo yanajumuisha Mishahara, Shilingi Bilioni 40.11 na Shilingi Bilioni 9.92 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Shilingi Bilioni 804.03, sawa na asilimia 102.2 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo Shilingi Bilioni 522.81 ni fedha za ndani

na Shilingi Bilioni 281.22 ni fedha za nje *(Kiambatisho Namba 2)*.

**Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02)**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) (Fungu Namba 02) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 15.65. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 14.98 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi Milioni 670.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia fedha za ndani. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha Shilingi Bilioni 8.27 za Mishahara na Shilingi Bilioni 6.70 za Matumizi Mengineyo.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02) imepokea jumla ya Shilingi Bilioni 7.80 sawa na asilimia 74.78 ya Shilingi Bilioni 10.43 zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi hicho. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi Bilioni 4.95 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi Bilioni 2.84 matumizi mengineyo *(Kiambatisho Namba 2)*.

**Mafungu 26 ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa yakijumuisha Halmashauri 184**
**Ofisi za Wakuu wa Mikoa**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Mikoa yote 26 iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi Milioni 249.28. Hadi Februari, 2023 Mikoa imekusanya Shilingi Milioni 92.26 sawa na asilimia 55.52 ya Shilingi Milioni 166.18 zilizotarajiwa kukusanywa katika kipindi hicho.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi za Wakuu wa Mikoa (Mafungu 26) ziliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 240.33, ambapo Shilingi Bilioni 155.30 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi Bilioni 85.03 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matumizi ya

Kawaida yanajumuisha Shilingi Bilioni 76.20 kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni 79.10 ni za Matumizi Mengineyo.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Ofisi za Wakuu wa Mikoa zilipokea jumla ya Shilingi Bilioni 152.74 sawa na asilimia 95.33 ya Shilingi Bilioni 160.22 zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi hicho. Kati ya fedha zilizopokelewa Mishahara ni Shilingi Bilioni 44.62, Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni 56.91 na Miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni 51.21 ambapo fedha za ndani ni Shilingi Bilioni 50.96 na fedha za nje ni Shilingi Milioni 259.92 *(Kiambatisho Namba 2)*.

**Halmashauri**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi Trilioni 1.01. Hadi Februari 2023, jumla ya Shilingi Bilioni 625.31 zimekusanywa sawa na asilimia 92.66 ya Shilingi Bilioni 674.85 zilizotarajiwa kukusanywa katika kipindi hicho.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Halmashauri ziliidhinishiwa jumla ya Shilingi Trilioni 7.56, kati ya fedha hizo Shilingi Trilioni 5.26 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Shilingi Trilioni 4.48 Mishahara na Shilingi Bilioni 784.64 Matumizi Mengineyo. Aidha, kati ya fedha za Matumizi Mengineyo, Shilingi Bilioni 167.16 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu na Shilingi Bilioni 617.48 ni Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Vilevile, Shilingi Trilioni 2.29 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 926.97 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu, Shilingi Bilioni 394.80 ni Mapato ya Ndani ya Halmashauri na Shilingi Bilioni 977.48 ni fedha za nje.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2023 Halmashauri zimepokea jumla ya Shilingi Trilioni 4.53 sawa na asilimia 89.88 ya Shilingi Trilioni 5.04 zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi

hicho. Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi Trilioni 2.86 ni kwa ajili ya mishahara, Shilingi Bilioni 574.73 ni matumizi mengineyo yakijumuisha Shilingi Bilioni 144.25 ruzuku kutoka Serikali Kuu na Shilingi Bilioni 430.48 zinatokana na Mapato ya Ndani ya Halmashauri. Aidha, Shilingi Trilioni 1.09 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha Shilingi Bilioni 850.18 ruzuku ya Serikali Kuu, Shilingi Bilioni 194.83 mapato ya ndani ya Halmashauri na Shilingi Bilioni 52.81 ni fedha za nje *(Kiambatisho Namba 2)*.

**Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri zimetekeleza shughuli zifuatazo: -

**Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa Shilingi Bilioni 143.15 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Afya ya Msingi. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 124.10 zimepokelewa sawa na asilimia 86.69 ya fedha iliyoidhinishwa. Maelezo ya utekelezaji ni kama ifuatavyo: -

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi Bilioni 15.50 ziliidhinishwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali 31 za Halmashauri zilizoanza ujenzi katika Mwaka wa Fedha wa 2020/21 ambapo kila Halmashauri iliidhinishiwa Shilingi Milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje na maabara. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 13.50 zimekwishatolewa, sawa na asilimia 87.09 na ujenzi upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji *(Kiambatisho Namba 3)*.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi Bilioni 25.15 ziliidhinishwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali 28 za Halmashauri zilizoanza ujenzi katika Mwaka wa Fedha wa 2021/22. Ujenzi huo ulihusisha majengo ya wodi 3 za wanaume, wanawake na watoto pamoja na jengo la kuhifadhia maiti. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 23.90, sawa na asilimia 95.03. Ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji *(Kiambatisho Namba 3)*.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi Bilioni 16.55 ziliidhinishwa kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali kongwe 19 za Halmashauri. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 16.55, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa. Ukarabati wa hospitali tisa (09) umeanza na kwa upande wa hospitali kumi (10) ukarabati upo katika hatua za awali *(Kiambatisho Namba 3)*.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi Bilioni 15 ziliidhinishwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 300 ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 14.60 zimepokelewa, sawa na asilimia 97.33 na ukamilishaji upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Shilingi Bilioni 1 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo 2 vya afya katika Halmashauri za Wilaya za Msalala na Ukerewe ambapo hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 1 sawa na asilimia 100 zimepokelewa na ujenzi upo katika hatua mbalimbali *(Kiambatisho Namba 3)*. Vilevile, hadi kufikia Februari, 2023 jumla ya wagonjwa wa nje (OPD) 16,143,151 na wagonjwa wa ndani waliolazwa (IPD) 416,628 walipatiwa huduma katika vituo vya kutolea huduma za Afya ya Msingi. Pia, kati ya akina mama wajawazito 1,227,234 waliojifungua, akina mama 1,146,510 sawa na asilimia 93.4 walijifungua kwa njia ya kawaida na akina mama 80,724 sawa na asilimia 6.6 walijifungua kwa njia ya upasuaji.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi Bilioni 69.95 ziliidhinishwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 15.15 ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa

tiba kwa zahanati 300, Shilingi Bilioni 47.70 kwa Vituo vya Afya 159 na Shilingi Bilioni 7.10 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba vya afya ya kinywa, meno na macho kwa hospitali za Halmashauri 71 zilizokamilika. Hadi Februari, 2023 jumla ya Shilingi Bilioni 54.55 zimepokelewa, sawa na asilimia 77.98. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 11.95 ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa zahanati, Shilingi Bilioni 36.75 kwa ajili ya Vituo vya Afya na Shilingi Bilioni 5.85 kwa ajili ya vifaa tiba vya kinywa na macho kwa Hospitali za Halmashauri 71 *(Kiambatisho Namba 4)*.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha huduma za Ustawi wa Jamii kwa makundi maalum, hadi Februari, 2023 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanikiwa kuwatambua jumla ya Watu Wenye Ulemavu 10,035 ambapo Wanawake ni 6,100 na Wanaume 3,935. Miongoni mwa Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi 2,400 kati yao Wanawake ni 1,300 na Wanaume 1,100; Watu Wenye Ulemavu wa Viungo 5,233 ambapo Wanawake ni 3,133 na Wanaume 2,100; Wasioona 510 ambapo Wanawake ni 203 na Wanaume 307; Viziwi 1,500 kati yake Wanawake ni 785 Wanaume 715; na Watu Wenye Ulemavu wa Akili 392 ambapo Wanawake ni 281 Wanaume 111.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Watu hao Wenye Ulemavu wametambuliwa na kupewa Vifaa saidizi ikiwemo miwani 754, miamvuli 934, mafuta ya Ngozi 1,741, fimbo nyeupe 306, kofia 915, na baiskeli za miguu mitatu 293 ili kuwawezesha kujimudu. Aidha, Kamati 5,024 za Watu Wenye Ulemavu zimeundwa katika Vijiji na Kamati 2,284 katika Mitaa. Kamati hizo zinahusisha wajumbe mchanganyiko (Watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu). Lengo la Kamati hizo ni kusimamia masuala ya watu wenye ulemavu na kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili ikiwepo mawasiliano ya lugha ya alama.

43. ***Mheshimiwa Spika**,* jumla ya wazee 2,117,637 wametambuliwa katika Mikoa 26, kati ya wazee hao wanawake ni 735,169 na wanaume ni 1,382,468. Kati yao wazee 585,672 sawa na asilimia 27.65 wamepatiwa vitambulisho vya Bima ya afya kwa ajili ya matibabu ambapo wanawake 330,176 na wanaume 255,496. Aidha, mabaraza ya ushauri ya wazee 20,748 yameundwa kwenye Mikoa/Halmashauri na Ngazi ya Kata, Vijiji/Mitaa kwa ajili ya usimamizi ya masuala ya wazee. Vilevile, madirisha 588 ya kutolea huduma za Afya ya Msingi kwa wazee yameanzishwa katika Hospitali za Halmashauri, vituo vya afya na zahanati.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilishughulikia mashauri ya ukatili dhidi ya Watoto, ambapo hadi Februari, 2023 mashauri yaliyotolewa taarifa na kusajiliwa katika ofisi za Ustawi wa Jamii ngazi za Halmashauri yalikuwa 13,926 kati ya hayo, mashauri dhidi ya wanawake yalikuwa 7,142 na ukatili dhidi ya Watoto yalikuwa 6,784. Aidha mashauri 12,727 sawa na asilimia 91.39 yalitatuliwa katika ofisi za ustawi wa jamii ngazi ya Halmashauri na mashauri 1,199 sawa na asilimia 8.61 yalifikishwa mahakamani kati yao mashauri 430 yametolewa hukumu na mashauri 769 yanaendelea na taratibu za kimahakama.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kushughulikia migogoro ya kifamilia, ambapo hadi kufikia Februari, 2023 migogoro ya ndoa na familia 1,513 ilipokelewa katika ofisi za Ustawi wa Jamii ngazi ya Halmashauri. Aidha, kati ya migogoro 1,513 iliyosajiliwa migogoro 868 ilifanyiwa usuluhisho kwenye Ofisi za Ustawi wa Jamii ngazi ya Halmashauri na migogoro 645 ilipewa rufaa kwenda mahakamani, ambapo migogoro 126 ilitolewa hukumu na migogoro 519 inaendelea na taratibu za Kimahakama.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na shughuli hizo, Halmashauri kupitia Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

inatoa huduma kwenye vituo jumuishi (*One stop Center*) ambapo hadi sasa kuna vituo 16 katika Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam, Halmashauri za Manispaa za Tabora, Kinondoni, Kigoma, Shinyanga, Iringa, Kahama na Halmashauri za Wilaya za Msalala, Kasulu, Ikungi, Kibaha, Hai na Mvomero.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Halmashauri zimeweza kushughulikia masuala ya Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Hadi Februari, 2023 watoto 335,971 wametambuliwa na kati yao watoto wa kike ni 167,337 na watoto 168,634 ni wa kiume. Aidha, watoto hao wameweza kupatiwa misaada mbalimbali ikiwemo chakula, malazi, mavazi, elimu, matibabu na watoto 26,000 waliunganishwa na familia zao na kuhakikisha watoto hao wanaishi kwa amani.

**Huduma za Lishe**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeendelea kuratibu Afua mbalimbali katika eneo la lishe katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Utafiti wa Afya na demografia uliofanyika Mwaka 2022, umebaini kuwa tatizo la udumavu nchini ni asilimia 30, ikilinganishwa na asilimia 34 iliyoripotiwa na utafiti wa Mwaka 2015/16. Kiwango kikubwa cha udumavu kimebainika katika Mikoa ya Iringa asilimia 56.9; Njombe asilimia 50.4; Tabora asilimia 33.1 na Dar es Salaam asilimia 18.4. Hivyo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kufanya usimamizi shirikishi na uratibu wa afua katika Mikoa hiyo ili kuhakikisha kiwango cha udumavu kinapungua zaidi.

49. *Mheshimiwa Spika,* katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kufanya utafiti wa visababishi vya udumavu kwa watoto walio chini ya miaka mitano (5) katika Mikoa inayozalisha vyakula kwa wingi hapa nchini, utafiti unafanyika kwa kushirikiana na Taasisi ya *Big Win*

*Philantropy* kutoka nchini Marekani kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Utafiti unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa Mei, 2023 ambao unafanyika katika Mikoa nane (8). Utafiti huo unafanyika katika Mikoa sita (6) ya Tanzania Bara ambayo ni Njombe, Iringa, Tabora, Dar es Salaam, Geita na Mtwara pamoja na Mikoa miwili (2) ya Zanzibar ambayo ni Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba.

**Mkataba wa Lishe**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa Mkataba wa Lishe ambao ulisainiwa tarehe 30 Septemba, 2022 baina ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wakuu wa Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara baada ya kumalizika kwa Mkataba wa Kwanza. Aidha, Wakuu wa Mikoa wamesaini Mikataba na Wakuu wa Wilaya; Wakurugenzi wa Halmashauri wamesaini na Watendaji wa Kata; na Watendaji wa Kata wamesaini Mikataba na Watendaji wa Vijiji/Mitaa.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** mkataba huu wa kusimamia masuala ya lishe kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri umesaidia kutoa msukumo mpya wa kusimamia masuala ya lishe nchini. Mkataba huu una jumla ya viashiria 14 vilivyojikita kwenye utengaji wa fedha, utoaji wa huduma na usimamizi wa utekelezaji wa afua za lishe ikiwemo matibabu ya utapiamlo mkali, kutoa nyongeza ya vitamini A, tathmini ya hali ya lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na makundi mengine na kutoa nyongeza ya vidonge vya kuongeza wekundu wa damu kwa akina mama wajawazito. Viashiria hivyo hupimwa mara moja kwa Mwaka ngazi ya Taifa, mara mbili kwa Mwaka ngazi ya Mkoa na mara nne kwa Mwaka ngazi ya Halmashauri. Utekelezaji wa Mkataba huu utafanyika kwa kipindi cha miaka nane (8) kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2022/23 hadi 2029/30.

**Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utoaji wa huduma ya ElimuMsingi na Sekondari. Shughuli zilizotekelezwa ni:

**Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Awali**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa masomo wa 2022 wanafunzi wapya wa Darasa la Awali walioandikishwa ni 1,411,810, sawa na asilimia 103.52 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,363,834. Katika Mwaka 2023, jumla ya wanafunzi 1,500,227 wameandikishwa sawa na asilimia 109.37 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,371,690 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,411 ambapo wasichana ni 1,211 na wavulana 1,200. Uandikishwaji huo ni ongezeko la wanafunzi 88,417 sawa na asilimia 3.38 ikilinganishwa na wanafunzi walioandikishwa kwa kipindi kama hiki kwa Mwaka wa 2022. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji wa jamii, ujenzi wa vituo shikizi na kuendelea kutoa ElimuMsingi Bila Ada *(Kiambatisho Namba 5)*.

**Uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa masomo wa 2022 wanafunzi 1,592,375 walitarajiwa kuandikishwa Darasa la Kwanza, ambapo walioandikishwa ni wanafunzi 1,726,165, sawa na asilimia 108.40 ya lengo. Katika Mwaka 2023 wanafunzi wa Darasa la Kwanza walioandikishwa hadi Februari, 2023 ni 1,786,485, ambapo wasichana 917,211 na wavulana ni 869,274. Uandikishwaji huo ni sawa na asilimia 109.07 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,637,897 na ni ongezeko la wanafunzi 60,320, sawa na asilimia 3.49, ikilinganishwa na wanafunzi walioandikishwa kwa kipindi kama hiki kwa Mwaka wa 2022. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji wa jamii, ujenzi wa vituo shikizi na kuendelea

kutoa ElimuMsingi Bila Ada. Kati ya wanafunzi walioandikishwa wenye mahitaji maalum ni 4,741 ambapo wasichana ni 2,097 na wavulana ni 2,644. Lengo ni kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapatiwa huduma bora ya elimu kulingana na Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2022– 2026, *(Kiambatisho Na. 6)*.

**Uandikishaji wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya wanafunzi 1,076,037 ambapo wasichana 560,118 na wavulana ni 515,919 walichaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka wa 2023. Hadi Februari, 2023 wanafunzi 1,003,982 ambapo wasichana 520,332 na wavulana ni 483,650 wameandikishwa sawa na asilimia 93.3 ya wanafunzi waliochaguliwa. Kati ya wanafunzi walioandikishwa, wanafunzi wenye mahitaji maalum ni 2,411 ambapo wasichana 1,211 na wavulana ni 1,200 *(Kiambatisho Na. 7)*.

**Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Idadi ya Wanafunzi wanaosajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne imekua ikiongezeka kutoka na uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Mwaka 2022 jumla ya wanafunzi 1.718,896 walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne. Kati yao Wavulana ni 847,897 na Wasichana 870,999. Idadi hii ni sawa na ongezeko la Wanafunzi 37,105 ukilinganisha na Wanafunzi 1,681,791 waliosajiliwa kufanya Upimaji huo wa mwaka 2021.

**Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi wa Mwaka wa masomo 2022, jumla ya wanafunzi 1,384,186 wakiwemo wasichana 723,027 na wavulana 661,159 walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi. Watahiniwa 1,350,881 walifanya mtihani wakiwemo

wasichana 709,556 na wavulana 641,325 pamoja na wanafunzi 3,240 wenye mahitaji maalum. Watahiniwa 1,076,037 walipata sifa ya kuendelea na Elimu ya Sekondari wasichana wakiwa 560,037 na wavulana 515,919 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,775 ambapo wasichana ni 1,284 na wavulana 1,491.

**Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu za Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili zinaonesha kuwa kwa Mwaka wa masomo wa 2022, jumla ya wanafunzi 690,341 walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kati yao wasichana ni 367,013 na wavulana ni 323,328. Idadi hii ni sawa na ongezeko la Wanafunzi 88,234 ukilinganisha na Wanafunzi 602,107 waliosajiliwa kufanya Upimaji huo Mwaka 2021. Ongezeko la Wanafunzi wanaosajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili limechagiwa na utekelezaji wa Sera ya Elimumsingi Bila Malipo na uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

**Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mtihani wa Kidato cha Nne, jumla ya Watahiniwa wa shule 456,975 wakiwemo wasichana 243,285 na wavulana 213,690 kati ya watahiniwa 520,558 waliofanya mtihani huo walifaulu. Idadi ya wanafunzi waliofaulu iliongezeka kwa 34,587 kutoka wanafunzi 422,388 Mwaka 2021 hadi 456,975 Mwaka 2022. Ongezeko hili la ufaulu limechangiwa na jitihada nzuri zinazofanywa na walimu wetu nchini pamoja na uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

**Elimu ya Sekondari**

**Wanafunzi waliochaguliwa Kujiunga na Kidato cha Tano Mwaka 2022**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kusimamia uchaguzi wa wanafunzi waliofaulu mtihani wa kidato cha nne ambapo jumla ya wanafunzi 90,898 kati yao wasichana 43,155 na wavulana 47,743, sawa na asilimia 52.41 ya wanafunzi 173,422 wenye sifa walichaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule 508 za Serikali. Kati yao, wanafunzi wenye mahitaji maalumu walikuwa ni 481 wakiwemo wasichana 204 na wavulana 277. Kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, wanafunzi 36,390 wakiwemo wasichana 15,327 na wavulana 21,063 sawa na asilimia 40.03 walichaguliwa kusoma tahasusi za Sayansi na Hisabati; wanafunzi 54,508 wakiwemo wasichana 27,828 na wavulana 26,680 sawa na asilimia 59.97 walichaguliwa kusoma tahasusi za masomo ya Sanaa na Biashara.

**Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** ufaulu wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa wa shule kwa Mwaka wa masomo wa 2022 ulikuwa ni asilimia 99.87 ambapo watahiniwa 84,404 kati ya watahiniwa 84,870 waliofanya mtihani walifaulu. Idadi ya waliofaulu imeongezeka kwa 4,808 kutoka 79,596 mwaka 2021 hadi 84,404 Mwaka 2022. Ufaulu wa Kidato cha Sita umeendelea kuimarika zaidi kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na walimu wetu nchini pamoja na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

**Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** uandikishaji wa wanafunzi wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Matokeo ya uandikishaji kwa wanafunzi hao hadi mwezi Februari 2023 yanaonesha kupungua ambapo wanafunzi 28,680 wakiwemo wasichana 13,691 na wavulana 14,989 wameandikishwa. Idadi hiyo imepungua kwa asilimia 47.4 ikilinganishwa na wanafunzi 54,420 wakiwemo wasichana

24,436 na wavulana 29,984 walioandikishwa mwaka 2022. Kupungua kwa idadi hii inatokana na wanafunzi kuandikishwa katika mfumo rasmi wa elimu, mafanikio ya utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo pamoja na uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

**Elimu Maalum**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia Shule Maalum 37 za bweni, Vitengo Maalum 710 vinavyoshughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule za Msingi na Shule Jumuishi 3,956 zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi. Kwa upande wa Sekondari, kuna Shule Maalum moja ya Patandi na Shule Jumuishi 127. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Serikali imeajiri walimu 766 waliosomea taaluma ya Elimu Maalum ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata elimu sawa na wanafunzi wengine. Aidha, Serikali imenunua vifaa saidizi na vifaa maalum 82,919 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.60 kwenye shule 1,517 zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**Michezo kwa Shule za Msingi na Sekondari**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeendelea kuhimiza na kusimamia maendeleo ya michezo katika Shule za Msingi na Sekondari. Kwa upande wa mashindano ya michezo ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) wanafunzi 3,360 walishiriki michezo mbalimbali iliyofanyika Julai, 2022 katika Manispaa ya Tabora. Aidha, mashindano ya Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) yalifanyika ambapo wanafunzi 3,242 walishiriki michezo hiyo iliyofanyika katika Manispaa ya

Tabora Agosti, 2022. Michezo hii ilihusisha wanafunzi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

**Mahitaji ya Walimu kwa Shule za Msingi na Sekondari**

65. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 kuna jumla ya Shule za Msingi 17,181 zenye jumla ya wanafunzi 12,362,571 ambapo wasichana ni 6,269,643 na wavulana ni 6,092,928 kati yao wenye mahitaji maalum ni 65,641 ambapo wasichana ni 28,116 na wavulana ni 37,525. Aidha, zipo Shule za Sekondari 5,540 zikijumuisha 4,211 za Serikali na Shule 1,329 za binafsi zenye jumla ya wanafunzi 2,823,588 ambapo wasichana ni 1,476,369 na wavulana ni 1,347,219 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 13,142 ambapo wasichana ni 6,720 na wavulana ni 6,422.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 mahitaji ya walimu katika Shule za Msingi ni 362,189 kwa kutumia uwiano wa 1:45 (Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45) ambapo walimu waliopo ni 175,864 na upungufu ni 186,325 sawa na asimilia 51.44 ya mahitaji. Aidha, mahitaji ya walimu kwa Shule za Sekondari ni 174,632 ambapo waliopo ni 84,700 na upungufu ni walimu 89,932 sawa na asilimia 51.5. Mahitaji ya walimu kwa shule za Sekondari yanatokana na masomo yanayofundishwa. Vilevile, mahitaji ya walimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa Shule za Msingi ni walimu 4,462 ambapo waliopo ni 1,517 na upungufu ni walimu 2,945 sawa na asilimia 66. Serikali inaendelea kuajiri walimu kulingana na hali ya uchumi inavyoruhusu.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa Shilingi Bilioni 793.97 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za elimu ikiwemo Elimumsingi na Sekondari Bila Ada, uendeshaji wa mitihani na ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya elimu. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 607.89 zimepokelewa, sawa

na asilimia 76.56 ya fedha iliyoidhinishwa. Maelezo ya utekelezaji kwa kila eneo ni kama ifuatavyo: -

**ElimuMsingi na Sekondari Bila Ada**

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 346.49 kwa ajili kugharamia programu ya Elimumsingi na Sekondari Bila Ada. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 147.52 ni kwa ajili ya shule za msingi na Shilingi Bilioni 198.97 kwa ajili ya shule za sekondari. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 235.75 zimepokelewa sawa na asilimia 68.04. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 98.34 ni kwa ajili ya shule za msingi na Shilingi Bilioni 137.40 ni kwa ajili ya shule za sekondari (*Kiambatisho Namba 8(a) na 8(b))*.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo ulianza kwa wanafunzi walioandikishwa Januari, 2016. Aidha, kuanzia Julai Mwaka 2022, Serikali ilielekeza kufutwa kwa ada za shule na mitihani ya taifa kwa ngazi ya Kidato cha Tano na Sita kwa Shule za Sekondari za Serikali. Utekelezaji wa Sera ya ElimuMsingi Bila Malipo kwa Shule za Msingi na Sekondari nchini umeleta mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na ongezeko la Wanafunzi wapya wanaoandikishwa kujiunga katika ngazi mbalimbali za Elimu. Kwa mfano; Idadi ya wanafunzi waliochaguliwa Kujiunga na Kidato cha Kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 425,743 Mwaka 2016 hadi wanafunzi 1,076,037 Mwaka 2023 sawa na asilimia 152.74. Aidha, utekelezaji wa sera hiyo unahusisha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa taaluma shuleni kwa kutoa posho ya madaraka kwa wakuu wa Shule za Msingi, Sekondari na Maafisa Elimu Kata.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha hizi zinatumika katika maeneo ya uendeshaji wa shule, chakula cha wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule za msingi na wanafunzi wa

bweni wa shule za sekondari, kwa wanafunzi wa kutwa na bweni wa Kidato cha Kwanza hadi cha Sita na posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule za Msingi, Sekondari na Maafisa Elimu Kata.

**Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundombinu ya Shule**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa jumla ya Shilingi Bilioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 8,000 vya madarasa katika Shule za Sekondari ambavyo vimesaidia kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kutokana na utekelezaji wa Sera ya ElimuMsingi na Sekondari Bila Malipo. Hadi Februari, 2023 vyumba 7,800 vya madarasa, sawa na asilimia 97.5 vimejengwa na kukamilika (*Kiambatisho Namba 9)*.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ufinyu wa maeneo ya ujenzi katika baadhi ya maeneo, ujenzi umefanyika kwa kujenga madarasa ya maghorofa kwa ajili ya vyumba 190 katika Halmashauri ya Jiji ya Dar es salaam 46, Mwanza 72, Arusha 8 pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke 64 na ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 55.57 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 809 za walimu zenye uwezo wa kuchukua kaya 1,916. Kati ya hizo, nyumba 298 (3 kwa 1) ni za walimu wa shule za msingi zinazojengwa kupitia fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa Shilingi Bilioni 30.02 na nyumba 511 (2 kwa 1) ni za walimu wa shule za sekondari ambazo zinajengwa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa Shilingi Bilioni 25.55. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 12.41 kutoka Serikali Kuu, sawa na asilimia 41.33 ya fedha zilizotengwa. Fedha zilizotolewa ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 170, ambapo

ujenzi wa nyumba 26 umekamilika na nyumba 144 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi (*Kiambatisho Namba 9)*.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa Shilingi Bilioni 10.67 kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 9,700 katika vituo shikizi 970. Hadi Februari, 2023 jumla ya Shilingi Bilioni 5.45 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa matundu 4,954 ya vyoo ambapo matundu 596 ya vyoo yamejengwa na kukamilika na matundu 4,358 ya vyoo yapo katika hatua za ukamilishaji *(Kiambatisho Namba 9).*

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa jumla ya Shilingi Bilioni 34 kwa ajili ya kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa vyumba 1,700 vya madarasa katika Shule Kongwe za Msingi. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 21.44 sawa na asilimia 63.06 ya fedha zilizoidhinishwa zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 1,072 vya madarasa ambapo vyumba 674 vimejengwa na kukamilika na vyumba 398 ujenzi upo katika hatua mbalimbali *(Kiambatisho Namba 9).*

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 15.60 kwa ajili ya ujenzi wa shule 39 mpya za msingi. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 2.40 kwa ajili ya ujenzi wa shule 5 mpya katika Halmashauri ya Mji Geita 1, Halmashauri za Wilaya za Chato 2, na Rufiji 1 zipo katika hatua za awali na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga 1 ujenzi upo hatua ya upauaji (*Kiambatisho Namba 9)*.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, ziliidhinishwa Shilingi Bilioni 2.97 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa mabweni 99 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 1.37 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa mabweni 45 ambapo ujenzi wa uzio wa mabweni 6 umekamilika na uzio wa mabweni 39 ujenzi unaendelea (*Kiambatisho Namba 9)*.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 23.88 katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa maboma 1,911 ya vyumba vya madarasa katika shule za msingi. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 10.11 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 809 ya vyumba vya madarasa. Maboma 404 ya vyumba vya madarasa yamekamilika na maboma 597 ya vyumba vya madarasa ukamilishaji unaendelea *(Kiambatisho Namba 10)*.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa jumla ya Shilingi Bilioni 8.73 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 291 vya maabara katika shule za sekondari. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 8.13 zimepokelewa, sawa na asilimia 93.12 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 271 vya maabara ambapo vyumba 86 vimekamilika na vyumba 185 ukamilishaji wake unaendelea *(Kiambatisho Namba 10)*.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 4.30 katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 kwa ajili ya ukamilishaji wa mabwalo 86. Kati ya hayo, mabwalo 80 ni kwa ajili ya shule za sekondari na mabwalo 6 ni kwa ajili ya shule za msingi. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 3.89 sawa na asilimia 90.40 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ukamilishaji wa mabwalo 78 kati ya 86 yaliyoidhinishiwa fedha ambapo 16 yamekamilika na mabwalo 62 ukamilishaji unaendelea *(Kiambatisho Namba 10)*.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 9.21 kwa ajili ya ukamilishaji wa mabweni 461. Kati ya hayo, mabweni 28 ni kwa ajili ya shule za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum na mabweni 433 kwa ajili ya shule za sekondari. Hadi Februari, 2023 jumla ya Shilingi

Bilioni 8.20 sawa na asilimia 89.03 ya fedha zilizoidhinishwa zimepokelewa kwa ajili ya mabweni 410 kati ya mabweni 461. Mabweni 340 yamekamilika na mabweni 70 utekelezaji upo katika hatua mbalimbali za ujenzi *(Kiambatisho Namba 10)*.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, ziliidhinishwa Shilingi Bilioni 142.33 kwa ajili ya kuwezesha kufanyika kwa mitihani ya Taifa ya Darasa la Nne, la Saba, Kidato cha Pili, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 138.72 sawa na asilimia 97.46.

**Utekelezaji wa Programu na Miradi Mbalimbali**

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi ya Kimkakati ilianza kutekelezwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ambapo Halmashauri 29 kutoka Mikoa 16 iliingia Mikataba na Wizara ya Fedha na Mipango kutekeleza Miradi 38. Katika Mwaka wa Fedha wa 2021/22, Serikali iliidhinisha miradi mingine 4 hivyo kufanya jumla ya miradi ya kimkakati kuwa 42.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi hiyo inakadiriwa kugharimu Shilingi Bilioni 329.12 ambapo hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 238.91 sawa na asilimia 72.59 zimepokelewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 40.11 zimeidhinishwa katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ambapo hadi Februari, 2023 kiasi cha Shilingi Bilioni 18.80 kimepokelewa sawa na asilimia 46.87 ya fedha iliyoidhinishwa. Hadi Februari, 2023 jumla ya Miradi 13 ya Kimkakati imekamilika na inatoa huduma; 18 ipo katika hatua ya ukamilishaji na baadhi yake imeanza kutoa huduma, na miradi 10 inaendelea na ujenzi.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais-TAMISEMI, iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 1.59 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa Sera na Mikakati ya Serikali. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 1.59 sawa na asilimia 100 ya fedha iliyoidhinishwa. Kazi

zilizotekelezwa ni kuandaa nyaraka 4 za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa maandiko ya miradi ya kimkakati 68 kutoka katika Halmashauri 46 pamoja na kusimika Mfumo wa kielektroniki wa TAUSI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa Halmashauri kuhusu Mfumo wa TAUSI.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 55.38 kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira (SRWSS) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za afya na usafi wa mazingira. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 23.84. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya vyoo bora 2,214 katika vituo 369 vya kutolea huduma za afya ya msingi, ukarabati wa majengo ya kujifungulia, miundombinu ya kunawia mikono, ujenzi wa visima vya maji na mashimo ya kondo la nyuma (Placenta Pit), kichomea taka na ujenzi wa matundu 6,634 ya vyoo katika shule za Msingi 446.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 3.1 kupitia Mradi wa Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Elimu ya Msingi Awamu ya Pili (Global Partnership for Education - GPE LANES II). Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 3.1 sawa na asilimia 100.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa ni ununuzi wa magari 13 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za programu; ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) katika Halmashauri 144 ambapo walimu 30,390 wamenufaika ikiwemo walimu wa awali 26,657, walimu wa elimu maalum 1,879 na walimu wa wanafunzi wa elimu nje ya mfumo rasmi 1,854; ufuatiliaji wa hali ya ujenzi wa madarasa ya awali 300 ya mfano katika Halmashauri 150 ambapo Shilingi Bilioni 8.37 zimetumika na mabweni 20 ya wanafunzi wenye Mahitaji Maalum katika Halmashauri 20 ambapo Shilingi Bilioni 2

zimetumika; ufuatiliaji wa hali ya Vituo vya Walimu vilivyopokea vifaa vya TEHAMA katika Halmashauri 19; Uandaaji wa Mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji za Shule za Awali na Msingi zinazotumia Lugha za Kingereza katika Kujifunzia na Kufundishia.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 87.90 kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 50.88, sawa na asilimia 57.88 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ukarabati mdogo katika vituo vya kutolea huduma za afya 106, ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika hospitali za Halmashauri 188, Vituo vya Afya 732 na Zahanati 5,536, ukaguzi wa dawa na vifaa tiba katika vituo 807 katika Mikoa 19 nchini, usimamizi shirikishi katika Halmashauri 184 na kuendesha kikao cha mwaka cha Waganga Wakuu wa Mikoa 26, Halmashauri 184 na Vituo vya Afya 37. Aidha, mafunzo kwa ajili ya huduma ya upasuaji wa dharura kwa akina mama wajawazito yametolewa kwa watumishi 1,826.

**Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

90. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya Shilingi Trilioni 1.01 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni 148.42, sawa na asilimia 17.18 ikilinganishwa na bajeti ya Shilingi Bilioni 863.85 ya Mwaka wa Fedha wa 2021/22. Hadi Februari, 2023 Halmashauri zimekusanya jumla ya Shilingi Bilioni 625.31 sawa na asilimia 62 ya makisio kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Makusanyo haya ni ongezeko la Shilingi Bilioni 9.70 sawa na asilimia 1.57 ikilinganishwa na makusanyo ya Shilingi Bilioni 615.61 yaliyokusanywa kwa kipindi kama hiki katika Mwaka wa Fedha wa 2021/22 (*Kiambatisho Namba 11)*.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** kuongezeka kwa mapato kumetokana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati ya pamoja ya kubuni vyanzo vipya, kuimarisha vyanzo vilivyopo, kuimarika kwa usimamizi wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kudhibiti mianya ya makusanyo pamoja na kuhakikisha fedha zinazokusanywa zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilifanya mapitio ya makisio ya mapato ya ndani kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22 kwa Halmashauri zinazokusanya zaidi ya Shilingi Bilioni 5 ili kupata uhalisia wa makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Pia, mapitio hayo yaliwezesha kuongezeka kwa makisio ya mapato ya ndani kutoka Shilingi Bilioni 863.85 kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22 hadi Shilingi Trilioni 1.01 kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea kuzisimamia Halmashauri ili ziongeze wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mikakati iliyowekwa ni pamoja na kuwajengea uwezo maafisa wanaokusanya mapato, kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato na utambuzi wa fursa na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kupima utendaji wa Halmashauri kwa kutumia vigezo vya upelekaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo kwa kuzingatia asilimia 70,60,40,20 na vigezo vingine vilivyowekwa.

**Miradi ya Maendeleo Iliyotekelezwa kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa jumla ya Shilingi Bilioni 394.80 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia fedha za mapato

ya ndani ya Halmashauri. Hadi Februari, 2023 jumla ya Shilingi Bilioni 194.80 sawa na asilimia 74.01 ya Shilingi Bilioni 263.20 zimepelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukamilishaji wa zahanati 314, vituo vya afya 196, nyumba za watumishi wa afya 63, maabara 17 katika vituo vya afya, wodi 55, vichomea taka 32; majengo 48 ya kuhudumia Wagonjwa wa nje; ujenzi wa shule 9 mpya; na ukamilishaji wa maboma ya vyumba 941 vya madarasa; mabweni 73, maabara za sayansi 138, nyumba 44 za walimu, ofisi za walimu 50, matundu 2,159 ya vyoo na utengenezaji wa viti na meza 48,919. Miradi mingine ni ukamilishaji wa masoko 49; ujenzi wa vituo vidogo vya mabasi 46; viwanja 3 vya mpira; uanzishwaji wa skimu za umwagiliaji 7; ununuzi wa magari mawili 2 ya taka na boti 2.

**Utoaji wa Mikopo Kutokana na Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Halmashauri ziliidhinishiwa Shilingi Bilioni 76.02 kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Hadi Februari 2023, jumla ya Shilingi Bilioni 53.01 zilikusanywa ikiwa ni asilimia kumi ya mapato yasiyolindwa, kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 37.59 zilipelekwa katika akaunti ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Hivyo, kutokana na fedha hizo, Halmashauri zimeweza kukopesha Shilingi Bilioni 31.9 kati ya Shilingi Bilioni 50.68 zilizotarajiwa kukopeshwa kwa kipindi hicho ambapo Shilingi Bilioni 15.76 zimetolewa kwa vikundi vya wanawake 3,308, Shilingi Bilioni 12.55 zimetolewa kwa vikundi vya vijana 1,880 na Shilingi Bilioni 3.58 zimetolewa kwa vikundi 939 vya Watu Wenye Ulemavu. Kulingana na maelekezo ya Mhe. Rais ya utoaji wa mikopo kupitia Taasisi za Kifedha, Ofisi ya Rais -

TAMISEMI imeanza maandalizi ya utoaji wa mikopo kupitia mfumo wa Benki.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetoa mikopo inayotokana na marejesho kiasi cha Shilingi Bilioni 28.18 ambazo zimekopeshwa kwa vikundi 3,007. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 15.14 zimekopeshwa kwa vikundi 1,812 vya Wanawake, Shilingi Bilioni 11.37 zimekopeshwa kwa vikundi 873 vya Vijana na Shilingi Bilioni 1.66 zimekopeshwa kwa vikundi 324 vya Watu Wenye Ulemavu.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia fedha za mapato ya ndani yasiyolindwa kwa Halmashauri 20 zenye mapato zaidi ya Shilingi Bilioni 5, jumla ya Shilingi Bilioni 17.69 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara. Kupitia mapato haya, Halmashauri zimefanikiwa kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 10 kwa kiwango cha lami, kilomita 0.22 kwa kiwango cha zege, kilomita 52.80 kwa kiwango cha changarawe, uwekaji wa taa 94 za barabarani, mifereji mita 330, ujenzi wa daraja 1 na ulipaji wa fidia eneo la ujenzi wa barabara ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 7.25 zimetumika hadi mwezi Februari, 2023.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi ambapo hadi Februari, 2023 jumla ya vikundi 9,134 vimewezeshwa kwa kupata mafunzo ya ujasiriamali katika shughuli wanazoziendesha kupitia fedha zinazotolewa na asilimia kumi ya mapato ya ndani. Kati ya vikundi hivyo, vikundi 5,120 ni vya Wanawake, Vikundi 2,753 ni vya Vijana na Vikundi 1,261 ni Watu Wenye Ulemavu. Wafanyabiashara ndogondogo 329,662 wamesajiliwa na kati yao 110,452 wamepangwa katika maeneo rasmi. Vilevile, jumla ya masoko 367 yameboreshwa kuweza kumudu wajasiriamali 136,041. Pia, jumla ya Shilingi milioni 260 zimetolewa katika Mikoa 26 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi za machinga na wa bodaboda katika maeneo

rasmi. Aidha, Umefanyika usajili wa vikundi 34,127 vya kijamii vya huduma ndogo za fedha lengo ikiwa kuvitambua, kuviimarisha ili viweze kuwa endelevu, kuongeza huduma jumuishi za kifedha na kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha.

**Utekelezaji wa Miradi ya Uwajibikaji kwa Jamii (*Corporate Social Responsibility – CSR*)**

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Halmashauri kwa kushirikiana na kampuni zinazochimba madini zimekuwa zikitekeleza miradi mbalimbali ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) kwa mujibu wa Kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini Sura ya 123. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, kila kampuni inayofanya shughuli za uchimbaji wa madini ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapaswa kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya uwajibikaji kwa jamii. Hadi Februari, 2023 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeweza kukusanya na kuchambua taarifa za miradi inayotekelezwa kwa CSR kutoka kampuni za Barrick North Mara; Geita Gold Mine – GGM; Barrick Bulyanhulu; Acacia Buzwagi, Mwadui Mine, Kiwanda cha Saruji cha Dangote, Kampuni ya Mantra, Kampuni ya Uranex, Kampuni ya gypsum ya Knauf, Kampuni ya madini ya Tembo Nickel, Shanta Mining, Mgodi wa ZEM na CATA Mining.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi inayotekelezwa kupitia CSR kwa mujibu wa Sheria hiyo inaibuliwa na Kamati za Maendeleo za Jamii (*Community Development Committee - CDC*) na kupitiwa na Vijiji, Mitaa na Kata na kuwasilishwa Halmashauri na Mikoa kwa ajili ya uchambuzi na hatimaye Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi na kuridhiwa.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2018/19 hadi 2021/22 jumla ya Shilingi Bilioni 87.31 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kijamii kupitia CSR. Hadi Juni, 2022 kiasi cha Shilingi Bilioni 60.13 zimetumika kwa ajili ya

utekelezaji wa miradi katika sekta ya elimu, afya, miundombinu ya barabara, masoko na maji. Halmashauri zilizonufaika ni Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Shilingi Bilioni 10.43; Halmashauri ya Mji Geita Shilingi Bilioni 19.60; Halmashauri za Wilaya za Msalala Shilingi Bilioni 10.43; Kishapu Shilingi Bilioni 3.60; Halmashauri za Wilaya za Tarime Shilingi Bilioni 19.59; Geita Shilingi Bilioni 17.20; Nyang'hwale Shilingi Bilioni 1.94; Mtwara Shilingi Bilioni 1; Moshi Shilingi Milioni 166 na Kilwa Shilingi Bilioni 3.33.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 18.01 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kijamii kupitia CSR. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 18.05 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika sekta ya elimu, afya, miundombinu ya barabara, masoko na maji. Halmashauri zilizonufaika ni Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Shilingi Bilioni 2.27; Halmashauri ya Mji Geita Shilingi Bilioni 4.9; Halmashauri za Wilaya za Msalala Shilingi Bilioni 2.27; Kishapu Shilingi Bilioni 2.27; Geita Shilingi Bilioni 4.30; Nyang'hwale Shilingi Milioni 989; Biharamulo Shilingi Milioni 180; Ngara Shilingi Milioni 199.95; Bagamoyo Shilingi Milioni 40.3; Kibiti Shilingi Milioni 43; Mkuranga Shilingi Milioni 87.37; Rufiji Shilingi Milioni 133.42; Butiama Shilingi Milioni 67.5, Mbozi Shilingi Milioni 150 na Songwe Shilingi Milioni 157.7.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zinazotokana na CSR ni mapato lindwa (protected) na yanapaswa kuingizwa kwenye mipango na bajeti za Halmashauri kwa ajili ya miradi ya maendeleo iliyokubalika na wananchi. Aidha, kupitia Bunge lako Tukufu nitumie nafasi hii kuwakumbusha Wakuu wa Mikoa kuwa uidhinishwaji wa matumizi ya fedha hizo unapaswa kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuchambuliwa na kuridhiwa. Vilevile, niwakumbushe Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha wanasimamia utekelezaji wa miradi iliyokubaliwa na utoaji wa taarifa kama ilivyo miradi mingine

inayotekelezwa kwa fedha za Serikali. Aidha, Mfumo wa Fursa na Vikwazo Ulioboreshwa utumike katika kuibua, kusimamia, kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu miradi inayotekelezwa kwa fedha za CSR.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na takwimu zilizooneshwa hapo juu kuhusu mapokezi ya fedha kutokana na Uwajibikaji wa Makampuni kwa Jamii zinaonesha faida kubwa kwa wananchi wetu ambao wanaishi karibu na makampuni yanayotoa fedha za uwajibikaji. Hivyo, Serikali itahakikisha inasimamia upatikanaji na matumizi ya fedha hizo ili kuleta faida zilizotarajiwa na Wananchi wetu. Kupitia ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya Uchimbaji wa Madini ya Twiga – Barrick Tanzania tunatarajia kupokea fedha kwa utaratibu wa *D - Fund* ambazo ni Dola za Kimarekani Milioni 30 kwa mikupuo 3 ya Dola za Kimarekani Milioni 10 kila mkupuo kwa mwaka wa fedha 2022/23. Fedha zitaelekezwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya madarasa 1,094, mabweni ya wanafunzi 273 na matundu ya vyoo 1,645 katika shule za kidato cha 6 Tanzania Bara. Mahitaji haya yanatokana na ongezeko la wanafunzi 116,139 ambao bila madarasa hayo watakosa fursa ya kujiunga na kidato cha tano 2023.

**Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi**

**Utawala Bora na Usimamizi wa Rasilimali**

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na maeneo yaliyopatiwa kipaumbele ni kama ifuatavyo: -

**Kushughulikia Malalamiko na Kero za Wananchi katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha Utawala Bora, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi

zilizopo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI zimeendelea kutekeleza dhana ya ''TAMISEMI ya Wananchi''. Katika kutekeleza dhana hiyo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha Kituo cha Huduma ya Mawasiliano kwa Mteja (*Call Centre*) kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi bila ya kuhitaji kusafiri kuja Ofisi ya Rais - TAMISEMI Dodoma.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2023, Kituo hiki cha Huduma ya mawasiliano kwa mteja kimeendelea kutoa huduma kwa wananchi ambapo kimehudumia jumla ya wananchi 77,454 kuhusu kero, malalamiko na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali. Kituo hiki kimesaidia kupunguza na kutatua changamoto ya kupata taarifa zinazohitajika na wananchi pamoja na kuwapunguzia gharama za safari ya kuja Dodoma kufuatilia kero, malalamiko na kupata ufafanuzi wa masuala mbalimbali.

**Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kutoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa fedha kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa fedha inayotolewa mara kwa mara ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kuhakikisha kuwa mapato yanakusanywa kwa ufanisi na kuziba mianya ya kuvuja kwa makusanyo na kudhibiti matumizi.

110. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imefanyia kazi changamoto zilizokuwepo katika mfumo wa mapato wa *Local Government Revenue Collection Information System* (LGRCIS) kwa kusanifu na kujenga mfumo mpya wa TAUSI ambao umeanza kutumika katika Mwaka wa Fedha wa

2022/23. Hadi Februari, 2023 Halmashauri 169 zimeanza kutumia mfumo wa TAUSI ambao umeboreshwa kulinganisha na mfumo wa awali wa *Local Government Revenue Collection Information System* uliotumika kwa zaidi ya miaka 7. Mfumo huu utadhibiti mianya ya upotevu wa mapato na kudhibiti matumizi hususan matumizi ya fedha mbichi.

111. ***Mheshimiwa Spika***, Mfumo wa TAUSI unamwezesha mteja kujihudumia mwenyewe na kupata huduma pasipo kufika ofisi za Halmashauri; kupata vibali vya ujenzi na leseni za biashara pamoja na kuuza na kununua viwanja vilivyopimwa na Halmashauri kwa njia ya mtandao. Vilevile, mfumo utawezesha fedha kuingizwa benki kwa wakati kwa kuweka mbinu mbalimbali ikiwemo kudhibiti kiasi kinachoweza kukusanywa nje ya mtandao na kumlazimu mkusanyaji kuwasilisha benki kiasi cha juu anachoruhusiwa kukusanya. Aidha, katika mfumo huu usimamizi wa mashine za kukusanyia mapato (Point of Sales -PoS) umeimarishwa tangu Desemba, 2022 ili kudhibiti mianya mbalimbali iliyojitokeza katika mfumo wa *Local Government Revenue Collection Information System*.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa usimamizi wa malipo na uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka, Halmashauri zote zimeendelea kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE) ambapo kwa mara ya kwanza, Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka wa Fedha wa 2021/22 zimeandaliwa kutoka katika mfumo huo kwa Halmashauri zote 184. Pamoja na uwezo wa kutoa Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka, mfumo huu pia hutunza nyaraka za malipo. Hivyo, matumizi ya mfumo huu yatapunguza kwa kiasi kikubwa hoja za ukaguzi zinazotokana na upotevu wa nyaraka.

**Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Jimbo**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais –TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 15.99 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Majimbo ya Uchaguzi 214 ya Tanzania Bara. Hadi Februari, 2023 fedha zote zilizoidhinishwa zimetolewa. Fedha za Mfuko wa Jimbo zimeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoanzishwa kwa nguvu za Wananchi ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za kijamii hususan katika sekta ya afya na elimu.

**Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA**

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwenye Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake na vituo vya kutolea huduma za Afya ya Msingi na shule ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Mifumo mbalimbali imefanyiwa usanifu na kutengenezwa na wataalam wa Serikali ili kukidhi mahitaji mbalimbali katika maeneo ya kiutendaji yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na changamoto zilizokuwa zinajitokeza katika usimamizi, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya asilimia kumi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesanifu na kujenga mfumo wa *Ten Percent Loan Management Information System-TPLMIS* ulioanza kutumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Mfumo huu tangu ulipoanza kutumika umesaidia kuondoa changamoto zilizokuwepo, kuimarisha usimamizi wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo hiyo na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati ili kuongeza tija, kuondoa rushwa, upendeleo na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Pamoja na matarajio hayo kumeendelea kuwepo na changamoto za ukopeshwaji kwa vikundi visivyostahili na hivyo kusababisha mikopo kutorejeshwa ipasavyo. Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeanza

kuyafanyia kazi maelekezo ya Mhe. Rais ili mikopo hiyo ianze kutolewa kupitia Taasisi za Fedha.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeboresha Mfumo wa Kihasibu na Utoaji wa Taarifa za Fedha katika Ngazi za Msingi (*Facility Financial Accounting and Reporting System - FFARS)*. Katika maboresho hayo, mfumo wa FFARS sasa umewezeshwa kutumika katika ngazi ya Kata, Vijiji na Mitaa ili kuleta uwazi, uwajibikaji na kudhibiti matumizi ya fedha katika ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika sekta ya Afya, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kuboresha na kuhimiza matumizi ya mfumo wa *Government of Tanzania Health Operations Management Information System* (GoTHOMIS). Katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuboresha mfumo wa GoTHOMIS na hadi kufikia mwezi Februari 2023, vituo vya kutolea huduma za afya 1,424 vinatumia mfumo huo kuendesha shughuli za kila siku katika utoaji wa huduma. Matumizi ya Mfumo huu yamesaidia kudhibiti upotevu wa dawa na vifaa tiba, kudhibiti na kuongeza makusanyo ya ada za kuchangia huduma na ubadilishanaji na utoaji wa taarifa kwa wakati. Aidha, vituo 33 vya kutolea huduma za afya vinafanyiwa majaribio ya mfumo ulioboreshwa na ambapo yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2023.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Vodacom Foundation imeanzisha mfumo wa huduma ya usafiri wa dharura kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga (M-MAMA) ambao ulizinduliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 6 Aprili, 2022. Tangu kuanza kwa majaribio ya Mfumo wa M-MAMA katika Wilaya ya Sengerema na Mkoa wa Shinyanga mwaka 2013, akina mama wajawazito na watoto wachanga 12,000 wamehudumiwa na hivyo kusaidia

kupunguza vifo vya kina mama vinavyotokana na ukosefu au kuchelewa kupata huduma ya usafiri wa dharura. Hadi Februari, 2023, huduma hii ya mfumo wa M-MAMA inapatikana katika Mikoa 8 ambayo ni Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara, Tanga, Morogoro, Lindi na Arusha kwa Tanzania Bara. Aidha, ifikapo Septemba, 2023 Mikoa yote Tanzania Bara itakuwa inatumia mfumo wa M-MAMA katika kushughulikia dharura ya mama mjamzito na mtoto mchanga.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (i-CHF) ili kuboresha utoaji wa huduma ya afya kwenye ngazi ya msingi. Usimamizi huo umewezesha kuongezeka kwa wanachama hadi kufikia 4,262,394 (wanawake 2,458,481 na wanaume 1,803,913) kati ya Julai 2018 hadi Disemba, 2022. Kiasi cha Shilingi Bilioni 30.2 kimekusanywa kutokana na michango ya wanachama ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 22.2 zimetumika kulipia gharama za matibabu katika vituo vya kutolea huduma za afya 6,130 vilivyowahudumia wanufaika wa mfuko wa i-CHF.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na changamoto zilizokuwa zinazikabili Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uandaaji wa Mipango na Bajeti, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, imehuisha Mfumo wa Mipango, Bajeti na utoaji wa taarifa (PlanRep) unaotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufika ngazi ya Kata na Vijiji/Mitaa. Uwepo wa mfumo huu, umeongeza uwazi katika uandaaji wa Mipango na Bajeti na kupunguza gharama za kuchapisha nyaraka mbalimbali. Aidha, mfumo umesaidia katika kufanya tathmini na ufuatiliaji wa fedha katika utekelezaji wa kazi zilizoainishwa kwenye Mipango na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, mfumo huu unatumika katika Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyoko chini ya Msajili wa Hazina.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeboresha Mfumo wa Sensa ya ElimuMsingi *(Annual School Census - ASC)* unaokusanya takwimu mbalimbali za uandikishwaji wa wanafunzi kama inavyokuwa tarehe 31 Machi kila mwaka. Maboresho hayo yatawezesha upatikanaji wa taarifa za Vituo vya Malezi ya Watoto Wadogo Mchana *(Early Childhood Development Centres- ECD).* Matokeo ya sensa hii yatabainisha hali halisi ya uandikishaji wa watoto katika vituo vya malezi na elimu ya awali ili kusaidia kuboresha jitihada mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa taarifa za shule *(School Information System - SIS)* umeboreshwa ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za wanafunzi kujifunza popote na wakati wowote mtandaoni (e-Learning). Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tunaandaa Mkakati wa Elimu kwa Mtandao ili kukabiliana na uhaba wa walimu uliopo mashuleni.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuhakikisha wanafunzi wanaomaliza kidato cha Nne wanapata fursa ya kuhuisha Tahasusi za awali kabla ya kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Kati. Utaratibu huu umewezesha wanafunzi kuchagua Tahasusi na Kozi mbalimbali kulingana na ufaulu na vipaumbele vyao. Aidha, ushirikishwaji huu umeonyesha mwitikio chanya ambapo idadi ya wanafunzi wanaoufikia mfumo kufanya mabadiliko imekuwa ikiongezeka tangu Mwaka 2019 zoezi hili lilipoanza kwa mara ya kwanza na kufikia hadi wanafunzi 51,000.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia Uchumi wa Kidijitali, Serikali inajielekeza katika kutoa huduma mbalimbali kwa njia ya Mifumo ya TEHAMA. Katika kufanikisha hilo Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Ofisi na Nyumba za Viongozi katika Tawala za Mikoa**

125. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa Shilingi Bilioni 40.87 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa Ikulu Ndogo, majengo ya utawala na nyumba za Viongozi. Hadi Februari, 2023 jumla ya Shilingi Bilioni 33.26 sawa na asilimia 81.37 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo hayo. Aidha, hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

**Ikulu Ndogo (Rest Houses)**

126. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 2.93 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ikulu Ndogo 11 ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 2.21 zilitolewa sawa na asilimia 75.42. Ujenzi wa Ikulu Ndogo 2 katika mkoa wa Dodoma upo hatua ya ghorofa ya kwanza; ujenzi wa Ikulu Ndogo Ludewa upo hatua ya kuta na ujenzi wa Ikulu Ndogo za Kigoma na Malinyi upo hatua ya msingi.

127. ***Mheshimiwa Spika.*** Ukarabati wa Ikulu Ndogo Mkoa wa Mwanza - Nyamagana) Ikulu Ndogo Kagera - Bukoba umekamilika na ukarabati wa Jengo la Ikulu Ndogo Ruvuma - Namtumbo unaendelea. Aidha, ukarabati wa majengo ya Ikulu Ndogo 3 za Wilaya za Moshi, Korogwe na Tanga upo katika hatua za manunuzi.

**Ofisi za Wakuu wa Mikoa**

128. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 11.99 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Ofisi 17 za Wakuu wa

Mikoa ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 9.58 zimetolewa sawa na asilimia 79.89 ya fedha zilizotengwa; Ujenzi wa Ofisi 3 za Wakuu wa Mikoa ya Geita, Mbeya na Songwe zimekamilika na zinatumika ambapo baadhi ya kazi za ukamilishaji zinaendelea; Ujenzi wa ofisi 3 za Wakuu wa Mikoa ya Njombe, Katavi na Simiyu upo hatua ya ukamilishaji; na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro upo hatua ya ghorofa ya kwanza.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** Ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa umekamilika; Ukarabati unaendelea kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa 5 ya Kigoma, Kagera, Pwani, Singida na Rukwa. Aidha, ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa 5 ya Dodoma, Mwanza, Ruvuma, na Kilimanjaro upo hatua ya ununuzi.

**Nyumba za Wakuu wa Mikoa**

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Milioni 829.30 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba 5 za Wakuu wa Mikoa ambapo Shilingi Milioni 773.80 zimetolewa sawa na asilimia 93.30. Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na ujenzi wa uzio nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe zipo katika hatua ya ukamilishaji. Aidha, ujenzi wa nyumba ya muhudumu wa Mkuu wa Mkoa wa Songwe ipo hatua ya upauaji, ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya unaendelea na ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani upo hatua ya manunuzi.

**Nyumba za Makatibu Tawala wa Mikoa**

131. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 1.63 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba 6 za Makatibu Tawala wa Mikoa ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 1.20 zimetolewa sawa na asilimia 73.61. Ujenzi wa nyumba za

Makatibu Tawala wa Mikoa ya Mbeya na Songwe upo hatua ya ukamilishaji; na nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma ipo hatua ya lenta. Aidha, ujenzi wa nyumba ya mhudumu na uzio katika nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi upo hatua ya ukamilishaji, ukarabati wa nyumba za Makatibu Tawala wa Mikoa ya Pwani na Njombe upo katika hatua za ununuzi.

**Nyumba za Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa**

132. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Milioni 774 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba 21 za Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa ambapo fedha zote zimetolewa sawa na asilimia 100. Ujenzi wa nyumba 2 za Makatibu Tawala Wasaidizi Mkoa wa Singida umekamilika na zinatumika, ujenzi wa uzio wa nyumba 2 za Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mkoa wa Songwe upo hatua ya kuta na uzio wa nyumba 2 za Makatibu Tawala Wasaidizi Mkoa wa Singida zipo hatua ya ukamilishaji, ukarabati wa nyumba 10 za Makatibu Tawala Wasaidizi mkoa wa Rukwa na ujenzi wa nyumba 5 za Mkoa wa Kigoma unaendelea.

**Ofisi za Wakuu wa Wilaya**

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 11.86 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba 32 za Wakuu wa Wilaya ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 8.24 sawa na asilimia 69.47 zimetolewa. Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe umekamilika; ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya 3 za Malinyi, Mbogwe na Nyang'hwale upo hatua ya ukamilishaji; ofisi za Wakuu wa Wilaya 2 za Momba na Ulanga yapo hatua ya upauaji, majengo ya ofisi 2 za Wakuu wa Wilaya za Nkasi na Dodoma zipo hatua ya kuta, majengo ya ofisi 2 za Wakuu wa Wilaya za Kakonko na Kahama zipo hatua ya Msingi. Vilevile, Ujenzi wa majengo ya

Ofisi za wakuu wa Wilaya 3 za Karagwe, Babati na Kiteto zipo hatua ya ununuzi.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa uzio wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya 5 za Newala, Mtwara, Tandahimba, Masasi na Nanyumbu upo hatua ya msingi, ujenzi wa uzio ofisi za Wakuu wa Wilaya 2 za Same na Hai upo hatua ya ununuzi.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Misenyi unaendelea na ukarabati wa ofisi za Wakuu wa Wilaya 11 za; Musoma, Ukerewe, Magu, Ilemela, Misungwi, Sengerema, Bagamoyo, Kinondoni, Temeke, Kibaha na Mafia upo hatua ya ununuzi.

**Nyumba za Wakuu wa Wilaya**

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 4.50 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji, na ukarabati wa nyumba na ujenzi wa uzio katika nyumba za Wakuu wa Wilaya 26 ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 4.50 zimetolewa, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Wilaya 2 za Mbinga na Buhigwe upo hatua ya msingi; nyumba 2 za Wakuu wa Wilaya za Kishapu na Bariadi upo hatua ya boma; nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Kalambo upo hatua ya ukamilishaji; na ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Wilaya 3 za Musoma, Nyamagana na Kibiti zipo hatua ya ununuzi.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa uzio na ofisi ya mlinzi kwenye nyumba ya Mkuu wa Wilaya Wanging'ombe umekamilika; nyumba za wahudumu katika nyumba 2 za Wakuu wa Wilaya za Butiama na Musoma upo hatua ya ununuzi, ujenzi wa nyumba za wahudumu katika nyumba 2 za Wakuu wa Wilaya za Gairo na Momba upo hatua ya boma.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Wilaya 4 za Songea, Bukoba, Kigoma na Ludewa unaendelea; na ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Wilaya 9 za Siha, Rorya, Tunduru, Pangani, Muheza, Mkinga, Musoma, Bunda na Tarime zipo hatua ya ununuzi.

**Nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya**

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 1.57 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba 16 za Makatibu Tawala wa Wilaya ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 1.57 zimetolewa sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa. Ujenzi wa nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya 3 za Momba, Chunya na Rungwe upo hatua ya ukamilishaji; nyumba 2 za Makatibu Tawala wa Wilaya za Newala na Masasi upo hatua ya Msingi na ujenzi wa nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya 5 za Lindi, Kilwa, Serengeti, Nyamagana na Kibiti upo hatua ya ununuzi. Aidha, ukarabati wa nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya 2 za Kibondo na Kigoma unaendelea. Vilevile, nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya 4 za Ileje, Bunda, Kibaha na Mafia zipo hatua za ununuzi.

**Ofisi za Maafisa Tarafa**

141. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 3.99 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji, ukarabati na ununuzi wa samani katika ofisi 57 za Tarafa. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 3.87 zimetolewa, sawa na asilimia 96.99 ya fedha zilizoidhinishwa. Ujenzi wa Ofisi za Maafisa Tarafa 3 katika mkoa wa Mbeya zipo hatua ya ukamilishaji, Ujenzi wa Ofisi za Tarafa katika Mikoa ya Kilimanjaro 5, Kigoma 1, Dar es Salaam 1 na Pwani 6 upo katika hatua ya ununuzi; na ofisi za tarafa 5 za Mkoa wa Mtwara zipo hatua ya msingi, ujenzi wa ofisi 6 za tarafa mkoa wa Songwe kati ya hizo ofisi 2 zipo hatua ya msingi, ofisi 2 boma na ofisi 2 hatua ya ukamilishaji; Ujenzi wa ofisi za

Maafisa tarafa katika Mkoa wa Dodoma 3 na Ruvuma 2 zipo hatua ya kuta, Morogoro ofisi 5 hatua ya upauaji, ujenzi wa ofisi 1 Mkoa wa Kagera upo hatua ya ukamilishaji. Aidha, ukamilishaji wa ofisi 5 za tarafa na ununuzi wa samani za ofisi za Tarafa 14 katika Mkoa wa Kilimanjaro upo katika hatua ya ununuzi.

**Nyumba za Maafisa Tarafa**

142. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi milioni 800.50 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 7 za Maafisa Tarafa ambapo jumla ya Shilingi milioni 545.50 zimepokelewa, sawa na asilimia 68.14 ya fedha zilizoidhinishwa. Ujenzi wa nyumba za Maafisa Tarafa zipo katika hatua mbalimbali, ambapo nyumba za Maafisa Tarafa 4 katika mkoa wa Mtwara, zipo hatua ya msingi; Shinyanga nyumba 1 ipo hatua ya kuta na nyumba 2 za Maafisa Tarafa katika mkoa wa Mara zipo hatua ya ununuzi.

**Ujenzi wa Soko la Kariakoo**

143. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 jumla ya Shilingi Bilioni 10 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Kariakoo unaohusisha ujenzi wa jengo jipya na Ukarabati wa Jengo la Soko la Zamani. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 4.16 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, sawa na asilimia 42 ya fedha zilizoidhinishwa. Ujenzi wa soko hili umefikia hatua ya kumwaga jamvi la ghorofa ya tano kati ya ghorofa sita ikihusisha ghorofa mbili za chini ya ardhi (basement). Aidha, ukarabati wa jengo la zamani unaendelea na umefikia asilimia 62.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa Soko hili kutachochea ukuaji wa biashara katika Jiji la Dar es Salaam, Mikoa mingine na nchi jirani. Soko hili linataraijwa kukamilika Oktoba, 2023 na litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 2,300 sawa na

ongezeko la wafanyabishara 638 ukilinganisha na wafanyabiashara 1,662 waliokuwepo kabla ya ukarabati wa jengo la zamani na ujenzi wa jengo jipya.

**Ununuzi wa Magari katika Tawala za Mikoa**

145. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa Shilingi Bilioni 2.08 kwa ajili ya ununuzi wa magari katika Tawala za Mikoa. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 1.71, sawa na asilimia 82.21 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 8 kwa ajili ya ununuzi wa magari ya Wakuu wa Mikoa ya Tabora, Kilimanjaro na Mara na magari ya Wakuu wa Idara katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Njombe 1, Kilimanjaro 2 na Mbeya 1 pamoja na gari 1 kwa ajili ya Mkuu wa Wilaya ya Ludewa. Taratibu za ununuzi zinaendelea chini ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).

**Majengo ya Utawala na Nyumba za Viongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 68.85 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri 83. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 59.94 sawa na asilimia 83 kwa ajili ya ujenzi wa majengo 80. Majengo 8 yamekamilika na majengo 72 yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, Shilingi Bilioni 13 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya 13 ya utawala katika Halmashauri. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 12 zimepokelewa sawa na asilimia 92 kwa ajili ya ujenzi wa majengo 12. Majengo hayo yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi *(Kiambatisho Namba 12)*.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 8.90 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 111 za Wakuu wa Idara na

Shilingi Bilioni 7.20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 47 za Wakurugenzi wa Halmashauri. Hadi Februari, 2023, zimepokelewa jumla ya Shilingi Bilioni 15.17, sawa na asilimia 94 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 6.75 ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 43 za Wakurugenzi wa Halmashauri na Shilingi Bilioni 8.42 ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 90 za Wakuu wa Idara. Aidha, nyumba hizo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**Huduma za Kiuchumi na Uzalishaji**
**Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agricultural Sector Development Programme Phase II – ASDP II)* kupitia Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans - DADPs*). Hadi Februari, 2023 jumla ya Shilingi Milioni 785.14 zimetumika. Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni 187.27 zimetumika katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Shilingi Milioni 597.86 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli zilizotekelezwa na Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika Halmashauri 184;
(ii) Kuwezesha ujenzi wa Skimu 11 za Umwagiliaji katika Halmashauri za Same 2, Siha 3, Kyela 3 na Mbalali 3;
(iii) Ujenzi wa nyumba 1 ya Afisa Ugani katika Halmashauri ya Mji Geita;
(iv) Ununuzi wa Madume Bora ya ng'ombe 50 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato;
(v) Kuchanja Ng'ombe 7,350 dhidi ya magonjwa mbalimbali katika Halmashauri 4 za Manispaa za Singida na Songea na Halmashauri za Wilaya za Ludewa na Kwimba;

(vi) Ukarabati wa majosho 4 katika Vijiji vya Luilo, Ibumi na Amani katika Halmashauri ya Ludewa na Kijiji cha Mtakuja Halmashauri ya Hai;
(vii) Ujenzi wa Vitalu Nyumba 2 (Green Houses) katika Halmashauri ya Geita Mjii;
(viii) Kutekeleza shughuli za lishe bora kwa binadamu na kudhibiti madhara ya upungufu Lishe bora (Nutrition-Specific and Nutrition-Sensitive Interventions) katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na Halmashauri ya Mji Mafinga; Shughuli hii ilihusisha kusambaza mbegu za viazi lishe tani 7 kwa wakulima ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo tani 3 na Hamashauri ya Mafinga Mji tani 4;
(ix) Ujenzi wa Majengo ya Machinjio 2 ya kati (slaughter houses) ya mifugo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma na Halmashauri ya Mji Mafinga;
(x) Kuwezesha ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao Halmashauri ya Wilaya ya Moshi;
(xi) Kuratibu na kusimamia shughuli za uhifadhi wa mazingira, ufugaji nyuki na utalii ndani kwa Mkoa wa Songwe;

149. ***Mheshimiwa Spika,*** Fedha hizo, zimetokana na vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri na ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**Uendelezaji wa Vijiji na Miji**

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali katika kuandaa na kutekeleza Mipango ya Uendelezaji wa Vijiji, Miji na Miji Midogo Inayochipukia ambayo imekuwa nyenzo muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi hususan katika Ngazi za Msingi. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imezisimamia Mamlaka za Upangaji na kuzishirikisha Wizara za kisekta, sekta binafsi, Wadau wa Maendeleo na

Jamii kwa jumla katika kuandaa Mipango 2,640 ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji na Mipango Kabambe 33 ya Ma-Jiji, Manispaa na Miji nchini ya kipindi kati ya Mwaka 2015 na 2039. Utekelezaji wa Mipango hiyo upo katika hatua mbalimbali. Vilevile, kutokana na kasi kubwa ya ukuaji wa miji nchini ambapo Mwaka 2022 ilikuwa kwa kiwango cha asilimia 5.3 kwa Mwaka ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.9 kwa Mwaka katika kipindi hicho kwa Bara la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, Ofisi ya Rais TAMISEMI katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, imeandaa kanzidata ambayo imesajilii Miji Midogo Inayochipukia 4,310. Aidha, kati ya Miji hiyo asilimia 91.5 ipo kwenye Mamlaka za Wilaya na asilimia 8.5 ipo kwenye Mamlaka za Miji.

151. ***Mheshimiwa Spika****;* kutokana na kasi kubwa ya ukuaji wa miji hiyo unaotokana na uwekezaji mkubwa unaondelea kufanywa na Serikali, Sekta binafsi na wadau wengine katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye sekta za huduma za kiuchumi na kijamii, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeandaa Mkakati wa Uendelezaji wa Miji Midogo Inayochipukia ili kuleta utangamano wa maendeleo Vijijini na Mijini, Miji Midogo Inayochipukia 194 na Vijiji vya mfano 194 vimeainishwa kwa kuzingatia kanda, jiografia ya maeneo husika na fursa zilizopo katika maeneo husika.

152. ***Mheshimiwa Spika;*** utangamano huo utawezesha kuweka msawazo katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa kuweka kipaumbele cha kuendeleza maeneo yenye mazingira magumu na yasiyofikika kwa urahisi. Mkakati wa kuendeleza miji inayochipukia unahusisha kubaini mtawanyiko wa kijiografia wa Vijiji na Miji, kuhuisha takwimu kwenye kanzidata ili kujumuisha makundi ya watu kwa jinsia na umri, kuratibu upatikanaji wa huduma muhimu; kuwajenga uelewa viongozi wa ngazi za msingi wa Kata, Vijiji, Vitongoji na Mitaa katika uendelezaji miji hiyo; kuweka au kuhakiki mipaka ya maeneo hayo kwa kutumia mifumo ya taarifa za kijiografia GIS; kuboresha au kurembesha mandhari

ya maeneo ya matumizi ya ardhi husika; na kujenga miundombinu muhimu ya kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo.

153. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau inaratibu utekelezaji wa Uanzishwaji, Upangaji na Uendelezaji wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji Kwala, Mkoa wa Pwani kwa maelekezo ya Serikali ya mwezi Mei 2022. Vilevile, kuendelea kukamilisha Mpango Kabambe Jumuishi wa Jiji la Kwala la ukubwa wa hekta **130,831** kwa kipindi cha Mwaka **2022 – 2050** ambalo limetangazwa kwenye **Gazeti la Serikali Namba 633** la tarehe 28 Oktoba, 2022.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango Kabambe wa Jiji la Kwala unajumuisha Vijiji 30 vya Halmashauri za Wilaya ya Kibaha (16), Chalinze (9) na Kisarawe (5). Aidha, kwenye Jiji hilo jipya tayari kuna Bandari Kavu ya Kwala na linapitiwa na reli ya kisasa ya *Standard Gauge – SGR*, reli ya Kati na reli ya TAZARA pamoja na Barabara Kuu ya Dar es Salaam – Morogoro. Pia, unazihusisha miundombinu iliyowekezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi *(Ruvu Livestock Holding Ground),* NARCO (Ranchi ya Ruvu), Kituo cha Kupozea Umeme (Pera) kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere na Mizani ya Vigwaza.

155. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zinazoendelea kufanyika kwenye eneo la Mpango la Kwala ni pamoja na ukamilishaji wa Ujenzi wa Bandari Kavu na Kongani ya Viwanda 350, Utwaaji shirikishi wa maeneo na fidia mbalimbali, ujenzi wa barabara na vipande vya reli ili kuunganisha vitovu vya uzalishaji na usafirishaji ndani ya eneo la Mpango. Serikali imelenga kuwa Mpango Kabambe wa Jiji la Kwala utekelezwe kwa kuihusisha zaidi sekta binafsi ili Jiji liwe na tija ya kipekee kitaifa na kimataifa.

**Mapitio ya Utekelezaji wa Malengo ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23**

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia taasisi 7, ambazo ni Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Chuo cha Serikali za Mitaa, Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), Shirika la Elimu Kibaha (KEC) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC). Aidha, utekelezaji uliofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 hadi Februari, 2023 kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

**Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

157. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 TARURA iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 838.15 kutoka Mfuko wa Barabara, Tozo za Mafuta, Mfuko Mkuu wa Serikali na Wadau wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara. Hadi Februari, 2023, TARURA imepokea Shilingi Bilioni 577.80, sawa na asilimia 69 ya bajeti iliyoidhinishwa kutoka katika vyanzo vinne.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 TARURA iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 257.04 kutoka Mfuko wa Barabara kutekeleza kazi za matengenezo ya barabara kilomita 24,015.77, ujenzi wa barabara kwa Kiwango cha lami kilomita 40.78, ujenzi wa barabara za changarawe kilomita 2,532.51, madaraja na makalavati 28. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 146.68, sawa na asilimia 85.60 ya Shilingi Bilioni 171.36 zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi hicho. Kazi zilizofanyika ni pamoja na matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 14,826.35, ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 12.52, kukarabati barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 84.97 na ujenzi wa madaraja na makalavati 7.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** TARURA katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 325.77 kutokana na

tozo ya mafuta (Shilingi 100 kwa lita) kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara za lami kilomita 180.21, changarawe kilomita 6,100.46, madaraja 218 na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 4,093.5. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 211.37 sawa na asilimia 97.32 ya Shilingi Bilioni 217.18 zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi hicho. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:- ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 97.79, ukarabati wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 3,304.14 na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 1,719.27.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 TARURA iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 127.50 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara za lami kilomita 93.09, changarawe kilomita 2,308.99, madaraja 75, makalavati 114 na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 8,449. Hadi Februari, 2023 zimepokelewa Shilingi Bilioni 62.53 sawa na asilimia 73.56 ya Shilingi Bilioni 85.00 zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi hicho. Kazi zilizofanyika ni: ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 53.52, ukarabati wa barabara za changarawe kilomita 1,335.04, ujenzi wa madaraja 68, makalavati 95 na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 3,548.58.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 71.38 kwa ajili ya Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam *(DMDP)* na Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 55.30 ni kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi wa DMDP na Shilingi Bilioni 16.08 ni kwa ajili ya uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizotekelezwa hadi Februari, 2023 ni ukamilishaji wa ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 5.3 kwa kiwango cha lami; ukamilishaji wa ujenzi wa

mitaro ya maji ya mvua kilomita 1.8 kupitia mradi wa DMDP uliopokea Shilingi Bilioni 71.38 sawa na asilimia 100 ambapo mradi huu umekamilika na kufungwa mwezi Desemba, 2022. Aidha, maandalizi ya mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness Project* (TACTIC) na uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi yanaendelea.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 6 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri za Wilaya za Mbogwe, Handeni, Iringa, Mufindi, Kilolo na Ruangwa ili kuwezesha utekelezaji wa Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini *(Tanzania Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities - RISE)* katika Halmashauri hizo. Aidha, mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 6 kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2021/22 hadi 2026/27 kwa mujibu kwa makubaliano ya mkataba wa utekelezaji ambapo kilomita 400 za barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami. Hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 10.13 zimepokelewa na kazi zilizotekelezwa ni usanifu na kutangazwa kwa zabuni za ujenzi wa barabara kilomita 19 katika Wilaya ya Mufindi na kilomita 14 katika Wilaya ya Iringa. Aidha, kazi inayoendelea ni ununuzi wa wataalam washauri kwa kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kilomita 200 za barabara za Wilaya za Ruangwa, Mbogwe, Handeni na Kilolo.

164. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia mradi wa TACTIC iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 16.80 kwa Awamu ya Kwanza (Tier I) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya msingi katika Halmashauri 12 ambayo inajumuisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 213.1 katika katika Majiji ya Arusha kilomita 20.0, Mwanza kilomita 14, Mbeya kilomita 24.8 na Dodoma kilomita 20.0, Manispaa za Tabora kilomita 15.0, Kigoma kilomita 16.5, Ilemela kilomita 15.8, Kahama kilomita 24.2, Morogoro kilomita 19.7, Songea kilomita 11.8 na

Sumbawanga kilomita 14.3; Halmashauri ya Mji wa Geita kilomita 17; ujenzi wa masoko 18 katika Majiji ya Arusha 2, Dodoma 4, Mbeya 3, Mwanza 1; Manispaa za Tabora 1, Kigoma 2, Ilemela 1, Kahama 2, Songea 2 na mitaro ya maji ya mvua kilomita 31.6 katika Majiji ya Dodoma kilomita 6.3 na Mwanza kilomita 6.0, Mbeya kilomita 6.5; Manispaa za Kahama kilomita 3.0, Kigoma kilomita 5.4 na Morogoro kilomita 4.4 na stendi za mabasi 5 katika Majiji ya Arusha na Mbeya; Manispaa za Tabora, Kahama na Mji wa Geita, na kituo cha mabasi ya abiria wa reli ya SGR katika Manispaa ya Morogoro, Vituo vidogo vya daladala 8 katika Majiji ya Arusha 1, Dodoma 5, Mbeya 1 na Manispaa ya Kahama 1; Madaraja Makubwa 4 katika Jiji la Arusha 1; Manispaa ya Kigoma Ujiji 2 na Morogoro 1; Vivuko katika SGR 2 katika Majiji ya Dodoma na Mwanza; Mabwawa ya kuhifadhi maji 4 katika Jiji la Dodoma, na maghala ya kuhifadhia mazao 2 katika Manispaa za Songea na Sumbawanga; Vivuko vya waenda kwa miguu 3 katika Jiji la Dodoma na bustani ya mapumziko 1 katika Jiji la Arusha. Aidha, mradi utatekelezwa katika Mamlaka za Miji 45.

**Mwongozo wa Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara.**

165. ***Mheshimiwa Spika***, kazi za matengenezo ya barabara za Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) huongozwa na mwongozo wa matumizi ya fedha zitokanazo na tozo ya mafuta chini ya Bodi ya Mfuko wa Barabara. Mwongozo huo unaelekeza kuwa matengenezo ya miundombinu ya barabara zenye hali nzuri na wastani zinafanyiwa matengenezo kwa asilimia 100 kwa lengo la kuhakikisha kuwa uwekezaji uliofanyika unatunzwa ili ufikishe umri wake uliokusudiwa wakati wa usanifu; kwa Barabara zenye hali mbaya zinafanyiwa matengenezo kwenye sehemu korofi ili kuziwezesha kupitika misimu yote kwa mwaka.

166. ***Mheshimiwa Spika***, kazi za Matengenezo ya kawaida (Routine and Recurrent Maintenance) zinahusisha kusafisha mifereji na makalavati, kuziba mashimo na kufyeka majani. Pia kurekebisha uharibifu unaosababishwa na watumia barabara na mvua kwenye madaraja na makalavati. Kazi hizi hujirudia kila mwaka. Aidha, kazi za Matengenezo ya sehemu korofi zinahusisha kurekebisha maeneo korofi ambayo yanasababisha barabara isipitike na yanahusisha ukarabati wa madaraja na makalavati, sehemu zenye udongo oevu na kuweka zege sehemu korofi zenye milima.

**Kanuni za Ugawaji wa Fedha za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara.**

167. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini umeandaa rasimu ya kanuni ya ugawaji wa fedha za Matengenezo ya miundombinu ya barabara ambapo kwa sasa hatua iliyofikiwa ni kufanyiwa mapitio na wataalamu wa kujitegemea (Independent Reviewers). Hivyo baada ya mapitio fomula itawasilishwa kwa wadau mbalimbali ili kupata maoni kabla ya kuanza kutumika.

**Matokeo ya Ongezeko la Bajeti kwa kazi za Ujenzi na Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara.**

168. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2021/22 umeongezewa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 449.66 na kufikia bajeti ya Shilingi Bilioni 722.19 sawa na asilimia 163.44. Ongezeko hili la fedha limewezesha kujenga barabara za lami kilomita 816.62, barabara za changarawe kilomita 19,786.38 na madaraja 2,311. Aidha, kutokana na ongezeko la fedha kazi zimeongezeka ambapo Makandarasi wa ndani wamenufaika na ongezeko hilo la fedha, hivyo wastani wa mikataba 844 ya kazi za barabara imeongezeka na kufikia wastani wa Mikataba 1,810.

**Matumizi ya Teknolojia Mbadala kwenye Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara**

169. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) iliunda timu ya ufuatiliaji wa ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia mbadala inayotumika Zanzibar. Kwa nyakati tofauti timu ilitembelea ujenzi wa miundombinu ya barabara Zanzibar kwa kutumia teknolojia mbadala. Aidha, hatua iliyokuwa imefikiwa kipindi hicho ni ujenzi wa kilomita 10 ambazo zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji, kilomita 6.1 (Barabara ya Mwela polisi -Kibanda Mzungu) kati ya hizo zilikuwa za majaribio na kilomita 4 zipo ndani ya mradi kwa barabara ya Dimani Sokoni – Dimani Pwani. Vilevile, timu ilitembelea barabara za Jumbi Sokoni – Fuonikibondeni kilomita 4.4, Dunga – Zuze kilomita 1.8 na Tunguu – Ndijani – Mkwajungoma kilomita 7.8 kwa ajili ya kujifunza na kuona mradi unavyotekelezwa.

170. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala unaendelea kufanya majaribio ya teknolojia mbalimbali ili kutumia udongo uliopo eneo la kazi badala ya kusomba kutoka maeneo mengine ya

mbali. Teknolojia hizo ni pamoja na ECOROADS, Ecozyme, na GeoPolymer. Hadi sasa kwa kutumia Teknolojia ya ECOROADS katika Jiji la Dodoma imejengwa kilomita 1 ambayo imekamilika na katika Wilaya ya Mufindi zitajengwa kilomita 10 na Mkandarasi yuko kwenye matayarisho ya kuanza kazi.

171. ***Mheshimiwa Spika***, Faida zinazoelezwa na kuwekwa kwenye machapisho mbalimbali za teknolojia mbadala kwa wadau ni kama ifuatavyo: Uhifadhi wa mazingira; kupunguza muda wa ujenzi wa barabara kulinganisha na ujenzi unaofanywa sasa kwa zaidi ya asilimia 40; na kupunguza gharama za matengenezo ya barabara. Aidha, faida mbalimbali kwa upande wa ukuaji wa uchumi ni pamoja na: - Wadau wa teknolojia mbadala kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa ambavyo vitaongeza ajira kwa wananchi wetu. Vilevile, kuongeza fedha za kigeni kwa kuwa malighafi itakayozalishwa itauzwa nje ya mipaka ya nchi yetu; na Elimu kwa Makandarasi wazawa (Local Contents) ambao sasa wataweza kujenga barabara kwa kutumia teknolojia mbadala.

172. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini umepanga kutekeleza ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia mbadala inayotumika Zanzibar zenye zaidi ya kilomita 100 zinazokisiwa kuwa na gharama ya Shilingi Bilioni 90 ikijumuisha fedha za usanifu, ufuatiliaji na usimamizi.

**Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02)**

173. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Utumishi wa Walimu *(Teachers Service Commission-TSC)* imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura ya 448, Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za Mwaka, 2016, Taratibu na Miongozo inayohusu usimamizi wa ajira, nidhamu, maadili na maendeleo ya walimu nchini.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Tume ya Utumishi wa Walimu iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 15.65. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 8.27 ni mishahara, Shilingi Bilioni 6.71 ni matumizi mengineyo na Shilingi Milioni 670 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Februari, 2023, Tume imepokea Shilingi Bilioni 7.83, sawa na asilimia 75.07 ya Shilingi Bilioni 10.33 zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 4.95 ni Mishahara na Shilingi Bilioni 2.87 ni Matumizi Mengineyo.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yaliyotekelezwa na TSC ni pamoja na kusajili walimu 9,800; kupandishwa vyeo walimu 1,003; walimu 3,347 wamethibitishwa kazini; walimu 3,388 wamebadilishiwa vyeo; kuhuisha TANGE za walimu kwenye Wilaya zote 139; Vikao 300 vya mashauri ya nidhamu kwa walimu vya kisheria vimefanyika; mashauri 273 ya nidhamu ya walimu yamefanyiwa uchunguzi na kuwasilishwa kwenye Kamati za Wilaya kwa ajili ya kutolewa uamuzi; rufaa 144 zilitolewa uamuzi, ambapo walimu 15 walirejeshwa kazini, walimu 74 walifukuzwa kazi, mwalimu 1 alishushwa cheo, walimu 6 walipunguziwa asilimia 15 ya mishahara, mashauri 33 yamerudishwa kwenye Kamati za Wilaya kuanza upya, na rufaa zilizokatwa nje ya muda ni 15, na Watumishi 133 wa Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya kutoka katika Mikoa 14 wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSC-MIS).

**Chuo cha Serikali za Mitaa**

176. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Chuo kiliidhinishiwa Shilingi Bilioni 15.24. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 5.34 ni kwa ajili ya mishahara, Shilingi Milioni 142.19 ni ya Matumizi Mengineyo na Shilingi Bilioni 9.75 ni mapato ya ndani. Hadi Februari, 2023 Chuo kimepokea Shilingi Bilioni 8.31 sawa na asilimia 55, ambapo Shilingi Bilioni 4.10 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara, Shilingi Milioni 124.55

ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Shilingi Bilioni 4.08 kutoka mapato ya ndani.

177. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Chuo kimeendelea kutekeleza majukumu ya kisheria ikiwemo mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wanafunzi 6,008 wamesajiliwa katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada ya Kwanza. Hadi Februari, 2023 washiriki 1,922 wamepewa mafunzo juu ya uongozi, usimamizi na uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Kati ya hao, washiriki 851 ni Waheshimiwa Madiwani, Watendaji 440 wa Kata na vijiji, Maafisa waandamizi 19 wa Serikali ya Nigeria kutoka Chuo cha *National Institute of Policy and Strategic Studies*-Guru, wajumbe 77 wa ALAT wa Mkoa wa Mwanza, Maafisa Mipango 272 kutoka Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji, Wajumbe 161 wa Kamati za kutolea Huduma za Afya na Watumishi Wapya102.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine yaliyotekelezwa na Chuo ni pamoja na kuendeleza watumishi katika fani mbalimbali ambapo watumishi 54 wapo katika mafunzo ya muda mrefu, Uendeshaji wa mitihani kwa ngazi za astashahada, stashahada na shahada kwa muhula wa kwanza, kuendesha mahafali ya 13 ya Chuo ambapo wanafunzi 4,993 walihitimu mafunzo yao. Aidha, Chuo kimefanya matengenezo ya miundombinu ya maji katika nyumba za watumishi na katika tenki kuu, ukarabati wa miundombinu ya umeme, kuwezesha vikao mbalimbali vya kisheria kufanyika na kulipa stahiki mbalimbali za watumishi. Chuo kimegharamia matumizi mbalimbali ya ofisi kama vile ankara za umeme, maji, mafuta, matengenezo ya magari, ulinzi, usafi, simu, "*internet*" na vifaa vya ofisi. Pia, Chuo kimeanzisha Shahada ya Kwanza ya Usimamizi wa Rasilimali Watu na kimetoa ufadhili kwa wanafunzi 4 katika kozi

mbalimbali za muda mrefu wanaotoka katika familia zisizojiweza katika Kata ya Hombolo.

**Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam**

179. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 38.57 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya Wakala. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 11.17 ni Matumizi ya Kawaida na Shilingi Bilioni 27.40 ni za miradi ya maendeleo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha Shilingi Bilioni 8 kutoka Serikali Kuu, Shilingi Bilioni 1.81 ni mapato ya ndani na Shilingi Bilioni 17.59 ni fedha za nje.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023, Wakala imekusanya na kupokea Shilingi Bilioni 15.25, sawa na asilimia 59.3 ya malengo ya kupokea na kukusanya Shilingi Bilioni 25.71 kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa na zilizokusanywa, Shilingi Bilioni 5.86 ni makusanyo ya mapato ya ndani na Shilingi Bilioni 1.52 ni fedha za matumizi ya kawaida kutoka Serikali Kuu ambapo Shilingi Bilioni 1.22 ni mishahara na Shilingi Milioni 298.86 ni matumizi mengineyo.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala imeendelea kusimamia ulinzi na usalama katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya kwanza kwenye vituo vikuu 5, vituo vidogo 27, madaraja ya watembea kwa miguu 3 pamoja na karakana ya Jangwani na Ubungo.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala imeendelea kufanya matengenezo katika Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka katika vituo vya Gerezani na Kimara na matengenezo ya mfumo wa maji taka katika vituo vya Kimara na Kivukoni. Aidha, matengenezo na marekebisho yamefanyika katika vibanda 20 vya kukatia tiketi (*Cashier booths*) kwenye vituo vya Stop over, Suka, Temboni, Kwa Msuguli, Kibanda cha

Mkaa, Mbezi Luis-2, Magufuli Bus Terminal, Mloganzila, Luguruni, Kwa Mangi na Gogoni. Vituo vingine ni pamoja na Kibamba Chama, Kibamba Shule, Kwa Komba na Madukani. Aidha, matengenezo hayo yamegharimu Shilingi Milioni 151.36 na kazi imekamilika.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala imeendelea kusimamia Huduma za Mpito, katika Awamu ya Kwanza ya Mfumo wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART zilizoanza na mabasi 140 kwenye njia kuu 7 zinazochukua kilomita 20.9 za njia kuu, vituo 27 na vituo vikuu 5 na kuongeza kilomita 7 za njia ya Kimara - Mbezi - Kibaha na Mloganzila. Aidha, Wakala umesimamia huduma za usafi katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza ya mradi.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala imeanza kufanya maandalizi ya utwaaji wa maeneo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mradi wa DART Awamu ya Nne na ya Tano; ambapo jumla ya wananchi wapatao 1,080 wanaostahili kulipwa fidia wametambuliwa na Tathmini imefanywa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Aidha, Wakala unaendelea kufanya maandalizi ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi wa ujenzi wa karakana ya mabasi ya Ubungo Maziwa kwa ajili ya awamu ya kwanza ya mradi na tayari Serikali imetoa Shilingi Bilioni 7.8.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Wakala imeendelea kushirikiana na Wataalam washauri (*Transaction Advisors*) kuhusu kuwapata watoa huduma ya mabasi kwenye mfumo wa DART Awamu ya Pili ambapo jumla ya mabasi 759 yatahitajika. Kati ya mabasi hayo, mabasi 245 yatakuwa na urefu wa mita 18 na yatatoa huduma katika njia kuu na mabasi 514 yenye urefu wa mita 12 yatatoa huduma katika njia za mlisho.

**Shirika la Elimu Kibaha**

186. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Shirika la Elimu Kibaha liliidhinishiwa Shilingi Bilioni 13.54, kwa ajili ya kuendelea kutekeleza majukumu ya msingi ya kuanzishwa kwake ya kutoa elimu ya kupambana na ujinga, umaskini na maradhi. Kati ya fedha zilizoidhinishwa, Shilingi Bilioni 9.82 ni mishahara, Shilingi Milioni 849.36 ni matumizi mengineyo, Shilingi Milioni 620 ni za miradi ya maendeleo, Shilingi Bilioni 1.71 ni mapato ya ndani na Shilingi Milioni 549.06 ni ruzuku ya ElimuMsingi na Sekondari Bila Ada.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Shirika limepokea Shilingi Bilioni 5.23. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 3.89 ni za mishahara, Shilingi Milioni 420.7 ni za matumizi mengineyo, Shilingi Milioni 620 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi Milioni 303.39 ni kwa ajili ya ElimuMsingi na Sekondari Bila Ada. Aidha, Shilingi Milioni 770.65 zimekusanywa kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani, sawa na asilimia 67.60 ya Shilingi Bilioni 1.14 zilizotarajiwa kukusanywa katika kipindi hicho.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023 Shirika limetoa mafunzo ya ElimuMsingi kwa wanafunzi 2,703 na elimu ya sekondari kwa wanafunzi 357. Aidha, Shirika limetoa huduma za maktaba kwa wananchi 12,855 ambapo wananchi 4,280 waliazima machapisho mbalimbali na wananchi 252 waliazima vitabu kwa ajili ya kwenda kujisomea majumbani.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Elimu Kibaha limeendelea kutoa elimu ya uuguzi na utabibu kwa wanachuo 572 kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha. Aidha, elimu ya Afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza imetolewa kwa Wananchi 450 (Wanawake 277 na Wanaume 173).

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Elimu Kibaha kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha limetoa mafunzo ya muda mrefu ya nadharia na vitendo kwa wanachuo 353

katika fani mbalimbali. Mafunzo yaliyotolewa ni ya fani za kilimo, mifugo, uashi, ufundi bomba, useremala, ushonaji, upishi, ufundi wa magari, umeme wa majumbani, uundaji na uchomeleaji vyuma. Aidha, mafunzo ya muda mfupi kwa wananchi 750 (wanawake 518 na wanaume 232) yametolewa katika fani za udereva, ujasiriamali, elimu ya kifedha, usimamizi wa mikopo na kilimo cha bustani.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Elimu Kibaha kwa mara ya kwanza limetoa mafunzo ya ujuzi kwa njia ya elimu mtandao (*e-learning*) ikifuatia na mafunzo ya vitendo katika kozi za kilimo, mifugo, ufundi uashi, bomba, useremala, umeme wa majumbani, upishi, ushonaji, magari, udereva, uundaji na uchomeleaji vyuma kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia kwa gharama ya Shilingi Milioni 131.22. Fedha hizo ni za mfuko wa ruzuku ya kuendeleza ujuzi kwa uratibu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA). Jumla ya wananchi 6,157 (wanawake 2,305 na wanaume 3,852) wamenufaika na mafunzo hayo wakiwemo waathirika wa dawa za kulevya 112 (mwanamke mmoja na wanaume 111). Mafunzo hayo yalitolewa kwa muda wa miezi mitatu.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya uandaaji wa mada za masomo na mitihani unaozingatia umahiri wa ujuzi (*competence-based education*) yalitolewa kwa walimu 100 wa shule za sekondari za Shirika (wanawake 38 na wanaume 62) na kuwezesha ongezeko la ufaulu ambapo wanafunzi wote 91 wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari ya Kibaha walipata daraja la kwanza katika mtihani wa taifa wa mwaka 2022. Aidha, wanafunzi 40 kati ya 157 wa Shule ya Sekondari ya Tumbi ambayo ni ya kutwa (inayopokea wanafunzi kutoka shule za Kata) walipata ufaulu mzuri wa daraja la I-III.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Elimu Kibaha limekarabati Shule ya Sekondari ya Tumbi kwa Shilingi Milioni 200 na ujenzi wa chumba kimoja cha darasa kwa Shilingi Milioni 20, kazi hii imekamilika. Aidha, Shirika limekarabati

Chuo cha Maendeleo ya wananchi Kibaha kwa Shilingi Milioni 350 kati ya Shilingi Milioni 400 iliyopokelewa. Kazi ya ukarabati imefanyika kwa asilimia 88.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 2.67, zikiwemo ruzuku kutoka Serikali Kuu Shilingi Milioni 61.95 na Mapato ya Ndani Shilingi Bilioni 2.61. Hadi Februari, 2023, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imekusanya marejesho ya mikopo na michango jumla ya Shilingi Milioni 333.74 kutoka kwenye Halmashauri zinazodaiwa. Bodi inaendelea kufanya Marekebisho ya Muundo wake na Sheria iliyounda Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

**Shirika la Masoko ya Kariakoo**

195. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 Shirika liliidhinishiwa Shilingi Bilioni 1.89. Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni 893.75 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, Shilingi Milioni 747.54 ni mishahara na Shilingi Milioni 251.3 ni fedha za maendeleo kutoka mapato ya ndani.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2023, Shilingi Milioni 734.43 zimepokelewa kati ya Shilingi Bilioni 1.64 zilizotarajiwa kupokelewa kutoka Serikali Kuu katika kipindi hicho sawa na asilimia 44.7. Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi Milioni 313.11 ni mishahara na Shilingi Milioni 421.32 ni matumizi mengineyo. Kwa upande wa mapato ya ndani, Shilingi Milioni 39.90 zilikusanywa sawa na asilimia 23.81 ya lengo la Shilingi Milioni 167.53 zilizotarajiwa kukusanywa katika kipindi hicho.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa wafanya biashara ambapo jumla ya wafanyabiashara 1,162 kati ya 1,418 wamehakikiwa; kuhuisha

mipaka katika viwanja vya Shirika namba 2002 na 2003 block "G" vilivyopo eneo la Mbezi Beach Makonde na kuhuisha Mpango Mkakati wa Shirika (2021/22 hadi 2025/26).

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/24

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24, yamezingatia Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mipango Mikakati ya Taasisi, Mikoa na Halmashauri; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24; Sheria ya Bajeti, Sura ya 439; Sera za Kisekta; Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo yaliyomo katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

### Ofisi ya Rais – TAMISEMI

199. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kusimamia masuala ya utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

(ii) Kuratibu maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwenye Vijiji 12,318, Mitaa 4,263 na Vitongoji 64,361 katika Halmashauri 184 utakaofanyika mwaka 2024;

(iii) Kuratibu suala la ulinzi na usalama katika Mikoa na Wilaya;

(iv) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya jamii katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa ElimuMsingi na Sekondari katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa ElimuMsingi na Sekondari Bila Ada;

(vii) Kuratibu na kusimamia Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(viii) Kuratibu ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya Barabara, Usafirishaji, Afya ya Msingi, ElimuMsingi na Sekondari na majengo ya utawala katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ix) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

(x) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi shindani kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya uanzishaji wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji hasa katika kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, nyuki, wanyamapori na utalii;

(xi) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

(xii) Kuratibu utaratibu mpya wa utoaji na urejeshwaji wa Mikopo ya asilimia kumi ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xiii) Kuratibu masuala ya michezo na utamaduni katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xiv) Kuratibu usimamizi wa masuala ya uhifadhi na utunzaji wa misitu, wanyamapori, nyuki, vyanzo vya maji, athari za mabadiliko ya Tabianchi pamoja na fursa za mabadiliko hayo kupitia biashara ya kaboni (Hewa Ukaa) na udhibiti wa uzalishaji taka katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xv) Kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zilizo chini yake;

(xvi) Kuendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kusajili vikundi vya ujasiriamali na vikundi vya huduma ndogo za fedha, kuboresha miundombinu ya masoko , ujenzi wa ofisi za machinga na bodaboda pamoja na kuandaa na kutoa mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kupitia utaratibu mpya wa mfumo wa kibenki kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais;

(xvii) Kuratibu Uendelezaji wa Vijiji na Miji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xviii) Kuzisimamia Mamlaka za Upangaji katika kupanga na kuendeleza mipango miji na matumizi endelevu ya ardhi vijijini, ujenzi wa nyumba bora na kudhibiti ujenzi holela, kutunza mipaka ya maeneo ya utawala na kuzuia na kutatua migogoro inayohusu ardhi; na

(xix) Kuratibu uendelezaji wa vijiji na miji kwa utangamano na shughuli za kilimo, uvuvi, mifugo, huduma za maji, umeme, barabara na sekta zingine za uzalishaji na masuala mengine mtambuka.

**Malengo ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI**

200. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 199.19 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zinazoombwa, Shilingi Bilioni 38.65 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni Shilingi Bilioni 10.53 na Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni 28.11. Aidha, jumla ya Shilingi Bilioni 160.53 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 112.12 ni fedha za nje na Shilingi Bilioni 48.41 ni fedha za ndani. Ofisi inapanga kutekeleza shughuli za maendeleo zifuatazo:-

**Ukarabati na Matengenezo ya Ofisi Shilingi 750,000,000.00 (Fedha za Ndani)**

201. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika kutimiza majukumu yake ya kila siku, inamiliki Jengo la Sokoine (Sokoine House) lililopo mkabala na Ofisi ya Jiji la Dodoma. Tangu kukamilika kwa Jengo la Sokoine (Sokoine House) na kuanza kutumika mwaka 2004 hadi sasa jengo hili halijawahi kufanyiwa ukarabati mkubwa. Hivyo, kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24 mradi huu unaomba kuidhinishiwa Shilingi Milioni 750 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya jengo hilo.

**Programu ya Kuimarisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Shilingi 7,860,000,000.00 (Fedha za Ndani)**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekuwa ikitekeleza azma ya kupeleka madaraka kwa umma ili kuwawezesha wananchi kuwa na maamuzi juu ya masuala yanayowahusu kimaendeleo, kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kwa msingi huo, Serikali imeanzisha program ya kuimarisha mafanikio yaliyopo katika ushirikishwaji wa wananchi katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo kuu ni kuendeleza na

kuimarisha huduma za jamii, utawala bora na kuwa na maendeleo endelevu. Mpango huu ulianza kutekelezwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 7.86 kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kuweka mfumo wezeshi wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji na changamoto ambazo zinajitokeza wakati wa utekelezaji wa Maendeleo ya Uchumi wa Maeneo (Local Economic Development (LED FRAME WORK);
(ii) Kuandaa Mwongozo wa utekelezaji wa Maendeleo ya Uchumi wa maeneo (Local Economic Development - LED);
(iii) Kuwezesha Mkakati wa kuzishindanisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato ya ndani zaidi ya ukusanyaji uliopo;
(iv) Kuwawezesha na kuwakutanisha wadau mbalimbali kwa ajili ya kujenga na kuimarisha mahusiano kati ya Serikali Kuu na ngazi za msingi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(v) Kuwezesha kuratibu usimamizi wa Programu ya Kuimarisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa Sera na Mikakati ya Serikali; na
(vi) Kuratibu uidhinishwaji wa Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Mji wa Kibiashara na Uwekezaji Kwala na kuweka Utangamano wa Mji na maneo yanayozunguka Mji huo.

**Mradi wa Ufuatiliaji na Tathmini Shilingi 4,400,000,000.00 (Fedha za Ndani)**

203. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi wa Ufuatiliaji na Tathmini unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 4.40 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yote ya maendeleo ikijumuisha Miradi inayotekelezwa kupitia

fedha za ndani katika ngazi ya OR-TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ukusanyaji na matumizi ya Mapato ya Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kuandaa vikao vya kujadili changamoto zinazotokana na ufuatiliaji na tathmini katika Taasisi, Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi ya maendeleo inayopokea fedha kutoka kwa Washirika na Wadau wa Maendeleo katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mradi wa Mpango wa Kaya Masikini Shilingi 150,000,000.00 (Fedha za Nje)**

204. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kwa mujibu wa Mkataba wa Maelewano (MoU) inasimamia masuala mbalimbali yanayohusu kupunguza umasikini ngazi ya kaya katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Mradi huo unaomba kuidhinishiwa Shilingi Milioni 150 katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24. Ushirikiano huo utahusisha usimamizi wa maeneo yafuatayo:

(i) Kutumia Mtandao Mpana na Mifumo ya TEHAMA ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kupeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Ujazaji wa taarifa za Walengwa wa Mpango wa TASAF katika mfumo wa PSSN kupitia miundombinu ya TEHAMA ya Ofisi ya Rais TAMISEMI; na

(iii) Kutoa msaada wa kiufundi katika miundombinu ya TEHAMA ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa inayotumiwa na PSSN.

**Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (Rise) Shilingi 25,092,570,000 (Fedha Za Nje)**

205. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE) inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 25.09 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri 6 za mradi ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Mbogwe, Handeni, Iringa, Mufindi, Kilolo na Ruangwa; na
(ii) Ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami kilomita 33 katika Halmashauri za Wilaya za Iringa na Mufindi.

**Mradi wa Matengenezo ya Barabara Shilingi 710,316,035,000.00 Chini ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Fedha za Ndani)**

206. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 710.31 kwa ajili ya kazi za miundombinu ya Barabara. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 257.03 ni za Mfuko wa Barabara; Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi Bilioni 127.50 na tozo ya mafuta ya Shilingi 100 kwa lita Shilingi Bilioni 325.77. Fedha hizo zitatumika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Utunzaji (Matengenezo) wa barabara za Vijijini na Mijini zenye urefu wa kilomita 21,109.70;
(ii) Ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 348.7;
(iii) Ujenzi wa barabara za changarawe urefu wa kilomita 8,528.72;
(iv) Ujenzi wa madaraja 231 na ukarabati wa madaraja 35;
(v) Ujenzi na matengenezo ya boksi kalavati 170 na vivuko (drifti) 30; na
(vi) Ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 85,700.20.

**Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi Katika Miji Tanzania (Tanzania Cities Transforming and Competitiveness – TACTIC) Shilingi 35,176,500,000.00 (Fedha za Nje)**

207. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 35.17 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa miundombinu msingi ya Mijini katika Halmashauri 12 ambazo ni Halmashauri za Majiji ya Dodoma, Arusha, Mwanza na Mbeya; Halmashauri za Manispaa ya Kigoma, Songea, Ilemela, Kahama, Morogoro, Sumbawanga na Tabora na Halmashauri ya Mji Geita. Miundombinu msingi inajumuisha ujenzi wa masoko, mitaro ya maji ya mvua, stendi za mabasi na maghala ya kuhifadhia mazao;
(ii) Kuendelea na usanifu wa miradi katika Miji 33 iliyobakia; na
(iii) Kuandaa nyaraka mbalimbali za tathmini ya kimazingira ili kuwezesha miradi kupata vibali vya kuanza utekelezaji wa mradi.

**Programu ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi Shilingi 47,441,373,000.00 (Fedha za Nje)**

208. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi wa Uboreshaji wa Bonde la Mto Msimbazi unaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 47.44 kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Maandalizi ya ujenzi wa daraja la Bonde la Mto Msimbazi;
(ii) Maandalizi ya kuanza ujenzi wa kingo za Bonde la Mto Msimbazi; na
(iii) Kupanda miti ya aina mbalimbali kwenye chanzo cha Mto Msimbazi ili kuzuia mmomonyoko.

**Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP - II) Shilingi 465,220,000.00 (Fedha za Nje)**

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu inaombewa Shilingi Milioni 465.22 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuratibu mikutano ya pamoja ya utekelezaji wa maendeleo ya programu ya ASDP II kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta;
(ii) Kuwezesha maandalizi ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo katika Mikoa 12 na Halmshauri 30;
(iii) Kushiriki mikutano ya kisheria ya utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo ya Kilimo (ASDP II);
(iv) Kuwezesha mafunzo ya uongozi na usimamizi katika kutekeleza afua za Mipango ya Maendeleo ya Kilimo awamu ya Pili;
(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo - ASDP II kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau wengine;
(vi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa ASDP II kwenye Halmashauri 184;
(vii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa kuendeleza Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Wilaya (DADPs) na kuandaa taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka; na
(viii) Kuandaa taarifa jumuishi za utendaji wa Program za kila robo.

**Mpango wa Kuratibu Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi Shilingi 63,317,700.00 (Fedha za Nje)**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 Mpango huu unaombewa kuidhinishiwa Shilingi Milioni 63.31 kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuibua miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Halmashauri 3 zinazotekeleza mradi ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Kondoa, Mpwapwa na Chamwino;
(ii) Uandaaji wa mipango na bajeti kwa Halmashauri zinazotekeleza mradi ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Kondoa, Mpwapwa na Chamwino;
(iii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika Halmashauri zinazotekeleza mradi;
(iv) Kufanya vikao vya Kamati Tendaji ya Mradi; na
(v) Kuendelea na mchakato wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupata ithibati (accreditation) ya Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund - GCF)

**Ukarabati wa Miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha Shilingi 700,000,000.00 (Fedha za Ndani)**

211. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha (Kibaha Folk Development College) kilianzishwa mnamo mwaka 1964 kikiwa kinajulikana kama "Farmers Training Centre" chini ya Mradi wa pamoja wa Serikali ya Tanganyika na Nchi za Nordic uitwao *Tanganyika Nordic Project*. Baada ya Mradi huu kukabidhiwa kwa Serikali ya Tanzania mnamo mwaka 1970 jina la mradi lilibadilishwa na kuitwa Shirika la Elimu Kibaha (Kibaha Education Centre). Majengo ya Chuo hiki yamechakaa na yameezekwa kwa *asbestos* ambayo siyo rafiki kwa afya ya binadamu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Shirika lilipokea Shilingi Milioni 400 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Chuo. Ukarabati umefanyika kwa baadhi ya majengo na kazi ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi

Milioni 700 ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo; -

(i) Kukarabati mabweni 4; Mwongozo (wanafunzi 80), Uhuru (wanafunzi 80), Ujamaa (wanafunzi 80) na Twiga (wanafunzi 80);
(ii) Kukarabati ukumbi wa Twiga unaotumika kama darasa unaochukua wanafunzi 506;
(iii) Kukarabati mifumo ya maji safi na maji taka;
(iv) Kukarabati choo cha nje chenye matundu 5; na
(v) Kukarabati Shamba Darasa la Mifugo na Mazao.

**Programu ya Uboreshaji Katika Sekta ya Fedha Awamu ya Tano (PFMRP V) Shilingi 1,000,000,000.00 (Fedha za Ndani)**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 1 ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo; -

(i) Kusimamia Ufungaji wa Hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii) Kupitia na kuhuisha mahitaji ya Mfumo wa TAUSI baada ya kuanza matumizi;
(iii) Kuandaa miongozo ya matumizi ya Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato wa TAUSI pamoja na mikataba ya mawakala; na
(iv) Kutengeneza kanuni za Sheria ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura ya 290.

**Mradi wa Mpango wa Kaya Maskini Shilingi 150,000,000.00 (Fedha za Nje)**

213. ***Mheshimiwa* Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi wa Mpango wa Kaya Maskini unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Milioni 150 kwa ajili ya kufanya

ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa na TASAF katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mradi wa Usafi wa Mazingira (SRWSS): Shilingi 333,175,350.00 (Fedha za Nje)**

214. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Milioni 333.17 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo;

(i) Kufanya usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa huduma endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Mikoa 17 na Halmashauri za Wilaya 86; na
(ii) Kufanya vikao mbalimbali vinavyohusu Kampeni ya Usafi wa Mazingira.

**Programu ya Uhamasishaji na Uchambuzi wa Sera (UNICEF) Shilingi 609,110,079.00 (Fedha za Nje)**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu inaombewa kuidhinishiwa Shilingi Milioni 609.11 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu zinazohusiana na uboreshaji wa huduma kwa jamii katika Mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe na Iringa;
(ii) Kufanya vikao vya wadau kuhusiana na shughuli zinazotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe na Iringa; na
(iii) Kuimarisha Mfumo wa Uratibu, Usimamizi na Ufuatiliaji wa shughuli zinazotekelezwa na Wadau mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe na Iringa.

**Mradi wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (Primary Student Learning - BOOST) Shilingi 20,259,163,825.00 (Fedha za Nje)**

216. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Programu ya Kuimarisha Ujifunzaji wa Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 20.25 kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kununua na kusambaza vifaa vya TEHAMA katika Shule za Msingi 200 ili kuboresha ujifunzaji wa wanafunzi na Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA);
(ii) Kutekeleza Mpango wa Shule Salama kwenye Shule za Msingi 2,500;
(iii) Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia Elimu ya Awali kwenye Shule za Msingi 3,000 na kutoa mafunzo kwa walimu wa Elimu ya Awali;
(iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmnini ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 4,730 na matundu ya vyoo 3,010; Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA); uandikishaji wa wanafunzi; ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Awali na Msingi katika Halmashauri 184;
(v) Kuhabarisha umma kuhusu shughuli za Uimarishaji wa Ujifunzaji wa Elimu ya Awali na Msingi kwa kutumia vyombo vya habari ikiwemo luninga, redio, mitandao ya kijamii na machapisho;
(vi) Kujenga uwezo wa kusimamia utekelezaji wa Mitaala kwa elimu ya awali na msingi na utawala bora katika utoaji wa elimu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(vii) Kuimarisha Mifumo ya kukusanya, kuhifadhi na kutumia Takwimu za Elimu (EMIS);
(viii) Kujenga uwezo wa wataalam wa Serikali katika kukusanya, kuchambua na kutumia takwimu mbalimbali za elimu ya awali na msingi; na
(ix) Kusimamia utekelezaji wa vipaumbele vya mradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

**Mradi wa Uimarishaji wa Ufundishaji na Ujifunzaji (GPE-LANES II): Shilingi 1,000,0000,000.00 (fedha za nje)**

217. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi unaombewa kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 1** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo;

(i) Kuandaa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wapya wanaoajiriwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii) Kuandaa Kihunzi cha Walimu wanaojitolea;
(iii) Kuwezesha kufanyika kwa vikao vinavyohusu utekelezaji wa Walimu wanaojitolea;
(iv) Kufanya uchambuzi wa hali ya ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya shule;
(v) Kuwezesha Ofisi ya Uratibu wa Mradi; na
(vi) Kuwezesha utangazaji wa utekelezaji wa shughuli za Mradi; na
(vii) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini.

**Programu ya Elimumsingi Bila Malipo – Ununuzi wa Vitabu Shule za Msingi Shilingi 17,200,000,000.00 (Fedha za Ndani)**

218. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 programu inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 17.20 kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa vitabu vya Shule za Msingi kupitia Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo.

**Programu ya Kuboresha Elimu Katika Shule za Sekondari (SEQUIP) Shilingi 25,346,770,000.00 (Fedha za Nje)**

219. ***Mheshimiwa* Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 25.34 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kununua vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya shule mpya 234 za sekondari za Kata zinazojengwa katika Halmashauri;
(ii) Kununua vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shule 1,000 za Sekondari za Kata kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;
(iii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi katika maeneo ya ujenzi wa shule mpya za sekondari;
(iv) Kuwezesha utendaji kazi wa ofisi ya Rais – TAMISEMI katika utekelezaji wa mradi wa kuboresha Elimu ya Sekondari;
(v) Kuwezesha utangazaji wa shughuli zinazotekelezwa na mradi wa kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) kwa wananchi ili waweze kufahamu jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuboresha elimu ya sekondari nchini; na
(vi) Kuwezesha kuwajengea uwezo watumishi 68 wa idara ya usimamizi wa elimu katika masuala yahusuyo ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

**Programu ya Elimumsingi Bila Malipo – Ununuzi wa Vitabu Shule za Sekondari Shilingi 17,200,000,000.00 (Fedha za Ndani)**

220. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, programu inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 17.20 kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa vitabu vya Shule za Sekondari kupitia Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo.

**Mradi wa Usafi wa Mazingira (SRWSS): Shilingi 740,965,500.00 (Fedha za Nje)**

221. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi unaombewa kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Milioni 740.96** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo;

(i) Kufanya usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa huduma endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Mikoa 17 na Halmashauri za Wilaya 86; na
(ii) Kufanya vikao mbalimbali vinavyohusu Kampeni ya Usafi wa mazingira.

**Programu ya Uhamasishaji na Uchambuzi wa Sera- (UNICEF) Shilingi 3,000,000,000.00 (Fedha za Nje).**

222. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 3 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwezesha usimamizi shirikishi wa shughuli za ulinzi wa mtoto na ukatili wa wanawake katika Mikoa 26 na Halmashauri 184;
(ii) Kufanya maandalizi ya awali ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2024/25 kwa ajili ya ulinzi na usalama wa mtoto pamoja na masuala ya lishe;
(iii) Kufanya Mkutano wa Wadau mara mbili kwa mwaka na kufanya mapitio ya Sheria zinazohusu ulinzi wa mtoto na ukatili kwa wanawake;
(iv) Kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto walio chini ya miaka 5 kwa Mikoa 23 inayofadhiliwa na programu ya UNICEF;
(v) Kuratibu na kufanya Mkutano na Makatibu Tawala wa mikoa 8 na Halmashuri 29 kuhusu utekelezaji wa masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto;
(vi) Kufanya mafunzo kwa wataalam wa Ustawi wa Jamii namna ya kutoa huduma ya Kisaikolojia na kijamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(vii) Kuwajengea uwezo Maafisa Ustawi wa Jamii katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

katika masuala ya ulinzi wa mtoto na ukatili kwa wanawake;

(viii) Kujenga uelewa kwa Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusu masuala ya ulinzi wa mtoto na ukatili kwa wanawake;

(ix) Kufanya usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa masuala ya UKIMWI na mtoto kwa Mikoa inayofadhiliwa na Program ya UNICEF;

(x) Kufanya kikao cha utekelezaji wa mradi wa M-mama;

(xi) Kutoa mafunzo kwa kamati za RCCE (Risk Communication and Community Engagement) za Halmashauri na Mikoa;

(xii) Kufanya Mkutano wa mwaka wa tathmini ya Utekelezaji wa mkataba wa lishe ngazi ya Taifa; na

(xiii) Kufanya Mapitio ya Utekelezaji wa mkataba wa lishe ngazi ya Taifa kabla ya Mkutano Mkuu wa tathmini ya utekelezaji wa lishe ngazi ya Taifa.

**Mradi wa Kuimarisha Huduma za Rufaa na Ubora wa Huduma za Afya ya Msingi Shilingi 44,895,193,483.00 (Fedha za Nje)**

223. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 44.89 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya upembuzi yakinifu katika vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi ili kubainisha mahitaji ya ujenzi na ukarabati;

(ii) Kutoa ajira ya mkataba kwa watumishi 300;

(iii) Utoaji wa huduma ya rufaa kwa mama na mtoto; na

(iv) Kufanya ufuatiliaji katika vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi.

**Mfuko wa Pamoja wa Afya Shilingi 1,644,564,000.00 (Fedha za Nje)**

224. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mfuko wa Pamoja wa Afya unaombewa

kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 1.64 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa wajumbe 30 wa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa (RHMT) kuhusu namna ya kutathmini na kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri (CCHP);
(ii) Kuandaa mitaala kwa ajili ya mafunzo kwa wataalamu wa Radiologia;
(iii) Kutoa mafunzo kwa wataalamu wa Radiologia kwa lengo la kuimarisha huduma za mionzi;
(iv) kutoa mafunzo kwa wataalamu wa usingizi watakaopangiwa katika vituo vya kutolea huduma vinavyoendelea kujengwa;
(v) Kuandaa, kuchambua na kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya robo mwaka kwenye ngazi ya Halmashauri pamoja na vituo vya kutolea huduma ya afyamsingi;
(vi) Kufanya kikao cha pamoja cha robo mwaka cha kuboresha utendaji kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Halmashauri 184;
(vii) Kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Pamoja wa Afya katika ngazi za Mikoa na Halmashauri;
(viii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Mfuko wa Pamoja wa Afya katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;
(ix) Kufanya mkutano wa waganga wafawidhi, waganga wakuu, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii;
(x) Kufanya ufuatiliaji, usimamizi na tathmini ya magonjwa ya mlipuko na majanga katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri;

**Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Utoaji wa Huduma za Chanjo Shilingi 200,000,000.00 - (Fedha za Nje)**

225. ***Mheshimiwa* Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaomba kuidhinishiwa Shilingi Milioni 200 kupitia Progamu ya Kuimarisha Mifumo ya Utoaji wa Huduma za Chanjo (GAVI) kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Kuratibu na kusimamia huduma za chanjo katika ngazi ya Wizara, Mikoa 26, Halmashauri 184 pamoja na vituo vya kutolea huduma za afya;
(ii) Kuongeza uwezo wa Halmashauri katika kutunza na kuhifadhi chanjo kwa kununua, kusambaza pamoja na kukarabati majokofu ya kuhifadhia chanjo; na
(iii) Kuwezesha huduma za chanjo kufikia jamii kwa kutoa huduma za Mkoba na Kliniki tembezi.

**Programu ya Kuboresha Chakula na Lishe kwa ajili ya Kuboresha Afya kwa Watoto Wanaoishi Kwenye Mazingira Hatarishi Pamoja na Wanawake (WPP & NI) Shilingi 158,481,653.00 - (Fedha za Nje)**

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Program ya kuboresha chakula na Lishe, inaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Milioni 158.48 kwa ajili ya kazi zifuatazo: -

(i) Kuboresha huduma ya utoaji wa matone ya Vitamini kwa watoto kwenye Halmashauri 58 zilizoko katika Mikoa 12 ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Manyara, Katavi na Simiyu;
(ii) Kuongeza madini joto kwenye chumvi inayozalishwa nchini (Universal Salt Iodization – USI); na
(iii) Kuboresha afya na lishe ya Mama, Watoto wachanga na vijana balehe kwenye Halmashauri 58 zilizopo katika Mikoa 12.

**Programu ya Kuimarisha Mifumo ya Afya (UNFPA) Shilingi 654,282,900.00 (Fedha za Nje)**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Programu ya Kuimarisha Mifumo ya Afya inaombewa kuidhinishwa jumla ya Shilingi Milioni 654.28 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kufanya ufuatiliaji kwenye ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya inayojengwa katika Mikoa ya mradi ambayo ni Mwanza, Geita, Shinyanga, Kagera, Simiyu, Dodoma, Kagera, Kigoma na Mara; na
(ii) Kufanya mafunzo kuhusu matumizi ya dawa mbalimbali zinazotolewa katika mikoa inayotekeleza mradi.

**Mradi wa Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko na Matukio Yenye Athari ya Usalama wa Afya ya Jamii (GHSA- CDC) Shilingi 3,750,703,692.00 (Fedha za Nje)**

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mradi wa Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko na Matukio yenye Athari ya Usalama wa Afya ya Jamii unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 3.75 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kuratibu na Kufatilia magonjwa ya mlipuko katika Mikoa na Halmashauri;
(ii) Kufanya usimamizi shirikishi wa shughuli za udhibiti wa magonjwa ya mlipuko na matukio yenye athari ya kiafya katika jamii; na
(iii) Kuimarisha uendeshaji wa vituo vya uratibu wa dharura katika mikoa sita (6) ya Dar es Salaam, Mwanza, Kagera, Kigoma, Arusha na Kilimanjaro.

**Programu ya Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund) Shilingi 8,708,942,818.00 (Fedha za Nje)**

229. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria unaombewa kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni 8.70 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kufanya mafunzo kazini na usimamizi shirikishi kwa shughuli za Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 38 .
(ii) Kufanya vikao 2 vya uratibu wa shughuli za Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria ikijumuisha waratibu wa mikoa wa UKIMWI na wadau mbalimbali;
(iii) Kufanya usimamizi saidizi kwa kamati za afya za Mikoa na Halmashauri (RHMT&CHMT) katika utekelezaji wa Afua za UKIMWI;
(iv) Kufanya ukaguzi wa fedha za Mfuko wa Dunia wa kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria mara moja kwa mwaka katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa 12 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 38;
(v) Kufanya usimamizi saidizi katika Mikoa 15 na Halmashauri 108 katika utekelezaji wa programu ya kifua kikuu;
(vi) Kufanya ufuatiliaji na usimamizi shirikishi kuhusu afya ya jamii na ustawi wa jamii kwenye Halmashauri 42;
(vii) Kufanya vikao na mafunzo kazini kwenye Halmashauri 109 kuhusu matumizi na usimamizi wa "force account" katika ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya;
(viii) Kuwezesha usimikaji wa miundombinu ya TEHAMA kwenye hospitali 33 za Wilaya kati ya 176;
(ix) Kuwezesha Hospitali za Halmashauri 33 kufanya maboresho ya mfumo wa GoTHOMIS ili kuweza kukusanya taarifa za vifaa tiba;
(x) Kufanya mafunzo kazini na usimamizi shirikishi kwa shughuli za Mfuko wa Dunia wa kupambana na

UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(xi) Kufanya ufuatiliaji wa mifumo ya taarifa za afya kwenye Mikoa na Halmashauri (GOTHOMIS, HRHIS, FFARS, HMIS, MVC-MIS).

## E. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS - TAMISEMI

**Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

230. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini inaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 855.37 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 37.35 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni 818.02 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo zinazoombwa Shilingi Bilioni 710.31 ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni 107.71 ni fedha za nje.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Matengenezo ya barabara kilomita 21,109.7 kupitia Mfuko wa Barabara;

(ii) Ujenzi wa kilomita 190.13 kwa kiwango cha lami, kilomita 5,986 za changarawe, madaraja 107, kalavati 185, mistari ya kalavati 949 na mifereji ya maji ya mvua kilomita 18.44 kupitia fedha za tozo ya Shilingi 100 ya mafuta ya dizeli na petroli; na

(iii) Ujenzi wa kilomita 110.48 kwa kiwango cha lami, kilomita 2,663.97 za changarawe, madaraja 61, kalavati 132, mitaro ya maji ya mvua mita 9,696 na drifti mbili (2) kupitia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** TARURA kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imepanga kutekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Ujenzi wa barabara kupitia Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE) ambapo barabara zenye urefu wa kilomita 33 zitajengwa kwa kiwango cha lami; usanifu wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 159.05; usanifu wa vikwazo vya miundombinu ya barabara kwa Mikoa 25; maandalizi ya kupata wataalam washauri na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara; kuanza utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri 6 za mradi (Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, Handeni, Iringa, Mufindi, Kilolo na Rungwe);

(ii) Kulipia wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi; ujenzi wa daraja, kingo katika Bonde la Mto Msimbazi na kupanda miti ya aina mbalimbali kwenye chanzo cha Mto Msimbazi ili kuzuia mmomonyoko kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi;

(iii) Kuanza ujenzi wa miundombinu ya msingi ya miji 12 kati ya 45 kupitia Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania (TACTIC) ambapo itahusisha ujenzi wa masoko, mitaro ya maji ya mvua, stendi za mabasi na maghala ya kuhifadhia mazao; Kuendelea na usanifu wa miradi katika Miji 33 iliyobakia; na Kuandaa nyaraka mbalimbali za kimazingira; na

(iv) Ujenzi wa barabara za kiwango cha lami zenye jumla ya urefu wa kilomita 43.82 katika Halmashauri za Wilaya za Wanging'ombe kilomita 19.3, Mbozi kilomita 11.01, Rungwe kilomita 6, Busokelo kilomita 6.41 na Kilolo kilomita 1.1 kupitia Mradi wa Agri-connect awamu ya pili unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya. Aidha, kuanzia Mwaka wa Fedha wa

2022/23 Mikataba yote ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zinahusisha uwekaji wa taa za barabarani.

**Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka inaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 3.03 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 2.30 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Milioni 731.21 ni kwa Matumizi Mengineyo.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuongeza Mtandao wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuendelea na Miundombinu ya Awamu ya Tatu itakayohusisha Barabara zenye urefu wa kilomita 20.6 za Nyerere (Gongolamboto - Posta kupitia Sokoine), Uhuru (Buguruni - Kariakoo Terminal kupitia Mtaa wa Shaurimoyo na Lindi) na Shaurimoyo (Nyerere - Lindi);

(ii) Kukamilisha taratibu za ununuzi wa Mtoa Huduma za mabasi ya Awamu ya Kwanza na ya Pili;

(iii) Kufanya ukarabati wa mara kwa mara wa miundombinu ya Mradi;

(iv) Kuboresha usafi wa mazingira katika mtandao wa wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka;

(v) Kudumisha usalama kwa kuimarisha ulinzi katika Mtandao wa Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART);

(vi) Kuendelea na taratibu za kubadilisha mfumo wa uendeshaji na ulipaji wa Watoa Huduma kutoka kupokea tozo kupita katika mfumo wa DART (Access Fee) na kuanza kutumia utaratibu wa malipo ya umbali wa mabasi yatakayokuwa yanatembea (per km mode);

(vii) Kukamilisha utengenezaji na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli (Automated Fare Collection System-AFCS) wa Serikali unaosimamiwa na DART ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongozea Magari (Intelligent Transport System-ITS) ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio mijini, na pia kuondoa mianya ya upotevu wa mapato ya nauli kwenye mfumo;

(viii) Kuendelea kubuni na kuongeza vyanzo vipya vya mapato yasiyotokana na nauli (*Non-Fare Tarriff Revenue*) ili kujenga uwezo wa kujitegemea kimapato na kuongeza uwezo wa Wakala kuwa endelevu katika utekelezaji wa majukumu yake; na

(ix) Kuendelea kufanya mapitio ya Amri ya Uanzishwaji wa Wakala ya Mwaka 2006 (*Review DART Agency Establishment Order*).

**Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Namba 02)**

235. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Tume ya Utumishi wa Walimu inaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 17.20 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 8.81 ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi Bilioni 7.71 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi Milioni 670 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea kusimamia Utumishi na maendeleo ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kuendesha mashauri ya nidhamu kwa Walimu ngazi ya Wilaya;

(iii) Kuendesha rufaa za Walimu waliokata rufaa ngazi ya Tume Makao Makuu;

(iv) Kuwapandisha vyeo Walimu wenye sifa kwa wakati baada ya kupata vibali kutoka kwenye Mamlaka husika;

(v) Kuwabadilisha vyeo Walimu baada ya kujiendeleza,

(vi) Kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume Makao Makuu;

(vii) Kuimarisha mfumo wa Kielektroniki (Teachers Service Management Information System-TSC-MIS);

(viii) Kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wa Tume na

(ix) Kuongeza uelewa wa wadau kuhusu kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu.

**Chuo cha Serikali za Mitaa**

237. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kinaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 6.37 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 6.02 ni kwa ajili ya

Mishahara na Shilingi Milioni 349.30 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Chuo cha Serikali za Mitaa kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kudahili wanafunzi wapya 9,500 kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Shahada ya Kwanza;
(ii) Kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala mbalimbali yahusuyo Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(iii) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Watumishi na Viongozi waliopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wadau kutoka maeneo mbalimbali;
(iv) Kuhuisha na kuandaa mitaala ili kuendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye;
(v) Kuanzisha Kampasi ya Shinyanga, na
(vi) Kuanza ujenzi wa jengo la Utawala Awamu ya Kwanza katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

**Shirika la Elimu Kibaha**

238. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Shirika la Elimu Kibaha linaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 8.58 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 7.88 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi Bilioni 5.99 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni 1.89 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Shilingi Milioni 700 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya ndani.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa ElimuMsingi kwa wanafunzi 2,703 na elimu ya Sekondari kwa wanafunzi 357;
(ii) Kuandaa na kusimamia mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao (*e-learning management system*) na

kutoa Elimu ya Sekondari mubashara *(Live teaching)* kwa shule za sekondari Tanzania;

(iii) Kuboresha utoaji wa elimu kwa wahudumu wa afya 572 katika fani ya utabibu na uuguzi kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha (KCOHAS), sambamba na kutoa elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi 500;

(iv) Kutoa elimu na mafunzo ya stadi mbalimbali za ujuzi na ubunifu katika fani kwa vijana 400 kwa kozi za muda mrefu na wananchi 1,000 kwa kozi za muda mfupi kwa mafunzo ya ana kwa ana na kwa njia ya mtandao (*e-learning*);

(v) Kuendelea na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha sambamba; na

(vi) Kuboresha miundombinu ya mashamba darasa ya kilimo na mifugo.

**Shirika la Masoko ya Kariakoo**

240. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Shirika la Masoko ya Kariakoo inaomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 1.68 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi Milioni 747.54 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Milioni 938.44 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Shirika litaendelea na ujenzi wa soko jipya na ukarabati wa soko lililoungua unaotarajiwa kukamilika Oktoba, 2023. Aidha, Shirika litaandaa Mpango wa Uwekezaji katika maeneo yanayomilikiwa na Shirika yaliyopo Mbezi Beach Makonde katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na Tabata Bima katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

241. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa inaomba kuidhinishiwa Shilingi Milioni 365.04 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bodi itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kukusanya marejesho ya Mikopo, makusanyo ya Michango kutoka kwenye Halmashauri na mapato mengine ya ndani ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 4.13 kinatarajiwa kukusanywa;
(ii) Kutoa Mikopo kwa Halmashauri yenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.96 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo;
(iii) Kukamilisha Maboresho ya Muundo wa Bodi ili kuiwezesha Bodi kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Sheria;
(iv) Kukamilisha Marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Bodi ili iendane na mabadiliko ya kisera na kiuchumi na mahitaji ya Halmashauri zetu;
(v) Kuendelea kutoa huduma ya kitaalam ya kuandaa maandiko ya miradi katika Halmashauri; na
(vi) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Bodi kuhusu uchambuzi wa maandiko ya miradi, utoaji na usimamizi wa mikopo na ufuatiliaji wa mikopo.

## F. MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI WA OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KATIKA MWAKA WA FEDHA WA 2023/24

242. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itazingatia mambo yafuatayo: -

### Mapato ya Ndani

243. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Halmashauri na Taasisi zilizo

chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI zimepanga kukusanya maduhuli na mapato ya ndani yenye jumla ya Shilingi Trilioni 1.19. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 55.14 zimepangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Shilingi Milioni 261.89 zitakusanywa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Shilingi Trilioni 1.14 zitakusanywa na Halmashauri.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa makusanyo ya Halmashauri, Shilingi Bilioni 689.46 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi Bilioni 454.41 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo huu, unatokana na madaraja ya Halmashauri ya kuchangia shughuli za maendeleo kutokana na mapato ya ndani kwa asilimia 70, 60, 40 na 20 *(Kiambatisho Namba 11)*.

**Sekta ya Elimu**

(i) Kuendelea kugharamia elimu bila ada kwa shule za msingi na sekondari ambapo Shilingi Bilioni 399.64 zimetengwa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 157.79 zimetengwa kwa ajili ya shule za msingi na Shilingi Bilioni 241.85 zimetengwa kwa ajili ya shule za sekondari. Bajeti hiyo ni sawa na ongezeko la Shilingi Bilioni 53.15 sawa na asilimia 15.34 ikilinganishwa na bajeti ya Shilingi Bilioni 346.49 iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, ongezeko hili linatokana na wanafunzi wa kidato cha tano na sita kujumuishwa katika Mpango wa Elimu Bila Ada *(Kiambatisho Namba 13);*

(ii) Kuendelea na mpango wa ujenzi wa matundu ya vyoo katika vituo shikizi ambapo Shilingi Bilioni 5.74 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa matundu 5,218 ya vyoo. Aidha, zimetengwa Shilingi Bilioni 5.52 kwa ajili ya ujenzi wa matundu 5,020 ya vyoo kwa kidato cha tano na sita kwa shule za sekondari *(Kiambatisho Namba 14);*

(iii) Ujenzi wa mabweni 61 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo Shilingi Bilioni 7.86 zimetengwa. Aidha,

zimetengwa Shilingi Bilioni 2.58 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa uzio wa mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum *(Kiambatisho Namba 14);*

(iv) Ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kidato cha tano na sita kwa shule za sekondari ambapo Shilingi Bilioni 47.89 zimetengwa *(Kiambatisho Namba 14);*

(v) Kuendelea na mpango wa ukarabati wa shule kongwe za msingi na sekondari ambapo Shilingi Bilioni 37.49 zimetengwa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 33.12 ni kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe 184 za msingi na Shilingi Bilioni 4.37 ni kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za sekondari (*Kiambatisho Namba 15);*

(vi) Usimamizi wa mitihani ambapo Shilingi Bilioni 243.61 zimetengwa (*Kiambatisho Namba 16)*.

**Sekta ya Afya**

(i) Kuendelea na ujenzi wa hospitali 41 za Halmashauri ambapo Shilingi Bilioni 30.29 zimetengwa (*Kiambatisho Namba 17);*
(ii) Kuendelea na mpango wa ukarabati wa hospitali kongwe za Halmashauri 31 ambapo Shilingi Bilioni 27.9 zimetengwa (*Kiambatisho Namba 17);*
(iii) Ujenzi wa vituo vya afya 16 na ukamilishaji wa vituo vya afya 6 ambapo Shilingi Bilioni 9.54 zimetengwa (*Kiambatisho Namba 17)*;
(iv) Kuendelea na mpango wa ukamilishaji wa zahanati 376 katika Halmashauri ambapo Shilingi Bilioni 18.80 zimetengwa (*Kiambatisho Namba 17)*, na
(v) Ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika hospitali za Halmashauri, vituo vya afya na zahanati, ambapo Shilingi Bilioni 116.92 zimetengwa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 15.50 zitatumika kununua vifaa na vifaa tiba katika hospitali 31, Shilingi Bilioni 83.07 kwa ajili ya

vituo vya afya 278 na Shilingi Bilioni 18.35 kwa ajili ya zahanati 364 (*Kiambatisho Namba 18)*.

**Majengo ya Utawala na Nyumba za Viongozi**

(i) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati Ofisi za Wakuu wa Mikoa 16 ambapo Shilingi Bilioni 7.84 zimetengwa;

(ii) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya 28 ambapo Shilingi Bilioni 8.93 zimetengwa;

(iii) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Ikulu Ndogo 8 ambapo Shilingi Bilioni 1.61 zimetengwa;

(iv) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba 11 za Wakuu wa Mikoa ambapo Shilingi Bilioni 1.52 zimetengwa;

(v) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba 4 za Makatibu Tawala wa Mikoa ambapo Shilingi Milioni 723.72 zimetengwa;

(vi) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za Maafisa Tarafa 7 kwa gharama ya Shilingi Milioni 560;

(vii) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa 13 ambapo Shilingi Bilioni 1.44 zimetengwa;

(viii) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya 4 ambapo Shilingi Milioni 435, zimetengwa;

(ix) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Wilaya 16 ambapo Shilingi Bilioni 2.56 zimetengwa; na

(x) Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Ofisi za Maafisa Tarafa 31 ambapo Shilingi Bilioni 3.24 zimetengwa.

## Majengo ya Utawala ya Halmashauri

245. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa Shilingi Bilioni 49.32 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri *71*. Aidha, Shilingi Bilioni 14.70 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika Halmashauri 50 (*Kiambatisho Namba 19)*.

## Nyumba za Wakurugenzi na Nyumba za Wakuu wa Idara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

246. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa Shilingi Bilioni 15.25 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Wakuu wa Idara. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 6.63 ni kwa ajili ya nyumba 35 za Wakurugenzi wa Halmashauri na Shilingi Bilioni 8.62 ni kwa ajili ya nyumba 25 za Wakuu wa Idara (*Kiambatisho Namba 19)*.

## Miradi ya Kimkakati

247. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa Shilingi Bilioni 26.98 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi 18 ya kimkakati katika Halmashauri. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inaboresha vigezo vya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kwa Halmashauri (*Kiambatisho Namba 20)*.

## Ununuzi wa Boti

248. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa Shilingi Bilioni 1.5 kwa ajili ya ununuzi wa boti 4 katika Halmashauri za Wilaya za

Ludewa, Buchosa, Nyasa na Sumbawanga ili kuimarisha doria, ulinzi na ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Halmashauri hizo.

**Ununuzi wa Magari**

249. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa Shilingi Bilioni 16.58 kwa ajili ya ununuzi wa magari 81 katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Kati ya magari hayo, magari 5 ni ya Wakuu wa Mikoa, magari 2 ni ya Makatibu Tawala wa Mikoa na magari 74 ni ya Wakuu wa Wilaya.

**Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo**

250. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetengewa Shilingi Bilioni 15.99 kwa ajili ya kuchochea maendeleo katika majimbo 214 ya Tanzania Bara.

**Uendelezaji wa Vijiji na Miji**

251. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali itaziimarisha taasisi za kijamii kwenye ngazi za msingi ziwe utangamano ili zilete tija na kuinua ustawi wa jamii kwa utaratibu maalum utakao kuwa jumuishi. Lengo ni kuleta mageuzi *(transformation)* yatakayo kuwa na tija katika Uendelezaji wa Vijiji nchini. Mambo yatayozingatiwa ni utangamano katika maendeleo ya Vijiji na Miji ikiwemo Miji Midogo Inayochipukia; Kuimarisha taasisi za kijamii kwenye ngazi za msingi katika kujenga Uchumi Mahalia; Aidha, kuimarisha ufikishaji sawia wa huduma za umma kwa wananchi walio wengi; Utunzaji wa mazingira na kuendeleza biashara ya Hewa Ukaa kwenye Vijiji. Pia kujenga uwezo na kuratibu utunzaji na matumizi ya raslimali; utalii na mila asilia

*(Cultural Values)* zilizoko Vijijini; Vilevile, kuimarisha Hatimiliki kwa usawa wa kijinsia na; Kusimamia uendelezaji wa Mipango Kabambe na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Vijijini pamoja na kusimamia vyema mipango ya uchumi ya Halmashauri.

252. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaendelea na utekelezaji wa Uanzishwaji, Upangaji na Uendelezaji wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji Kwala, Mkoa wa Pwani kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Ikulu; Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na Wizara za Kisekta, ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi – Uchukuzi; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Maji; Wizara ya Nishati; na Wizara inayohusu Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani; Halmashauri za Wilaya za Kibaha, Chalinze na Kisarawe pamoja na Taasisi nyingine za umma na Sekta Binafsi. Eneo la Mpango lina ukubwa wa hekta 130,831 na limetangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 633 la tarehe 28 Oktoba, 2022. Mpango Kabambe Jumuishi wa Jiji hilo wa Mwaka 2022 – 2050 utaendelea kukamilishwa na unajumuisha Vijiji 30 vya Halmashauri za Wilaya ya Kibaha (16), Chalinze (9) na Kisarawe (5).

**Uendelezaji wa Ardhi**

253. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Taasisi na wadau wengine inatekeleza Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Halmashauri 55 zilipata mkopo wa jumla ya Shilingi Bilioni 49.47. Mradi wa KKK ambao unalenga kuboresha utoaji wa huduma za ardhi umeleta mafanikio makubwa ya kuwezesha kupima jumla ya viwanja 232,537 sawa na asilimia 91.73 kati ya lengo la viwanja 253,500 na hivyo kusaidia kupunguza tatizo la uendelezaji holela wa ardhi kwenye maeneo ya miji

husika. Hadi Februari 2023, jumla ya Shilingi Bilioni 16.75 sawa na asilimia 33.85 ya fedha zilizotolewa zimerejeshwa.

254. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa mipaka ya maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Tarafa, Kata, Mitaa, Vijiji na Vitongoji sanjari na kuboresha utoaji wa huduma za umma kwenye maeneo hayo. Aidha, kwa kushirikiana na wadau na wananchi wa maeneo husika jumla ya migogoro 162 kati ya 257 ya mipaka, fidia na ardhi ilipatiwa ufumbuzi na mingine iko katika hatua mbalimbali za kutatuliwa. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo na ushauri wake ambayo yaliwezesha kuwa na maeneo sahihi ya kuhesabu na kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi mwezi Agosti 2022 kwa ufanisi mkubwa. Vilevile, Ofisi imeanza kufanya maandalizi ya kuhakiki Mipaka ya Maeneo ya Utawala kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika Mwezi Oktoba 2024.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa masuala ya usimamizi wa ardhi kutawezesha kujumuisha wadau na taasisi za kijamii kwenye ngazi ya msingi na hivyo kuleta utangamano, uwiano wa maendeleo baina ya maeneo ya mijini na vijijini na pia kuongeza tija katika kuinua ustawi wa jamii hasa zenye mazingira magumu sambamba na kusimamia vyema Mipango ya Uchumi ya Halmashauri.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 Ofisi ya Rais TAMISEMI itaimarisha shughuli za ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji pamoja na ukaguzi na ufuatiliaji wa fedha katika Mikoa na Serikali za Mitaa. Hii ni kutokana na uundwaji wa idara ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Ukaguzi (MMI) katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa ikiwa ni pamoja na ongezeko la fedha za ufuatiliaji na tathmini kutoka shilingi Bilioni 3 hadi Shilingi Bilioni 9.46 zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24. Uboreshaji huu utasaidia ukamilishaji wa Miradi kwa thamani ya fedha,

kuimarisha matumizi ya fedha na kuchukua hatua za haraka katika maeneo ya miradi ambayo haijatekelezwa vizuri. Aidha, kufuatia uanzishwaji wa idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara katika ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa utaimarisha shughuli za uwekezaji, viwanda na biashara katika mamlaka za serikali za mitaa. Itasaidia kutenga maeneo ya uwekezaji, viwanda na biashara na hivyo kurahisha upatikanaji wa maeneo hayo.

**Maelekezo Mahususi**

257. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa Maelekezo kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Wakuu wa Mikoa kusimamia Miradi inayotekelezwa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili iweze kukamilika kwa wakati hususan baada ya ofisi hizi kuongezewa Bajeti pamoja na magari 26 kwa ajili ya Ufuatuliaji, Usimamizi na Ujifunzaji katika mikoa yote;

(ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa kuviwezesha Vitengo vya ukaguzi wa ndani kwa kuvipatia vitendea kazi na bajeti kupitia mapato ya ndani. Aidha, Halmashauri zenye mapato makubwa yasiyolindwa kuanzia shilingi Bilioni 5 na kuendelea wahakikishe wananunua magari kwa ajili ya vitengo hivyo;

(iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuziwezesha Ofisi za Kata kwa kuziwekea Bajeti ili ziweze kusimamia ngazi za msingi za Halmashauri katika kusimamia shughuli za Serikali katika maeneo yao;

(iv) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zifanye usimamizi maalum wa Miradi inayokamilishwa na fedha zilizovuka mwaka kwa

kuzingatia muda uliowekwa kisheria na Sheria ya Bajeti Sura ya 439;

(v) Uidhinishwaji wa Mpango wa Miradi inayotekelezwa na fedha za uwajibikaji wa makampuni utafanywa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya miradi hiyo kuanza kutekelezwa;

(vi) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaelekezwa kusimamia na kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga na kutekeleza Miradi ya Maendeleo kupitia mapato ya ndani kulingana na ngazi za asilimia 70,60,40 na 20 kama ilivyoelekezwa kwenye mwongozo wa Mpango na Bajeti;

(vii) Halmashauri zote zilizopewa mkopo wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi zifanye marejesho ya fedha hizo kabla au ifikapo tarehe 31 Oktoba, 2023. Aidha, Fedha zinazopatikana kupitia mradi wa KKK zisiwe sehemu ya mapato ya ndani ya Halmashauri bali iwe ni miradi inayojitegemea na zirejeshwe katika utekelezaji na uendelezaji wa mradi huo;

(viii) Mamlaka za Serikali za Mitaa zisifanye mabadiliko ya miradi iliyopangwa kutekelezwa bila ya kupewa idhini na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa;

(ix) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zihakikishe zinaratibu uombaji wa fedha za utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Halmashauri kulingana na Waraka wa Hazina wa utekelezaji wa Bajeti unaotolewa kila mwaka ili kuwa na muda wa kutosha wa kutekeleza miradi ya maendeleo;

(x) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Chama katika maeneo yao ya utawala hususani maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu

wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Tanzania Bara, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, msistizo unatolewa kuwa kila mkoa na Halmashauri ziwe na Kanzidata ya Maelekezo yaliyotolewa katika kipindi cha mwaka 2020, 2021, 2022 na 2023 katika mikoa pamoja na taarifa za utekelezaji;

(xi) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kuratibu, Kusimamia na kujibu Hoja za Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alizozitoa Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xii) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kufanya tathmini na kufanya masawazo wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuleta uwiano katika utoaji wa huduma za jamii katika Halmshauri Moja na nyingine. Aidha, watumishi wanaozidi katika baadhi ya maeneo hususan katika vituo vya kutolea huduma katika miji wapelekwe katika maeneo ya pembezoni. Vilevile Halmashauri zitoe motisha kwa watumishi wanaoanza kazi katika vituo vya pembezoni ikiwa ni pamoja na vifaa vya kuanzia kazi;

(xiii) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zisimamie Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuendeleza na kuendesha Miji midogo inayochipukia sambamba na maendeleo ya Vijiji; na

(xiv) Ofisi za Wakuu wa Mikoa zisimamie ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kuhimiza matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato na utoaji wa taarifa ili kufikia malengo yaliyowekwa katika Mpango na Bajeti.

## G. SHUKRANI

258. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninamshukuru

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais (TAMISEMI). Ninamuahidi kuwa nitaendelea kutimiza wajibu wangu kwa weledi katika kuisimamia Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa nguvu zangu zote.

259. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Aidha, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inayoongozwa na Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo na wajumbe wote wa kamati kwa kazi nzuri ya kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

260. ***Mheshimiwa Spika,*** maoni na ushauri wa Kamati umesaidia sana kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

261. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Daniel Barran Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Omary Mohammed Kigua, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wa Kamati kwa maoni, maagizo na maelekezo mengine ambayo wanaendelea kutuelekeza kuhusu utekelezaji wa Mipango na Bajeti.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) inayoongozwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge

wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, maelekezo na maagizo yao katika uboreshaji wa usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo za Bunge, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini na Wajumbe wa Kamati kwa ushauri, maelekezo na maoni yao katika utungaji wa Sheria Ndogo za Halmashauri.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hawa ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (FAD), Shirika la Maendeleo la Uingereza (Foreign, Commonwealth and Development Office-FCDO), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Shirika la Kuleta Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA) na Nchi zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya ambazo ni Denmark, Ireland, Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Maendeleo (SIDA), Global Partnership for Education - (GPE), Switzerland na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF) na Makampuni ya Migodi ya Geita Gold Mines (GGM) na Twiga - Barrick Tanzania, Benki za NMB na CRDB.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Taasisi za Kidini, Taasisi za Kifedha, Asasi za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Makampuni mbalimbali kwa mchango wao wanaoutoa kwa Serikali.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa Miradi na Programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

266. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutambua mchango wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Kipekee, ninawashukuru sana Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge wa Jimbo la Chamwino kwa usaidizi na ushirikiano mkubwa wanaotoa kwangu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

267. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru pia Katibu Mkuu, Ndg. Adolf Hyasinth Ndunguru na Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Charles Enock Msonde, Dkt. Wilson Charles Mahera na Ndg. Sospeter Mambile Mtwale kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha maandalizi ya Mpango na Bajeti na usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Aidha, ninamshukuru Bi. Paulina Mbena Nkwama Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kusimamia vyema Tume ya Utumishi wa Walimu. Ninawashukuru Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala Wasidizi wa Mikoa, Waheshimiwa Wastahiki Mameya, Wenyeviti wa Halmashauri Waheshimiwa Madiwani, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Timu za

Menejimenti za Halmashauri (CMT's) pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake mpaka ngazi ya msingi ya Serikali za Mitaa ikiwemo Tarafa, Kata, Mitaa/Vijiji na Vitongoji kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

## H. MAJUMUISHO

268. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Mafungu yote 28 yaliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI inatarajia kuongeza kasi ya kuwahudumia na kuwafikia wanachi kwa uharaka kwa kufanya yafuatayo: Kufungua barabara mahali kusikofikika na kulinda uwekezaji ambao ulishafanyika katika miundombinu ya barabara; Kutumia teknolojia mbadala ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ili kuongeza ufanisi; Kutoa huduma bora za afya ya msingi kwa kuongeza vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya; Kuboresha huduma jumuishi za wazee ikiwemo uwepo wa dirisha la kuwahudumia; Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo ili kuwapunguzia gharama wananchi na kuongeza uandikishaji wa wananfunzi; Kuongeza miundombinu ya elimu ili kuboresha na kusogeza mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

269. ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ni kuimarisha usimamizi wa rasilimali fedha na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kupitia mifumo ya Kieletroniki; Kuimarisha Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Kuimarishaji Utawala Bora kwa kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa ili kuimarisha utoaji wa huduma na usimamizi wa shughuli za Serikali katika ngazi ya msingi; Kuimarisha kituo cha huduma kwa mteja ili kushughulikia kwa haraka kero na malalamiko kwa wananchi; Kuimarisha utendaji kazi wa ofisi za kata kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi. Uendelezaji wa Vijiji na Miji na

Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi; na Kufanya maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Mwaka 2024.

## I. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/24

### Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani

270. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 184 inaomba idhini ya kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani jumla ya Shilingi Trilioni Moja Bilioni Mia Moja Tisini na Tisa Milioni Mia Mbili Themanini na Saba Mia Tano Tisini na Mbili Elfu na Mia Moja Arobaini na Sita (Shilingi 1,199,287,592,146). Makusanyo haya yatatokana na maduhuli, ada za wanafunzi za Chuo cha Serikali za Mitaa, ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, tozo na faini. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Namba 1

**Jedwali Namba 1 : Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24**

| OFISI/TAASISI | MAKADIRIO (Shilingi) |
|---|---:|
| Taasisi | 55,142,420,746 |
| Mikoa | 261,890,400 |
| Halmashauri | 1,143,883,281,000 |
| **JUMLA KUU** | **1,199,287,592,146** |

271. ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24 yenye jumla ya Shilingi Trilioni Tisa Bilioni Mia Moja Arobaini na Nne Milioni Ishirini na Moja na Mia Sita Tisini na Tisa Elfu (**Shilingi 9,144,021,699,000**) kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 2 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 184.

272. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zinazoombwa, Shilingi Trilioni Tano Bilioni Mia Sita Hamsini na Nane Milioni Ishirini na Mbili na Hamsini na Nane Elfu (Shilingi 5,658,022,058,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara Shilingi Trilioni Nne Bilioni Mia Tano Tisini na Saba Milioni Mia Sita Thelathini na Mbili na Mia Moja Themanini na Tatu Elfu (Shilingi 4,597,632,183,000) na Matumizi Mengineyo Shilingi Trilioni Moja Bilioni Sitini Milioni Mia Tatu Themanini na Tisa na Mia Nane Sabini na Tano Elfu (Shilingi 1,060,389,875,000).

273. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi Trilioni Tatu Bilioni Mia Nne Themanini na Tano Milioni Mia Tisa Tisini na Tisa na Mia Sita Arobaini na Moja Elfu (Shilingi 3,485,999,641,000) zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo Shilingi Trilioni Mbili Bilioni Mia Tatu Sitini na Mbili Milioni Mia Saba na Mia Nne Themanini na Saba Elfu (Shilingi 2,362,700,487,000) ni fedha za ndani na Shilingi Trilioni Moja Bilioni Mia Moja Ishirini na Tatu Milioni Mia Mbili Tisini na Tisa na Mia Moja Hamsini na Nne Elfu (Shilingi 1,123,299,154,000) ni fedha za nje *(Mchanganuo wa fedha zinazoombwa katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 umeoneshwa katika Jedwali Namba 2)*.

**Jedwali Namba 2: Mchanganuo wa Makisio katika Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/24 (Shilingi) |
|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida Ofisi ya Rais -TAMISEMI** | |
| **Mishahara** | |
| Mishahara Makao Makuu | 10,531,502,000 |
| Mishahara ya Taasisi | 52,425,682,000 |

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/24 (Shilingi) |
|---|---|
| **Jumla Mishahara Ofisi ya Rais - TAMISEMI** | **62,957,184,000** |
| | |
| **Matumizi Mengineyo** | |
| Makao Makuu | 28,118,998,500 |
| Taasisi | 4,275,853,500 |
| **Jumla ya Matumizi Mengineyo** | **32,394,852,000** |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **95,352,036,000** |
| | |
| **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)** | |
| Mishahara | 8,819,516,000 |
| Matumizi Mengineyo | 7,714,432,000 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida TSC** | **16,533,948,000** |
| | |
| **MIKOA NA HALMASHAURI** | |
| **MIKOA:** | |
| Mishahara | 73,778,256,000 |
| Matumizi Mengineyo | 108,206,120,000 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | **181,984,376,000** |
| | |
| **HALMASHAURI** | |
| Mishahara | 4,452,077,227,000 |
| Matumizi Mengineyo (Serikali Kuu) | 222,606,048,000 |
| Matumizi Mengineyo (Mapato ya Ndani) | 689,468,423,000 |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **5,364,151,698,000** |
| | |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | |
| **OFISI YA RAIS -TAMISEMI** | |

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/24 (Shilingi) |
|---|---|
| Fedha za Ndani | 759,426,035,000 |
| Fedha za Nje | 219,840,334,000 |
| **Jumla Maendeleo** | **979,266,369,000** |
| | |
| **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU** | |
| Fedha za Ndani | 670,000,000 |
| **Jumla** | **670,000,000** |
| | |
| **MIKOA** | |
| Fedha za Ndani | 69,618,865,000 |
| Fedha za Nje | 30,201,175,000 |
| **Jumla Maendeleo** | **99,820,040,000** |
| | |
| **HALMASHAURI** | |
| Fedha za Ndani (Serikali Kuu) | 1,078,570,729,000 |
| Fedha za Ndani (Mapato ya Ndani) | 454,414,858,000 |
| Fedha za Nje | 873,257,645,000 |
| **Jumla Maendeleo Halmashauri** | **2,406,243,232,000** |
| **JUMLA KUU** | **9,144,021,699,000** |

274. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Fungu Namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Namba 02 na Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184 ambayo ni sehemu ya Hotuba hii.

275. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Sasa nitamwita Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, aje awasilishe maoni ya Kamati yetu kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. DENNIS L. LONDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye imempendeza yeye, leo kwa niaba ya Kamati, kuwasilisha kwako Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, natoa kwako shukurani kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa ya Kamati hii iingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati imejikita katika kueleza maeneo yafuatayo:-

(a) Maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(b) Uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya kamati kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(c) Uchambuzi wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 (makadirio ya maduhuli na matumizi); na mwisho,

(d) Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge lako shilingi trilioni 3.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha na iliyotekezwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2022/2023. Miradi iliyotembelewa ni miradi ya elimu, miradi ya afya, miradi ya masoko na miradi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za

Bunge za mwaka 2023. Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua miradi katika Mikoa mitano kwa maana ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga pamoja na Singida. Jumla ya miradi 12 iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilikaguliwa.

Mheshimiwa Spika, faida za miradi iliyotembelewa na Kamati: Kwa ujumla miradi yote iliyotembelewa na Kamati ililenga kuondoa ujinga, kuondoa maradhi, kuondoa umasikini katika Halmashauri zetu kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya utoaji elimu nchini, kujenga, kukarabati na kuimarisha miundombinu ya utoaji wa afya nchini, kujenga na kukarabati na kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya barabara na masoko katika Halmashauri zetu zote. Yote hii inalenga kuleta maendeleo endelevu kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla miradi yote iliyokaguliwa na kamati imefikia wastani wa asilimia 40 mpaka 85 na kamati imeridhika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi. Kwa ujumla miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati ina changamoto zinazofanana na baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kukosekana kwa ushirikiano kati ya Idara na vitengo vya Serikali ndani ya Halmashauri ama Wilaya husika;

(b) Kutofanyika kwa upembuzi yakinifu wa kina katika utekelezaji wa mradi hiyo;

(c) Kuchelewa kuanza kwa miradi kutokana na sababu za kimfumo zilizosababisha Halmashauri kushindwa kubaini kwa wakati uwepo wa fedha za miradi katika akaunti zao;

(d) Kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi, mfano saruji, mabati na nondo wakati wa utekelezaji wa miradi na kusababisha gharama za ujenzi kuwa kubwa ukilinganisha na makisio yaliyopangwa; na

(e) Kufungwa kwa mfumo wa malipo wa *MUSE* mwishoni mwa mwezi Juni, 2022 jambo ambalo liliathiri malipo mbalimbali katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kutokana na ziara za Kamati za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga na Singida, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na kutoa maoni na ushauri wa ujumla kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Rais, TAMISEMI wahakikishe Halmashauri zote zinatumia ramani na miongozo iliyotolewa katika ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya na shule za sekondari; *(Makofi)*

(ii) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wahakikishe kunakuwa na uwiano wa kiasi cha fedha kilichotolewa na ubora wa kazi iliyofanyika katika ujenzi wa vituo vya afya na shule za sekondari; *(Makofi)*

(iii) Ofisi ya Rais, TAMISEMI wahakikishe wanafanya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* kwa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kina na kuondoa changamoto za tofauti *(variation)* ya gharama zinazotumika katika majengo hayo hali inayoathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama kutokana na kuongeza kwa kazi;

(iv) Serikali pia iweke utaratibu wa kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi iliyotengewa

fedha ili kuepusha ubadhirifu na hivyo kuwezesha kupatikana kwa thamani ya fedha.

(v) Linapokuja suala zima la utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri, Kamati inashauri kuwa pawepo na ushirikishwaji wa karibu kati ya Idara na vitengo vya Serikali ndani ya Halmashauri ili kuwezesha utekelezaji wa miradi hiyo kufanyika bila ya kuwa na mikwamo.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2022/2023: Baada ya Wizara pamoja na mikoa kuwasilisha bajeti zao kwa mafungu 28 kuanzia tarehe 20 hadi 29 Machi, 2023, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia kutoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo Nane. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati itaendelea kusisitiza katika Taarifa hii likiwemo suala la bakaa kuhusu utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; Wizara pamoja na mikoa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi trilioni moja. Taarifa ya kina kuhusu ukusanyaji wa maduhuli hayo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, hadi Mwezi Februari 2023, jumla ya shilingi bilioni 647.9, sawa na asilimia 60.4 ya lengo zilikusanywa. Maelezo zaidi kuhusu makusanyo ya maduhuli hadi Mwezi Februari ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2 cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati; katika uchambuzi wa Kamati, Kamati ilibaini kuwa upokeaji wa jumla wa fedha ulifikia asilimia 63.4 ambapo fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa kwa asilimia 64.5 na fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo imepokelewa kwa asilimia 35 ya fedha zote zilizopokelewa.

Mheshimiwa Spika, aidha, fedha kwa ajili ya matumizi mishahara zilipokelewa kwa asilimia 53 na fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo zilipokelewa kwa asilimia 12.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujua kiasi cha asilimia 35.7 kilichopokelewa hadi Februari, 2022 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kimefikisha asilimia ngapi ya utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo. Kamati pia ilihoji ili kufahamu ikiwa kiasi kilichobaki kikitolewa kitaweza kamilisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa kipindi kichowekwa. Kamati ilijulishwa kuwa kama Wizara taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na mikoa itapokea fedha hizo itaweza kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; mpango wa utekelezaji wa majukumu, mapato na matumizi ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imepangwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo, sera mbalimbali kama vile Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapindizi (CCM) ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli hizo za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara na taasisi zake pamoja na mikoa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni jumla ya shilingi trilioni 1.2; makadirio haya ni sawa na ongezeko la asilimia 11. Maelezo ya kina kuhusu makadirio ya maduhuli ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 6 kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili; uchambuzi wa bajeti ya Wizara (Fungu 56) pamoja na mafungu 26 kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Fungu 56, Fungu 02 pamoja na mafungu yote 26 ya mikoa inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi trilioni 9.1. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 5.6, sawa na asilimia 61.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi trilioni 3.4, sawa na asilimia 38.1 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 7.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, sura ya Bajeti ya Wizara inajumuisha shilingi trilioni 4.5, sawa na asilimia 50.2 kwa ajili ya mishahara, shilingi trilioni 1.6, sawa na asilimia 11.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya shilingi trilioni 3.5 sawa na asilimia 38.1 za miradi ya Kielelezo Na 8 (a) na (b).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la asilimia 6.6 kwenye bajeti ya maendeleo, kutoka shilingi trilioni 3.3 mwaka 2022/2023 hadi 3.5 mwaka 2023/2024;

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la asilimia 10 kutoka shilingi trilioni 2.1 mwaka 2022/2023 hadi trilioni 2.4 mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024; uchambuzi huu wa Kamati ulilenga kubaini athari za Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa dhidi ya Bajeti ya Fungu 56, Fungu 02 na mafungu yote 26 ya Mikoa. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo: -

(i) Wakati Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2023/2024 ikiwa imeongezeka kwa asilimia 7 bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeongezeka kwa asilimia 4.1;

(ii) Wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo ikiwa imeongezeka kwa asilimia 01 bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeongezeka kwa asilimia 6.6;

(iii) Wakati bajeti ya Taifa ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa asilimia 10.4, bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeongezeka kwa asilimia 2.6.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni asilimia 20.6 ya bajeti Kuu ya Serikali. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; baada ya uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi: -

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa Shirika la Elimu Kibaha; Shirika la Elimu Kibaha ni shirika la Umma lililoanzishwa mwaka 1963 chini ya wafadhili watano ambao ni Serikali ya Tanganyika kwa kipindi hicho na Serikali nne za Nchi za Kinordic (Dernmark, Norway, Finland na Sweden). Shirika hili lilisajiliwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na.17 ya Mwaka 1969 na marejeo ya sheria hiyo ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha lilianzishwa likiwa na dhima kuu tatu, yaani kuondoa ujinga, maradhi na umasikini. Ili kulifanya shirika kutimiza dhima yake lilianzisha mambo makuu matatu muhimu kama ifuatavyo: -

(i) Kuanzisha hospitali ambayo inajulikana kama Hospitali ya Tumbi ili kukabiliana na changamoto ya maradhi;

(ii) Kuanzisha miradi ya ujasiriamali illi kukabiliana na changamoto ya umasikini; na

(iii) Kuanzishwa kwa kozi mbalimbali ili kuwaondoa Watanzania kwenye changamoto ya ujinga.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeihamisha Hospitali ya Tumbi kutoka Shirika la ELimu Kibaha kwenda Wizara ya Afya. Kamati inapongeza mpango huu, ikiwa ni sehemu ya kuboresha hospitali hii iliyo muhimu kabisa katika kuwahudumia wananchi wa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kuondolewa kwa hospitali hii kutoka Shirika la ELimu Kibaha kwenda Wizara ya Afya kunatengeneza tena ombwe la kutotekelezeka kwa sehemu ya dhima ya uanzishwaji wa shirika hili, hasa kwa kipengele cha afya. Kutokana na hilo Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali kuacha kuendelea kuhamisha taasisi zilizo chini ya Shirika la Elimu Kibaha;

(ii) Serikali ifikirie upya uamuzi wake wa kuitoa Hospitali ya Tumbi kutoka Shirika la Elimu Kibaha kwenda Wizara ya Afya; na

(iii) Serikali ifanye tathmini ya uendeshaji wa shirika hili ili kuona kama malengo na dhima ya kuanzishwa kwake inaendana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, suala la ukamilishaji wa maboma ya shule na zahanati; ili kuimarisha elimu na huduma za hospitali katika ngazi za halmashauri za wilaya, kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilitoa hamasa kubwa kwa wananchi kujitolea katika ujenzi wa majengo kwa ajili ya vituo vya afya, zahanati na shule katika halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kuna maeneo mengi nchini wananchi wamejitolea kujenga majengo kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na shule. Aidha, majengo mengi yaliyojengwa na wananchi yameishia katika ngazi ya upauaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuwa majengo hayo yangemaliziwa kutokana na fedha kutoka Serikalini. Hata hivyo, hadi sasa majengo mengi yaliyojengwa na wananchi hayajamaliziwa kutokana na Serikali kutopeleka fedha za umaliziaji wa majengo hayo kama ilivyoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inashaishauri Serikali kupeleka fedha za kumalizia maboma hayo ili kuondoa hasara inayoweza kupatikana kutokana na kuchakaa kwa majengo hayo kabla ya kutumika.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa vifaa mbalimbali vya hospitali na zahanati kutoka Bohari Kuu ya Dawa *(MSD);* Kamati inaipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa inayoufanya kwa kujenga majengo ya hospitali na zahanati

pamoja na kutenga fedha za kununulia vifaatiba, vitendanishi na dawa kwa ajili ya zahanati na hospitali zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna halmashauri nyingi zimepelekewa fedha na Serikali kwa ajili ya kununua vifaatiba, vitendanishi na dawa kwa ajili ya hospitali na zahanati nchini ili ziagize vifaa hivyo kupitia Bohari ya Dawa *(MSD)*. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa zahanati na hospitali nyingi zilizoagiza vifaatiba, vitendanishi na dawa kupitia *MSD,* vifaa hivyo vinachelewa kupelekwa katika hospitali na zahanati hizo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Ofisi ya Rais, TAMISEMI kukaa na Wizara ya Afya na *MSD* kujadiliana namna bora ya kuwasilisha vitendanishi, vifaatiba na dawa zote zilizoagizwa kwa ajili ya halmashauri zote nchini; na

(ii) Serikali kuweka mifumo itakayowezesha uagizaji wa vitendanishi, vifaatiba na dawa kupitia *MSD* itakayowezesha uwasilishaji wa vifaa hivyo bila kuchelewa ili kufikia malengo ya Serikali ya kufikisha huduma kwa wananchi kwa haraka na kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa uwekezaji wa kampuni/mashirika kwa jamii *(Cooperate Social Responsibility);* Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano mzuri kati yake na wawekezaji mbalimbali nchini. Wawekezaji hawa wamekuwa wakileta ahueni kubwa kwa Serikali katika kupeleka huduma mbalimbali kwa wananchi katika mikoa na halmashauri mbalimbali nchini kwa kutumia sehemu ya faida ya uwekezaji wao kwa ajili ya jamii katika halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wilaya ya Tarime walipokea takriban shilingi bilioni saba kutoka Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara* kwa ajili ya kusaidia shughuli mbalimbali za kijamii. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa ya fedha iliyotumika haiakisi thamani halisi ya fedha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Halmashauri husika kuweka vipaumbele vya matumizi ya fedha za *CSR,* hasa miradi mikubwa, kabla ya kupokea fedha hizo;

(ii) Ofisi ya Rais, TAMISEMI kutengeneza mwongozo mzuri wa matumizi ya fedha za *CSR;* na

(iii) Serikali ifanye tathimini kuhusu maeneo yote yanayonufaika na *CSR* ili kuona namna bora jamii inavyonufaika na miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na programu ya *SEQUIP; Secondary Education Quality Improvement Program (SEQUIP)* ni mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia unaolenga kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa ajili ya shule za sekondari nchini. Mradi huu ulianza Mwaka wa Fedha 2020/2021 na unatarajiwa kukamilika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapeleka shilingi milioni 470 katika maeneo mbalimbali ya halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa maeneo mengi ya halmashauri fedha zilizopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu hazikutosheleza.

Mheshimiwa Spika, hali hii imezilazimisha baadhi ya halmashauri kutumia fedha za mapato yao ya ndani kwa ajili

ya kumalizia majengo yanayofadhiliwa na mradi huu. Hali hii imekuwa ikisababisha baadhi ya shughuli za halmashauri kutokufanyika. Kamati inatilia shaka kuwa baadhi ya halmashauri huenda zikashindwa kabisa kumalizia majengo haya kutokana na halmashauri hizo kuwa na vyanzo dhaifu vya mapato.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta fedha za kuongezea umaliziaji wa majengo yanayofadhiliwa na mradi huu;

(ii) Serikali ibainishe vyanzo vya fedha zitakazoweza kutumika kumalizia majengo hayo;

(iii) Serikali ifanye marejeo ya makadirio ya ujenzi kulingana na hali halisi chini ya Ofisi za Mkuu wa Mkoa na kuwasilisha kwa TAMISEMI; na
(iv) Serikali ifanye uchunguzi kujua sababu ya fedha hizo kutotosha na wahusika kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, ubora wa upembuzi yakinifu katika miradi inayotekelezwa na halmashauri nchini; katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa miradi mingi inayotekelezwa katika halmashauri nchini inakumbwa na changamoto ya kuibuka kwa kazi za ziada ambazo awali hazikuwa sehemu ya ukadiriaji. Kwa mfano kububujika maji wakati wa ujenzi wa msingi wa Soko la Mjini Kati la Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa changamoto hizo zimetokana na udhaifu wa wataalam waliofanya upembuzi yakinifu. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inasimamia na kudhibiti shughuli za upembuzi

yakini unaofanywa na wataalam kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yote katika halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, utofauti wa michoro na ukadiriaji katika miradi ya ujenzi wa majengo ya shule, zahanati na vituo vya afya katika halmashauri zetu; kumekuwa na ramani tofauti tofauti katika miradi mbalimbali ya ujenzi wa shule, zahanati na vituo vya afya katika halmashauri zote nchini, hasa ujenzi wa majengo ya miradi inayotekelezwa na programu za *SEQUIP, EP4R BOOST* na *COVID*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kuweka michoro iliyo ya kudumu na ya kufanana *(consistent)* itakayotumika kwa muda mrefu ili kutumia fursa ya uzoefu itakayopatikana kutoka mradi mmoja kwenda mwingine kwa majengo hayo na kuleta sura ya mfanano kwa majengo yote ya aina hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la utoaji wa mafunzo ya awali ya utumishi wa Umma kwa maafisa watendaji wa kata na vijiji; Kamati hii iliitaka Serikali kuratibu mafunzo maalum ya awali kuhusu shughuli za Serikali, utumishi wa Umma, usalama na huduma kwa jamii kwa watendaji wa kata na vijiji wakati wa Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti. Hata hivyo agizo hili kwa sehemu kubwa halikutekelezwa. Aidha, mikoa imetoa taarifa za mafunzo ya watumishi wa makao makuu ya halmashauri ambayo hutolewa na vyuo mbalimbali vya Umma na binafsi badala ya Chuo cha Utumishi wa Umma kama agizo la Bunge lilivyotaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI iratibu mafunzo hayo ya utumishi wa Umma kwa watendaji wa kata na vijiji ili kuongeza uwajibikaji wa watumishi katika ngazi za vijiji na kata. Aidha, nasisitiza tena, mafunzo hayo yatolewe na Chuo cha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa taulo za kike kwa wanafunzi; Serikali inafanya jitihadi kubwa kuhamasisha wadau mbalimbali na halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike wawapo shuleni kupata taulo za kike.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jambo hili Kamati inatoa ushauri ufuataο:-

(i) Halmashauri ziongeze kiwango cha fedha kwa ajili ya ugharamiaji wa taulo za watoto wa kike;

(ii) Serikali iweke utaratibu wa kuratibu vizuri masuala ya ubora, thamani ya fedha, upokeaji na uwiano wa usambazaji wa ya taulo hizo; na

(iii) Serikali itambue michango ya wadau wengine na thamani ya fedha zao ijulikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuwepo kwa bakaa katika bajeti za halmashauri; Kamati katika uchambuzi wake imebaini kuwa mikoa yote imekuwa ikibakisha bakaa, hasa kutoka kwenye miradi ya maendeleo. Kamati inaona kwamba kubakisha bakaa kila mwaka kunaweza kuwa chanzo cha miradi mingi kutokamilika kwa wakati na shughuli nyingine za maendeleo na utendaji kutokwenda kama ilivyopangwa. Aidha, kwa sababu utaratibu wa matumizi ya bakaa hauko wazi kuna viashiria kwamba fedha za bakaa zinaweza kutumika katika matumizi ambayo hayakupangwa, jambo ambalo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Serikali kuangalia upya sheria ya matumizi ya bakaa;

(ii) Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuweka mikakati ya kupunguza kiwango cha fedha za bakaa sambamba na kuweka utaratibu wa kuongeza uwajibikaji kwa fedha zinazovuka mwaka; na

(iii) Serikali kuangalia upya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma ambazo kwa mfumo na muundo wa majukumu ya Serikali za Mitaa utekelezaji wa sheria hii umekuwa mgumu kwa halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa asilimia 40 vijijini; imebainika kuwa halmashauri nyingi nchini hazipeleki asilimia 40 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kupeleka huduma vijijini kama inavyotakiwa na sheria. Hali hii imekuwa ikisababisha huduma duni kwa wananchi wanaoishi vijijini. Kamati inashauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuweka utaratibu wa ufuatiliaji wa upelekaji wa asilimia 40 vijijini katika kila kipindi cha robo mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Shule za Michepuo ya Kiingereza; halmashauri nyingi nchini zinaendelea kujikita katika kuanzisha na kuendeleza Shule za Michepuo ya Kiingereza kwa ajili ya kuongeza ubora wa elimu nchini. Kamati inapongeza jitihada hizi kutokana na sababu kuwa Tanzania si kijiji kisichokuwa na mwingiliano na mataifa ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa uwekezaji wa shule hizi ni mkubwa na unahitaji rasiliamali watu yenye ujuzi, uwezo na umahiri mkubwa ili kuwa katika viwango vinavyohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, imebainika kuwa shule hizi zinaongezeka kwa kasi, hali inayoweza kuathiri mfumo mzima wa utoaji wa elimu nchini, hasa kuathiri shule wanazosoma wananchi wa kawaida. Pia zinatumia walimu walioajiriwa na Serikali katika Halmashauri na hivyo kuleta

upungufu kwa watumishi wa kada hiyo ya ualimu na kuhamisha walimu wabobevu kutoka shule za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapata mashaka juu ya uanzishwaji wa shule hizi kwa wingi kuwa unaweza kuleta ubaguzi na matabaka kwa wananchi wa Tanzania ilhali Serikali ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri ifuatavyo: -

(i) Serikali itazame utaratibu uliotumika na unaotumika kuhusu mfumo wa uanzishwaji, uendeshaji na usimamizi, wa Shule za Michepuo ya Kiingereza zinazoanzishwa, kumilikiwa na kuendeshwa na Serikali ili kutokuathiri shule za kawaida;

(ii) Kwa kuwa shule hizi zinaanzishwa kama miradi, ni rai ya Kamati kuwa mpango wa uanzishwaji huo uende sambamba katika kujitegemea kiuanzishaji na kiuendeshaji;

(iii) Serikali ihakikishe kuwa uwekezaji huu hauathiri rasilimali watu (hasa walimu) ambao tayari wako kwenye mfumo wa ajira za Serikali);

(iv) Serikali itoe mwongozo wa uanzishwaji na uendeshwaji wa shule za mkondo wa Kiingereza, ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu usiokuwa wa upendeleo utakaofanana kwa halmashauri zote nchini;

(v) Kamati inaishauri Serikali ipitie upya haja na malengo ya uanzishwaji wa shule hizi katika muktadha wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014; na

(vi) Serikali ichukue juhudi za makusudi za kuimarisha ufundishaji wa Lugha za Kiswahili na Kiingereza katika shule zake zote za msingi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika halmashauri zetu; kwa mujibu Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 jukumu la kupanga, kupima na kuendeleza ardhi liko chini ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilitoa fedha kama mkopo kwa halmashauri zetu kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Halmashauri nyingi zimeshindwa kurejesha mkopo na haziendelei tena na shughuli za kupima viwanja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo eneo kubwa la ardhi katika halmashauri zetu linaendelea kubaki bila kupimwa, hali inayosababisha migogoro ya ardhi miongoni mwa jamii kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri: -

(i) Serikali kufanya tathmini ya matumizi ya mkopo huo na mafanikio katika upimaji wa ardhi za halmashauri;

(ii) Serikali kuangalia mapato yanatokana na uuzwaji wa ardhi iliyopimwa kuendelea kutumika kupima maeneo mengine;

(iii) Serikali isimamie na kuratibu urejeshwaji wa mikopo hiyo kutoka halmashauri zote zilizopata mkopo huo; na

(iv) Halmashauri ziendelee kuweka mikakati kwa kutumia mapato ya ndani kuendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uanzishwaji wa miradi ya kimkakati na utekelezaji wake, imebainika kuwa Serikali imeanzisha miradi mingi ya kimkakati inayoanzishwa katika halmashauri zetu nchini, aidha miradi hii inatolewa kwa

kuzingatia pamoja na mambo mengine inahitaji maandika ya utaalam uliyobobea, hata hivyo imebainika kuwa halmashauri nyingi nchini hazina wataalam hao kuandika maandiko bora yanayoweza kusaidia kupata miradi hiyo ya kimkakati kutoka kwa wadau mbalimbali hasa Serikalini. Hii inatokana na halmashauri nyingi kukosa uwezo wa kuajiri wataalam wa uandikaji wa maandiko hayo. Hali hii imekuwa ikisababisha halmashauri nyingi kushindwa kupata miradi ya kimkakati kutokana na kushindwa kuandaa maandiko bora.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwa pamoja na mianzo hiyo ya miradi hii ya kimkakati, utaratibu uliowekwa uangaliwe upya ili halmashauri zisizokuwa na uwezo na wataalam zinufaike na miradi hii. Kutokana na hilo, Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali kuweka utaratibu wa kuisadia halmashauri kuandaa maandiko ya miradi.

ii. Serikali ifanye tathmini ya marejeo, mapitio ya mwongozo wa miradi ya kimkakati ili kutatua changamoto ambazo zipo katika mwongozo wa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upungufu wa watumishi; Kamati inapongeza Serikali kwa jitihada za kuona tatizo hilo na kuomba kibali cha ajira katika halmashauri zetu. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa kibali cha kuajiri watumishi zaidi ya 21,000 katika sekta ya afya na ualimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo tunatoa rai kwa Serikali kufanya tathmini ya upungufu wa watumishi katika halmashauri zetu zote nchini. Serikali pia tunatoa rai kuweka mkakati wa kupunguza upungufu katika maeneo yenye upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa mara nyingine napenda kutoa shukurani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu vyema. Nawashuru sana Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais *TAMISEMI,* Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi Naibu Waziri Ofisi ya Rais *TAMISEMI,* Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Naibu Waziri Ofisi ya Rais *TAMISEMI*. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Ofisi ya Rais *TAMISEMI* ndugu Adolf Ndunguru na Manaibu wake Dkt. Wilson Mahera, Dkt. Charles Msonde na ndugu Sospeter Mtwale pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati yangu tangu tulipoanza kufanya kazi hii, na walishiriki vizuri kwenye uchambuzi wa bajeti ya Wazira.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na wote namshukuru kipekee kabisa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao amenipa, wajumbe ambao ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa bajeti na kuhakikisha wanahoji na kupata ufafanuzi wa kina kwa niaba ya Bunge lako. Nawapongeza sana na ninaomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(hansard)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja naye namshukuru Ndugu Michael Chikokoto, *ndc,* Kaimu Mkurugrenzi Idara ya Kamati za Bunge na Mkurugenzi Msaidizi ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano walio ipa Kamati yetu katika kipindi chote cha kazi hii. Aidha, tunawashukuru sana na kipekee kabisa Makatibu wetu wa Kamati, Ndugu Emanuel Mdidi na Ndugu Sikudhani Mbinga pamoja na msaidizi wa Kamati ndugu

Frank Ngonyani kwa kuhakikisha shughuli zetu za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikli za Mitaa pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya Kamati imejikita katika kueleza maeneo yafuatayo:-

(a) Maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(b) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(c) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na

(d) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 3,267,492,570,200.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotelekezwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2022/2023. Miradi iliyotembelewa ni miradi ya elimu, miradi ya afya, miradi ya masoko na miradi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

## 2.1 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua miradi katika Mikoa mitano ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga pamoja na Singida ambako jumla ya miradi 12 iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilikaguliwa. Matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mwanza (Mradi Na. – 4390)

**Mheshimiwa Spika,** Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mwanza ipo katika Kijiji cha Ihushi, Kata ya Bujashi, Halmahsauri ya Wilaya ya Magu. Shule hii inajengwa kupitia mradi wa *SEQUIP*, kwa gharama ya **Shilingi 4,000,000,000,** ambapo awamu ya kwanza ya mradi inatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 3,000,000,000** kwa mfumo wa "*force Account*". Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 13 Mei, 2022 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Aprili, 2023.

### i. Faida ya Mradi

**Mheshimiwa Spika,** faida inayotegemewa kupatikana kutokana na mradi huu ni pamoja na kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana na kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora ya sekondari. Aidha, mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kupokea wanafunzi wapatao 1,000, kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita.

### ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mwanza uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kamati imetaarifiwa kuwa kwa sasa mradi unakadiriwa kufikia asilimia 85 na inatarajiwa kufikia tarehe 30/04/2023 utakuwa umekamilika.

**iii. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi**

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Shule hii unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: -

(a) Kukosekana kwa ushirikiano kati ya Idara na vitengo vya Serikali ndani ya Halmashauri;

(b) Kutofanyika kwa Upembuzi yakinifu wa kina katika utekelezaji wa mradi;

(c) Kuchelewa kuanza kwa mradi kulikotokana na sababu za kimfumo zilizosababisha Halmashauri kushindwa kubaini uwepo wa fedha za mradi kwenye akaunti mpaka ilipofika tarehe16 Machi, 2022;

(d) Kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi, mfano saruji, mabati na nondo wakati wa utekelezaji wa mradi na kupelekea gharama za ujenzi kuwa kubwa ukilinganisha na makisio yaliyopangwa, hali iliyochangia kuongezeka kwa gharama za ujenzi kwa kiasi cha shilingi milioni 23; na

(e) Kufungwa kwa mfumo wa malipo wa MUSE mwishoni mwa mwezi Juni, 2022 jambo ambalo liliathiri malipo ya mafundi na hali hii ilisababisha ujenzi kwenda kwa kasi ndogo.

**iv. Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa eneo la mradi hakuna barabara rasmi iliyojengwa kwa ajili ya kuwezesha usafirishaji wa vifaa vya ujenzi na

itakayoweza kutumika baada ya mradi kukamilika. Aidha, jengo la utawala liko nyuma ya majengo ya madarasa, hali inayofanya wageni wakiingia shuleni kuanza kuyafikia madarasa kabla ya jengo la utawala.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati ilibaini kuwa mradi huu umejengwa katika eneo lililo wazi na lenye vichaka vingi. Aidha, katika mradi huu ujenzi wa uzio haukujumuishwa wakati wa upembuzi yakinifu. Hali hii inaweza kuhatarisha usalama kwa wanafunzi watakaoanza masomo mara tu mradi ukikamilika.

**Mheshimiwa Spika**, jambo lingine lililobainika ni kuwa mradi ulianza huku kukiwa hakuna huduma za maji ambayo yalihitajika kwa ajili ya matumizi ya ujenzi. Hali hii iliongeza ugumu wa kazi. Aidha, Halmashauri ililazimika kutumia shilingi milioni 23, ambazo hazikuwa sehemu ya makadirio ya mradi, kwa ajili ya uchimbaji wa kisima, jambo ambalo liliongeza gharama ya mradi.

**Mheshimiwa Spika,** nia ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuimarisha mazingira. Ni imani ya Kamati kuwa miradi yote ya shule, zahanati na vituo vya afya inayoanzishwa nchini inazingatia utunzaji wa mazingira, hasa kwa kuweka mkakati wa upandaji wa miti maeneo miradi hiyo inapofanyika. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mwanza inayojengwa Wilayani Magu haina programu ya upandaji wa miti ili kutunza mazingira.

**v. Maoni na ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa maoni yafuatayo kuhusiana na mradi huu wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mwanza: -

(a) Wakati wa utekelezaji wa miradi yoyote ndani ya Halmashauri, pawepo na ushirikishwaji wa Idara zote za Serikali kama vile TARURA na Mamlaka ya Maji ili ziweze kuwajibika kwa pamoja na kufanikisha mradi kukamilika kwa wakati;

(b) Wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, upembuzi yakinifu ufanyike kwa kina ili kuepuka gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi mingine ya Serikali;

(c) Serikali kuweka tayari mifumo yote ya fedha ili mara tu mradi unapohitajika kuanza kusiwe na ucheleweshwaji wa aina yoyote ya kuanza kwa mradi husika; na

(d) Wakati wa utekelezaji wa miradi ya Serikali mamlaka zote zinazohusika na utekelezaji wa mradi husika kuwasiliana ili kuondo changamoto za kimaamuzi.

**2.1.2 Mradi wa Matengenezo ya Barabara ya Kisesa – Bujora (1.32 km) kwa kiwango cha lami (Mradi Na. 6401)**

**Mheshimiwa Spika,** Barabara ya Kisesa – Bujora (1.32 km) ni mojawapo ya barabara zilizopo katika mtandao wa barabara wa jumla ya Km 1,524.15 katika Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza. Barabara hii inajengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilianza kujengwa katika kiwango cha lami Km 0.4 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa fedha za mfuko wa maendeleo.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu utakapokamilika utasaidia kurahisisha usafirishaji wa watu na mizigo kutoka barabara kuu kuelekea kwenye Kituo cha Utalii cha Bujora, hali ambayo itaongeza idadi ya watu (watalii) wa nje na wa ndani kwenda kwenye kituo cha Utalii cha Bujora pamoja na kurahisisha kuzifikia huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi wa Bujora na Kisesa.

### ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi

**Mheshimiwa Spika,** awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa barabara ya Kisesa – Bujora ilishakamilika. Aidha, awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi ilianza rasmi tarehe 6 Oktoba, 2022 na unatekelezwa kwa gharama ya jumla ya **Shilingi 1,421,671,295.20**, ambapo Unatekelezwa na Mkandarasi MUMANGI CONSTRUCTION CO. LTD, S.L.P 699 – Mwanza chini ya usimamizi wa TARURA Wilaya ya Magu kwa kushirikiana na TARURA Mkoa.

**Mheshimiwa Spika,** awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huu ilitegemewa kufanyika kwa kipindi cha miezi sita, ambapo ilitegemewa kukamilika rasmi tarehe 04 Aprili, 2023. Hata hivyo, mradi hautaweza kukamilika kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa kuanza utekelezaji wa mradi. Kamati ilielezwa kuwa wakati wa kuanza utekelezaji wa mradi ilijitokeza changamoto kubwa ya wingi wa miamba ya mawe katika maeneo inakopita barabara. Kwa sababu hiyo, mkandarasi anayetekeleza mradi huu imebidi aombe kuongezewa muda wa utekelezaji kutoka kwa mwajiri, hadi tarehe 5 Juni, 2023 ili kuweza kukamilisha mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kamati inatembelea mradi huu kazi zilizofanyika ni kusafisha eneo la kazi, kuchimba tabaka la udongo usiofaa *(top soil),* kuchimba mawe (rock excavation) na kuandaa kitanda cha barabara ambapo tayari tabaka la kwanza *(G15)* limeshawekwa. Aidha, kazi ya kuweka tabaka la pili *(G45)* inaendelea kwa sasa. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 38.

### iii. Changamoto zilizojitokeza wakati wa Utekelezaji wa Mradi

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ambazo Kamati ilizibaini katika utekelezaji wa Mradi huu ni pamoja na: -

(a) Kuwepo kwa miundombinu ya huduma mbalimbali za jamii kama vile maji, simu na umeme kwenye maeneo inakopita barabara, hali iliyopelekea miundombinu hiyo kuharibiwa, na hivyo Wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya mradi kukosa huduma muhimu;

(b) Kuwepo na majengo ya nyumba za kuishi pamoja na uzio kwenye maeneo barabara inakopita; na

(c) Uwepo na mawe mengi sana kwenye eneo la barabara.

**iv. Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini mambo kadhaa kama ifuatavyo: -

**(a) Ucheleweshaji wa mradi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa utekelezwaji wa mradi kwa sababu iliyoelezwa kuwa ni kutokana na uwepo wa mawe mengi kwenye eneo inakopita barabara, hali iliyosababisha kuongezeka kwa kazi na hivyo kumlazimisha Mkandarasi kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa sababu hii inatokana na upembuzi yakinifu kufanywa kwa kiwango hafifu. Kamati inaamini kuwa kama upembuzi yakinifu ungefanyika kwa kiwango kinachotakiwa suala la wingi wa mawe lingeonekana wakati wa upembuzi yakinifu na hivyo lingewekewa makadirio sahihi.

**(b) Kuwepo kwa miundombinu mbalimbali ya huduma kwa wananchi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kuwa sababu nyingine ya kuchelewa na kuleta ugumu wakati wa utekelezaji wa mradi ni kuwepo kwa miundombinu ya huduma mbalimbali za jamii kama vile maji, simu na umeme kwenye maeneo inakopita barabara. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa

sababu hii pia imesababishwa na udhaifu wakati wa upembuzi yakinifu. Aidha, hali hii imesababishwa pia na kutokuwa na mawasiliano miongoni mwa idara na taasisi za Serikali katika ngazi ya Halmashauri na Mkoa. Kamati inaamini kuwa kama *TARURA* ingekuwa na mawasiliano na idara na taasisi nyingine za Serikali ndani ya Halmashauri na Mkoa, kama vile RUWASA na TANESCO changamoto hizi zingewekewa mkakati wa kutatuliwa wakati wa kuanza kwa utekelezaji wa mradi.

**(c) Uwepo wa majengo maeneo inamopita barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kuwa kuwepo na majengo ya nyumba za kuishi pamoja na uzio kwenye maeneo barabara inakopita kumeongeza ukubwa wa kazi na muda, na kwamba Kamati inaamini kuwa kuna ongezeko la gharama za utekelezaji wa mradi kwa *TARURA* yenyewe na taasisi nyingine za Serikali kama vile *TANESCO* na *RUWASA* ingawa mkandarasi anakiri kuwa hakuna gharama iliyoongezeka. Kamati inaona kuwa uwepo wa majengo haya maeneo ya mradi yaliyosababisha kuongezeka kwa muda, kazi na gharama ya utekelezaji wa mradi ni matokeo ya upembuzi yakinifu usiozingatia mazingira.

**(d) Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati katika utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo: -

(a) Kutokana na kubainika kutokuwepo kwa ushirikiano kati ya Idara na vitengo vya Serikali ndani ya Halmashauri, Kamati inashauri kuwa wakati wa utekelezaji wa miradi yoyote ndani ya Halmashauri, idara zote za Serikali zishirikishwe na kuwajibika kwa pamoja; na

(b) Upembuzi yakinifu ufanyike kwa kina ili kuepuka gharama zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi mingine ya Serikali.

### 2.1.3 Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mjini Kati – Mwanza

**Mheshimiwa Spika**, Soko Kuu la Mjini Kati linajengwa katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa fedha za Ruzuku kutoka Serikalini kiasi cha **Shilingi 38,514,709,000.00** ambazo zilipatikana baada ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuingia mkataba na Wizara ya Fedha wa kupatiwa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Kimkakati.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya ukamilikaji wa mradi kutakuwa na ongezeko la mapato ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza, kutoka **Shilingi Milioni 720** zilizokuwa zinakusanywa awali hadi kufikia **Shilingi bilioni 3.8** kwa mwaka. Aidha, takriban wafanyabiashara 1,400 wanatarajiwa kupata maeneo mazuri ya kufanya biashara pamoja na kuliweka Jiji la Mwanza kuwa la kisasa zaidi.

**ii. Hali ya utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Soko Kuu la Mjini kati ulianza kutekelezwa mwezi Februari, 2019, baada ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuingia mkataba wenye thamani ya **Shilingi 23,367,192,262.81** na Mkandarasi *Mohammed Builders Ltd.* na, hatua ya utekelezaji wa mradi Iliyofikiwa wakati wa ukaguzi wa Kamati ni **asilimia 87%.**

**iii. Changamoto zilitojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na faida zilizotajwa kupatikana kwenye mradi huu, Kamati imebaini changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) Mradi kuchelewa kukamilika katika muda uliopangwa kulikosababishwa na Wakandarasi kutofanya upembuzi yakinifu wa mradi kwa umakini hivyo kukosa kubaini changamoto ya uwepo wa chemchemi za maji katika eneo la mradi; na

(b) Kupanda kwa gharam za vifaa vya ujenzi.

**iv. Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa iliyowasilishwa, Kamati ilifanya uchambuzi kama ifuatavyo: -

**(a) Upungufu wa vizimba**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa eneo linapojengwa soko ni eneo ambalo wamachinga wapatao 1,400 walihamishwa kwa lengo la kuboresha mazingira yao ili waweze kufanya biashara katika maeneo toshelevu na yaliyoboreshwa. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa ramani ya ujenzi wa soko hili imetenga vizimba 360 ambavyo ndivyo vitakavyotumika na wamachinga. Idadi hii ya vizimba ni ndogo sana ukilinganisha na idadi ya wamachinga walioondolewa eneo hilo. Kamati inatia shaka kama dhumuni la msingi la ujenzi wa soko hili halitafikiwa. Aidha nia ya Serikali ya kuwaondoa wamachinga mitaani haitafikiwa;

**(b) Kuchelewa kumalizika kwa mradi katika muda uliopangwa**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine Kamati imebaini kuwa mradi umechelewa kumalizika katika muda uliopangwa kutokana na kuwepo kwa chemchemi nyingi na kubwa za maji. Hali hii ilisababisha utekelezaji wa mradi huu kuongeza shughuli nyingine ya kudhibiti chemchemi hizo ambazo awali hazikuwa sehemu ya makadirio ya ujenzi wakati wa upembuzi yakinifu. Hii ilitokana na wataalam waliofanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kutofanya kazi yao kwa umakini;

**(c) Ramani ya Ujenzi wa Soko Kutokidhi Dhumuni la Awali la Ujenzi wa Soko**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa soko hili limeweka maeneo mengi sana ya sehemu ya burudani, michezo ya watoto na maduka makubwa. Awali soko hili lilipangwa kujengwa ili kupunguza wamachinga wanaosambaa mitaani na kuwaboreshea mazingira yao. Hata hivyo dhumuni hilo sasa limepindishwa na kuweka eneo

hili kuwa kama mkusanyiko wa maduka mbalimbali *(shopping mall)* na si soko la wafanyabiashara wadogo wadogo.

Kamati imebaini kuwa soko hili sasa limeweka maeneo makubwa kwa ajili ya kufanya biashara za maduka, kuuza vileo (Baa) na sehemu ya michezo ya Watoto.

**(d) Kukosekana Miundombinu ya Kuzuia Majanga ya Moto**

**Mheshimiwa Spika**, vile vile Kamati katika ukaguzi wake kwa soko hili imebaini kuwa bajeti iliyopitishwa ilipitishwa huku kukiwa kumeondolewa miundombinu ya moto. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa mradi ikalazimika kufanyika tathmini upya ya sababu ya kutowekwa miundombinu ya kuzimia moto hivyo kuona haja ya kuifanyia marekebisho ramani hiyo kwa kuweka miundombinu ya kuzuia na kudhibiti majanga ya moto. Hali hii ilisababisha kuongezeka tena gharama ya ujenzi na hivyo kuisababishia Serikali pamoja na wafanyabiashara hasara kubwa.

**v. Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa Mradi huu, na hasa changamoto zilizoelezwa kukwamisha mradi huo, kwa kuwa changamoto hizo zilitakiwa kubainika kabla ya mradi kuanza kutekelezwa na kupatiwa ufumbuzi wa kina. Kutokana na hayo Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

(a) Kamati haijaridhishwa na utendaji kazi wa Mkandarasi anayetekeleza mradi huo Mohammed Builders Ltd. Kutokana na gharama na kasi ya utekelezaji kwa ujumla. Kamati inafahamu kuwa mhandisi huyu kuna miradi mingi amejenga kama vile Dodoma, (Soko la Ndugai) na Arusha. Kwa kuwa Kamati imetilia shaka mradi huu, na kwa kuwa Kamati inaitaka kufahamu kujua kwa kuwa ana historia ya kutokamilisha miradi anayopatiwa kwa wakati, kwa sababu mbalimbali na hivyo kuisababishia Serikali kuingia gharama

zisizo za lazima. Kamati inashauri Serikali kufanya tathmini ya utendaji kazi wa mkandarasi huyu na kutoa mapendekezo yatakayofaa;

(b) Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie upya ugawaji wa vizimba vya biashara katika soko hilo, kwa wafanyabiashara wamachinga;

(c) Serikali ipunguze utengaji wa huduma nyingine zisizo za wamachinga ili kuwapa nafasi wamachinga ambao soko lilijengwa kwa ajili yao;

(d) Serikali ifanye tathimini ya ujenzi wa Soko la Mjini Kati la Jijini Mwanza ili kuona kama thamani ya fedha imefikiwa wakati wa utekelezaji wa mradi huu;

(e) Aidha, Kamati haijaridhishwa na utendaji kazi wa Mkandarasi anayetekeleza mradi huo, ambaye ni Mohammed Builders Ltd kutokana na soko hilo kujengwa kwa gharama kubwa na kasi ndogo ya ujenzi wa soko hilo. Kamati inaishauri Serikali kuuangalia upya mkataba iliyoingia na mkandarasi huyu; na

(f) Kamati inaitaka TAMISEMI kuhakikisha kuwa Halmashauri zote nchini zinakatia Bima masoko yote likiwemo Soko la Mjini Kati Mwanza kwa ajili ya kuyakinga na majanga mbalimbali yakiowemo ya moto.

### 2.1.4 Ujenzi wa Mradi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Shinyanga

**Mheshimiwa Spika**, Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa Mikoa 10 nchini inayotekeleza mradi wa ujenzi wa shule za sekondari za wasichana za Mkoa awamu ya kwanza chini ya Mradi wa kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP). Shule hii inajengwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Mtaa wa Butengwa uliopo katika Kata ya Ndembezi.

#### i. Faida ya mradi

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu utakapokamilika utaongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya Sekondari kwa idadi kubwa ya watoto wa kike, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana na kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora ya sekondari. Aidha, mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kupokea wanafunzi wapatao 1,000 na zaidi, kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita.

**ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga iliidhinishiwa na kupokea **Shilingi 3,000,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa shule hii. Kiasi hiki cha fedha kilipokelewa tarehe 25 Januari, 2022 kwa ajili ya kuanza ujenzi huo kwa awamu ya kwanza. Mradi huu unatekelezwa kwa kupitia mfumo wa manunuzi wa *Force Account*. Mradi huu unatarajiwa kukamilika kwa **Shilingi 4,000,000,000**. Hadi kufikia sasa kiasi cha **Shilingi 3,000,000,000** kimepokelewa. Aidha, hadi tarehe 28, Februari 2023 kiasi cha fedha kilichotumika ni **Shilingi 2,934,197,806.09.**

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri imefanikiwa kukamilisha miundombinu ambayo itawezesha kupokea wanafunzi wa kidato cha tano wanaotarajiwa kuanza masomo Julai, 2023.

**iii. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto kadhaa zilizjitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu kama ifuatavyo: -

(a) Fedha za kutotosheleza kutokana na kupanda kwa gharama ya malighafi za ujenzi kinyume na makadirio yaliyowekwa mwanzo; na

(b) Kusimama kwa ujenzi wa jengo la Bwalo kwa zaidi ya mwezi mmoja kutokana na mgogoro wa kimkataba kati ya Halmashauri na Fundi Mjenzi;

**iv. Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kuijadili taarifa ya mradi huu Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini mambo kama ifuatavyo:-

**a) Uzingatiaji wa Ramani za Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa wakati wa ujenzi wa bwalo kulikuwa na kiasi kikubwa cha kutozingatia maelekezo ya Wizara kuhusu ramani ya ujenzi. Kamati ilibaini kuwa jengo la utawala linalojengwa lina ramani ya peke yake. Aidha, ramani ya ujenzi wa jengo la Bwalo inatofautiana na ile iliyoelekezwa na TAMISEMI.

**b) Udhaifu wa Upembuzi Yakinifu**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa utekelezaji wa mradi huu ilijitokeza changamoto ya ulazima wa kuchimba msingi mkubwa zaidi kutokana na aina ya udongo wa maeneo mradi unakofanyika. Aidha, kutokana na ramani ya ujenzi wa bwalo lililohitaji ujenzi wa msingi mkubwa mkandarasi alilazimika kuongeza kuchimba Kwenda chini kutumia saruji, nondo, kokoto na nguvukazi ambazo awali wakati wa upembuzi yakinifu haikuwa sehemu ya makadirio. Hali hii iliongeza gharama ya ujenzi wa mradi na kumfanya mkandarasi kuomba kuongezewa zaidi ya Shilingi milioni 60 ili kukamilisha jengo hilo.

**c) Ramani ya choo kuwa eneo lisilo sahihi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa choo kilichojengwa katika shule hii kimejengwa eneo ambalo liko karibu kabisa na madarasa. Hali hii inaweza kusababisha, kama hapatakuwa na usafi wa kutosha, kuleta hewa mbaya madarasani. Aidha, choo hicho kimejengwa katikati ya madarasa hivyo kitanyima faragha kwa watumiaji. Pia choo kimejengwa upande ambao upepo huvuma kuelekea madarasani na katika maabara.

**d) Ukamilishaji wa Mradi kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa Halmashauri imejitahidi sana katika kuukamilisha mradi huu kulingana na muda uliopangwa.

**v. Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huo wa taarifa ya mradi, Kamati inatoa maoni kama ifuatavyo:-

**(a) Uzingatiaji wa ramani**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kubaini kuwa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Shinyanga haukufuata ramani iliyopendekezwa, hasa ujenzi wa choo kuwa katikati ya madarasa Kamati inashauri kuwa wakati wa uchoraji wa ramani zote zinazopitishwa wakati wa ujenzi wa shule hizi kuwe na uwakilishi kutoka halmashauri;

**(b) Kukwama kwa ujenzi wa bwalo**

Serikali iongeze fedha kwa ajili ya umailiziaji wa jengo la bwalo ambalo limekwama kutokana na upungufu wa fedha.

**(c) Kuanza kudahili wanafunzi**

Kwa kuwa shule hii imeshakamilika kwa zaidi ya asilimia 70 Kamati inashauri Serikali kuanza udahili mwaka huu ili kuwe na matumizi bora ya thamani ya fedha iliyotumika katika ujenzi wa mradi huu.

**2.1.5 Ujenzi wa Jengo la Utawala Tarime Vijijini (Mradi Na. 6389)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 15 Machi, 2023 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitembelea na kukagua mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, ambao unatekelezwa katika Kata ya Nyamwaga, kwa lengo la kuboresha mazingira ya utoaji wa wa huduma kwa Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ambapo huduma zote zitaweza kutolewa katika eneo moja *(One stop centre)*.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, faida zinazotarajiwa kupatikana baada ya ukamilikaji wa mradi huu ni pamoja na uboreshaji mazingira ya utoaji huduma kwa Watumishi na pia kuhudumia Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime katika sehemu moja *(One stop centre)*.

**ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa thamani ya mradi huu ni **Shilingi 2,900,000,000**, na utekelezaji wake ulianza tarehe 10 Mei, 2021 baada ya kupokea fedha za awamu ya kwanza **Shilingi 1,000,0000,000** kutoka Serikali Kuu, ambapo mradi huu unatekelezwa kwa njia ya ***Force Account*** na Fundi Mjenzi ni SUMA JKT, chini ya usimamizi wa watalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ambapo usanifu wa michoro na mahitaji ya vifaa vya ujenzi *(schedule of materials)* yameandaliwa na wataalam kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Idara ya Miundombinu.

**iii. Changamoto Zilizobainika Wakati wa Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa** Spika, wakati wa ukaguzi wa mradi huu, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zikiwemo: -

(a) Fundi Mjenzi (SUMA JKT) kuweka nguvu kazi ndogo (Mafundi na Vibarua);
(b) Utekelezaji wa mradi kukumbwa na kufungwa kwa mfumo wa malipo ya Serikali wakati wa mwisho wa mwaka wa fedha na hivyo kusababisha manunuzi ya vifaa vya ujenzi kukwama na malipo ya fundi kutofanyika kwa wakati; na
(c) Kuadimika na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi mfano saruji pindi vinapohitajika ukilinganisha na kipindi cha makadirio ya ujenzi wa jengo yalipoandaliwa.

**iv. Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa taarifa ya mradi huu, Kamati inatoa maoni kama ifuatavyo: -

**(a) Umailiziaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mradi huu ni muhimu sana kwa utoaji huduma kwa wananchi wa Tarime Vijijini Kamati inashauri Serikali kusimamia ujenzi wa mradi huu na kuhakikisha kuwa unakwisha kwa haraka.

**(b) Kumaliza Tofauti Iliyopo Kati ya Uongozi wa Halmashauri na Fundi Mjenzi**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kumekuwa na mawasiliano dhaifu kati ya Fundi Mjenzi na uongozi wa Halmashauri. Aidha Kamati imebaini kuwa fedha zote kwa ajili ya mradi huu imeshatolewa, Kamati imeenda mbali zaidi na kubaini kuwa kuna mabishano na yasiyona tija kati ya uongozi wa Halmashauri na Fundi Mjenzi juu ya ujenzi wa mradi huu. Kamati inashauri Serikali kuingilia kati na kukaa na makundi haya mawili ili kumaliza changamoto ya mawasiliano iliyopo.

**2.1.6 Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi (Mradi Na. 5421)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 12 Januari, 2019 katika Kijiji cha Sengerema Kata ya Dutwa Mkoani Simiyu kwa gharama ya **Shilingi 3,472,770,573.59,** ikiwa ni fedha kutoka Mfuko Mkuu. Mradi huu unajengwa kwa Mfumo wa ***Force Account*** chini ya usimamizi wa Kamati tano zilizoundwa ili kusimamia ujenzi huo, ambazo ni Kamati ya Usimamizi, Kamati ya Ujenzi, Kamati ya Manunuzi, Kamati ya Mapokezi na Kamati ya Utunzaji wa vifaa.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, faida kubwa itakayopatikana kutokana na mradi huu ni kuwapatia wananchi wa Bariadi huduma

bora za afya zenye kukidhi viwango vilivyowekwa na Wizara ya Afya.

**ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi, unatekelezwa kwa awamu sita (6) tofauti. Ambapo hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa Kamati, hali ya utekelezaji wa awamu hizo umefikia kati ya **asilimia 55** na **asilimia 100**. Aidha, baadhi ya majengo ya Hospitali hii kama vile jengo la utawala, jengo la wagonjwa wa nje, jengo la mionzi, jengo la maabara, jengo la kufulia, jengo la kuhifadhia dawa na jengo la wazazi yameshakamilika na yameanza kutoa huduma kwa wananchi.

**iii. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa changamoto zilizobainiwa na Kamati katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na: -

(a) Ubovu wa barabara inayoelekea kwenye mradi;

(b) Ukosefu wa mipaka ya uhakika katika eneo la mradi;

(c) Kukosekana kwa wataalamu wa kutoa mafunzo ya kutumia vifaa tiba vilivyopokelewa hospitalini hapo kutoka Serikali Kuu. Miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na vifaa tiba mbalimbali vifaa vya upasuaji, ambavyo ni mashine ya usingizi (Universal Anasthetic Machine) 1, kitanda cha upasuaji (Operating Table) 1, taa ya upasuaji (Operating lamp) 1, mashine 2 za kutakasa vifaa tiba (Autoclave), na vifaa tiba vingine ambavyo ni mashine ya X-ray 1, Defibrilator 2, Crush cut Troley 1, Patient Troley 2 na Kompyuta ya kisasa 1 na mashine kubwa ya kukaushia nguo (Dry linen machine);

(d) Upembuzi yakinifu (Feasibility Study) kutofanyika kwa umakini; na

(e) Upungufu wa nyumba za watumishi.

**iv. Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea na kuijadili taarifa ya mradi huu Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini mambo kadhaa kama ifuatavyo: -

**(a) Ukosefu wa mafunzo ya utumiaji wa vifaa vya matibabu na vitendanishi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa Serikali tayari imeshapeleka vifaa kama vile mashine za X-Ray na Utrasound kwenye hospitali hiyo. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa pamoja na vifaa hivyo kupelekwa katika hospitali hii lakini havina wataalam wa kuvitumia. Kamati imebaini kuwa Wizara iliahidi kupeleka wataalam hao lakini bado hawajapelekwa.

**(b) Kuwepo kwa mipaka iliyo wazi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa eneo kubwa la hospitali hii liko wazi na mipaka yake haijawekewa vigingi. Hali hii inaweza kusababisha wananchi kuvamia eneo la hospitali kwa shughuli mbalimbali za kijamii.

**v. Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto zilizobainiwa na Kamati wakati wa ukaguzi wa mradi huu, yafuatayo ni maoni ya Kamati: -

(a) Halmashauri zinapotaka kuanza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo wahakikishe kuwa katika maeneo ya mradi wanaweka mikakati Madhubuti ya kuweza kufikisha huduma muhimu na za msingi kwenye maeneo ya mradi ili kuuwezesha mradi kuweza kutekelezeka kwa urahisi ili uweze kuleta tija iliyokusudiwa na Serikali ya kutaka kusogeza huduma muhimu kwa wananchi wake;

(b) Uongozi wa Halmashauri ya Bariadi ufanye utaratibu wa kubainisha mipaka ya hospitali ili kuepusha migogoro ambayo inaweza kujitokeza kwa siku za baadaye baina yao na wananchi wanaozunguka eneo la mradi;

(c) TAMISEMI wanapopeleka vifaa vipya kwenye miradi ya maendeleo kama vile zahanati na hospitali, iweke utaratibu wa kutoa mafunzo juu ya matumizi ya vifaa hivyo kwa Watendaji wa hospitali zilizopatiwa vifaa, ili kutimiza lengo zuri la Serikali ya Awamu ya Sita, la kusogeza huduma za afya karibu na wanachi, badala ya kuviacha vikikaa muda mrefu bila kutumika;

(d) upembuzi yakinifu uwe unafanyika wakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuiondolea Serikali hasara ya kufanya ukarabati wa mara kwa mara kwa uharibifu unaoweza kutokea kwenye miradi hiyo; na

(e) Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ufanye haraka utaratibu wa kujenga nyumba za watumishi katika eneo la mradi ili kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu na kuongeza tija katika utendaji kazi wao.

**2.1.7 Mradi wa Uboreshaji wa Kituo cha Afya Kambarage (Mradi Na. 5410).**

**Mheshimiwa Spika**, Manispaa ya Shinyanga ilipokea kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya kujenga Hospitali mpya ya Manispaa. Hata hivyo, Manispaa ya Shinyanga ilipata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kubadilisha matumizi ya fedha za awali **Shilingi 500,000,000.00** kwenda kituo cha Afya Kambarage kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu. Hii ilitokana na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga inayotumika sasa kuwa katika mpango wa kukabidhiwa Manispaa ya Shinyanga na kuwa Hospitali ya Manispaa kutokana na Mkoa kujenga Hospitali ya Rufaa mpya eneo la Mwawaza.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, faida itakayopatikana kutokana na mradi huu ni kuboreka kwa utoaji wa huduma mbalimbali za afya katika Kata ya Kambarage na wakazi wa maeneo ya Halmashauri ya Manispaa wanaozunguka kata hii, ambapo huduma za uchunguzi, wagonjwa wa nje na wagonjwa watakaolazwa zitaboreka zaidi.

**ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 10 Machi, 2023 ujenzi huu ulikuwa umegharimu kiasi cha **Shilingi 405,043,814** ikiwa ni malipo ya mafundi na ununuzi ya vifaa mbalimbali vya ujenzi, ambapo mchango wa wananchi wa Kata ya Kambarage katika mradi huu inakadiriwa kuwa **Shilingi. 400,000,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utendaji mzuri wa Halmashauri katika suala zima la usimamizi wa ujenzi wa hospitali hii. Aidha, Kamati imeridhishwa na kazi nzuri iliyofanywa na fundi mjenzi hasa katika sehemu ya umaliziaji *(finishing)*.

**2.1.8 Mradi wa Ujenzi wa Soko la Halmashauri ya Shinyaga (Machinga) (Mradi Na. 4946)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa ujenzi wa Soko la Halmashauri ya Shinyanga, ambalo ni soko la Mitumba lililopo katika Kata ya Ngokolo Manispaa ya Shinyanga ulianza kutekelezwa tarehe 01 Novemba, 2022 na ulitarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Machi, 2023. Mradi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi 480,000,000.00** kutoka mapato ya ndani. Mpaka kipindi cha ukaguzi wa Kamati, fedha kiasi cha **Shilingi 376,770,000.00** kilikuwa kimeshatumika, na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni asilimia 90.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mabanda katika soko hili, umezingatia mahitaji ya Watu Wenye Mahitaji Maalum ambapo njia za watu wenye ulemavu *(ramps)* zimejengwa ili

kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum kupata huduma kwa urahisi.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wa mitumba na kuiwezesha Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kukusanya mapato makubwa kwani wafanyabiashara wa mitumba watafanya biashara katika eneo moja linalotambulika hivyo kuwezesha kurahisisha ukusanyaji wa mapato na kupendezesha mji. Aidha, Wafanyabiashara wadogo 200 watapata vizimba vya kuuzia bihashara zao kwa wakati mmoja.

**2.1.9 Mradi wa Ujenzi Mabanda 106 ya Biashara katika Soko Kuu la Manispaa ya Shinyanga (Mradi Na. 4946)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa ujenzi wa vyumba 106 vya Wafanyabiashara katika Soko Kuu Kata ya Mjini Manispaa ya Shinyanga ulianza kutekelezwa tarehe 01 Oktoba, 2022 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2023. Mradi huu unatarajiwa kuhudumia Wafanyabiashara 106 na unatekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani, ambapo mpaka kukamilika mradi huu, umekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,840,000,000.00** zinazotokana na mapato ya ndani.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilika mradi huu utaboesha mazingira ya wafanyabishara waliokuwa wanafanya biashara zao katika vyumba ambavyo vimechakaa na havikuwa na muonekano mzuri wa kimazingira kuendana na mazingira ya nje ya soko. Mradi huu pia utaiwezesha Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kukusanya mapato kwa urahisi, kupendezesha mji pamoja na kuongeza wigo wa makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

**ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha ukaguzi wa Kamati, mradi huu ambao unatekelezwa na mafundi wazawa, ulikuwa umefikia **asilimia 48,** na hatua ya ujenzi iliyokuwa inaendelea ilikuwa ni kufunga nondo za sakafu ya ghorofa ya kwanza na kusimika nguzo wima na nguzo mlalo za varanda. Aidha, ujenzi wa vyumba hivi umezingatia mahitaji ya watu wenye mahitaji maalum ambapo njia za watu wenye ulemavu *(ramps)* zitajengwa ili kuwasaidia kupata huduma kwa urahisi.

### 2.1.10 Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Ikungi (Mradi Na. 5401)

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ikungi iliyopo mkoani Singida umeanza kutekelezwa mwezi Juni, 2020 kwa fedha kutoka Serikali Kuu. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia utaratibu wa *force account*. Mradi huu unatekelezwa katika Kijiji cha Mahambe kilichopo katika Kata ya Unyahati kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 30.

### i. Faida ya Mradi

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kutoa huduma bora za afya kwa Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi wapatao 411,262 na wananchi wengine wote watakaofika kupata huduma katika khospitali hii.

### ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatakelezwa kwa awamu nne kulingana na mapokezi ya fedha kutoka Serikali Kuu, ambapo mpaka sasa fedha zilizokwishakupokelewa ni **Shilingi 3,140,000,000** na mchango wa Halmashauri ni **Shilingi 14,104,000. Aidha,** majengo ya hospitali hiyo yamefikia hatua mbalimbai za umaliziaji, na baadhi ya majengo yameshaanza kutumika.

### iii. Changamoto Zilizojitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Mradi

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa inayokabili utekelezaji wa mradi huu ni kutokamilika kwa wakati majengo tisa ya *OPD*, maabara, chumba cha famasi, utawala, mionzi, chumba cha kufulia, wodi ya wazazi na kichomea taka na njia za wagonjwa (walkways) kunakotokana na fedha kiasi cha **Shillingi 325,193,815** zilizovuka mwaka wa fedha 2019/2020 kuchukuliwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, pamoja na juhudi kubwa inayofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kuomba kurejeshewa fedha hizo, lakini mpaka sasa bado hazijarejeshwa.

**iv. Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa ya mradi huu Kamati ilibaini kuwa mradi wa ujenzi wa hospitali hii umefikiwa kwa kiwango kilichotakiwa. Aidha, Kamati inaipongeza sana Serikali na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwa ushirikiano kati ya idara za Serikali kama vile *TARURA*, *TANESCO* na Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Ikungu ambao wamewezesha kufikisha huduma za umeme, barabara na maji vilivyorahisisha ujenzi wa mradi huu. Vilevile Kamati inaipongeza halmashauri kwa kujumuisha upandaji wa miti katika maeneo ya hospitali hii sambamba na ujenzi wa mradi huu.

**v. Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, maoni na ushauri wa Kamati katika utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo: -

(a) Hazina wawe wanatoa fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati mwafaka na si kusubiria mwaka wa fedha unapokaribia kwisha, hali inayozipelekea Halmashauri kushindwa kumalizia matumizi ya fedha hizo na hivyo kukwamisha utekelezaji wa mradi uliolengwa;

(b) Kamati inaendelea kutoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa wanapotaka kuanzisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi katika Halmashauri zao wahakikishe kuwa wanaweka mikakati madhubuti ya kuweza kufikisha huduma muhimu na za msingi kwenye

maeneo ya miradi kama vile maji, umeme na barabara zinazopitika wakati wote, ili kuuwezesha mradi kutekelezeka kiurahisi;

(c) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa waweke utaratibu mzuri wa kutoa mafunzo kwa wakati juu ya utumiaji wa vifaa tiba na vitendanishi vinavyopelekwa kwenye hospitali mbalimbali nchini, ili lengo lililokusudiwa liweze kutimia kwa wakati; na

(d) Uongozi wa Halmashauri kuongeza idadi ya miti inayotakiwa kupandwa ili kuboresha mazingira ya eneo la mradi unapotekelezwa.

**2.1.11 Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Mkoa wa Singida (Mradi Na. 4390)**

**Mheshmiwa Spika**, Shule ya Wasichana ya Mkoa wa Singida inajengwa katika Wilaya ya Manyoni, Halmashauri ya Manyoni, Tarafa ya Kilimatinde, Kata ya Solya na Kijiji cha Solya. Shule hii inajengwa kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 87, ambalo limetolewa na kijiji kwa kushirikiana na wananchi wenye ardhi katika eneo hilo. Ujenzi wa shule hii ulianza rasmi baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kupokea awamu ya kwanza fedha kiasi cha **Shilingi 3,000,000,000.00**. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia mfumo wa "*Force Account*" ambapo inazingatia miongozo kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI inayojumuisha michoro, mpango wa manunuzi ya vifaa na mpangilio.

**i. Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha Watoto wa Kike hasa walio maeneo ya vijijini kupata sehemu nzuri ya kusomea na hivyo kutekeleza adhma ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kumkomboa mtoto wa kike kwa kumpatia elimu bora. Aidha, watoto wa kike watapata mazingira bora ya kusomea.

**ii. Hali ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 16 Machi, 2023 ujenzi wa majengo wa shule hii ulifikia **asilimia 80.** Hata hivyo kazi nyingi zilizobaki ni kwenye jengo la Bwalo ambalo kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa ukuta na ufungaji wa mbao za sahani kwa ajili ya lenta ya kwanza.

**iii. Changamoto Zilizojitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua nzuri iliyofikiwa kwenye utekelezaji wa mradi huu, pia zipo changamoto zilizojiteokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu kama ifuatavyo: -

(a) Kutokana na Wilaya ya Manyoni kuwa katika bonde la ufa, tahadhari kubwa imechukuliwa wakati wa ujenzi kwa kuongeza baadhi ya nguzo pamoja kujenga kuta zuio *(retaining wall)* ili kuimarisha majengo, hivyo kuongeza gharama za ujenzi;

(b) Baadhi ya kazi kutokuwepo katika mpango wa manunuzi *(schedule of materials)* ikiwemo gharama za uunganishaji wa umeme kutoka katika chanzo, usafishaji wa eneo, na gharama za maji ya kujengea;

(c) Kuongezeka kwa idadi ya bati, kofia, moramu (vifusi), tofali na mbao, kutoendana na uhitaji halisi wa michoro ya majengo; na

(d) Uelewa mdogo wa matumizi ya mfumo wa *force account* miongoni mwa wahusika wakuu katika Halmashauri uliosababisha ujenzi kuchukua muda mrefu kuanza kutekelezwa kutokana na kukosekana kwa maelekezo sahihi.

**iv. Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ukaguzi wa mradi huu, Kamati inaishauti Ofisi ya Rais-TAMISEMI wahakikishe kuwa upembuzi yakinifu unafanyika kwa uhakika ili kuweza kuondoa tofauti

*(variation)* ya bei za vifaa vya ujenzi na fedha ambao unaweza kutokea na hivyo kusababisha mradi kuchelewa kukamilika au kujengwa kwa kulipua ili mradi ukamilike na hivyo kuipa hasara Serikali.

## 2.2 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga na Singida, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na ingependa kutoa maoni na ushauri wa ujumla kama ifuatavyo: -

i. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wahakikishe Halmashauri zote zinatumia ramani na miongozo iliyotolewa katika ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya na shule za sekondari;
ii. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wahakikishe kunakuwa na uwiano wa kiasi cha fedha kilichotolewa na ubora wa kazi iliyofanyika katika ujenzi wa vituo vya afya na shule za sekondari;

iii. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wahakikishe wahakikishe upembuzi yakinifu *(feasibility study)* wa miradi mbalimbali ya maendeleo unafanyika kwa kina ili kuweza kuondoa changamoto za tofauti *(variation)* ya gharama zinazotumika katika majengo hayo hali inayoathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama kutokana na kuongeza kazi;

iv. Serikali iweke utaratibu wa kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha ili kuepusha ubadhilifu na hivyo kuwezesha kupatikana kwa thamani ya fedha *(value for money);* na

v. Linapokuja suala zima la utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri, Kamati inashauri kuwa

pawepo na ushirikishwaji wa karibu kati ya Idara na vitengo vya Serikali ndani ya halmashauri ili kuwezesha utekelezaji wa miradi kufanyika bila ya kuwa na mikwamo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Wizara pamoja na Sekretarieti za mikoa kuwasilisha Bajeti zao kwa mafungu 28 Kuanzia tarehe 20 hadi 29 Machi, 2023, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

### 3.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo Nane (8). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi Maoni na Ushauri.** Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu Kamati itaendelea kuyasisitiza katika Taarifa hii likiwemo suala la bakaa.

### 3.2 UCHAMBUZI WA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia **Fungu 56** (Makao Makuu ya Wizara), Fungu 02 (Tume ya Utumishi wa Walimu) na Mafungu 26 kutoka Sekretarieti za Mikoa katika mwaka wa

fedha 2022/2023 ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,071,730,886,415.50.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,341,953,000.00** sawa na **asilimia 0.4** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Elimu Kibaha, **Shilingi 10,986,269,522.00 sawa na asilimia 1.02** kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam, **Shilingi 9,757,074,400.00** sawa na **asilimia 0.9** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, **Shilingi 3,663,155,634.00** sawa na **asilimia 0.34,** kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, **Shilingi 30,447,063,547.50** sawa na **asilimia 2.84** kutoka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini, **Shilingi 249,281,312.00** sawa na **asilimia 0.023** Kutoka Makao Makuu ya Mikoa na **Shilingi 1,012,286,089,000.00** sawa na **asilimia 94.45** kutoka Halmashauri zote nchini. Jedwali Na 1 linaeleza zaidi.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, hadi Mwezi Februari 2023, jumla ya **Shilingi 647,886,031,554.41** sawa na **asilimia 60.45** ya lengo zilikusanywa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,867,429,435.00** sawa na **asilimia 0.59** zilikusanywa kutoka Shirika la Elimu Kibaha, **Shilingi 7,324,179,681.33** sawa na **asilimia 0.68** kutoka Wakala wa Mabasi yaendayo Kasi (BRT), **Shilingi 3,867,429,435.00** sawa na **asilimia 3.61** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, **Shilingi 1,261,101,972.95** sawa na **asilimia 0.19** kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, **Shilingi 10,675,082,691.87** sawa na **asilimia 1.65** kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini, **Shilingi 39,904,100.00** sawa na **asilimia 0.006** kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo, **Shilingi 92,266,789.00** sawa na **asilimia 0.014** kutoka Makao Makuu ya Mikoa na **Shilingi 625,319,158,432.00** sawa na **asilimia 96.5** kutoka halmashauri. **Kielelezo Na. 2 linatoa mchanganuo zaidi.**

**Kielelezo Na. 1**: Hali ya ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023

| Na. | Taasisi | Makisio | Kiasi Kilichokusanywa | Kiasi kilichobaki | Asilimia ya makusa nyo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shirika la Elimu Kibaha | 4,341,953,000 | 3,867,429,435 | 474,523,565 | 89.07 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar (BRT) | 10,986,269,522 | 10,675,082,691.87 | 311,186,830.13 | 97.16 |
| 3. | Chuo cha Serikali za Mitaa | 9,757,074,400 | 3,867,429,435.00 | 5,889,644,965 | 39.6 |
| 4. | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 3,663,155,634 | 1,261,101,972.95 | 2,402,053,661.05 | 34.4 |
| 5. | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini | 30,447,063,547.50 | 10,675,082,691.87 | 19,771,980,855.63 | 35.06 |
| 6. | Makao Makuu ya Mikoa | 249,281,312.00 | 92,266,789.00 | 157,014,523 | 37.01 |
| 7. | Shirika la Masoko ya Kariakoo | 0 | 39,904,100.00 | 0 | N/A |
| 8. | Halmashauri za Wilaya | 1,012,286,089,000 | 625,319,158,432 | 386,966,930,568 | 61.7 |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*




***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*


**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, makusanyo makubwa ambayo ni **asilimia 96.5** ya makusanyo yote ya maduhuli yaliyokusanywa hadi Februari, 2023 ni kutoka katika halmashauri. Aidha Shirika la Masoko ya Kariakoo lilikusanya kwa asilimia 0.006, kiasi ambacho hakikukisiwa katika makisio ya makusanyo ya maduhuli ya mwaka 2022/2023. Kamati inazipongeza sana halmashauri kwa makusanyo hayo. Hata hivyo, Wizara pamoja na taasisi zake na Sekretarieti za Mikoa hazikuweza kufikia kiwango cha asilimia 66.6 cha lengo lililopaswa kukusanywa hadi hadi kufikia Februari, 2023. **Kamati Kamati inazipongeza sana Shirika la Elimu Kibaha na Wakala wa Mabasi yaendayo Kasi Dar es Salaam *(BRT)* kwa kuvuka lengo la asilimia 66.6 lililopangwa kufikiwa hadi Februari, 2023.** Aidha, Kamati inaishauri Wizara na taasisi zake pamoja na Mikoa ambao hawakufikia lengo la asilimia 66.6 hadi Februari, 2023 kuweka mikakati itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kufikiwa kiwango kilichoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaa *(BRT)* wamekusanya kiasi kikubwa cha maoteo ambapo hadi Februari, 2023 Wakala huyo alikusanya kwa **asilimia 97.16. Kamati inawapongeza sana BRT kwa ukusanyaji huu. Kamati inaishauri Wizara kuona namna ya kuongeza maduhuli katika wakala huyu kwa kuwa inaonekana kuwa ilitengewa maoteo kiadi kidogo kuliko uwezo wao halisi wa ukusanyaji.**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake pia Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kutoka **Shilingi 915,391,298,564.50** zilizotengwa mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 1,071,730,886,415.50. kwa mwaka 2022/2023,** sawa na ongezeko la **Shilingi 156,339,586,851.00** sawa na **asilimia 17.07**, Aidha, makisio ya maduhuli yameongezeka kutoka **Shilingi 1,071,730,886,415.50** mwaka 2022/2023 na kufikia **Shilinigi 1,192,721,936,870.00, sawa na Ongezeko la Shilingi 120,991,050,454.50 ongezeko**

**ambalo ni sawa na asilimia 11.3.** Kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3**




**Chanzo:** *Randama ya Wizara (Machi, 2023) na usanifu wa Kamati*

## 3.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023


**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti ya mwaka 2022/2023 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni, 2022 Wizara kupitia **Fungu 56, Fungu 02 pamoja na mafungu yote 26 ya mikoa** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 8,779,838,763,200.00.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,511,846,193,000.00** sawa na **asilimia 62.8** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 3,267,992,570,200.00** sawa na **asilimia 37.**2 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya **Shilingi 5,511,846,193,000.00** za matumizi ya Kawaida **Shilingi 4,626,253,868,000.00** sawa na **asilimia 83.94** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 885,592,325,000.00 asilimia 16;06** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha, Hadi Mwezi Februari, 2023 Wizara pamoja na taasisi zake na Mikoa zilipokea jumla ya Shilingi **5,568,517,156,164.01** sawa na **asilimia 63.42** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya

fedha hizo, Shilingi **3,592,082,222,469.14 sawa na asilimia 64.5** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,976,434,933,694.87** sawa na **asilimia 35.5** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya **Shilingi 3,592,082,222,469.14** zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinajumuisha mishahara na matumizi mengineyo *(OC),* ambapo **Shilingi 2,947,663,630,558.63** sawa na **asilimia 82.1** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 644,418,591,910.51** sawa na **asilimia 17.9** ni kwa ajili ya mtumizi mengineyo *(OC),* kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 04.




**Chanzo:** *Randama ya Wizara (Machi, 2023) na usanifu wa Kamati.*




**Chanzo:** *Randama ya Wizara (Fungu 56) na Usanifu wa Kamati (Machi, 2023)*




**Chanzo:** Randama ya Wizara (Machi, 2023) (Fungu 56) na Usanifu wa Kamati

### 3.4 UCHAMBUZI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa upokeaji wa jumla wa fedha ulifikia **asilimia 63.42** ambapo, fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa kwa **asilimia 64.5**; na fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo imepokelewa kwa **asilimia 35** ya fedha zote zilizopokelewa. Aidha, fedha kwa ajili ya matumizi ya mishahara zilipokelewa kwa **asilimia 53** na fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo zilipokelewa kwa **asilimia 12.**

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilitaka kujua Kiasi cha **asilimia 35.7** kilichopokelewa hadi Februari, 2022 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kimefikisha asilimia ngapi ya utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo. Kamati pia ilihoji ili kufahamu ikiwa kiasi kilichobaki kikitolewa kitaweza kamilisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa kipindi kichobakia ili kumaliza mwaka wa fedha. Kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na taasisi zake pamoja na Sekretarieti za Mikoa ipo katika hatua mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** iwapo Wizara (pamoja na Sekretarieti za Mikoa) itapokea fedha kwa mujibu wa mpango kazi wa utekelezaji, malengo ya utekelezaji wa kila mradi yatafikiwa kwa kipindi kilichobaki. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hadi kufikia Februari, 2023 Wizara na Sekretarieti za Mikoa, ilitakiwa kuwa imepokea **asilimia 66.6** ya fedha za matumizdi ya kawaida. Hata hivyo, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **asilimia 64.5** tu. Kamati inaona kuwa kiwango hiki cha upokeaji wa fedha hakiwiani na wastani uliotarajiwa kutolewa kwa Wizara. Kamati inasisitiza fedha hasa za miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili miradi iliyopangwa kutekelezwa ikamilike kwa wakati.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024


**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa utekelezaji wa majukumu, mapato na matumizi ya kawaida pamoja na ile ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wizara katika mwaka wa fedha 2023/2024 imepangwa kwa kuzingatia mambo mbalimbali kama vile **Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025),** Sera mbalimbali kama vile **Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**, **Malengo ya Maendeleo Endelevu,** na **Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020** kama yalivyofafanuliwa na Mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli hizo za Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ifuatavyo:-

### 4.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara na taasisi zake (**Fungu 56, Fungu 02** pamoja na

mafungu 26 ya Mikoa) katika mwaka wa fedha 2023/2024 ni jumla ya **Shilingi 1,192,721,936,870.00** Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,634,835,000** sawa na **asilimia 0.14** zinakadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Elimu Kibaha, **Shilingi 17,172,749,540.00** sawa na **asilimia 1.4** kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam (BRT), **Shilingi 10,437,966,865 sawa na asilimia 0.9** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, **Shilingi 4,131,215,065.00** sawa na **asilimia 0.35** kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, **Shilingi 15,200,000,000.00** sawa **na asilimia 1.3** kutoka wakala wa barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA),* **Shilingi 261,890,400.00** sawa na **asilimia 0.02** kutoka Makao Makuu ya Mikoa na **Shilingi 1,143,883,280,000** sawa na **asilimia 95.9** kutoka Halmashauri za Wilaya kama inavyoonekana kwenye ***Kielelezo Na. 5***




**Chanzo:** *Randama ya Wizara (Machi, 2023) (Fungu 56) na*

*Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa maduhuli kutoka Shilingi **1,071,730,886,415.50** mwaka 2022/2023 hadi Shilingi **1,192,721,936,870.00** mwaka 2023/2024. Hili ni ongezeko la Shilingi **120,991,050,454.50,** sawa na **asilimia 11.3.** Kamati inaipongeza sana Wizara kwa ongezeko hili. Aidha, Kamati ilibaini kuwa kumekuwa na ongezeko la makadirio ya maduhuli kuanzia mwaka 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024


kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 6 (a) hadi (c).** Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuendelea kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyoonesha kukua kwa sekta mbalimbali za kijamii na hivyo kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwa wabunifu wa vyanzo mbalimbali ili kuiwezesha Serikali kutekeleza malengo yake kwa ufanisi mkubwa.

**Kielelezo Na. 6 (a):** *Mwenendo wa Makadirio ya Maduhuli ya Wizara na Taasisi zake kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024*

| Na. | MWAKA | KIASI | ONGEZEKO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2021/2022 | 926,035,543,846.46 | | |
| 2. | 2022/2023 | 1,071,730,886,415.50 | 145,695,342,569.04 | 17.7 |
| 3. | 2023/2024 | 1,192,721,936,870.00 | 120,991,050,454.50 | 11.3 |


**Chanzo:** *Randama ya Wizara (Fungu56) na Usanifu wa Kamati.*

**Kielelezo Na. 6 (b):**




**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kumekuwa na ongezeko la ukadiriaji wa maduhili kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 kwa Wizara, taasisi za Wizara na Sekretarieti za Mikoa. Ambapo kuna taasisi pia zimekuwa zikishuka ama kupoteza kabisa uwezo wa

kukusanya. Muhtasari wa ukadiriaji wa maduhuli ni kama inavyonekana katika **kielelezo Na. 06 (c).**




**Chanzo:** *Randama ya Wizara (Machi, 2023) (Fungu 56) na*

*Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliendelea kubaini kuwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini wamepunguza kwa kiasi kikubwa makadirio ya maduhuli, upungufu ambao ni kwa asilimia 50 ya makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2023/2024. Kamati ilitaka kufahamu sababu za kupungua kwa makadirio hayo na kuelezwa kuwa ni kutokana na kwamba jukumu la kukusanya mapato ushuru wa maegesho ya magari limekabidhiwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa makadirio ya maduhuli kwa upande wa halmashauri yameendelea kuongezeka. Kamati ilihoji sababu za kuongezeka kwa maduhuli hayo na kutaarifiwa kuwa ni kutokana na Kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato ikijumuisha fedha kupelekwa benki mara baada ya kukusanywa ili kuziba mianya ya ukusanyaji wa mapato; na kuendelea kuboresha matumizi mifumo ya kielektroniki ikiwemo kuongeza *PoS* kwenye baadhi ya Halmashauri. Aidha, Kamati imeendelea kubaini kuwa makadirio ya makusanyo kwa Halmashauri yameendelea kuimarika kwa ukuaji wa wastani wa **asilimia 15.1** kwa mwaka. **Kamati imeridhishwa na wastani huu wa ukuaji wa makadirio ya maduhuli kwa upande wa Halmashauri.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa taasisi, Makao Makuu ya Mikoa ambao makadirio yao ya mapato yanaendelea kushuka Kamati inashauri taasisi na mikoa hiyo kuongeza ubunifu wa vyanzo vingine vya mapato ili kuendelea kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake.


## 4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, Bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha 2023/2024 inalenga kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa Taifa ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na siha bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za Ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Bajeti hiyo inapangwa kwa ajili ya kutekeleza mipango mbalimbali ya Serikali kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ule wa Mwaka mmoja pamoja na miongozo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo:-

**(a) Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI (Fungu 56), (Fungu 02) pamoja na mafungu 26 ya Mikoa kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoainishwa katika randama za fungu 56, fungu 02 na mafungu yote 26 ya Mikoa, ili kuweza kutekeleza malengo mbalimbali ya Wizara pamoja na Mikoa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 56, Fungu 02 pamoja na mafungu yote 26 ya Mikoa inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 9,144,021,699,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,658,022,058,000.00** sawa na **asilimia 61.9** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 3,485,999,641,000.00** sawa na **asilimia 38.1** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Namba 7.**




**Chanzo:** *Randama ya Wizara (Machi, 2023) na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, sura ya Bajeti ya Wizara inajumuisha **Shilingi 4,597,632,183,000.00** sawa na **asilimia 50.28** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 1,060,389,875,000.00** sawa na **asilimia**

**11.59** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), Aidha, kati ya **Shilingi 3,485,999,641,000.00** sawa na **asilimia 38.12** za Miradi ya Maendeleo **Shilingi 2,362,700,487,000.00** sawa na **asilimia 67.77** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,123,299,154,000.00** sawa na **asilimia 32.22** ni fedha za nje. **Kielelezo Na 8 (a) na (b).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuishia hapo, ilifanya uchambuzi zaidi na kubaini kuwa, **Bajeti ya Fungu 56, Fungu 02 pamoja na mafungu yote 26 ya mikoa** imeongezeka kwa kwa **Shilingi 364,182,935,800.00** sawa na **asilimia 4.14** kutoka **Shilingi 8,779,838,763,200.00** mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 9,144,021,699,000.00** mwaka 2023/2024 kama ifuatavyo: -

i. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la **Shilingi 218,007,070,800.00** ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 6.67** kwenye bajeti ya maendeleo, kutoka **3,267,992,570,200.00** mwaka 2022/2023 hadi **3,485,999,641,000.00** mwaka 2023/2024;

ii. Kwa upande wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la **Shilingi 215,014,115,800.00** sawa na **asilimia 10.01** kutoka **Shilingi 2,147,686,371,200.00** mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 2,362,700,487,000.00** mwaka 2023/2024. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa ongezeko hili la asilimia 10 la utengaji wa bajeti ya maendeleo. **Kamati inashauri fedha hizo zilizotengwa zitolewe zote na kwa wakati ili kuwezesha maendeleo yaliyopangwa kwa wananchi kufikiwa;**


iii. Kwa upande wa fedha za nje za miradi ya maendeleo Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la Shilingi **2,992,955,000.00** sawa na **asilimia 0.6,** kutoka **Shilingi 1,120,306,199,000.00** mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 1,123,299,154,000.00.00** mwaka 2023/2024. **Kamati inaona kuwa kiwango hiki kinaendelea kuiweka nchi katika hali nzuri ya kuiondoa nchi kutoka kwenye utegemezi wa miradi ya**

**maendeleo kutoka fedha za nje. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa juhudi hizi;** na

iv. Aidha Kamati ilibaini kuwa bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **Shilingi 146,175,865,000.00 asilimia 2.65** Kutoka **Shilingi 5,511,846,193,000.00** mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 5,658,022,058,000.00** mwaka 2023/2024. Hata hivyo uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa matumizi ya kawaida kwa ajili ya mishahara yamepungua kwa **asilimia hasi (-) 3.46** kutoka **Shilingi 4,626,253,868,000.** Hadi **Shilingi 4,597,632,183,000.00** mwaka 2023/2024; ambao ni upungufu wa **Shilingi 197,889,981,300.00** huku matumizi mengineyo (OC) yakiongezeka kwa **Shilingi 174,797,550,000** sawa na **asilimia 19.73;** kutoka **Shilingi 885,592,325,000.00** mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 1,060,389,875,000.00** mwaka 2023/2024. Kamati ilielezwa kuwa ongezeko la fedha za matumizi mengineyo limetokana na ongezeko la posho ya kujikimu kwa siku.

**Kielelezo Na 8 (a): ULINGANISHO WA BAJETI (FUNGU 56, FUNGU 02 NA MAFUNGU YOTE 26 YA MIKOA) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA 2023/2024**

| **MATUMIZI** | **2022/2023** | **2023/2024** | **ONGEZEKO/ UPUNGUFU** | **%** |
|---|---|---|---|---|
| Mishahara | 4,626,253,868,000 | 4,597,632,183,000 | 28,621,685,000 | 3.46 |
| Oc | 885,592,325,000 | 1,060,389,875,000 | 174,797,550,000 | 19.73 |
| Maendeleo Ndani | 2,147,686,371,200 | 2,147,686,371,000 | 215,014,115,800 | 10.01 |
| Maendeleo Nje | 1,120,306,199,000 | 1,123,299,154,000 | 2,992,955,000.00 | 0.26 |
| **JUMLA** | **8,779,838,763,200.00** | **9,144,021,699,000.00** | **364,182,935,800** | **4.14** |




**(b) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu wa Kamati ulilenga kubaini athari za Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa dhidi ya Bajeti ya **Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa**. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

i) Wakati Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2023/2024 ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 7** bajeti ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa imeongezeka kwa **asilimia 4.14**;

ii) Wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 01** bajeti ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 6.67;**


iii) Wakati bajeti ya Taifa ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **asilimia 10.4,** bajeti ya matumizi ya

kawaida ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa imeongezeka kwa **asilimia 2.65**.

**Mheshimiwa Spika,** tafsiri tunayopata katika uchambuzi huu ni kuwa, ongezeko la mafungu yote kwa pamoja lililowekwa katika bajeti ya Taifa, linawiana na ongezeko la bajeti ya Wizara hii, Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa. Hii inaonesha kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zilizopewa kipaumbele katika tengeo la fedha za bajeti**. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo la tengeo katika sekta hii muhimu inayogusa maisha ya Watanzania.**

**Kielelezo Na 9:** Ulinganisho wa Bajeti Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa Dhidi ya Bajeti ya Taifa 2022/2023 na 2023/2024 (kwa milioni)

| **Mwaka wa Fedha** | **2022/2023** | **2023/2024** | **Ongezeko** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| **Bajeti Kuu ya Serikali** | 41,480,580 | 44,388,067 | 2,907,487 | 07 |
| **Bajeti ya Wizara** | 8,779.00 | 9,144 | 365 | **4.14** |




**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Bajeti ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa imeongezeka kutoka **asilimia 2.46** mwaka 2022/2023 hadi kufikia **asilimia 3.11** mwaka 2023/2024 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 10. **Kamati inaendelea kuipongeza Serikali na kushauri kiasi hiki cha fedha kitolewe chote na kiendelee kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kuendelea kuboresha Maisha na maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.**

**Kielelezo Na.10:** Ulinganisho wa Bajeti Kuu na Bajeti ya OR TAMISEMI kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024 kwa milioni

| | BAJETI KUU YA SERIKALI | | | BAJETI YA WIZARA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2022/2023 | 2023/2024 | % | 2022/2023 | 2023/2024 | % |
| Mishahara | 9,830,753 | 10,882,126 | 10.7% | 4,626,253 | 4,597,632 | 3.46 |
| Oc | 5,335,461 | 5,578,433 | 4.6% | 885,592 | 1,060,389 | 19.73 |
| Maendeleo Ndani | 12,306,921 | 11,873,894 | -3.5% | 2,147,686 | 2,147,686 | 10.01 |
| Maendeleo Nje | 2,699,081 | 3,282,081 | 21.6% | 1,120,306 | 1,123,299 | 0.26 |
| JUMLA | 41,480,580 | 44,388,067 | 7.0% | 8,779,838 | 9,144,021 | 4.14 |

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo kwa lengo la Kuboresha Utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi:-

### 5.1 UIMARISHAJI WA SHIRIKA LA ELIMU KIBAHA

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Elimu Kibaha ni Shirika la umma lilianzishwa mwaka 1963 chini ya wafadhili watano ambao ni Serikali ya Tanganyika kwa kipindi hicho na nchi nne za Kinordic (Dernmark, Norway, Finland na Sweden). Shirika hili lilisajiliwa chini ya sheria ya Mashirika ya Umma Na.17 ya Mwaka 1969 na marejeo ya sheria hiyo ya mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Elimu Kibaha lilianzishwa likiwa na dhima kuu ya kuondoa ujinga, maradhi na umasikini.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulifanya Shirika kutimiza dhima yake lilianzisha mambo makuu matatu muhimu kama ifuatavyo: -

i. Kuanzisha hospitali ambayo inajulikana kama hospitali ya Tumbi ili kukabiliana na chanamoto ya maradhi,

ii. Kuanzisha miradi ya ujasiriamali illi kukabiliana na changamoto ya umasikini, na

iii. Kuanzishwa kwa kozi mbalimbali ili kuwaondoa Watanzania kwenye changamoto ya ujinga.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa Serikali imeihamisha Hospitali ya Tumbi kutoka Shirika la ELimu Kibaha Kwenda Wizara ya Afya. Kamati inapongeza mpango huu, ikiwa ni sehemu ya kuboresha hospitali hii iliyo muhimu kabisa katika kuwahudumia wananchi wa Mkoa wa Pwani.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo kuondolewa kwa hospitali hii kutoka Shirika la ELimu Kibaha na Kwenda Wizara ya Afya kunatengeneza tena ombwe la kutotekelezeka kwa sehemu ya dhima ya Shirika hili kwa kipengele cha Afya. Kutokana na hilo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali kuacha kuendelea kuhamisha taasisi zilizopo chini ya Shirika;

ii. Serikali ifikirie upya uamuzi wake wa kuitoa Hospitali ya Tumbi kutoka Shirika la Elimu Kibaha Kwenda Wizara ya Afya; na

iii. Serikali ifanye tathmini ya uendeshaji wa shirika hili ili kuona kama malengo na dhima ya kuanzishwa kwake inaendana na mazingira ya sasa.

### 5.2 UKAMILISHAJI WA MABOMA YA SHULE NA ZAHANATI

**Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha elimu na huduma za hospitali nchini katika ngazi za Halmashauri za Wilaya Serikali kupitia Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilitoa hamasa kubwa kwa wananchi kujitolea katika ujenzi wa majengo kwa ajili ya vituo vya afya, zahanati na shule katika Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kuna maeneo mengi nchini Wananchi wamejitolea kujenga majengo kwa ajili ya zahanati vituo vya afya na shule. Aidha majengo mengi yaliyojengwa na wananchi yameishia ngazi ya upauaji.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliahidi kuwa majengo hayo yangemaliziwa kutokana na fedha kutoka Serikalini. Hata hivyo, hadi sasa majengo mengi yaliyojengwa na wananchi hayajamaliziwa kutokana na Serikali kutopeleka fedha za umaliziaji wa majengo hayo kama ilivyoahidi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inashaishauri Serikali kupeleka fedha za kumalizia maboma haya ili kuondoa hasara inayoweza kupatikana kutokana na kuchakaa kwa majengo haya kabla hata ya kutumika.

## 5.3 UCHELEWESHAJI WA VIFAA MBALIMBALI VYA HOSPITALI NA ZAHANATI KUTOKA MSD

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Sana Serikali kwa uwekezaji mkubwa inayoufanya kwa kujenga majengo ya hospitali na zahanati pamoja na kutenga fedha za kununulia vifaatiba, vitendanishi na dawa kwa ajili ya zahanati na hospitali zetu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kuna Halmashauri nyingi zimepelekewa fedha na Serikali kwa ajili ya kununua vifaatiba, vitendanishi na dawa kwa ajili ya hospitali na zahanati nchini ili ziagize vifaa hivyo kupitia Bohari ya Dawa *(MSD)*. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa zahanati na hospitali nyingi zilizoagiza vifaatiba, vitendanishi na dawa kupitia Bohari ya Dawa vifaa hivyo vinachelewa kupelekwa katika hospitali na zahanati hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Wizara ya TAMISEMI kukaa pamoja na Wizara ya Afya na *MSD* kujadiliana namna bora ya kuwasilisha vitendanishi, vifaatiba na dawa zote zilizoagizwa kwa ajili ya Halmashauri zote nchini; na

ii. Serikali kuweka mifumo itakayowezesha uagizaji wa vitendanishi, vifaatiba na dawa kupitia *MSD* itakayowezesha uwasilishaji wa vifaa hivyo bila kuchelewa ili kufikia malengo ya Serikali ya kufikisha huduma kwa wananchi kwa haraka na kwa ubora zaidi.

## 5.4 WAJIBU WA UWEKEZAJI WA KAMPUNI/MASHIRIKA KWA JAMII *(COOPORATE SOCIAL RESPONSIBILITY)*

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano mzuri kati yake na wawekezaji mbalimbali nchini. Wawekezaji hawa wamekuwa wakileta ahueni kubwa kwa Serikali katika kupeleka huduma mbalimbali kwa wananchi katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini kwa kutumia sehemu ya faida ya uwekezaji wao kwa ajili ya jamii katika halmashauri hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wilaya ya Tarime walipokea takriban **Shilingi 7,000,000,000** kutoka Mgodi wa Dhahabu wa North Mara kwa ajili ya kusaidia shughuli mbalimbali za kijamii. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa ya fedha iliyotumika haiakisi thamani halisi ya fedha hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Halmashauri husika kuweka vipaumbele vya matumizi ya fedha za *CSR*, hasa miradi mikubwa, kabla ya kupokea fedha hizo,

ii. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kutengeneza mwongozo mzuri wa matumizi ya fedha za *CSR*;

iii. Serikali ifanye tathimini kuhusu maeneo yote yanayonufaika na *CSR* ili kuona namna jamii inavyonufaika na miradi hiyo.

## 5.5 UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOFADHILIWA NA PROGRAMU YA *SEQUIP*

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa *Secondary Education Quality Improvement Program (SEQUIP)* ni mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia unaolenga kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa ajili ya shule za sekondari nchini. Mradi huu ulianza

Mwaka wa Fedha 2020/2021 na unatarajiwa kukamilika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapeleka **Shilingi milioni 470** kwa kila halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.
Hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa maeneo mengi ya halmashauri fedha zilizopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu hazikutosheleza. Hali hii imezilazimisha baadhi ya halmashauri kutumia fedha za mapato yao ya ndani kwa ajili ya kumalizia majengo yanayofadhiliwa na mradi huu. Hali hii imekuwa ikisababisha baadhi ya shughuli ndani ya halmashauri kutokufanyika. Kamati inatilia shaka kuwa baadhi ya halmashauri huenda zikashindwa kabisa kumalizia majengo haya kutokana na halmashauri hizo kuwa na vyanzo dhaifu vya mapato ya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

i. Serikali kuangalie uwezekano wa kutafuta fedha za kuongezea umaliziaji wa majengo yanayofadhiliwa na mradi huu.

ii. Serikali ibainishe vyanzo vya fedha zitakazoweza kutumika kumalizia majengo hayo.

iii. Serikali ifanye marejeo ya makadirio ya ujenzi kulingana na hali halisi chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa *(schedule of material)* na kuwasilisha kwa TAMISEMI; na

iv. Serikali ifanye uchunguzi kujua sababu ya fedha kutotosha na wahusika kuchukuliwa hatua.

## 5.6 UBORA WA UPEMBUZI YAKINIFU KATIKA MIRADI INAYOTEKELEZWA NA HALMASHAURI NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa miradi mingi inayotekelezwa katika halmashauri nchini

inakumbwa na changamoto ya kuibuka kwa kazi za ziada ambazo awali hazikuwa sehemu ya ukadiriaji *(BOQ)*. Kwa mfano kububujika maji wakati wa ujenzi wa msingi wa Soko la Mjini Kati, la Jijini Mwanza, ujenzi wa Barabara ya Kisesa – Bujora kuchelewa kutokana na uwepo wa miamba mikubwa ambayo awali haikukisiwa wakati mkandarasi anapewa mradi, na kukosa maji na barabara za kupitishia vifaa vya ujenzi katika mradi wa ujenzi wa Shule za Wasichana za Mwanza na Shinyanga.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa changamoto hizo zote zimetokana na udhaifu wa wataalam waliofanya upembuzi yakinifu. **Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inasimamia na kudhibiti shughuli za upembuzi yakini unaofanywa na wataalam kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yote katika halmashauri zote nchini.**

### 5.7 UTOFAUTI WA MICHORO NA UKADIRIAJI KATIKA MIRADI YA UJENZI WA MAJENGO YA SHULE, ZAHANATI NA VITUO VYA AFYA KATIKA HALMASHAURI NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ramani tofauti tofauti katika miradi mbalimbali ya ujenzi wa shule, zahanati na vituo vya afya katika halmashauri zote nchini, hasa ujenzi wa majengo ya miradi inayotekelezwa na programu za *SEQUIP, EP4R BOOST na COVID.*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kuweka michoro iliyo ya kudumu na ya kufanana *(consistence)* itakayotumika kwa muda mrefu na ili kutumia fursa ya uzoefu itakayopatikana kupitia ujenzi wa majengo hayo na kuleta sura ya mfanano kwa majengo yote ya aina hiyo hapa nchini.

### 5.8 UTOAJI WA MAFUNZO YA AWALI *(INDUCTION)* NA HUDUMA KWA JAMII KWA MAAFISA KATA NA VIJIJI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliitaka Serikali kuratibu mafunzo maalum ya awali kuhusu shughuli za Serikali, utumishi wa

umma, usalama na huduma kwa jamii kwa watendaji wa kata na vijiji wakati wa Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti. Hata hivyo agizo hili kwa sehemu kubwa halikutekelezwa. Aidha, mikoa imetoa taarifa za mafunzo ya watumishi wa makao makuu ya Halmashauri ambayo hutolewa na vyuo mbalimbali vya umma na binafsi badala ya Chuo cha Utumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI iratibu mafunzo ya awali *(induction)* na mafunzo ya utumishi wa umma, usalama na huduma kwa jamii kwa watendaji wa kata na vijiji ili kuongeza uwajibikaji wa watumishi katika ngazi za vijiji na kata. Aidha, mafunzo hayo yatolewe na Chuo cha Utumishi wa Umma.

### 5.9 USAMBAZAJI WA TAULO ZA KIKE KWA WANAFUNZI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inafanya jitihadi kubwa kuhamasisha wadau mbalimbali na Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike wawapo shuleni kupata taulo za kike.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na jambo hilo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Halmashauri ziongeze kiwango cha fedha kwa ajili ya ugharamiaji wa taulo za watoto wa kike shuleni,

ii. Serikali iweke utaratibu wa kuratibu vizuri kwa masuala ya ubora, thamani ya fedha, upokeaji na uwiano wa usambazaji wa ya taulo hizo, na

iii. Serikali itambue michango ya wadau wengine na thamani ya michango yao.

### 5.10 KUENDELEA KUWEPO KWA BAKAA KATIKA BAJETI ZA HALMASHAURI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika uchambuzi wake imebaini kuwa mikoa yote imekuwa ikibakisha bakaa, hasa kutoka

kwenye miradi ya maendeleo. Kamati inaona kwamba kubakisha bakaa kila mwaka kunaweza kuwa chanzo cha miradi mingi kutokamilika kwa wakati na shughuli nyingine za maendeleo na utendaji kutokwenda kama ilivyopangwa. Aidha, kwa sababu utaratibu wa matumizi ya bakaa hauko wazi kuna viashiria kwamba fedha za bakaa zinaweza kutumipa katika matumizi ambayo hayakupangwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali kuangalia upya sheria ya matumizi ya bakaa;

ii. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuweka mikakati ya kupunguza kiwango cha fedha za bakaa sambamba na kuweka utaratibu wa kuongeza uwajibikaji kwa fedha zinazovuka mwaka; na

iii. Serikali kuangalia upya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma ambazo kwa mfumo na muundo wa majukumu ya Serikali za Mitaa utekelezaji ya wa sheria hii umekuwa mgumu.

**5.11 UPELEKAJI WA ASILIMIA 40 VIJIJINI**

**Mheshimiwa Spika,** imebainika kuwa halmashauri nyingi nchini hazipeleki asilimia 40 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kupeleka huduma vijijini kama inavyotakiwa na sheria. Hali hii imekuwa ikisababisha huduma duni kwa wananchi wanaoishi vijijini. Kamati inashauri wizara ya TAMISEMI kuweka utaratibu wa ufuatiliaji wa upelekaji wa asilimia 40 vijijini katika kila kipindi cha robo mwaka.

**5.12 UANZISHWAJI WA SHULE ZA MICHEPUO YA KIINGEREZA**

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri nyingi nchini zinaendelea kujikita katika kuanzisha na kuendeleza Shule za Michepuo ya Kiingereza kwa ajili ya kuongeza ubora wa elimu nchini.

Kamati inapongeza juhudi hizi kutokana na sababu kuwa Tanzania si kijiji kisichokuwa na mwingiliano na mataifa ya nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa uwekezaji wa shule hizi ni mkubwa unahitaji rasiliamali watu yenye ujuzi, uwezo na umahili mkubwa ili kuwa katika viwango vinavyohitajika.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, imebainika kuwa shule hizi zinaongezeka kwa kasi, hali inayoweza kuathiri mfumo mzima wa utoaji wa elimu nchini, hasa kuathiri shule wanazosoma wananchi wa hali ya chini. Pia zinatumia walimu walioajiriwa na Serikali katika Halmashauri na hivyo kuleta upungufu kwa watumishi wa kada hiyo ya ualimu na kuhamisha walimu wabobevu kutoka shule za kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapata mashaka juu ya uanzishwaji wa shule hizi kwa wingi kuwa unaweza kuleta ubaguzi na matabaka kwa wananchi wa Tanzania ilhali Serikali ni moja.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali itazame utaratibu uliotumika na unaotumika kuhusu mfumo wa uanzishwaji, uendeshaji na usimamizi, wa shule za Michepuo ya Kiingereza *(English Medium Schools)* zinazoanzishwa, kumilikiwa na kuendeshwa na Serikali ili kutokuathiri shule za kawaida;

ii. Kwa kuwa shule hizi zinaanzishwa kama miradi, ni rai ya Kamati kuwa mpango wa uanzishwaji huo uende sambamba katika kujitegemea kiuanzishaji na kiuendeshaji;

iii. Serikali ihakikishe kuwa uwekezaji huu hauathiri rasilimali watu (hasa walimu) ambao tayari wako kwenye mfumo wa ajira za Serikali);

iv. Serikali itoe mwongozo wa uanzishwaji na uendeshwaji wa shule za mkondo wa Kiingereza, ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu usiokuwa wa upendeleo utakaofanana kwa halmashauri zote nchini;

v. Kamati inaishauri Serikali ipitie upya haja na malengo ya uanzishwaji wa shule hizi katika muktadha wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014; na

vi. Aidha, Serikali ichukue juhudi za maksudi za kuimarisha ufundishaji wa lugha za Kiswahili na Kiingereza katika shule zake zote za msingi.

## 5.13 UTEKELEZAJI WA MRADI WA KUPANGA, KUPIMA NA KUMILIKISHA ARDHI KATIKA HALMASHAURI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 inatoa jukumu la kupima, kumilikisha,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepeleka katika baadhi ya Halmashauri Shilingi 1,000,000,000 kama mkopo kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika Halmashauri hizo. Hata hivyo, imebainika kuwa halmashauri nyingi zilizopata mkopo huo zimeshindwa kurejesha mkopo na haziendelei tena na shughuli za kupima viwanja.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo eneo kubwa la ardhi katika halmashauri nchini linaendelea kubaki bila kupimwa, hali inayosababisha migogoro ya ardhi miongoni mwa jamii kuendelea kuwepo.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali kufanya tathmini ya matumizi ya mkopo huo na mafanikio katika upimaji wa ardhi za halmashauri;

ii. Serikali kuratibu mapato yanatokana na uuzwaji wa ardhi iliyopimwa kuendelea kutumika kupima maeneo mengine;

iii. Serikali isimamie na kuratibu urejeshwaji wa mikopo hiyo kutoka halmashauri zote zilizopata mkopo huo; na

iv. Halmashauri ziendelee kuweka mikakati kwa kutumia mapato ya ndani kuendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

### 5.14 UANZISHWAJI WA MIRADI YA KIMKAKATI

**Mheshimwia Spika,** Imebainika kuwa Serikali imeanzisha miradi mingi ya kimkakati inayoanzishwa katika halmashauri nchini. Aidha, miradi hii inatolewa kwa kuzingatia, pamoja na mambo mengine, inayohitaji maandiko yaliyoandikwa kwa utaalam.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, imeimebainika kuwa Halmashauri nyingi nchini hazina wataalama wa kuandika maandiko bora yanayoweza kuasidia kupata miradi ya kimkakati kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo (kwa mfano Mkoa wa Kigoma). Hii ni kutokana na halmashauri nyingi kukosa uwezo wa kuwaajiri wataalam waandaaji wa maandiko hayo. Hali hii imekuwa ikisababisha halmashauri nyingi kushindwa kupata miradi ya Kimkakati kutokana na kushindwa kuandaa maandiko bora.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa, pamoja na nia nzuri ya miradi hii ya kimkakati, lakini utaratibu wa uliowekwa

uangaliwe upya ili halmashauri zisizokuwa na uwezo na wataalam zinufaike na miradi hii.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri Ofisi ya Rais – TAMISEMI: -

i. Serikali iweke utaratibu wa kuzisaidia Halmashauri kuandaa maandiko ya miradi ya kimkakati; na

ii. Serikali ifanye tathmini marejeo mapitio ya mwongozo wa miradi ya kimkakati ili kutatua changamoto ambazo zipo katika mwongozo wa sasa.

**5.15 UBORESHAJI WA MAZINGIRA KATIKA MIRADI YOTE YA UJENZI KATIKA HALMASHAURI**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeweka mikakati kwa ajili ya kutunza na kuboresha mazingira nchini ikiwa ni pamoja na kuanzisha programu mbalimbali za upandaji wa miti, uhifadhi wa uoto wa asili, uhifadhi vyanzo vya maji na uzuiaji wa ukataji wa miti hovyo.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo Kamati imebaini kuwa katika miradi mingi inayotekelezwa na halmashauri nchini, hasa ya majengo ya shule na zahanati hakuna uzingatiaji wa program hizi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kama ifuatavyo: -

i. TAMISEMI itoe mwongozo wa upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira kabla na wakati wote wa utekelezaji wa miradi katika halmashauri;

ii. Wataalam wa upembuzi yakinifu waweke vipengele vya uoteshaji wa miti wakati utekelezaji wa miradi ya ujenzi;

iii. Serikali iweke mwongozo wa ushiriki wa Serikali za Mitaa katika programu za uhifadhi wa mazingira, kwa mfano ulindaji wa Mlima Kilimanjaro; na

iv. Aidha, upandaji wa miti uzingatie tafiti za kina kuhusu aina ya miti inayofaa kupandwa katika mazingira husika.

5.16 **UPUNGUFU WA WATUMISHI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada kwa kuona tatizo hilo na kuomba kibali cha ajira katika halmashauri. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa vibali vya kuajiri watumishi zaidi ya 21,200 katika sekta ya afya na ualimu.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hatua hiyo Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali ifanye tathimini ya upungufu wa watumishi katika halmashauri zote nchini; na

ii. Serikali kuweka mkakati wa kupunguza upungufu huo.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Angelah Jasmina Kairuki (Mb) – Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Festo John Dugange Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wanaoipa Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, Ndg. Adolf Ndunguru, Naibu

Makatibu Wakuu Ndg. Dkt. Wilson Mahera, Ndg. Dkt. Charls Msonda na Ndg. Sospeter Mtwale. pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Denis Lazaro Londo, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. William Vagimembe Lukuvi, Mb.
4. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb.
5. Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi, Mb.
6. Mhe. Sylvestry Fransis Koka, Mb.
7. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb.
8. Mhe. Zacharial Paulo Issaay, Mb.
9. Mhe. Salome Wycliff Makamba, Mb.
10. Mhe. Mwita Mwik abe Waitara, Mb.
11. Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb.
12. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb.
13. Mhe. Amandus Julius Chingulile, Mb.
14. Mhe. Dorothy George Kilave, Mb.
15. Mhe. Elinikyo Mafuwe Saashisha, Mb.
16. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb.
17. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb.
18. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mb.
19. Mhe. Erick James Shigongo, Mb.
20. Mhe. Ameir Abdalla Ameir, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja nae namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, *ndc,* na Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu, Ndg. Emmanuel Mdidi na Ndg. Sikudhani Mbinga pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Frank Ngonyani kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, **Fungu 56, 02, 36 ,47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, na 95** jumla ya **Shilingi 9,144,021,699,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Dennis Lazaro Londo (Mb),
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
14 APRILI, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa uwasilishaji mzuri wa maoni ya Kamati yetu ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge kwa utaratibu wetu ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia.

Tutaanza uchangiaji leo na Makadirio haya ya Mapato na Matumizi Ofisi ya TAMISEMI yamepangiwa siku tatu. Kwa hiyo tutaanza leo, jumatatu na jumanne tutahitimisha. Tutaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Lucy John Sabu, atafuatiwa, Mheshimiwa Rose Vicent Busiga ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hoja hii iliyoko katika Bunge letu Tukufu. Kwa dhati kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa nzuri sana ambayo ameendelea kuifanya kwa Taifa letu. Naamini Waheshimiwa Wabunge wote watakubaliana nami kwamba kwa kipindi hiki kifupi cha miaka miwili, miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yetu katika halmashauri, manispaa, majiji na miji ni kwa kiwango kikubwa sana. Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizira ya Nchi Ofisi ya Rais *TAMISEMI* na Wasaidizi wake Manaibu Waziri na Makatibu na watumishi wote kwa ujumla wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kazi hii kubwa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza kuchangia katika eneo zima la barabara za vijijini, kwa maana ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(Tanzania Rural Urban Road Agency - TARURA)*. *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana, kazi ambayo katika ile programu ya *SDP* wana *component* ya kutengeneza barabara kutoka maeneo ya uzalishaji kuyapeleka katika masoko na magulio. Kazi hiyo wanaifanya vizuri, mafungu yanaenda vizuri na usimamizi ni mzuri, kwa kweli tunaona tofauti kubwa sana tangu tulivyokuwa tunazisimamia hizi barabara kupitia halmashauri; na sasa tangu mamlaka hii imeingia tunaona kwamba kuna ufanisi umeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nauliza hapa kwamba mamlaka kama ya *DAWASA* imepata ithibati ile ya ubora wa Dunia, lakini ninaamini kabisa kwamba sitashangaa siku moja nikiona kwamba *TARURA* nao wanapata ile *International Standard Organisation* kwa maana ya ubora wa kazi ambayo wanaifanya, lakini pia sitashangaa *Engineer* Victor Seff akitunukiwa udaktari wa heshima kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa namna ambavyo ameifungua Tanzania hasa katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,pamoja na sifa hizo lakini kuna changamoto ndogo ambayo naiona. Changamoto iko katika *disbursement* ya pesa hasa zinazotokana na Mfuko wa Barabara. *TARURA* ina vyanzo vikuu vitatu, chanzo cha kwanza ni jimbo cha pili ni tozo na cha tatu ni Mfuko wa Barabara. Sasa fedha za jimbo na za tozo zinaenda kwa wakati lakini fedha hizi zinazotokana na Mfuko wa Barabara zinachelewa, hivyo zinasababisha baadhi ya wakandarasi kuto omba zabuni za barabara ambazo fedha zake zinatokana na barabara. Kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, kwamba tujitahidi kupeleka mafungu ya hizi fedha zinazotokana na mfuko wa barabara kwa wakati

Mheshimiwa Spika, lakini kwakule Lushoto ambako kazi kubwa imefanyika tunachangamoto kubwa mbili. Changamoto ya kwanza ni kwamba *TARURA* hawana ofisi, ofisi waliyokuwa nayo sasa hivi inavuja kiasi kwamba wakati wa mvua wanaingia na miamvuli ndani ya ofisi, hili si jambo zuri. Sisi tumefanya jitihada kubwa, tumewapa kiwanja jirani kabisa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ni eneo zuri mno ambalo linafaa kwa ujenzi wa ofisi ya *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili Wilaya ya Lushoto ni wilaya ambayo asilimia 95 ni milima; magari waliyokuwa nayo yamechakaa sana kila siku yanafanyiwa ukarabati. Inafikia hatua ili waweze kutimiza wajibu wao wakati mwingine

lazima hata sisi Wabunge tunawaazima magari yetu, hii si sawa. Tunaomba wapatiwe magari ya kuhudumia majimbo yote matatu ya Wilaya ya Lushoto kwa sababu Wilaya ya Lushoto ni milima na mabonde hivyo inahitaji magari ambayo ni madhubuti sana ili waweze kufanya kazi hizi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nihame katika eneo hili niende katika eneo la elimu. Tuna changamoto kubwa sana ya watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, na mara kadhaa nikisimama hapa ndani ya Bunge lako nimekuwa nikizungumza jambo hili. Kipekee nipongeze jitihada hizi za Mheshimiwa Rais kutangaza ajira takriban 21,200. Mimi niombe, hizi 200 ambazo zimekaa pale juu zenyewe azielekeze Lushoto; na azielekeze Lushoto kwa sababu hizi zifuatazo.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Idara ya Elimu Sekondari mahitaji ya walimu ni walimu 1000, waliopo ni walimu 841 tunaupungufu 159, kidogo hapo kuna uhafadhari. Hata hivyo, mwaka 2022 wamehama walimu 35, 2023 wamehama 25 na bado wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini wanahama huku hatujawahi kuona wakihamishwi kutoka maeneo mengine kuja Lushoto, hili ndilo tatizo kubwa. Ukienda kwenye idara ya elimu msingi mahitaji ni 2,250 waliopo ni 1333 upungufu ni 917; 2020 wamehama 34; 2021 wamehama 34 tena; 2022 wmehama 23; 2023 bado sijapata takwimu zake, lakini wanaohamia kuja Lushoto hatuwaoni kila unaye muuliza anakwambia changamoto ni baridi. Sasa mimi nauliza mbona wakipewa viza za kwenda Ulaya hawakatai na Ulaya na kwenyewe kuna baridi?

Mheshimiwa Spika, hizi sababu hatutaki kuzisikia, kwenye ajira hizi mpya zinazotangazwa tunataka tuletewe watumishi ambao wako *committed* kufanya kazi popote

katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na ikikupendeza tuletee ambao wako *single*, kama ni wanawake wawe hawajaolewa na kama ni wanaume wawe hawajaoa ili wasianze kuleta sababu za kuanza kuhama. Kule wako mabinti wa kisambaa wazuri weupe, watapata wachumba wazuri kule kule.

Mheshimiwa Spika,katika zoezi lile la vyeti *fake* tumepungukiwa na zaidi ya watumishi 216 ambao walikutwa na tatizo la vyeti; lakini hatuja pata ile *compensation* ya ile idadi ambayo walipunguzwa. Niombe sana, pamoja na mapungufu haya ninayo yataja basi angalau tupate wale 216 katika mkupuo mmoja ili kuziba lile *gape* ambalo limetokana na wenye matatizo ya vyeti.

Mheshimiwa Spika,eneo lingine ambalo ningetaka kulisemea pia, wapo walimu ambao wanajitolea katika shule zetu; na katika halmashauri ya Lushoto tunao walimu 97 ambao wanajitolea. Ningependa sana kuomba kwa ridhaa yako Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, hebu tutafute hawa ambao wanajitolea, hawa wamekaa zaidi ya miaka miwili wanajitolea lakini leo wanakuja kushindanishwa na wengine ambao walikuwa wanafanya shughuli nyingine na inawezekana wakakosa. Nikuombe sana hawa hebu tuwapeni kipa umbele. Hii iwe pia ni zoezi endelevu, Serikali inaweza ikawa na *data base* ya Watumishi wote na tukawa na utaratibu kwamba kila mwalimu anaye maliza chuo basi apate angalau mwaka mmoja wa kujitolea na hata ikiwezekana muundo wa kuwaajiri ubadilike sasa waajiriwe wale ambao wako katika maeneo ambayo tayari wanajitolea kwa kipindi fulani.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu afya. Kama ambavyo tuna changamoto ya watumishi katika sekta ya elimu na afya ni vivyo hivyo. Ikama katika halmashauri ya Lushoto ni watumishi 662 ndio wanaohitajika waliopo ni 391 sawa na asilimia 59,

upungufu 270 sawa na asilimia 41. Ungufu huo uko katika kada hizi zifuatazo;

i. Madaktari mahitaji ni 29 waliopo ni 11 upungufu ni 18 sawa na asilimia 38,

ii. Madaktari wasaidizi wanao hitajika ni 39 waliopo ni 2 ungufu 37 sawa na asilimia 5,

iii. Maafisa Wauguzi wanao hitajika 24 walipo ni 2 tu upungufu 22 sawa na asilimia 8,

iv. Wauguzi wako 132 wanaohitajika walipo ni 63 upungufu ni 69.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, bajeti za miaka miwili, mitatu huko nyuma tumepeleka pesa nyingi sana kwenye miundombinu. Haitakuwa na maana yoyote tutakapokuwa na miundo mbinu lakini ikakosa watumishi.

Mheshimiwa Spika, niombe sana kwa ridhaa yako tuendelee kuhakikisha kwamba maeneo haya yanapata watumishi. Hivi tunapozungumza hivi ni kwamba wakati mwingine si lazima zitokee ajira mpya, hata kufanya *restructuring* katika muundo mzima wa ajira. Yako maeneo hasa mijini unakuta wamejaa katika maeneo ya miji lakini huku vijijini hakuna wanao hudumia Watanzania. Sasa nchi hii ni yetu sote tungependa *kuona regional secretariat* zifanye kazi ya ziada kuangalia katika maeneo ya miji lakini na maeneo ya vijijini yawe na usawa wa ikama ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Lucy John Sabu, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Vicent Busiga, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais *TAMISEMI*. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba ya bajeti; lakini kwa namna ya pekee nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuleta maendeleo kwa wananchi. Sote ni mashuhuda, katika kipindi chake cha miaka hii miwili, tumejionea namna ambavyo anatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi; hususan katika eneo la elimu, sote ni mashuhuda shule nyingi zimejengwa, zaidi ya Shule 23,000. Pia ujenzi wa shule maalum za za bweni kwa wasichana kuanzia *form one* hadi *form six.* Pia vituo vya Afya vimejengwa katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na mambo matatu. Jambo la kwanza ni kuhusiana na hili suala la mikopo ya asilimia kumi kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu. Sote tulisikia hotuba aliyohitimisha jana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika maelekezo ambayo aliyatoa ni kwamba usitishaji wa mikopo hiyo ni hadi hapo Serikali itakapojipanga na kuboresha mfumo wa utoaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, na mimi nikiwa kama mwakilishi wa vijana nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuona jambo hili na umuhimu wake kwa sababu mikopo hii imekuwa ikitunufaisha kwa namna moja ama nyingine hususan kwa vijana ambao wanapomaliza vyuo wanakuwa hawana sehemu ya kuanzia. Hivyo basi mikopo hii imekuwa mkombozi mkubwa sana, na mimi naunga mkono maelekezo ambayo aliyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na maelekezo ambayo aliyatoa Mheshimiwa Rais. Kwamba ipo haja ya Serikali kuangalia namna ya kuingiza katika mfumo wa kibenki ili kuratibu suala zima la utoaji na urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kwamba kumekuwa na vikundi hewa vikiendelea na wakati mwingine uwazi kwenye mikopo hii unakuwa hauonekani. Hivyo basi sisi kama vijana tunaunga mkono jambo hili na tuna imani kwamba Serikali inaenda kutengeneza mfumo ambao utasaidia vijana wengi waweze kunufaika. Hii ni kwa sababu kwenye mikopo iliyokuwa ikitolewa na wakati mwingine vikundi vinavyoundwa vijana wanakuwa hawana uelewa mzuri wa *project* ambayo wanaiendea; lakini na elimu ya biashara pia na upande wa ku-*manage* fedha ambazo wanafanya katika miradi yao. hivyo Serikali iweze kuangalia jambo hili kwa uzito mkubwa ili vijana wengi waweze kupata na mikopo hii iweze kuwa na tija. Hivyo basi kama itawezekana, kama wengine wataendelea na vikundi ama kutolewa mkopo wa mtu mmoja mmoja ili kila kijana kadri ambavyo atakuwa amejipanga aweze kuona anatumiaje fedha ambazo zinatolewa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni taulo za kike shuleni. Kwa muda sasa jambo hili limekuwa halina majawabu kwa sababu kama sote tunavyotambua tumefanya uboreshaji mkubwa katika eneo zima la elimu kwenye shule. Kwa namna ambavyo tunapambana katika kuboresha elimu lakini pia mtoto wa kike ni lazima aangaliwe kwa jicho la kitofauti kwa sababu mabinti wanapoingia katika siku zao wanapata changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, takwimu za *UNICEF* zinaonesha asilimia 10 ya watoto duniani wanakosa masomo kutokana na kipindi cha hedhi lakini pia wakiwa kwenye siku zao wanakosa kujiamini. Hivyo, tuiombe Serikali na nimefurahi nimeona upande wa maoni na ushauri wa Kamati wameongelea juu ya jambo hili. Hivyo basi. niiombe Serikali iweze kuona namna bora ya kuratibu jambo hili ili watoto au mabinti wa kike walioko mashuleni waweze kusaidiwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu natambua katika Serikali ya awamu ya nne ilitoa waraka ambao utatoa *pad* kwa watoto wa kike mashuleni, lakini waraka huu umekuwa hautekelezwi ipasavyo. Hivyo basi, niiombe Serikali iweze kutenga bajeti mahususi kwa ajili ya mbinti mashuleni ili waweze kuondokana na adha hii ambayo wanakumbana nayo.

Mheshimiwa Spika, nina imani hata tukianzisha viwanda vidogo vidogo kwenye halmashauri zetu ama kwenye ngazi za mkoa kwa ajili ya kutengeneza hizi taulo za kike, tutakuwa tumemlinda mtoto wa kike, lakini pia mtoto wa kike atasoma kwa kujiamini pasipokuwa na changamoto ama adha ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba sisi Wabunge tumekuwa tukipeleka *pad* mashuleni lakini pia kuna baadhi ya wadau mbalimbali wamekuwa waki-*support* jambo hili lakini bado uhitaji ni mkubwa. Kule vijijini uhitaji ni mkubwa sana kwa sababu baadhi ya watoto wamekuwa wanakata kanga, vitenge ama magazeti wakati mwingine na hii ni hatarishi kwa afya zao. Hivyo basi, tunaomba Wizara ya TAMISEMI waweze kuangalia jambo hili ili kumsaidia mtoto wa kike aweze kuondokana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, sisi Mkoa wa Simiyu ni kinara katika uzalishaji wa zao la pamba na kulikuwa na mpango wa Serikali wa kuanzisha kiwanda cha vifaatiba na moja ya malighafi ilikuwa ni kutumia pamba ikiwemo kuzalisha taulo za kike. Niombe basi kama jambo hili litakuwa gumu kutekelezwa kwenye halmashauri basi kwa kuwa sisi Mkoa wa Simiyu tunazalisha pamba kwa wingi waweze kutupa jukumu hili ili tutakapokuwa tunazalisha hizi taulo za kike ziweze kuwanufaisha nchi nzima. Vile vile TAMISEMI waweze kutusaidia ili kuharakisha jambo hili liweze kutekelezwa kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama *MSD* wameweza kutengeneza mipira ya wanaume na kugawa bure, iweje basi jambo hili lishindikane kutekelezwa kwa kutoa *pads* za watoto wa kike? Hivyo basi, niombe jambo hili waliangalie kwa jicho la kitofauti ili kuweza kumsaidia huyu mtoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kulizungumzia, kwenye halmashauri zetu kuna miradi ya kimkakati ambayo ilianzishwa kwa lengo la kuongeza mapato kwenye halmashauri, lakini pia kupunguza utegemezi katika bajeti ya Serikali Kuu. Katika Wilaya yetu ya Maswa, Mkoani Simiyu kuna Kiwanda cha Chaki kilianzishwa. Hivyo basi, niombe kwa sababu kulikuwa kuna fedha ambayo haijakamilika kutolewa kiasi cha Shilingi Bilioni mbili kwa ajili ya *operating cost* na umuhimu wa kiwanda hiki ni kutoa ajira kwa vijana 250, vile vile zitaweza kuzalishwa chaki ambazo zitasambazwa nchi nzima, niombe basi Serikali iweze kukamilisha jambo hili na fedha iweze kutolewa ili kiwanda hiki kiweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa fursa hii na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rose Vincent Busiga atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ameweza kutupatia zawadi ya uhai, lakini nikushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu kipenzi kwa namna ambavyo

ameendelea kufanya kazi kwa kujituma na naomba tu nizungumze kutoka kwenye vilindi vya moyo wangu kwamba, niwarudishe kidogo nyuma Watanzania wote, ikumbukwe tu Mama alipokea nafasi hii katika mazingira magumu sana, binafsi nilijiuliza hivi itakuwaje na Watanzania wote walijiuliza hivi itakuwaje? Majibu sisi wenyewe tunayaona kwa macho yetu, tunaona Mama ambavyo anaendelea kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nilieleze Bunge hili Tukufu, kuna miradi ya kimikakati ambayo tayari ilikuwa imekwishaanzishwa na Mtangulizi wake na sisi kama Wanageita tuna kauli yetu tunasema hakuna kilichosimama. Uzuri Mkuu wangu wa Mkoa yupo na anaendelea kusisitiza, sisi kama Wanageita hakuna kilichosimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze tu kwamba mimi binafsi niko kwenye Kamati ya Miundombinu, nimetembea mwenyewe kwa macho yangu bila kusimuliwa na mtu, kwa macho yangu Mradi wa *SGR* Mama alikabidhiwa ukiwa na kilomita za mraba 700, lakini sasa hivi ni zaidi ya kilomita 2000 nani kama Rais Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Binafsi nakumbuka nilichangia hapa Bungeni, nikaomba suala la watendaji wa kata wapewe posho lakini wapewe pikipiki, jamani mimi mwenyewe dada ya Kairuki alinipa mwaliko nilienda kukabidhi pikipiki 916. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kidogo tu, Dada yangu Kairuki ambapo ametoka kupewa sasa donge nono na Mama tayari amekwishakamilisha. Hiyo *speed* aliyonayo Dada Kairuki nimwombe aendelee na *speed* hiyo hiyo na kila Mbunge hapa anaenda anamweleza tatizo lake anamsikiliza, Mheshimiwa Kairuki asigeuke nyuma, achape raba aendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba univumilie kidogo, nilisema kwamba leo nikipata nafasi hii lazima niitendee haki. Nikaenda mbele zaidi, sisi watendaji wa Kata tulikuwa tunapita tunachangisha michango ya madarasa. Rais huyu huyu aliweza kutoa fedha za madarasa 23,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watendaji wamefanya kazi katika mazingira mazuri hata likizo walipata, walikuwa hawapati likizo kwa sababu ya kwenda kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Namshukuru sana Rais wangu kwa namna ambavyo anaendelea kuona sekta hii ya elimu, lakini nimwombe sana Waziri wangu Mheshimiwa Kairuki, kuna madarasa ambayo wananchi wamejenga kwa fedha zao za mfukoni, kwenye bajeti hii tunaomba maboma ambayo yako hatua ya upauaji, Serikali waweze kutenga fedha ili kwenda kuzichukua zile nguvu za wananchi waamini Serikali yao iko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sisi Mkoa wa Geita, tuna maboma 1,016; ya msingi 713 na ya sekondari 303. Mheshimiwa Kairuki akishuka pale Geita akaja akatembea kidogo na Mkuu wangu wa Mkoa ananisikiliza, atakupokea na utayaona yale maboma.

Mheshimiwa Spika, niende mbele zaidi, narudi kwenye afya. Kule kwetu Geita tuna Hospitali ya Chato ya Kanda, ukifika pale ni kama umefika Dar es Salaam ndogo. Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Kairuki atupe watumishi. Kabla ya hospitali ile tulikuwa tunaenda Mwanza sasa hivi tutakuwa tunaishia Chato.

Mheshimiwa Spika, kuna vituo vya afya, hivyo hivyo na vyenyewe wananchi walijichangisha fedha zao za mifukoni mwao, lakini mpaka sasa hivi vituo vile vya afya vipo. Kwa ridhaa yako nitaje hata vitatu au vinne ili ujue kwamba ninavijua. Kuna Kituo cha Afya cha Buhela, Chikobe, Ng'homolwa, Kafita na Nyijondo. Naomba sana sana kwa

ridhaa yako Dada yangu Mheshimiwa Kairuki afike kwenye vituo vya afya na fedha ambazo zimetengwa kati ya hivi vituo nilivyovitaja na vinginevyo aone haja ya kunisaidia hata kwa vituo viwili au vitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza sana, lakini nisiposema hili nitakuwa sijawatendea haki Waheshimiwa Madiwani. Waheshimiwa Madiwani wanafanya kazi nyingi sana na katika ziara yangu niliyoifanya Mwezi Machi Waheshimiwa Madiwani waliniomba sana, kwa heshima hiyo wakasema Mheshimiwa Mbunge wewe ulienda kuwasemea Watendaji wa Kata, tunaomba tena ukaliseme na hili, ikimpendeza Mheshimiwa Kairuki Dada yangu awasaidie na wao kidogo kaposho kao kale kaongezeke kidogo, wanatusaidia kazi, sisi tuko Bungeni sasa hivi lakini Madiwani wetu wanaendelea kufanya kazi kule. Kwa hiyo, kwa heshima hiyo hiyo Mheshimiwa Waziri anavyoendelea kuchapa raba na aendelee kuchapa mpaka kwa Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalize kwa kusema tuna daraja letu la Busisi na lenyewe mambo yanaendelea. Hata hivyo, Mheshimiwa Kairuki, watendaji wa Kata kipindi alipokuwa yupo kaka yangu Bashungwa waliahidiwa watakutana na Mama waje kidogo waangalie Ikulu jinsi inavyojengeka. Kwa heshima hiyo hiyo ya Dada yangu Mheshimiwa Kairuki, namwamini hana choyo, namwomba Watendaji wa Kata waje watembee Ikulu nami niwepo nawaongoza. Waje watembee Ikulu, waone jinsi Rais wao anavyoendelea kuchapa kazi, anavyoendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimesikia kengele yangu, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu na Mheshimiwa Bryceson Magesa Tumaini ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba ambayo imetoka kusomwa hapa ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na pongezi kwa *TARURA*. Sisi Wabunge tunaotoka maeneo ya vijijini tunajua umuhimu wa *TARURA,* pamoja na changamoto nyingine zote lakini tunapenda kuwapongeza namna wanavyofanya kazi, wameweza kuwaunganisha Watanzania kwa kupitia miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kuna kata ambazo zilikuwa hazijawahi kupata kabisa kuunganishwa kwa barabara. Ni kwa kipindi hiki baada ya ongezeko la Bajeti *TARURA* wananchi sasa wameona umuhimu wa chombo hiki cha *TARURA*. Naomba nitoe ushauri kidogo hapa *TARURA*. Kwanza, uangaliwe upya ule muundo wake wa *TARURA* ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tukitaka kupima ubora wa barabara wanazotengeneza *TARURA* kwa kulinganisha na *TANROAD,* nafikiri tutakuwa hatuwatendei haki sana watu wa *TARURA*. Madaraja yale ya vijijini, sasa hivi tunazungumza hapa mafuriko kila kona hasa sisi tunaotoka Mkoa wa Rukwa. Ukiangalia bajeti waliyonayo madaraja mawili tu bajeti inakwisha. Kwa hiyo kama tutasema tupime ubora wake, ni lazima leo tuone tena umuhimu wa chombo hiki tukiongezee bajeti zaidi, sasa tutaweza kuwapima kulingana na kile ambacho wanakipata.

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya yetu ya Nkasi bado tuko gizani, wanapotengeneza hizo barabara tunaomba

watuwekee taa za barabarani. Wilaya ya Nkasi ni sawa na wilaya nyingine tunaomba tupate taa za barabarani.

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto ya Vivuko. Nimekwishapeleka ofisini kwa Mheshimiwa Waziri mara kadhaa, lakini nasikitika mpaka hapa nazungumza kuna kivuko kinachotoka Kata ya Namanyele kwenda Kata ya Isunta, kwa mara nyingine nimepeleka taarifa ofisini amefariki mwanafunzi wa darasa la saba, tunataka nani afe tena ili tuone uzito wa kutengeneza kivuko hiki? Inaumiza inaumiza sana, tunaomba tupate majibu katika vivuko 23 angalau vivuko saba ambavyo vinaunganisha taasisi ikiwemo upande shule za sekondari na *primary* tusiue watoto wetu ambao tunategemea kesho wawe viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na ubora wa barabara hizi, ukiangalia vijijini sisi tunalima. Ukija kwenye ile sheria ya tani 10 unategemea sasa huyu mkulima anayelima pale anawezaje kusafirisha mazao yake kwa kuweka hicho kigezo? Kwa hiyo, ni vizuri pia tukaangalia kama kuna namna nyingine ya kuwasaidia wananchi hawa wa vijijini, waone barabara hizi ni baraka na sio balaa tena. Nayasema haya kwa sababu sisi tuna barabara moja ya mkoani ambayo inatoka Mkoa wa Katavi kwenda Rukwa, zile barabara nyingine ambazo magari yanapita lazima tutapitisha kule ambayo ni zaidi ya tani 10. Kwa hiyo niombe kwa namna bora ambayo tunaweza kufanya kama ambavyo wamepokea fedha hizi na kuona baraka ya *TARURA* iendelee kuwa baraka badala ya kugeuka kuwa balaa.

Mheshimiwa Spika, naomba niongeze tena neno moja la kushauri upande wa *TARURA,* tuwaongezee wataalam. Tukiwaongezea wataaalam, nafikiri wataboresha zaidi utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni mgawanyo wa fedha za miradi inayoendelea. Ukitazama mgawanyo wa

fedha hizi unakuta fedha labda za madarasa, fedha za kumalizia vituo vya afya, mtu wa Dar es Salaam na mtu wa Nkasi wakipewa sawa haiwezekani. Sisi tunaotoka kule ukiangalia kwanza eneo lenyewe ambalo vifaa vinakwenda ni gharama zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, gharama ya vifaa haiwezi kuwa sawa yaani mtu aliyenunua Dar es Salaam haiwezi kuwa sawa na mtu wa Nkansi. Kwa hiyo ukitoa kipimo hicho cha kwamba madarasa yote ni milioni 20, hatuyatendei haki maeneo mengine yakiwemo maeneo ya Nkasi. Kwa hiyo, tuangalie upya namna ya kugawa hizo fedha kulingana na uhalisia wa maeneo yenyewe.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie jambo kidogo hapo. Pamoja na miradi inayoendelea, ni kweli wataalam wetu wanasimamia miradi hiyo. Ukiangalia tu miradi ya kipindi cha *COVID,* yale madarasa ubora wake sijui ni kwa sababu ya *speed* au kwa sababu ya jina nilizungumza na mwaka jana hapa. Kuna haja hata kama tunawatumia Walimu wetu kwa sababu ya uhaba wa watalaam, tusiwahukumu kwa makosa yale ambayo hayaendani na taaluma zao. Tupeleke wataalam wa kutosha ili tuwahukumu kwa sababu hizo nafasi ni za kwao na wamesomea mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye Sera ya Afya. Mkoa wetu wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa ambayo bado hatujabahatika sana sera hii kutekelezwa kikamilifu. Nianze tu kwenye jimbo langu. Jimbo la Nkasi Kaskazini lina kata 17, katika kata 17 ni vituo viwili tu kwa maana ya kata mbili kati ya kata 17. Kwa hiyo, tunaomba sera hii ikamilike kikamilifu. Nimesikia kauli mbalimbali zinazungumzwa, mara tunaanza kujenga kwa tarafa, hii sera imebadilishwa lini kutoka kwenye kila kata kituo cha afya, zahanati kila kijiji na mpaka waje tena kwenye tarafa? Kama sera imebadilishwa

tujulishwe kwamba kwa sasa sio tena kila kata kituo cha afya badala yake ni tarafa kituo kimoja.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba kuna ujenzi unaendelea Kituo cha Afya Kabwe, nashukuru kwa jambo hilo, lakini ukiangalia umbali wa wanachi wanaotoka Kata ya Korongwe waje Kata ya Kabwe bado tutakuwa hatujakwenda kwenye hiyo sera yenyewe ya namna ya kuwasaidia Watanzania, lakini huduma zitolewe kulingana na hadhi.  Kama ni kituo cha afya kitoe huduma kulingana na hadhi ya kituo cha afya, lakini kama tutajenga jengo hakuna vifaatiba, hakuna watumishi, lengo letu sio majengo, tunategemea tupate huduma na kusogeza huduma kwa wananchi.  Tukifanya hivyo tutapunguza sasa idadi ya watu wanaokwenda hospitali za wilaya na mkoa kwa sababu huduma kule chini zitakuwa zinatolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, vijiji viko 64 ni vijiji 20 tu vyenye zahanati. Sasa hivyo vijiiji 20 utakuta zahanati moja ina mhudumu mmoja na hiyo zahanati inahudumia zaidi ya vijiji sita.  Ndio maana tunasema watu wa mjini kidogo anaweza akatoka pale akaenda eneo lingine, lakini watu wa vijijini aki-*move* zaidi ya kilomita 90 tumemsaidiaje huyo mwananchi?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu waliohitimu upande wa afya wapo, kuna shida gani ya kuwapa ajira? Tuone namna ya kusaidia afya za Watanzania na hiyo itakuwa na maana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia upande wa afya tukipeleka watumishi, kuna maeneo tumejenga Hospitali za Wilaya kwa ajili ya kuangalia eneo kubwa, kwa hiyo, unaangalia mtumishi ili atoke kwake aende pale ni zaidi ya kilomita Sita, tuombe gari kwa ajili ya watumishi hawa ili watimize wajibu wao, badala ya kuwahukumu kwa kutokwenda kwa wakati na kuwasaidia wananchi kulingana

na umbali uliopo anakotoka na anakokwenda kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya ya Nkasi watumishi wanafanya kazi nzuri sana ya kujitolea, hata wananchi wana-*appreciate* kwa kazi ambayo wanaiona wanavyopokelewa na huduma wanazopewa lakini umbali itakuwa ni changamoto ya watumishi kushindwa kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde thelathini malizia.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kushauri ajira hizi ambazo zimetoka muangalie sehemu zenye changamoto nyingi ikiwepo Nkasi kwa kutazama kwa upendeleo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii iliyowasillishwa na Mheshimiwa Waziri ya Fungu 56 pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kwa haraka kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais nami natambua Dada yangu huyu ana uwezo mkubwa na anafanya kazi vizuri sana. Pamoja na timu yake nzima ya Naibu Mawaziri wawili pia kwa Wataalam Kaka yangu Adolph Ndunguru na Wasaidizi wako au Naibu Makatibu wote watatu.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka na kwa kipekee sana nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli wananchi wa Wilaya ya Ubungo, wananchi wa Jimbo la Kibamba tuna kila sababu ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Wengi wamesema hapa nitakuwa mchoyo wa fadhila hizi za kushukuru kama sitasema dakika moja kwenye muda wangu wa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, tumeona mambo mengi sana ndani ya Jimbo la Kibamba, ndani ya kipindi chake kidogo tu tayari ametujengea shule Nne za sekondari, ikiwepo shule maalum ambayo kaleta Bilioni Tatu imejenga shule maalumu ya Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Sita ya Wasichana hili ni jambo kubwa sana. Pia juzi tu tayari siku ya Jumatatu inawezekana tukazindua uanzishaji wa ujenzi wa Chuo cha *VETA* kule pembezoni kabisa ndani ya Jimbo la Kibamba - Kata ya kibamba, jambo kubwa. Mengine mazuri mengi sana tunaendelea kumsemea Mheshimiwa Rais wetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba iliyowasilishwa hapa nitajielekeza katika maeneo mawili hivi kama muda utaniruhusu, nilikuwa nina zaidi hata ya mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni hili la asilimia 10 limesemwa na wengi. Jambo hili limenihuzunisha sana na limenihuzunisha kwa sababu ya kuona machozi ya Mheshimiwa Rais kwenye nia njema ambayo kama Taifa tulitamani kuona ile ajenda ya kuwainua wananchi wetu kiuchumi inafikiwa, lakini zimetoka fedha, na nikuambie kwa 2022/2023 zilitengwa bilioni 75 kwa ajili ya eneo hili na hizo ni sehemu tu ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo karibu bilioni 394 zikasogea kidogo katika eneo hilo la asilimia 10, bilioni 75 kwa nchi nzima, lakini tunaambiwa na *CAG* katika mwaka huo tu uliokaguliwa 2021/2022 *almost* bilioni 88.8. maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, maana yake hata zile tunazotengwa za mwaka mzima kwa nchi nzima zinapigwa zote. Ndiyo tafsiri tu ya kihesabu! Kama 2022/2023 tumetenga bilioni 75 lakini 2021/2022 tumetoka kukaguliwa zimepigwa bilioni 88, maana yake asilimia 100 tuliyotengewa imepigwa, hii ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo hapa kwenye hili, kupigwa tumezoea lakini kuna changamoto kwenye hili. Tunaambiwa vipo vikundi vingine hata havipo, vina fedha nyingi tu. Mimi ninashauri katika eneo hili, kubwa limesemwa na Kamati tumesikia, patakuwa hakuna mahusiano mazuri kati ya Wasimamizi Madiwani lakini na *CMT* katika maeneo mengi ambayo ukiangalia na *analysis* imejionesha kwenye Halmashauri nyingi tu ambazo zimeangaliwa au *CAG* kaziona Tatu zimeaharibu sana.

Mheshimiwa Spika, katika ya milioni 200 karibu milioni 774 ambazo fedha zilitolewa milioni 774 wakajigawia watu wenyewe, miongoni mwa wanakikundi nje ya miradi iliyozingatiwa. Tafsiri yake nini? Unaona Wilaya ya Ubungo ninayotokea mimi milioni 218 zaidi ya asilimia 40, yaani tumeziiba eti! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawaona Halmashauri ya Makambako na Geita wanaenda zaidi ya Milioni 172 Makambako, Halmashauri ya Geita Milioni 112, ni nyingi! NI nini hapa nataka kusema? Kanuni zetu na Mheshimiwa Waziri ulizoziweka kwenye kusimamia hii, nikukumbushe tu tunaongozwa na Kanuni ya 24 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya mwaka 2019, tumekubaliana adhabu maana wanaoiba lazima adhabu ziwepo *intact,* faini ni kati ya shilingi laki mbili na milioni moja au kifungo kati ya miezi 12 na 24.

Mheshimiwa Spika, hebu ona watu wamepiga Milioni 700 unaenda kumwambia adhabu yake ni kukulipa kati ya

Laki Mbili na Milioni Moja tumekuwa wapi? Hii ni changamoto kweli! Au Kifungo cha kati ya miezi 12 na 24 mojawapo, lakini wangapi wamefungwa? Mpaka leo hatuoni. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakuamini sana kwenye hili, tuendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais nia yake ya kuona watu wanachukuliwa hatua haraka wachukuliwe hatua haraka na sheria zinakuongoza tu, hata kabla hatujakaa mwezi wa Nane na wa Kumi na Moja kwa maana ya Taarifa ya CAG. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, utakumbuka sana mara nyingi huwa nachangia sana Wizara ya Afya na mwaka huu nimeomba lakini sidhani kama nitafanikiwa kuichangia, eneo lenyewe leo nimelijua ni la nani. Mheshimiwa Waziri kazungumzia juu ya K tatu, Kupima, Kupanga na Kurasimisha ardhi, kumbe ni jukumu la msingi la Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ubungo Jimbo la Kibamba tunalia hapa kila siku, tumefeli kabisa kwenye jambo la urasimishaji, mara nyingi nimechangia hapa nakuonyesha zaidi ya bilioni tatu zimepotea Mheshimiwa Waziri anashuka mara kwa mara Wilayani lakini tumefanikisha mimi na yeye kukubaliana dhamana ya kwake kama Msimamizi wa Sera ni kutoa Hati, lakini jukumu la Kupima, Kupanga na Kuthaminisha ni jukumu hili ambalo lipo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Bilioni zetu Tatu na zaidi zilishapotea, nimeomba hata Waziri Mkuu aingilie kuzitafuta hizi hela hamna.

Mheshimiwa Spika, nimeshangaa hotuba ya Mheshimiwa Waziri naikuta najua hili janga kalikuta, kuna Bilioni 49.9 kazitamka yeye zimeenda kwenye Halmashauri huko kama *revolving* kwa jukumu la KKK, na yeye anasema kwenye ripoti amefanikiwa kwa asilimia zaidi ya 90 ya jambo hilo, lakini CAG sasa wakati anamkabidhi Mheshimiwa Rais anazungumza bilioni 29.9 zaidi ya asilimia 59.6 zimepigwa hazijarudishwa mpaka sasa, eneo hilo hilo katika Bilioni 50

zimetoka, nyuma yake tulitoa Bilioni 46 zaidi ya asilimia 50 hela zinapotea.

Mheshimiwa Spika, ni lazima wenyewe tujionee huruma, wananchi kule Kibamba wametoa wenyewe zaidi ya Bilioni Tatu za kwao, Halmashauri nyingine zinapewa na hela hazirudi, tujitahidi kwenda na Kibamba zile hela wale waliopima kupanga au wameshatoa hela zao laki mbili hadi laki tatu tuone jinsi gani ya kuwasaidia wapate hati zao badala ya kuendelea kuwatesa. Niliona hilo niliweke katika sura hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu na la mwisho ni jambo la *TARURA* limesemwa na waliotangulia. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, wakati wa *reference* ya mwaka 2020/2021 tulikuta *TARURA* inapokea takribani Bilioni 250 hivi, lakini kwa kuingia ule mwaka wa 2021/2022 Mheshimiwa Rais kwa kufikiria kwa kina sana akaona hela haitoshi, Wabunge tukalia hapa akaingiza Shilingi Mia Moja ya tozo ya mafuta ya *diesel*, *petrol* na mafuta ya taa ikatuongezea tukafika Bilioni 700. Kwa hiyo, unaweza kumuona Mheshimiwa Rais alituvusha na tukiona kwenye Halmashauri zetu, tumeona kwenye Majimbo yetu mambo mazuri yamefanyika. Kuanzia 2022/2023 ongezeko kutoka pale ni dogo sana lakini hata leo anatamka tena Mheshimiwa Waziri kiasi kilichoongezwa *TARURA* bado hatuioni ile nia tena ileile iliyoanza, madhara yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, mimi na wewe ni mashahidi hata kule kwenye Jimbo lako la Mbeya, *population* inaongezeka kwa mujibu wa *statistics* iliyotolewa sasa hivi ya mwaka 2020, vilevile maombi mengi ya barabara za vumbi kuelekea *TARURA* ni makubwa sana lakini na mtandao wa barabara wa muda mrefu ni 144,000 lakini za vumbi ni zaidi ya kilomita 130,000 hivi, maana yake hali ni mbaya sana! Nini kinaweza kikafanyika?

Mheshimiwa Spika, tukitaka kujenga barabara zote na akili kubwa tukaipeleka kwa wananchi ambao ndiyo tunawawakilisha, maana yake tukapeleke angalau kwa kilomita 130, 000 zilizobaki hazijawahi kushughulikiwa Milioni 500 tukajenga lami, maana yake unaweza ukaenda ukatafuta Trilioni 65 unazitoa wapi, kama kuanzia leo hatuna nia njema ya kupeleka hela nyingi kama alivyofanya Rais mwaka 2022/2023 kwenda kuogeza zaidi ya bilioni 500 pale kupitia shilingi 100 ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nia yangu ni kuona kama Taifa tunapeleka nia njema ya kujenga barabara za vumbi na changarawe zikawe za lami ili maendeleo haya yaende kwa kasi sana, kuliko yale ambayo tunayaona ni ya kimkakati, miradi ya vielelezo ni vizuri lakini wananchi wa pale Kibamba kule ndani ambao hawawezi hata kupata huduma ya afya kwa sababu ya vumbi na udongo, anashindwa kuweza kuelewa ataenda saa ngapi kwenye reli ataenda saa ngapi kwenye maeneo yenye ndege ataenda saa ngapi kwenye maeneo mengine, kwa hiyo tufungamanishe miradi ya kielelezo na miradi inayowagusa wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, nafikiri nimetendea haki siku uliyonipa na kwa kutumia nafasi hii niunge mkono hoja iliyopo mbele yetu. Nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, vilevile namshukuru sana Mwenyezi Mungu kutujalia tena leo kukutana hapa na kutupa nafasi ya kuweza kuzungumza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya nchi

hii, vilevile kazi kubwa ambayo wananchi wa busanda wanaiona inaendelea kwenye maeneo yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hilo, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa TAMISEMI kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi nijikite kwenye maeneo matatu, kwanza Elimu ya Shule ya Msingi ambayo hata mwaka jana niliizungumzia. Tumeingia kama Taifa kwenye mmomonyoko wa maadili ambao kila mmoja sasa hivi anapiga kelele sitaki nirudie tena, lakini mahali fulani kwa sababu misingi yetu haikuwa imara ndiyo sababu tuna mashaka na kile kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuna kazi kubwa ya kutengeneza msingi ili huu msingi ukiwepo basi tusipate kuyumbayumba kama kuna vitu vinaingia vipya na hapa lazima tunaanza kwenye familia zetu ambako siyo Wizara hii lakini tunakwenda kwenye Shule za Msingi ambako tunapeleka watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote watakuwa ni mashahidi kwamba Shule za Msingi nyingi zimechakaa na uchakavu wake TAMISEMI kwa ubunifu wamekuja na miradi mingi *BOOST, LANES, SRWSS* kuhakikisha kwamba tunaweza kuboresha shule za msingi, lakini kiukweli uchakavu ni mkubwa sana na pesa inayokwenda hiyo ni kidogo kurudisha Shule za Msingi kwenye hali yake ya kawaida. Hivi watakuwa na kumbukumbu nzuri tu kwamba hata mdororo ile *drop out* itakuwa ni kubwa. Watoto wengi sasa hawako- *interested* sana kwenda kwa sababu wanajua mazingira ya nyumbani yanaweza kuwa ni mazuri kuliko Shule ya Msingi anayokwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunategemea sasa waongeze pesa kuhakikisha kwamba shule za msingi

zimeboreshwa na zikiboreshwa kama ilivyo sekondari, bahati nzuri ni kwamba sekondari zimeboreshwa, baada ya kuboresha sekondari sasa ni rahisi kujua kwamba Shule ya Msingi hii siyo bora kwa sababu sekondari ina vioo na Shule ya Msingi inaonekana wazi kwamba hii siyo bora, kwa hiyo kuna kazi kubwa ya kufanya ya kuboresha shule za msingi na tujenge msingi kwa kuweka *content* ambazo watoto wetu hawatayumba kama maadili yatakuwa yameyumbishwa na dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wasemaji wa kwanza walivyosema juu ya shule za msingi, tuna maboma mengi yaliyojengwa na wananchi kwa nguvu za wananchi yanatakiwa kumaliziwa haya. Ni changamoto kubwa inapokuja kujenga madarasa mapya wakati kuna madarasa hayajaezekwa yako matano shuleni pale. Wananchi wanajiuliza hawa wameona nini waje wajenge mapya haya ya kwetu wayaache? Kwa hiyo, ni ombi langu TAMISEMI waangalie uwezekano wa kuyamalizia hayo maboma ambayo yamekwisha anzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo yangu kwa uchakavu huu tu nina mifano michache, nina shule kwa mfano ya *primary* ya Lurama kwenye Kata ya Bukondo, ukifika tu unajua ukweli hii shule ni chakavu, shule ya Lubanda kwenye Kata ya Busanda ukifika tu unajua shule hii ni chakavu, shule ya Lukumbo katika Kata ya Butundwe ukifika tu unajua shule ni chakavu, hii ni mifano michache tu lakini ziko nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni ombi langu kwamba, pesa hizi tunazozitoa ziwe ni za kutosha ili kasi ya kurekebisha shule zetu za msingi ionekane kwenye maeneo yetu. Kwa mfano, kuna miradi ya *BOOST* ambayo ilibajetiwa nafikiri mwaka jana, ukiuliza kule Halmashauri wanakuambia pesa haijafika hadi leo! Sasa kama haijafika maana yake tutakuwa tumewaambia wananchi mwezi wa Nane kwamba kuna

*BOOST* inakuja kurekebisha shule za msingi na pesa haijafika, kwa hiyo kinachoonekana ni Mbunge amesema uwongo nafikiri ndiyo ukweli wenyewe huo, ama Mbunge kasema uongo kwenye eneo lake. Kwa hiyo, niombe sana hizo pesa za *BOOST* zilizosemwa ziende kufanya kazi ile ili tuwezwe kuhakikisha kwamba yale tuliyoyasema ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni *TARURA*. Kwenye *TARURA* hapa kuna kazi kubwa wamefanya inaonekana kazi yao, lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuongeza fedha kwenye Mfuko huu wa *TARURA* tumeendelea kujenga barabara zetu. Changamoto ambayo nataka kuisema hapa, Mfuko wa *TARURA* hauna fedha ya dharura, kwa hiyo inapotokea kwa mfano sasa hivi mvua zinanyesha kwenye maeneo mengi, barabara ikiharibika huyu Meneja au Injinia wa *TARURA* wa Wilaya hana uwezo wa kwenda kufanya kitu chochote atakuambia tusubiri bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Spika, sasa kama barabara imekatika watoto hawawezi kwenda shule, bajeti inayokuja itakuja lini? Nina mfano mdogo kwenye eneo langu, barabara kutoka Nyakagwe kwenda Butobela ambako ndiko kuna *secondary school* daraja limekatika, lakini maelezo yake ni kwamba tutaomba kwenye bajeti inayokuja kwa sababu hana uwezo wa kufanya kitu chochote, watoto wasiende shule?

Mheshimiwa Spika, hivyo, tuone tu namna gani tunaweza kuwa na pesa ya dharura kwenye maeneo hayo ili watoto wetu waendelee kupata huduma kwa utaratibu ule ambao unakubalika. Kama inaonekana fedha ni kidogo siyo vibaya kuiga kama *TANROADS* walivyo wameingiza *EPC+F* nao waongeze *EPC+F* na pesa yao iwe ndogo ili tuweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipopita pale kwangu Katoro tuliomba Bilioni 15 kufungua barabara za Katoro, akasema atatoa pesa kidogo kidogo, bahati mbaya

sijaziona ninaamini Mheshimiwa Waziri utakuwa umeziandika mahali fulani nisipoziona maana yake nitajua kwamba Mheshimiwa sasa wananchi watakuwa wanasema Mheshimiwa Rais alichokisema siyo sahihi, ningeomba sana ziingie mahali fulani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba haya yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni sekta ya afya. Mwaka juzi tulitembezewa karatasi hapa Bungeni kila mmoja aka-*suggest* vituo vyake vya afya anavyotaka vijengwe. Mimi niandika vitatu hakijatokea hata kimoja sasa nikawa najiuliza huu ni muujiza au ni kitu gani, kwa sababu niliandika vitatu na hakikutokea hata kimoja. Bahati nzuri sana Kata niliyoiandika kwa mfano Kata ya Lwamgasa ni kwa wachimba madini, kuna wananchi takribani 40,000 kwenye Kata ile, wanahitaji kituo cha afya lakini kituo hakikupatikana. Nikaandika Kata ya pili ya Nyakagomba ina wananchi takribani 30,000 kituo hakikupatikana, nikaandika Kata ya Tatu ya Magenge kuna wananchi karibu takribani 17,000 haikupatikana. Ni kweli inawezekana *criteria* iliyotumika ilitutoa nje kwamba inahitaji Tarafa, lakini hawa wananchi wote tutawahudumiaje?

Mheshimiwa Spika, ni ombi langu sasa Mheshimiwa Waziri uangalie uwezekano wa vituo hivi tuvipate kwa ajili ya kuhudumia wananchi wetu, wananchi 40,000 hawana kituo cha afya tutawahudumiaje wanahamia kwenda kununua dawa kwenye *pharmacy*, wanapougua tu wanahisi hii yawezekana ni malaria acha nifanye nini, ninunue dawa tu nipone wengine watakuwa wanapoteza maisha kwa mtindo huo. Kwa hiyo, ni ombi langu Mheshimiwa Waziri kwamba hili utalikumbuka na utaweza kulifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwenye afya nako tuna maboma, nimeona maboma 300 kwenye ukurasa Namba 21 yanaonekana yamejengwa, kule Busanda yapo maboma mengi tu ya zahanati yamejengwa yanahitaji kumaliziwa, niombe sana kwenye bajeti hii Wizara iangalie uwezekano

wa kuyamalizia hayo maboma, yako yaliyoezekwa yanahitaji umaliziaji, yako ambayo hayajaezekwa yanahitaji kumaliziwa tu ili wananchi waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa haya niliyoyasema machache kama yakiguswa nitajua hii bajeti kule kwangu watasema ni bajeti ya wananchi. Baada ya maneno haya naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu siku ya leo, tutaendelea Alasiri leo. Niwataje Wabunge wachache ambao tutaanza nao kwa michango yao hapo mchana ni Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokuwa unaendelea tutakapo kutana alasiri.

Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni wa Mheshimiwa Olelekaita Kisau ambae hakupata nafasi ya kutangazwa wakati tukitangaza wageni ile asubuhi na huyu ni Ndugu Jeremia Mwimbe Maina. Nimejulishwa kwamba huyu ndiyo Mwenyekiti wa Watumiaji ama Wakulima wale ambao wanatumia yale Matrekta ya *Ursus* kwa hiyo mpaka wamejiunga wamekuwa na umoja wao na huyu ndiye Mwenyekiti wao.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao ni wageni wangu wameingia mchana huu, huu ni ugeni wa kutoka nchi ya Slovenia anayeongoza ugeni huu ni… sasa inabidi niseme kiingereze siyo? Ili tuende nao sambamba lakini Kiongozi anayeongoza ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Slovenia lakini pia yeye ni Naibu Waziri Mkuu wa Slovania kwa hiyo nitaanza kuwatangaza. Kwa hiyo huyo ni:-

*Honorable Tanja Fajon; Deputy Prime Minister and Minister for Foreign Affairs of Slovenia. You are warmly welcome to Tanzania with all your delegation. Now, I will proceed to mention their names as well. (Applause)*

*Ambassador Mateja Prevolsek, Head of Department for Africa and Middle East, Ministry of Foreign and European Affairs of Slovenia, Thank you very much. We also have Maja Kezunovic Krasek, Deputy of Head of Minister Cabinet, Member of Delegation. Thank you. (Applause)*

*We also have Dragan Barbutovski, Head of Strategic Communication Services, Ministry of Foreign and European Affairs of Slovenia. Thank you so much. We also have Rok Hlade Weis, who is accompanying Official. Thank you so much. We also have Damijan Dimic, who is also their accompanying Official. We also have Ales Miklavcic, accompanying Official. Thank you so much. (Applause)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ugeni huu umeambatana na viongozi wengine kutoka Wizara yetu ya Mambo ya Nje, yupo Balozi Swahiba Mdeme - Mkurugenzi wa Idara ya Ulaya na Amerika Wizara ya Mambo ya Nje. karibu sana. Ameongozana pia na Ndugu Gerald Mbwafu - Mkurugenzi Msaidizi Wizara ya Mambo ya Nje, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Jacob Msekwa ambaye ni Afisa Mwandamizi Wizara ya Mambo ya Nje, Karibu sana. Pia Ndugu Mariam Kilongo - Afisa Itifaki Wizara ya Mambo ya Nje, haya naona yeye hayupo. Yupo Ndugu Theo Komba - Afisa Mawasiliano Wizara ya Mambo ya Nje, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine nilikuwa nimeshawatambulisha asubuhi, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi Kamili Alasiri leo.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, mchangiaji wetu wa kwanza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwa mtu wa kwanza katika kuchangia hotuba ya TAMISEMI kwa jioni ya leo ya tarehe 14 mwenzi wa nne mwaka huu wa 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wananchi wa Buhigwe wamenituma nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Tanzania kwa fedha nyingi sana ambazo amepeleka katika Wilaya ya Buhigwe. Amefungua wilaya yetu na ameendelea kufungua mkoa wetu. Amefanya nini katika Wilaya yetu ya

Buhigwe? Amegusa Maisha ya wananchi ya kila siku katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 tulipata shilingi 3,336,624,000,901 ambazo zilikuja kwenye ukamilishaji wa maboma ya shule za msingi, ukarabati wa shule kongwe, ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule za msingi, ukamilishaji wa zahanati, ununuzi wa vifaa tiba kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati. Wananchi wa Buhigwe wanasema ahsante sana. Wanatoa shukrani za dhati kwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Kairuki pamoja na Manaibu wake Mawaziri akiwepo Mheshimiwa Festo pamoja na Mheshimiwa Ndejembi kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi ya pekee kwa kuwashukuru kwa utaratibu mzuri ambao mwaka huu tumeuona. Walituita wakiwa na kikosi kazi cha TAMISEMI, tukakaa nao sisi kama Wabunge wa kila mkoa na wakatupa nafasi ya kutoa vipaumbele vyetu na changamoto. Katika nafasi hiyo, kuna methali Waswahili wanasema, "kiu isiyoweza kuishia kwenye mto, hiyo ni kifo." Basi tuliweza kutoa changamoto zetu, tukatoa vipaumbele vyetu na tumeona kwa uhakika waliyapeleka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ameyajibu kwa matendo. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa afya, tumeona kazi kubwa sana kwa wilaya ambayo ni changa. Tumepata vituo vitatu vya afya. Kituo cha Kajana, tulipata shilingi milioni 500, Mayaya shilingi milioni 500 na Lusaba shilingi milioni 500. Tunategemea mwezi wa Saba vitaanza kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo tumepata fedha za kumalizia maboma ya zahanati katika vijiji sita, tulipata shilingi milioni 300. Wananchi wa Buhigwe pamoja na

viongozi wote wa vyama vyote na wa madhehebu yote wamenituma nije nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *TARURA*, katika miaka hii miwili ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametusaidia pakubwa. Japokuwa mahitaji yetu ni makubwa, lakini tulipata shilingi bilioni 5.9 ambazo zimeweza kutujengea kilometa tano za lami Makao Makuu ya Wilaya na tukajengewa kilometa 1.2 ya lami na kilometa moja. Mpaka sasa hivi tunao mradi mwingine ambao tumeupata, na tumepatiwa fedha. Mradi huo unatoka katika Kata ya Muyama kupitia Kasumo kwenda Kasulu kilometa 12, ambazo zitagharimu fedha ya Kitanzania shilingi bilioni 15.6, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utawala bora, Mheshimiwa Rais ametusaidia parefu na pakubwa sana. Kwa miaka mingi tulikuwa hatuna Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, alitoa fedha na mwaka 2022 tarehe 16 Mwezi wa Kumi yeye mwenyewe amekuja kuizindua. Sambamba na hilo, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya umeshakamilika na huduma zinaendelea kutolewa. Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Buhigwe umeanza kujengwa. Tunamshukuru sana, tunampongeza sana na Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani, bado tunazo changamoto nyingi. Moja, tunao upungufu mkubwa kwenye kada ya watumishi wa afya. Mahitaji yetu kwenye afya ni wafanyakazi 819, waliopo ni 210 pungufu ni 609. Tuna upungufu wa asilimia 75. Tunaomba ajira mpya mtupe kipaumbele mlete watumishi. Kwenye upande wa elimu, mahitaji ni walimu 1,487; waliopo ni 692, pungufu ni 794, sawa na asilimia 55. Kwenye ajira hizi mpya tunaomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma na kwa upendo mkubwa mwaelekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi maalumu kwa vijana wanaojitolea wa tasnia ya elimu. Kuna vijana wengi ambao wamejitolea baada ya kumaliza vyuo vyao, wapo kwenye shule zetu za kata, wapo kwenye shule zetu za Serikali, hao ndio wahimili, ndio wazalishaji, na wameshatoa mchango mkubwa. Naomba sana, katika hizi ajira mpya ambazo zimetolewa kwa moyo wa dhati na kwa huruma ya Mungu, hawa wapewe kipaumbele. Wapewe kipaumbele katika ajira hizi zilizotangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, pamoja na kwamba tumepata vituo vya afya, bado tuna kata ambazo zina idadi kubwa ya watu, na uzuri watu wa kule Buhigwe wameshajipanga kwa ajili ya kuchangia kwenye shughuli za maendeleo. Kata ya Muhinda na Kata ya Mubanga wameshachagua sehemu ambayo wakipata fedha ya kujenga kituo cha afya ambacho kitasaidia wananchi zaidi ya 45, wameshaanza na mchakato wa kufyatua tofali. Tunaomba kituo cha afya kijengwe katikati ya Kata ya Muhinda na Mubanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine ni kituo cha afya tena ambacho kitasaidia tena kata mbili na ni mpakani mwa Burundi kabisa kuna watu wengi, zaidi ya 44,000, nayo ni Kata ya Mkatanga na Kata ya Kibwigwa. Kituo hicho kije kijengwe katikati ya Kata ya Kibwigwa na Mkatanga, nao wameshachagua sehemu yao ambayo inaitwa Muharuro hapo ni *center* nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo marefu, nakushukuru sana, naishukuru Serikali, najua imesikia na itatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Kavejuru Felix. Namwita Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, wakati

huo Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea wanajiandaa.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami kama ilivyo ada nianze na neno la shukurani. Mimi ni Mjumbe kutoka TAMISEMI, kwa hiyo, kwa kiwango kikubwa, haya ambayo tumeyaona yanaakisi yale ambayo tulishiriki katika Kamati. Kwa hiyo, mchango wangu nitajielekeza katika maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naanza na shukurani. Awali ni kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia naomba kwa namna ya pekee, najua tunaye Waziri wetu na Manaibu Waziri; mkononi mwangu hapa ninayo barua ambayo Mheshimiwa Waziri ametupatia Wabunge wote ikiieleza taarifa za fedha za miradi ya maendeleo na matumizi mengineo kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Mheshimiwa Waziri, jambo hili ni jema. Kwetu sisi, hiki ni kitendea kazi. Mimi mtu wa Mpanda Manispaa, kwa taarifa hii ya fedha ambayo umetuelekeza Wabunge, ikawe kitendea kazi. Takribani Shilingi bilioni 5.9 ikilenga maeneo mbalimbali. *Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba, Wabunge tunafahamu, nami shukurani hizi nilizozitoa kwako naomba pia nizipeleke wa Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Madiwani. Kwa sababu gani? Mabilioni haya peke yetu hatuwezi, ni lazima iwe kwa kupitia ushirikiano.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Kwa hiyo, ndiyo maana wapo Madiwani, wapo Wenyeviti, wapo Mameya, na kwa pamoja tunalisukuma hili gurudumu. Kwa hiyo, naomba huko Madiwani huko waliko, wapokee shukurani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nijikite katika eneo la *TARURA,* najua kweli wanafanya kazi nzuri na siku zote hapa tumekuwa tukawasifia, bila kumsahau *Engineer* Seif. Nami nimesemaje? Siku zote yule ndugu yetu ni mtu rahimu. Ukimsifia mtu, unamtia moyo kwamba siku nyingine anajipanga vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba, najua kwa maana eneo letu la Katavi, Manispaa ya Mpanda, Mheshimiwa Waziri kipindi hiki cha mvua yapo maeneo katika nchi hii hayana mvua za kutosha. Sisi tumebahatika kupata mvua za kutosha. Sasa neema ile ya mvua imepelekea uharibifu mkubwa wa miundombinu. Nikiomba fedha Mheshimiwa kupitia *TARURA* lengo langu ni nini? Mazao mazuri yaliyozalishwa Katavi yaweze kukufikieni nyie ambao hamkubahatika kupata mvua. Kwa hiyo, nikiomba fedha, tafsiri yangu ni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwa maana ya matengenezo, tumetengewa Shilingi bilioni 1.1, ndiyo maana tulikuwa tunaomba watu wa *TARURA* waongezewe fedha. Kwa jinsi mvua ilivyoharibu miundombinu, ukija kwangu utanionea huruma. Nimesema wale watu wemelima vizuri, tunatamani mazao yatoke kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dada yangu Mheshimiwa Lupembe, yeye amebahatika kupata *boost,* wametengenea barabara ya lami mpaka kuisogeza kwenye mpaka na Manispaa. Nimeletewa kuchonganishwa na wananchi kule, wanasema, angalia mwenzake wa vijijini kapata lami, yeye wa mjini hana lami. Kwa hiyo, Waziri nafikiri ukilisikia hili, na wananchi kule wananisikia, kwamba jamani, mimi niliwasemeeni Bungeni. Ni kilometa chache tu Mheshimiwa Waziri. Ni kilometa kama nane hivi. Lengo ni nini? Lami nzuri iliyotengenezwa kule, isipounganika kuja mjini, inapoteza tafsiri. Jambo hilo nafikiri unaweza ukaliona na ukaona namna ya kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *MSD*. Tumezunguka maeneo mbalimbali katika nchi hii, ni kweli najua nao wana changamoto kama Serikali, lakini naomba, kwa kuwa kuna fedha nyingi zimepelekwa huko, mimi tu kwa upande wa Katavi kuna zaidi ya shilingi bilioni tano kwa maana ya vifaa. Wanajitahidi kwa kiwango chake, lakini wafanye zaidi, kwa sababu kuna fedha imewekezwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upungufu wa watumishi. Nina upungufu wa watumishi 969 katika maeneo yafuatayo: Walimu wa shule ya msingi 265, sekondari 148, watumishi afya 405, huo ni upungufu wa watumishi katika eneo letu la Katavi. Najua Serikali imefanya kazi nzuri kwa maana ya miundombinu, tumejengewa madarasa, vituo vya afya, lakini bila uwepo wa watumishi, kazi inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna suala la upembuzi yakinifu kuhusiana na suala la miradi, Naomba sana wataalamu wetu, tumepita pale Mwanza tukaliona hilo, kama suala la upembuzi yakinifu ni jambo la kuanza nalo, nashangaa pale ambapo kazi imeshakwenda, inafika mwisho, mtu anawarudisha nyuma akisema kuna gharama moja, mbili, tatu. Hili jambo linatuchelewesha kama Serikali. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana katika eneo hilo tena Serikali ijitafakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa maana ya *SEQUIP;* najua kuna Shilingi milioni 470. Kama walivyozungumza wazungumzaji wengine, naomba kwa maana ya thamani halisi ya fedha, Mheshimiwa Wizara yako iliangalie hili kwa jicho la pekee, ni kweli haiwezekani ikawa sare nchi zima, uwiano nchi nzima, na najua hilo kama Kamati tumelijadili na tukaomba mwangalie watu na jiografia za maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu anaweza akawa anapata mchanga sehemu ya karibu lakini akakosa *cement*.

Kuna mtu anaweza akapata kokoto, lakini akakosa mchanga, hivyo; mabati na vitu vingine kwa upande wa vifaa hivyo vya ujenzi. Kwa hiyo hilo nalo ilikuwa ni vizuri tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba eneo la Watendaji wa Kata, Vijiji kupata mafunzo kutoka Chuo cha Utumishi. Ni kwanini tunasema hili? Tunazungumzia Chuo cha Utumishi kwa sababu ndilo eneo ambalo watendaji wetu wanaweza wakapata ladha ya utumishi bora. Eneo la utumishi wa umma ni maeneo ambayo wanawaandaa watu wetu wajue Serikali inataka nini? Kwa hiyo, tukikuomba Mheshimiwa Waziri kwamba watu wetu hawa wapelekwe kwenye Chuo cha Utumishi wa Umma, tafsiri yake ni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, mpaka mwananchi akakukute wewe huko Wizarani, anaanza kucheza na Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji. Kwa hiyo, kule ndiko ambako taswira sahihi ya Serikali inajionesha. Kwa hiyo, tukiwa na mtu ambaye amefanya kazi vizuri katika ngazi ile, anamsaidia Mheshimiwa Rais, anakusaidia wewe na nchi inakuwa na ustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CSR*, kama ilivyozungumzwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya muda, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mambo anayoitendea Tanzania tangu ameingia madarakani ni makubwa, nasi wote ni mashaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, na kwenye hili nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Kairuki kwa kazi nzuri, na *speed* hii aliyoanza nayo naamini Halmashauri zetu sasa ziko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Naibu Waziri Mheshimiwa Festo Dugange na Mheshimiwa Deo Ndejembi kwa kweli wamekuwa wakizunguka kwenye halmashauri zetu wakikagua utekelezaji wa maono ya Mheshimiwa Rais namna fedha ambavyo amezipeleka. Hawa wanaendelea kufuatilia kwamba zinakwenda kufanya kazi sawa sawa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nimesema ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI. Kwenye ziara yetu tuliona miradi mingine ambayo imechelewa kukamilika na kati ya sababu wanasema ni mvutano wa wapi mradi utekelezwe. Wala haiingii akilini na kwenye jambo hili niiombe sana sana sana TAMISEMI hapa kubwa ni ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati miradi inakwenda wenzetu wataalamu kule *site* hawashirikishi wadau muhimu wanaohusika kwenye ile miradi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Huku ndani tunafanya kazi ya kusemea Majimbo yetu sasa miradi ikiwa inakwenda ni vizuri tushirikishwe ili kwenda sawa sawa kutokwamisha hii miradi kwa sababu ya kuvutana ni wapi mradi ukajengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Wizara ielekeze wataalam wetu kule watushirikishe, washirikishe Waheshimiwa Wabunge, lakini pia na wadau wengine ili kwenda kutekeleza miradi hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Nachingwea na Makao Makuu ya Wilaya ya Nachingwea ni mamlaka ya Mji Mdogo zaidi ya miaka 10 sasa. Tumeshatuma maombi ya kuwa Mji kamili zaidi ya miaka saba iliyopita. Niiombe sana sana Wizara jambo hili ni jema na sisi litakwenda kutuongezea uwezo kama halmashauri. Niwaombe sana muone namna ambavyo mtaharakisha jambo hili jema ili Nachingwea sasa Mamlaka ya Mji Mdogo iwe Mji kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao upungufu kwenye Sekta ya Afya na kwenye Sekta ya Elimu. Kwenye eneo hili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa sasa kibali kwa ajili ya kuajiri watumishi wapya kwenye eneo hili la elimu pamoja na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu kwa mfano; tukiwa tunazungumzia habari ya kuboresha miundombinu kwa maana ya majengo, yako majengo chungu nzima ambayo bado wananchi walijitolea bado hayajakamilishwa. Tunashukuru kwa namna ambavyo Serikali imetuletea madarasa, imetuletea vituo vya afya ni jambo jema lakini ziko nguvu za wananchi ambazo zimelala na bado hazijulikani hatma yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana sana sana Wizara waende kumalizia yale maboma ambayo wananchi walijitolea na nguvu zao wanaziona. Tuna vituo vya afya, tuna shule lakini pia tunazo zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kidogo kuzungumza kwa habari ya upungufu wa nyumba za waalimu. Mfano

mdogo Nachingwea mahitaji nyumba ni 413; zilizoko ni 72. Sasa utaona hiyo walimu wa sekondari mahitaji ni 413, zilizopo ni hizo 72, upungufu ni 341. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walimu wetu wanafanya kazi nzuri namimi nitumie nafasi hii kuwapongeza watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye elimu, kwenye afya na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu Nachingwea tunajivunia hata kwenye rekodi ya sasa tumekwenda sana na Lindi kiujumla kama Mkoa lakini kwa hali hii tuiombe sana Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu ambazo kwa kweli upungufu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matundu ya choo kwenye shule za sekondari. Mahitaji ni 564, yaliyoko ni 318; upungufu ni 246. Hebu angalia hiyo tofauti bado tuna kazi ya kufanya. Tunatambua na tunashukuru kwa kazi kubwa iliyofanyika lakini bado tunaomba zaidi kuendelea kutusaidia kwenye halmashauri hasa hasa hizi zilizoko vijijini kwa sababu zilisahaulika kwa muda mrefu. Sina mashaka na Mheshimiwa Waziri najua kazi hii utakwenda kuibeba vizuri na kazi hii itakwenda kufanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA*. Wenzangu wamesema hapa kazi nzuri inayofanyika na *TARURA* hakuna asiyeiona. Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana kwamba *TARURA* wanafanya kazi nzuri chini ya Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi wetu wa barabara *Engineer* Komba wanafanya kazi nzuri pamoja na watumishi wote wakiwemo wale wa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Nachingwea. Wanafanya kazi nzuri. Basi tuiombe sana Wizara iendelee kuangalia namna ambavyo wataongeza fedha ili hawa watendaji wetu mahiri kabisa watuboreshee miundombinu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kabla Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kuingia; Nachingwea fedha ya matengenezo ya barabara tulikuwa tunapata shilingi bilioni moja. Baada ya kuingia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imebadilika bajeti ya mwaka ni zaidi Shilingi bilioni tatu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jema na sisi kama Wabunge tunapaswa kuungana kwa kauli moja kuendelea kumtia moyo Mheshimiwa Rais, anatuheshimisha. Kazi inayofanyika kwenye Majimbo kwa kweli kila mmoja anajua na tunacho kitu cha kusema 2025 na kule Nachingwea wanasema wao 2025 na Mama Samia wala hawafichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanasema na Mama Samia. Wanajua haya yaliyobaki kama changamoto anakwenda kuyatatua kwa kipindi hiki ambacho kipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo habari ya Shule ya Mchepuo wa Kiingereza, shule za msingi. Kuna utitiri huo wa halmashauri zetu kuanzisha hizo shule za mchepuo wa kiingereza, ni jambo jema lakini jambo hili linakwenda kuweka matabaka tena. Niiombe Wizara twende tukaboreshe shule zetu za msingi zillizoko kwenye vijiji vyetu. Tupeleke waalimu wa kutosha, tupeleke vitendea kazi vya muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chinguile kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea wakati huo Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela na Mheshimiwa Deus Clement Sangu anajiandaa.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia Hotuba nzuri ya Wizara ya TAMISEMI na niweze kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze kwa ujumla Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, bado tuna changamoto nyingi. Nitachangia maeneo matatu lakini naomba nianze na *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana *TARURA* kwa kazi nzuri zinazofanywa na sisi wananchi tunaotoka mikoa ambayo maeneo mengi ni vijijini hasa Mkoa wa Tabora maeneo mengi ni vijijini tunatumia sana barabara za vumbi ambazo *TARURA* zinafanya kazi. Pamoja na kazi nzuri zinazofanywa lakini bado tuna changamoto kwenye maeneo ya majimbo yetu na wilaya zetu. Kwa mfano; naweza nikatoa mfano wa maeneo ambayo bado yana changamoto ili Serikali iweze kuchukulia hatua katika bajeti hii ambayo tunaenda kuipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Jimbo la Igalula Wilaya ya Uyui. Jimbo hili ni jimbo ambalo limekaa vibaya sana, yaani wilaya imekaa vibaya lakini vile vile bado kuna changamoto katika Kata ya Loya kuna daraja ambalo Mheshimiwa Rais mwaka jana 2022 alitoa ahadi pale lakini nashukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jenista jana amesemea yeye anahusika sana na ahadi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba Mheshimiwa Waziri ulichukue hili. Wananchi wa Loya wanateseka ni kama wapo kisiwani kwa sababu daraja kipindi hiki cha masika na ardhi ile inashika maji kwa muda mrefu na bahati nzuri kwa Mkoa wetu wa Tabora mvua zinanyesha sana mpaka hivi

sasa mvua ni nyingi na kuja kukauka inaweza maji yakaanza kupungua kuanzia mwezi wa nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa shughuli zao za uchumi ni mpunga. Sasa ule mpunga ambao wameuivisha kuanzia miezi hii ya mavuno watautoaje kule kwenda kupeleka kwenye maeneo ya kufanyia masoko? Kwa sababu daraja linakuwa limekatika watu wako visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna kijiji ambacho kiko kwenye hiyo hiyo kata…

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ndiyo taarifa Mheshimiwa

**T A A R I F A**

**MHE.VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri ambao anaendelea kuutoa dada yangu hapa amezigusia katika Jimbo la Igalula. Ni kweli Mheshimiwa Rais alifika tarehe 17 mwezi wa tano na akatoa maelekezo Wizara ya Ujenzi ianze kujenga Daraja la Loya. Nataka nimtoe wasi wasi Mheshimiwa Rais ahadi hiyo imeanza kutekelezeka lakini walianza kufanya mchakato, mchakato huo kwa sasa umesimama. Niiombe Serikali waendelee kusukuma kwa sababu maafa yanaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja unapokea taarifa ya Mheshimiwa Venant Protas?

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipokee, naomba niendelee. Katika hiyo kata imebahatika kuwa na kituo cha afya lakini kuna kijiji ambacho kinaitwa Mama Bona. Kutoka kwenda kupata

huduma za afya na za maendeleo ya jamii kwa ajili ya kijiji chao ni changamoto. Hawana mahusiano kwa sababu pale kuna mto ambao kuuvuka tumeshapata hasara ya wananchi ambao wameshafariki katika mto ule. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali iweke nguvu ya kuhakikisha daraja lile linatengenezwa na kata ile ina wananchi wengi karibia 38,000. Kwa hiyo, tukihakikisha daraja hilo linatengenezwa bajeti hii ipeleke nguvu katika lile daraja la Kata hiyo Loya katika Jimbo la Igalula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado jimbo hilo hilo ambayo Jografia yake ni mbaya kuna kata ambazo kufikika kwake ni lazima mwananchi akiwa Tabora mjini mkoani kurudi kwenye makazi yake ni lazima apite Nzega – Ndala ndiyo aende kwenye lile eneo. Inakuwa ni mzunguko mrefu sana. Wakati kuna barabara ambayo ingemuwezesha kutoka Tabora mjini kuingia jimboni kwake wilayani kwake kwenye kilometa 89 ikitengenezwa kwa kiwango cha changarawe wananchi wale wataweza kufaidika katika suala zima la uzalishaji wa uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie kwenye suala zima la huduma za afya. Tunaendelea kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri zinazofanya hasa kuhakikisha wanatuwekea majengo ya vituo vya afya ikiwepo zahanati. Lakini vituo vya afya hivi ambavyo ni Sera ya Afya inayosema zahanati kwa kila kijiji, vituo vya afya kwa kila kata. Bado tuna changamoto nyingi ya vifaatiba ambayo Wabunge wengi kila tukisimama hapa tunaongelea suala la vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano naweza nikatoa kwa Mkoa wangu, bado tuna changamoto hiyo unakuta mfano Wilaya ya Igunga tumepata vituo vya kutolea huduma nane. Katika nane, viwili ni vituo vya afya na sita ni zahanati, bado tuna changamoto ya vifaatiba na wahudumu wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumejenga yale majengo lakini bado hatujawatendea haki hawa wananchi. Nilikuwa naomba niishauri Serikali, tunapoendelea kukamilisha hii sera ya zahanati kila kijiji na vituo vya afya kwa kila kata, hebu tu-*focus* zaidi kwenye *quality* wakati tunaenda kuendelea kumaliza *quantity* kwa maana ya kwamba unakuta kuna vijiji vimepangana na jiografia yake viko mashariki pamoja; vijiji kama vinne, vitano vina zahanati kila kijiji lakini zahanati hizo tano mgonjwa anapoenda anaambulia kupata *paracetamol* na ataambulia kupata labda *Alu* lakini vipimo hapati kwa sababu vifaatiba hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hebu tupunguze badala ya kujenga vituo vyote vile vitano ambavyo vimejipanga kwa upande wa mashariki ikiwa magharibi hakuna hata kituo kimoja, vile vitano ile nguvu tukamilishe kwanza kimoja tu-*deal* kwenye *quality service* ambayo mtu akienda pale atapata huduma moja kwa moja kuliko mtu anaenda pale huduma hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuanenda kwenye suala la watumishi. Naipongeza Serikali imetoa watumishi 21,200. Bado ni wachache sana lakini niombe kwa Mkoa wetu wa Tabora ambao bado ni mkubwa, tunaomba watumishi tupate idadi ya kutosha. Kwa mfano, mahitaji yetu kwa sasa hivi tunaohitaji ni watumishi 6,299 lakini mapungufu tuliyonayo ni watumishi 3,860 sawa na 61% na waliopo ni 2,439 sawa na 39%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali katika bajeti hii ya watumishi idadi hii ya watumishi basi kwa Tabora tufanye *vice versa* ile 39% ndiyo yawe mapungufu na 61% iwe ndiyo mahitaji ambayo tutakuwa nayo, niombe Serikali izingatie hilo. Lakini pia katika hizi ajira muangalie namna nzuri ya kutoa ajira, tupunguze ile michongo. Kila maeneo yapate

hizo ajira, ajira zinaenda kwa michongo sana. Watu wasiokuwa na mabavu hawapati ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakuja na suala la kusema tunaangalia *intake* labda ya 2019,2018,2020 lakini utakuta kuna watu wame-*apply* wenye hivyo vigezo vya *intake* ya 2019 halafu anaajiriwa mtu wa *intake* ya 2022 ambaye amefanyiwa mchongo, inakatisha tamaa kwa vijana ambao tumewaomba wajiajiri. Serikali tunaomba mfuate vigezo na masharti ambavyo mmejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Kainja. Naona Mheshimiwa Waziri anatikisa kichwa kuashiria kwamba amepokea taarifa yako ya ajira zile za kujuana. Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela wakati huo Mheshimiwa Deus Clement Sangu pamoja na Mheshimiwa Shabiby wanajiandaa.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nikushukuru, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika Wizara ya TAMISEMI utajikita sana katika mambo matano. Mambo ambayo nitajitahidi kuchangia kama muda utanifaa au ntapata muda wa kutosha nitachangia kuzungumzia ufinyu wa nguvu kazi, nitachangia kuhusiana na mifumo ya kazi, nitachangia pia kuhusiana na changamoto ya kimaadili, nitachangia pia kuhusiana na tatizo la ajira na jinsi ya kulitatua lakini pia nitazungumzia ushauri jinsi gani tunaweza tukatatua baadhi ya changamoto kama muda utanitosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba Wizara ya TAMISEMI ni Wizara kubwa lakini ni Wizara muhimu sana na Wizara hii ni mtambuka.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Mheshimiwa Mchungahela anahutubia Taifa. Endelea Mheshimiwa. (*Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kama nilivyosema Wizara ya TAMISEMI ni Wizara kubwa lakini ni Wizara muhimu na ni Wizara mtambuka. Pamoja na umuhimu wake na ukubwa wa Wizara hii kama Wizara nyingine kwenye nchi hii zina changamoto. Changamoto kubwa iliyoko katika Wizara ya TAMISEMI iko katika ufinyu wa nguvukazi. Licha ya kwamba kuna changamoto nyingine lakini eneo hili naliona ni eneo ambalo lina sumbua sana kiasi cha kufanya kwamba hata utekelezaji wake wa majukumu ukawa hauwezi kwenda sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida iliyoko hapa kuna uchache wa watendaji lakini hata wale walioko baadhi yao ni wachache tu ambao ni bora kwa maana ya kwamba *quality*. Hata hao wenye *quality* bado baadhi yao wanakosa weledi. Hali hii inasababisha changamoto nyingi zikiwapo ni pamoja na hasara zinazojitokeza katika maeneo mbalimbali hususani katika maeneo ya walaji kwa maana ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi inayokwenda kule kutokana na changamoto nilizozigusia hapo zinasababisha kusimamiwa na watendaji ambao baadhi yao hawana weledi lakini wengine hawana sifa lakini hata ufahamu wa jinsi ya kufanya hiyo kazi aliyotumwa inakuwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na u-*sensitivity* wa taarifa ambazo nitazitoa sitataka kuzungumza *in details* hizi taarifa. Nitazungumza tu *generally. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna watu wamepewa kazi ilikuwa ni ya injinia lakini amepewa mtu wa *certificate* na hana uelewa wa kufanya kazi hiyo, hali ambayo imepelekea kutokea na hasara kubwa katika usimamizi wa miradi hususan katika miradi ya elimu pamoja na miradi ya afya. Kama nilivyosema sitataka kwenda kuingia kwenye *details* ninazungumza tu *generally* ninafikiri hizi *details* nitazituma kupitia mchango wa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya mifumo pia, mfumo unaotumika hapa TAMISEMI, mifumo ya kifedha kwa mfano haioani, hashirikiani, haisomani. Unaweza ukakuta kuna taarifa zinatakiwa zipelekwe zinakwenda taarifa ambazo si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kumekuwa na changamoto ya watendaji kukaidi taratibu za utekelezaji wa majukumu yao, pia kukaidi maelekezo kutoka kwenye mamlaka zinazowatuma. Pia, kama nilivyosema, kwamba nahitaji kuzungumzia kidogo kwenye tatizo la ajira. Hapa naomba kidogo kama ushauri. Kwa bahati nzuri tulikuwa na ajira mwaka jana au muhula uliopita, zile ajira kwa kweli zimetuletea changamoto kubwa sana Wabunge, zimetuletea changamoo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani? maeneo yote takribani ya vijijini kuna shida ya ajira; na ajira zimetangazwa na wengi wamekuwa na matumaini kwamba kwa namna moja au nyingine wanaweza wakazipata lakini kilichotokea ni kwamba kuna maeneo hawakupelekewa kabisa; yaani kwamba watu hawakuajiriwa lakini kuna maeneo mengine wameajiriwa idadi ya watu wengi. Hatutaki kuzungumza kwamba wapi ilikuwa vipi lakini kwa mfano tu

mimi Jimboni kwangu katika ajira zote zilizotoka za elimu pamoja na shule ni watu wawili tu ndio walipata ajira ile, kwa kweli sio *fair* ilhali kuna idadi ya watu wengi sana ambao wamekosa ajira na lakini wamesoma na wanatarajia pia na wanaomba. Kwa hiyo unapopeleka watu wawili katika jimbo zima sidhani kama huu mgawanyo wa cake uko sawa, naliomba jambo hili tuliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba katika hizi ajira 21,000 basi tutenge ajira 5,000 zibaki kwenye wizara kama msawazo lakini zile ajira nyingine yaani kwamba 21,000 ukitoa 5000 hizo zitakazobaki tuzigawe kimajimbo. Tuangalie *proportional amount* ambayo kila jimbo inaweza ikapata, kila jimbo lipate kwa kiwango kadhaa, halafu zile zingine 5,000 ndizo ziende katika kufuata hizo taratibu ambazo mlizfanya huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela ulipozungumzia majimbo ikabidi nikuongeze sekunde kidogo maana najua sasa na Mufindi Kusini watapata. Haya tunaendelea nilimwita Mheshimiwa Deus Clement Sangu wakati huo Mheshimiwa Shabiby na Mheshimiwa Njau wanajiandaa.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti hii ya Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kwanza kabisa nikupongeze Mheshimiwa Waziri na timu yako hapa ya wachapakazi na mnafanya kazi nzuri katika wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii ndani ya Bunge hili kutoa pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kwela katika Kijiji cha Talanda Kata ya Mileka kwa maafa yaliyotokea, ambapo mafuriko makubwa yamesababisha

vifo vya watu saba na zaidi ya kaya 20 zimekosa makazi. Nishukuru Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuahidi atatuma timu na dada yangu Jenista uko hapa mtusaidie kwenda kutoa msaada wa kibinadamu kwenye ofisi yako kwa maana ya Kitengo cha Maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya Jimbo la Kwela. Nina mirad mikubwa mingi ambayo nikianza kusema hapa nitatumia muda mrefu sana lakini nina *forum* ambayo tutaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo machache ya kijimbo na baadaye nitaongea mambo ya jumla ya kitaifa. Jambo la kwanza ambalo nakuja kwenu ni ombi. Katika Jimbo langu la Kwela Mji Mdogo wa Lahela hatuna hospitali kabisa. Tuna jengo ambalo ni Mji wa Makao Makuu ya Wilaya ni mji ambao ndio *center* kubwa katika ndani ya Jimbo la Kwela lakini hatuna hospitali. Kwa maana ya kwamba tuna kituo ambacho kinamilikiwa na Kanisa Katoliki, wametupangisha pale kwa muda wa miaka 40 na hatuna umiliki wowote kama Serikali. Sasa makao makuu ya wilaya kukosa hospitali na huduma pale kimezidiwa kwa sababu *population* imekuwa kubwa. Niwaombe, ombi hili nimelileta mara nyingi wizarani mnalijua, naomba tulipe kipaumbele ili kuipa hadhi makao Makuu ya Wilaya, Halmashauri yetu ya Sumbawanga ambayo ni mji mdogo wa Lahela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la pili kwenu ndugu zangu Mheshimiwa Waziri naamini ni wasikivu, bajeti yetu ya *TARURA* ipo inafanya kazi yake nashukuru imeongezeka na hili nampa sifa Mheshimiwa Rais. Lakini kuna barabara maalum, kuna barabara ya kutoka Chombe, Kiandaigonda kwenda mpaka Kaozi ni kilomita 18.8. Barabara hii ni korofi na na barabara muhimu ya kimkakati katika uchumi wa kukuza na kupata mapato ndani ya

halmashauri yangu. Ombi langu kwenu, naombeni mfanye hima ili mtusaidie na sisi Halmashauri ya Sumbawanga tuweze kukusanya mapato na tufikie malengo yetu ndani ya halmashauri; mtupatie fedha za dharura kutengeneza barabara hii muhimu. Najua jambo hili liko ndani ya uwezo wenu bajeti ya kwaisa ya *TARURA* haitoshi muifanyie udharura wake tuweze kuwasaidia wananchi wangu kama hivyo nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ambalo nawaletea leo ni maboma ya zahanati. Wananchi wangu wamejitahidi, ndani ya vijiji 16 wamejenga zahanati ambazo zimefikia hatua ya mwisho kiasi kwamba tukiwapa fedha kidogo zahanati zile zinaenda kufanya kazi. Kuna Kamsamba, Mtetevu, Tapewa, Kazi, kuna zahanati nyingine ya Mtapenda, zahanati ya Mumba, Zahanati ya Lilolyambula, Zahanati ya Kawila, Zahanati ya Ilambo; ziko zahanati 16 kwa sababu ya muda nitawaletea mzione hapa. Nawaombeni hizi zahanati zinahitaji kupelekewa fedha kidogo zahanati zile zinaanza kufanya kazi na wananchi watapata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo vituo vya afya. Wananchi wangu wa Kata ya Ilemba, wananchi wangu wa Kata ya Mwive wamepambana wamejenga, wamejitolea zaidi ya miaka 10 kujenga vituo vya afya lakini wamefika mahali nguvu imeisha wanahitaji msaada wa Serikali. Nilishaleta maombi haya hapo wizarani nimesema mara nyingi ndani ya Bunge hili niwaombe sasa na sisi tuweze kufurahia neema ili wananchi wa Ilemba, wananchi wa Mwive wafurahie kupata vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uhaba wa watumishi. Na hili naomba mnisikilize Mheshimiwa Waziri. Pale mnawapa ajira zinatoka vijana wanaripoti vizuri mnawaleta Sumbawanga. Wakishafika Mkoa wa Rukwa wanaanza kuomba uhamisho na uhamisho huo mnatoa mara moja bila kuzingatia hata kwamba wanatakiwa wakae hata miaka

mitano kwa mujibu wa taratibu. Kwa hiyo pale imekuwa ni kama sehemu ya kupatia *cheque number*. Mtu anachukua *cheque number* anaondoka anaendelea na maisha mengine. Tumepelekea uhaba wa watumishi ambapo kada ya ualimu tu ina upungufu wa walimu 1187, kada ya afya 867. Hali ni mbaya, tumeshindwa, kuna baadhi ya shule hakuna, nina shule 19 hazina hata mwalimu mmoja wa kike nikuombe sana ni hali ya hatari tunaongelea mambo ya unyanyasi wa kijinsia. Halafu shule nzima hakuna hata mwalimu mmoja wa kike, shule 19, hii ni *disaster*. Tutakuta mama na mwana wanakuja kulaumiwa mimba za utotoni, ubakaji na mambo mengine mabaya yaliyosemwa ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri haya muyachukue na kwenda kunisaidia tupate ajira hizi mpya zitakapotoka muwape kipaumbele Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la nne ambalo ni muhimu nataka niongelee mambo ya usimamizi madhubuti wa fedha tunazopeleka kwenye miradi. Kuna jambo ambalo ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais ndani ya mkoa wetu tunaenda kupata mradi mkubwa kwenye Manispa yetu ya Sumbawanga Jimbo la Mheshimiwa Aeshi, bilioni 27 zinaenda kujenga barabara na kwenda kujenga soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nitoe tahadhari, tuko kwenye mchakato wa manunuzi sasa hivi, kuna mambo tumeyaona sehemu nyngine, hayafurahishi na yanatia dosari Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri dada yangu wewe ni mchapakazi, tulifanya ziara pale Dar es Salaam kwenye mradi wa *DMDP* ambao ulikuwa ni Dola za Kimarekani milioni 330, tumekutana na mambo ya ajabu sana. Tulipokutana pale Ofisi Ndogo ya Bunge tukiwa na timu yako ya Wizara kila mtu ameshika tama anasikitika. Vifurushi

vyote, *package* 19 za miradi ile kuna ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha. Nakupa tu mfano ili mpate picha kwamba miradi hii ya *TaCTIC* ambayo inaenda kufanyika nchi nzima mmejipangaje, mmejiandaa kuifanya miradi hii au tui-*suspend* kwa kuwa ubadhirifu unakuwa mkubwa na unakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano stendi ile ya Buza mkandarasi walimchelewesha kutofanya kazi kwa siku 289. Hawajamwambia chochote, wako kimya watalamu wako. Baada ya hapo akawaletea madai ya milioni 488 kwamba mmenichelewesha wakalipa bila wasiwasi wowote. Mkandarasi huyo huyo akafanya kazi akamaliza, baadaye wakamchelewesha malipo, alivyoleta *certificate* wakachelewesha kwa zaidi ya siku 100 akaleta riba ya milioni 879, hasara bilioni moja na kidogo mmeisababishia hasara Serikali. mimi ninalia zahanati 16 kuna mabilioni huku yanaliwa kirahisi tu ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haitoshi, jambo la kusikitisha kabisa, *certificate* mpaka leo ninavyoongea, ni jambo tumeliona wiki mbili zilizopita nendeni mka-*verify;* inawezekanaje mtu analipwa *certificate* kabla hajamaliza kazi? Kuna miradi iko asilimia 68, asilimia 79, asilimia 80 wameshalipa *certificate* zote na wengine wako *site* walishalipwa hela zao, akiamua anaweza akaondoka zake hamna cha kumfanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuko makini, kila mtu anajifanyia jambo anavyotaka. Niwaombe sana mama anahangaika kutafuta fedha ukiukwaji wa taratibu za manunuzi umekidhiri kwenye miradi hii. Tumekuta pale kuna *variation* mpaka ya asilimia 125, yaani mradi ni ya milioni 720 mtu ameenda kufanya *variation* wakati imekuwa bilioni 2.3 nashangaa haya mambo yanafanyikaje? Kwa hiyo ukienda kupitia *package* ili upate somo zuri Mheshimiwa Waziri kapitie *package* 19 zote za miradi ule wa *DMDP* utakuta kuna

madudu. Uki- *sum-up* ile *cost* wewe mwenyewe kichwa kitakuuma utaenda kutafuta maji unywe Panadol, kwa sababu mpaka sasa hivi natafakari jambo hili linasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana naunga mkono hoja, *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sangu ulishamaliza hoja yako ya pili hiyo? Ulishamaliza eeh! Haya ahsante sana nashukuru sana. Nilimwita Mheshimiwa Ahmed Shabiby aweze kuchangia.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mmoja wa wachangiaji kwenye Wizara yetu ya TAMISEMI. Mimi leo nitachangia vitu vichache tu; lakini kwanza kabla sijachangia naunga mkono hoja ya TAMISEMI. Si kwamba naunga mkono hoja ya TAMISEMI kwamba wanafanya vizuri, hapana isipokuwa naona wageni. Kwa hiyo kwa hili safari hii tunaunga mkono hoja kwa sababu tunajua kuna dada yetu Kairuki, kuna akina Deo na mwenzetu Dugange huwa ni wazuri wanapokea simu zetu wa Wabunge. Kwa hiyo na mkiona makofi haya msivimbe kichwa halafu muache kupokea tena. Kwa hiyo tunaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila tunaka kusema, kwamba mmekabidhiwa gari bovu, ambapo hili gari ni la tani 30 lakini lina injini ya bodaboda, huo ndio ukweli, tusitake kila kitu tunasifu. Kwa hiyo dada yangu hapa pana kazi ya ziada na pana kazi ya ziada kuanzia kwako TAMISEMI kwa watumishi wa TAMISEMI. Nimeona Wabunge hapa waliochangia, hawa wawili kabla yangu nimeona wamezungumza kwa uchungu hata yale niliyotaka kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mgao wa watumishi hasa walimu, watumishi wa hospitali ukiangalia mara nyingi ukiona

jimbo la Waziri utaona lina mgao mkubwa, jimbo la Mbunge lina mgao mdogo. Hiki kitu kiko wazi; na juzi niliongea na wewe na ndiyo maana leo nimekuwa mpole, na nilikuonesha mfano nikakutajia mahali fulani, na mimi huwa naongea kitu kwa uchunguzi. Utakuta, kwa mfano vituo vya afya; sisi Gairo kuna Kata ya Chanjare, iko umbali wa kilometa 90 mpaka kufika Gairo Mjini. Tumeomba kituo cha afya, Naibu wako hapo Dkt. Dugange hapo anafahamu, amenisaidia sana, lakini kile kituo hakijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamwonesha sehemu vituo vya afya vimejengwa kuna watu hata 2,000 hawafiki kuna kituo cha afya. Mwenyekiti wako wa Kamati, Mheshimiwa Londo anajua. Sasa, hivi kweli, mama,Mheshimiwa Rais, anatoa vituo vya afya kwa ajili ya kusaidia wananchi wake; hivi vituo mvifanye viwe vya mkakati. Muangalie, si lazima iwe kila kata inapata kituo cha afya lakini *at least* muangalie kwamba hapa pana kata labda tatu kimkakati kwamba wapi tuweke kituo cha afya ambapo watu wana shida. Sasa ninyi wenyewe kwa wenyewe huko mnagawana tu vituo. Waheshimiwa Wabunge nachosema ni kweli, wengine tumepata kimoja, viwili lakini kuna watu wamepata vinne, kumi, sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naombeni sana jamani, dada yangu naomba sana uwe makini na hilo. Kama Kata yetu ya Chanjari sisi ni lazima tupate kituo cha afya hata kama havimo kwenye mpango mkakati, mkatafute hela mtuletee kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye watumishi walimu hivyo hivyo ukiona mtu anapelekwa Sumbawanga, anapelekwa wapi, ujue anapelekwa tayari hapo TAMISEMI wameshamwajiri halafu wao ndio wanaandika vimemo huyo mpe uhamisho, msaidie arudi huku. Utakuja kukuta ile wilaya imepelekewa walimu 50 baadaye unakuja kukuta ina walimu 24, wale wote wametoka. Safari hii kwenye mgao huu mimi

kwenye shule za msingi nina uhaba wa walimu takriban 800, huwezi ukaja ukanipa walimu 100 ukaniambia eti tunapunguza polepole wakati mijini wamejaa huko, wachumba, wote mmewaweka kwenye miji huko, hii haitowezekana. Mtupe, na muhakikishe kabisa wakija hawatoki sio mnawaleta halafu mnaandika vimemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninavyo vimemo nitakuletea apewe mkurugenzi huyo. Fanyeni uchunguzi huko mnakosema kwamba walimu wanahamishwa, wanahamishwa kutoka TAMISEMI. Wale mabosi huko wanaandika tu vimemo basi wanaondoka. Kwa hiyo wanajiajiri kwa undugu halafu wanawatoa ndugu zao wanawapeleka sehemu nzuri hawataki wakae vijijini.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamelalamika sana hapa kuhusu habari ya wale walimu wanaojitolea…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabiby subiri kidogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale.

**T A A R I F A**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe taarifa mchangiaji, ameizungumzia ile Kata ya Chanjale. Mimi nimefanya ziara kutembelea maeneo yale, ukweli kuna shida kubwa na mimi namuunga mkono namwongezea Mheshimiwa Waziri alifikirie hilo la kuweka Kituo cha Afya Chanjale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabiby unapokea taarifa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo nilikuwa nahitaji hii, nimeipokea. Ni ukweli na ndiyo maana saa nyingine hata mnasema kwamba aah! kuna chuki kati ya Wabunge hivyo inakuwaje kama ukienda sehemu zingine uko utakuta kuna kituo cha afya cha ghorofa halafu kwako cha mabati ya kienyeji, utampendaje hapo? Kwa hiyo kwenye ajira hizi ajira ya afya hivyo hivyo; sehemu kama Gairo tuna upungufu wa watu karibia 200 na kitu, lakini ukiangalia hawaji. Safari hii kwa kweli tunao, na kama vipi tuje tuazimie humu Wabunge, tuazimia hapa watu wafukuzwe kazi na Spika naye kama hataki naye tunamuazimia sisi si ndio tuliomchagua? Ndiyo maana yake. Sasa sisi hapa bosi wetu ni Spika na Rais, kwa hiyo kama tunaye humu watu wanatufanyia vituko huko majimboni tuna kazi ya kulalamikalalamika humu tunajifichaficha, haiwezekani kitu kama hicho. Tuje tuazimie tu Spika alete hapa, TAMISEMI pale huyu, huyu, huyu hatakiwi sisi ndio tunasimamia Serikali na Spika naye akituletea siasa zake tunamwambia naye kaa pembeni na wewe tunakuazimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwenye vituo vya afya na walimu tunaomba kabisa wafanyakazi hao tuwapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* kwa kweli inafanya kazi nzuri sana lazima tuseme ukweli. Hata Mkurugenzi wa *TARURA* huyu *CEO* wao ni mtu mzuri sana, lazima tuseme ukweli, pale wanapofanya watu ukweli huwa tunasema vitu vya ukweli. Mama Rais wetu ametupa ile mia mia za barabara, kweli tunaona zinafanya kazi, lakini bado hazitoshi na sijaona watu wanatafuta hata ile vyanzo huko Serikalini hawatafuti vyanzo. *TARURA* lazima itafute vyanzo siyo lazima iwe mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *service levy,* hivyo ukiichukua *service levy* ile ni kodi ya nini? Hujui! Unaambiwa

kodi ya huduma, ukiangalia mfanyabiashara analipa yeye; kuzoa uchafu, zimamoto, sijui nini, kila kitu analipa halafu kuna *service levy*, halafu *service levy* wanakwenda wanajenga majumba, majumba tu eti kitega uchumi, kitega uchumi kipi? Hapa Dodoma wamejengajenga magorofa yale, sasa hivi wanalala panya na watu wawili, watatu, kitega uchumi, kwa nini wasichukue hizi hela za *service levy* basi angalau iwe na maana ziende *TARURA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ukweli. Hii *service levy* Waheshimiwa Wabunge wazifanyie uchunguzi, haya mashirika yote yanayohusika na TAMISEMI angalia hata yale majengo waliyojenga kwa mfano haya ya Shirika la *LAPF,* si wamejenga majengo, majengo kama ile *Millennium Tower* na mengine, mwende mkaangalie kama wamerudisha robo ya pesa ya gharama iliyotumika, mimi najiuzulu Bunge hapa. Kila siku baada ya miaka fulani wanatoa bilioni nne au tano ukarabati, wakati hata bilioni mbili halijaleta yaani kuna pesa, Mheshimiwa Waziri, Dada yetu uwe makini. Halafu kuna vitu vingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa unga mkono hoja, kengele ya pili imegonga.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea na uchangiaji hii ni kengele ya pili kiti ndivyo kinavyoelekeza Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, haya ahsante. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mimi hapo nakuunga mkono pia kwenye hoja ya vituo vya afya hata kwangu mwaka wa tatu nawaomba wenzetu wa TAMISEMI hawajaleta kituo hata kimoja. Tumeshuhudia maeneo mengine vinajengwa tu, kwa hiyo nadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri, ukalichukua hilo jambo kwa sababu kuna manung'uniko miongoni mwa Wabunge, *issue* iko *very serious* na mimi ni mmoja wa mashuhuda.

Tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Felista Njau, wakati huo Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili niweze kuchangia kidogo. Mwaka 2022/2023, Bunge letu Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni tano milioni mia moja na arobaini na nane ikiwa ni mpango wa kuboresha elimu ya sekondari katika shule zilizojengwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ilipofika Februari, haikupelekwa hata shilingi mia. Ipo desturi ya Bunge lako Tukufu kuidhinisha fedha kuelekea kwenye miradi ya maendeleo na fedha hizi haziendi, umekuwa kama ni ugonjwa sugu, lakini pia tunafifisha maendeleo yetu. Katika hili kuna shida kwa sababu fedha hizi zilikuwa zinatakiwa ziende kwenye kununua vifaa vya maabara, lakini zikanunue kemikali ili watoto wetu ambao wanasoma shule za sekondari waweze kusoma kwa ufanisi na kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu walikosa fursa hii mwaka jana. Kuna tatizo ambalo linatokea baada ya watoto wetu hawa kukosa vifaa vya sayansi. Kuna athari kubwa 2021 wanafunzi 158,185 walipata daraja la sifuri na daraja la nne katika shule za sekondari. Huu ni ukosefu wa vifaa, tumemwona Mama yetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, siwezi kubeza jitihada zake, huyu Mama amejitolea

kwa kiwango kikubwa kuilinda na kuitetea Tanzania kwa wivu mkubwa. Kwa sababu tu Rais Samia, aliidhinisha ujenzi wa majengo ya shule za msingi na sekondari kila Mbunge akisimama anajinasibu katika hilo na nitakuwa ni mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanafunzi asilimia 66 mwaka 2021, walipata madaraja haya zaidi ya nusu ya watahiniwa. Maana yake nini? Tunakwenda nje ya malengo ya ushindani wa kielimu, kwa nia njema na thabiti kabisa ya Taifa langu naomba nishauri, zipo shule za *private* ambazo zinafanya vizuri. Zikifanya vizuri siyo kuzifichia matokeo twende tuka–*compete* nao tuwe *partner*s nao tusi–*compete* nao, tuwasaidie ili wasaidie Serikali kuweza kufanya vizuri katika matokeo ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na shule nyingi za *private* zinazofanya vizuri, siyo uchawi ni jitihada katika miundombinu ya elimu, Walimu wanalipwa vizuri, wanalipwa mafao vizuri, ndiyo wanafanya vizuri. Kujenga majengo pekee haitoshi katika elimu. Katika shule za *private* kumekuwa na mlolongo wa tozo na kodi hii ni kuwarudisha nyuma, tuna–*compete* nao hawa tunawaweza tuungane nao, tuboreshe elimu ya Tanzania, tuondoe tozo na kodi, ziko zaidi ya 15, akija mtu anawekeza kwenye elimu anaanza kuogopa, tuige kwa wenzetu Uganda na Kenya waliwaleta karibu, wakaungana nao, elimu imeboreshwa. Tuungane na *private sector* twende tukadumishe elimu kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna shida kwenye elimu. Watu wengi wameitika elimu bila ada, wameitika siyo siri. Hata hivyo, wanaokwenda kumaliza shule elimu ya msingi na sekondari wanakuwa ni nusu ya wale walioanza. Katika Ripoti ya CAG inaeleza katika halmashauri 11 za shule ya msingi tayari wanafunzi zaidi ya nusu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njau, Ripoti ya CAG ya mwaka gani?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya mwaka 2021. Halmashauri ya Kwimba wanafunzi waliandikishwa 6,950, waliomaliza shule ya msingi ni 3,783 sawa na asilimia 49, ndiyo iliyoongoza kwa wanafunzi kuacha shule. Huenda ni miundombinu lakini sisi kama Taifa tuboreshe miundombinu yetu ili tuweze ku–*compete* na elimu yetu. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Huku, mie Tabasam

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Nataka kumpa taarifa muongeaji kwamba Wilaya ya Kwimba wanafunzi ambao hawakwenda kumaliza elimu yao ya msingi ni kwa sababu ya fisi walikuwa wametanda maeneo hayo kwa muda mrefu, lakini siyo kwamba labda eti watoto wale wameshindwa kumaliza elimu ya msingi kwa sababu wamekwenda kuchunga ng'ombe, Hapana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njau, unapokea taarifa?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amenibeza. Inayofuata ni Halmashauri ya Kinondoni Mjini, ambayo wanafunzi walioandikishwa kuanza shule walikuwa 15,000, waliomaliza ni 4,652. Tayari tumeshuka sawa na asilimia 46. Kwa hiyo tunaweza kusema ni kijijini lakini pia mijini lipo hili tatizo, kuna nini? Ni lazima tufuatilie kwa ukaribu ili tujue kwa nini watoto wetu hawamalizi shule? Kwa nini

wanakuwa na ari ya kwenda shule lakini hawamalizi shule. Kwa hiyo kuna tatizo ambalo liko hapa katikati, tutakapoacha tutaliacha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Katika shule za sekondari walioanza katika Halmashauri ya Newala, kati ya wanafunzi 7,950, waliomaliza ni elfu nne na kitu.  Hii idadi bado inazidi kupungua.  Kwa hiyo ushauri wangu tuungane na sekta binafsi, tuboreshe elimu yetu, tuangalie changamoto iko wapi, twende tuka–*solve* changamoto, lakini tusisahau maslahi kwa Walimu. Walimu wana wakati mgumu japo hawatoshi, lakini wale waliopo wanalia ukata. Mishahara midogo, pesa zao za malimbikizo ya kupandishwa vyeo hawana, miundombinu ni mibovu. Tukienda kuboresha hapa nafikiri tunaweza tukapata kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye asilimia kumi ya mikopo. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla, jana walitoa kauli thabiti ambayo akinamama waliokuwa wanategemea wa waliyokuwa wanayategemea walisikia ile kauli wakawa na wasiwasi. Nasema leo nawaondoa wasiwasi, kauli ya Serikali ni thabiti kwa sababu kulikuwa na mianya ya rushwa, pesa zilikuwa zinapewa watu, si wahusika, kwa hiyo kimsingi ni lazima ufuatiliaji upatikane na watu waanze kufanya utafiti, ndipo pesa hizi zitolewe tena. Naiungana mkono Serikali katika hili.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, wakati huo Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma anajiandaa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Niungane na wenzangu waliotangulia, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa

hatua iliyochukua siku ya jana katika mikopo ya asilimia 10 ya kuhakikisha wanabadili utaratibu, namna ya utoaji wa hiyo mikopo. Ukweli ni kwamba sasa Mfuko huu ulikuwa unakwenda kufa, kwa nini ulikuwa unakwenda kufa? Ni kutokana na utaratibu ambao ulikuwa unatumika katika suala zima la utoaji wa mikopo. Jambo la pili, mikopo hii ilikuwa haiwafikii walengwa na badala yake ilikuwa inawanufaisha watu chache kwa ajili ya maslahi yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ukweli sisi sote tunajua utaratibu wa mikopo hii inavyotolewa kwenye halmashauri zetu, lakini ukisoma Ripoti ya *CAG* ya mwaka huu 2022/2023, ni masikitiko makubwa sana kuona kwamba bilioni 88 zimepotea na hazijulikani ziliko na hata vikundu vilivyopewa mikopo hii ya bilioni 88 havijulikani vilipo. Hili ni jambo la aibu kwa watu waliopewa dhamana ya kusimamia mikopo hii ili iweze kuwafikia welangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kauli ya Serikali naomba nishauri mambo machache:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza tunaomba waliohusika katika suala zima la utoaji wa mikopo hiyo ambayo haijulikani ilipo wachukuliwe hatua ili liwe fundisho huko mbele tuendako, mambo yako wazi kabisa. Ukisoma katika Ripoti ya *CAG*, ukienda katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, vikundi 34 vimepewa mikopo zaidi ya milioni 600 na pointi lakini vikundi hivyo havijulikani, havijulikani kwa maendeleo hawavijui kabisa. Hili ni jambo la ajabu, kikundi ili kipewe mkopo kwanza jambo la kwanza ni lazima Afisa Maendeleo wa eneo husika akajiridhishe kwamba kikundi kipo na kina mradi kinaouendesha ndipo kikundi kinapata sifa ya kukopa mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tunaliona kwenye halmashauri zetu, ili kikundi kipewe mkopo ni lazima

kiwe na mdhamini mwenye mali zisizohamishika. Kikundi hiki ndipo kinapewa mkopo, sasa hivi vikundi vilipewaje mkopo wakati Maafisa Maendeleo wa maeneo husika hawavijui na wala hawavitambui kwenye maeneo yao. Utaona hiki ni kitu cha ajabu sana. Tuna watu wachache ambao wanakwamisha juhudi za Serikali, hawa wanatakiwa kuchukuliwa hatua ili huko mbele tuendako hayo mambo yasijirudie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nizungumzie kwenye Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Sisi sote tutakuwa ni mashahidi na hata Waziri inawezekana anajua, ndani ya miezi sita wananchi wa Mji wa Tunduma wamekuwa wakikutana na adha kubwa ya stendi na hili liko wazi na hili limekuwa ni janga ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Stendi ilikojengwa hatukatai kujengwa stendi ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma na hilo ni hitaji la kila mmoja kuona maendeleo yanafanyika kwenye eneo lake na hili jambo sisi Wabunge tunashukuru, lakini changamoto ambayo wananchi wamekuwa wakikutana nayo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tunduma wamekuwa wakikutana na adha na mateso makubwa sana ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Stendi iko ndani ya Kata ya Mpemba, Kata ya Mpemba ni Kata ambayo iko mwanzoni unapoingia ndani ya Mji wa Tunduma, Kata ya Mpemba imepakana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi lakini kushoto imepakana na Halmashauri ya Wilaya ya Ileje. Kutoka katika Kata ya Mpemba kwenda kufika ndani ya Mji wa Tunduma Mjini ni kilomita 12, mwananchi anatoka Wilaya ya Mbeya amepanda gari analipia nauli Sh.4,000, lakini akishashushwa ndani ya Stendi ya Mpemba kutoka pale kuja kufika Mjini anatumia zaidi ya nauli aliyotumia kutoka Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi wananchi wamekuwa wakikutana na changamoto kwa sababu jambo la kwanza daladala hazitoshelezi za kuwatoa katika eneo la Mpemba kwenda kuwafikisha Tunduma Mjini hazitoshi. Jambo la pili, wananchi mpaka wamekuwa wakifikia hatua ya kuibiwa, wamekuwa wakikutana na changamoto nyingi wengine wametembea kwa mguu umbali mrefu kiasi kwamba wamekutana na changamoto mbalimbali ambazo zinahatarisha usalama wa maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, alichukue hili aende akapitie Halmashauri ya Mji wa Tunduma aone namna wananchi wanavyokutana na changamoto kubwa ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma na najua kwa nafasi yake ana uwezo wa kushauri kwa sababu kama Baraza tumeshauri lakini mawazo yetu kama Baraza hayajafanyiwa kazi. Badala yake watu wachache ambao wanaona jambo hili linaweza kufaa ama kwa maslahi yao, wanalichukua jambo hili kana kwamba sasa imekuwa ni siasa, lakini siasa hii inawaumiza wananchi wa Mji wa Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivi tusisubiri wananchi wa Mji wa Tunduma waje waandamane kwa sababu tumeona migomo ya waendesha daladala imefanyika, migomo ya waendesha mabasi yaendayo mikoani imefanyika. Sasa tusisubiri migomo ya wananchi wa kawaida ndipo tuje Mji wa Tunduma kwa ajili ya kutatua changamoto hii. Niombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni eneo lake alichukue jambo hili, aone ni namna gani anaweza kutusaidia kukabiliana na changamoto hii ambayo imekuwa ni mateso na changamoto kubwa kwa wananchi wa Mji wa Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeki, jambo la tatu naomba nizungumzie suala zima la elimu. Sisi sote tunajua na wananchi wetu wanajua kwamba elimu ya sasa ni elimu bila

ada, lakini changamoto ambayo wananchi wamekuwa wakiikuta ni afadhali ya ada. Tuseme ukweli kabisa, changamoto ambayo wananchi wamekuwa wakikutana nayo ni afadhali ya kulipa ada, lakini si changamoto hii ambayo wananchi wanakutana nayo sasa, ni afadhali Serikali ikawa wazi na ikasema ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hela hizi ambazo zinatolewa kwa ajili ya kusapoti elimu ya bila ada hazipelekwi ipasavyo mashuleni. Badala yake Walimu na wanafunzi wamekuwa wakikutana na mazingira magumu sana huko mashuleni kwa sababu bajeti yao haitekelezwi ipasavyo na badala yake ile bajeti inapelekwa kidogo jambo ambalo linashindwa kukidhi mahitaji ya wanafunzi na Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la vitabu vya kufundisha na kufundishia. Ukisoma katika Ripoti ya *CAG* iliyotolewa Februari, mwaka huu 2023 inasema wazi kabisa, kulikuwa na bajeti ambayo ilikuwa imetengwa katika Mradi wa Fungu 4393. Mradi huu ulikuwa umetengewa kiasi cha bilioni 22.850 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya wanafunzi milioni 2.25, lakini badala yake mpaka kufikia Februari mwaka huu 2023 hakuna hata shilingi mia ambayo imetolewa kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya wanafunzi, ni nini tunafanya kwa wanafunzi wetu? Tumewaweka Walimu katika mazingira magumu, lakini tumewaweka wanafunzi katika mazingira magumu ya kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenda miundombinu na madawati hali ni mbaya, mtoto anakalia jiwe kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la saba halafu mnategemea akiwa Dokta akutibu vizuri?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** …Haiwezekani! Hatuwezi kufika kwa utaratibu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Ahsante sana, haujaunga mkono hoja au sijakusikia vizuri? Haya, Ahsante tunaendelea. Nilimuita Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, wakati huo Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, anajiandaa.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya TAMISEMI. Awali ya yote nipende sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisimamisha mbele ya Bunge lake tukufu, pia napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Angellah Kairuki na Manaibu wake Dkt. Festo Dugange pamoja na Deo Ndejembi kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa uwasilishaji wao wa hotuba hii yenye kurasa takribani 286, napenda kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni miongoni mwa Mawaziri ambao wanatoa ushirikiano, wanapokea simu na wanajibu meseji pindi unapowapa changamoto za watu wetu huko Majimboni, kwa hiyo napenda kuwapongeza sana na muendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa kasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza nitakwenda kwa kuanza kumpongeza Dkt. Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya nchini Tanzania. Nimesoma bajeti mbili zilizopita za Rais Samia kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa Mkoa wetu wa

Pwani namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwani Halmashauri zote Tisa za Mkoa wa Pwani zimepata miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na miradi ya sekta za afya. Kwa upande wa Mkoa wa Pwani tumepata Hospitali mpya za Wilaya Tatu na siyo Tatu niseme Nne ikiwepo Hospitali ya Wilaya ya Kibiti, Kibaha *DC*, Kibaha Mji pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, kilichokuwa Kituo cha Afya Msoga tumepatiwa fedha nyingi sana na tumejenga majengo na kimeshapandishwa hadhi na sasa na yenyewe imekuwa hospitali ya Wilaya. Kwa kusema hivyo ni kwamba tunazo Hospitali mpya 4 ndani ya Mkoa wetu wa Pwani. Tunayo kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusema hapa ni kwamba Mheshimiwa Rais amesogeza huduma ya afya karibu kabisa na wananchi wake na kimsingi kama ambavyo tunafahamu afya ni jambo muhimu sana kwenye maisha ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninachotaka kukisisitiza ni kwamba Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametimiza wajibu wake, ametupa Mabilioni lakini ametupa hospitali ya Wilaya. Jukumu na kazi iliyobaki hapa ni kwa Wizara na nitaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wako muweze kunisikiliza. Mheshimiwa Waziri tunayo changamoto kubwa ya upungufu wa Watumishi, haitakuwa na maana na haitakuwa na afya, Rais katoa Mabilioni ya fedha, tumejenga Hospitali ya Wilaya, lakini tunakosa Watumishi, wananchi wetu wanaenda pale wanakosa kupata huduma kwa sababu watoa huduma hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wa Pwani tuna watumishi wa kada hii ya afya asilimia 48 tu kwa kusema hivyo tunakuwa na upungufu wa watumishi wa kada ya afya kwa asilimia 52. Nitaomba ili u ende kuliandika na peni yako ya kijani. Katika zile ajira 21,200 zilizotolewa na Mheshimiwa

Rais, nitaomba Pwani uiangalie kwa jicho la dharura ili tuweze kupata watumishi wa Kada ya Afya, tuweze kupunguza hii asilimia 52 kwani imekuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo Mheshimiwa Waziri naomba uende kuandika kwa peni yako ya kijani ni suala la upungufu wa vifaatiba. Tunashukuru tumepata hospitali Nne za Wilaya lakini tunakosa vifaatiba. Katika hili Mheshimiwa Waziri umelisema katika hotuba yako ukurasa wa 150, kwamba umetenga Bilioni 15 *point* au niseme Bilioni 16 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Kwa hiyo ombi langu hapa ni lilelile kwa hiyo niangaliwe kwa jicho la huruma, ili tuweze kupatiwa vifaatiba katika Hospitali zetu hizo za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo Mheshimiwa Waziri na lenyewe nenda kaliandike na kalamu yako ya kijani, ni kuhusiana na suala zima la hospitali kongwe. Kama nilivyotangulia kusema katika Halmashauri zetu Tisa Halmashauri Nne mmetupa Hospitali za Wilaya tunawashukuru sana. Halmashauri Tano zimebaki ni hospitali kongwe ambapo kimsingi majengo yake pamoja na mifumo ya kutolea huduma imekuwa chakavu sana inahitahi ukarabati, amezungumza kwenye hotuba yake kwenye ukurasa wa 149 kwamba umetenga Shilingi Bilioni 27.9 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe. Nikuombe sana usizisahau Halmashauri za Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, jambo la nne ninaloomba ukaliandike kwa peni ya kijani, ni vizuri sana kukawa kuna mawasialiano kati ya zahanati, kituo cha afya na hospitali ya Wilaya. Ndani ya Mkoa wa Pwani tunao upungufu wa magari ya wagonjwa, kwa hiyo nimetoa mambo haya manne ambayo nimekuomba na kukusisitiza yaandikwe kwa peni ya kijani kwa sababu nitaomba uyahifadhi na uyafanyie kazi pindi tunapokuja hapa mwakani kwa ajili ya Bajeti.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa mchango wako.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi yake ya uhai, pia nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hasssan kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya wote tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya nasi tutawapa ushirikiano, tunaomba tu yale ambayo tutakuwa tunajadiliana basi ya ninyi mpate kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hii tunaona kabisa maeneo mengi ya pembezoni, Halmashauri za pembezoni Tanzania nzima zina upungufu mkubwa sana wa watumishi ukilinganisha na maeneo mengine, Serikali inaenda kuajiri Sekta ya afya na elimu watumishi 21,000, ombi langu kwa TAMISEMI pamoja na afya ni kuona kwamba tupange idadi ya watumishi hawa kulingana na uhitaji wa maeneo husika, siyo kusambaza tu kwasababu kila mmoja apate, kuna maeneo hali ni mbaya huduma haziendi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Newala imepokea zaidi ya Bilioni 8.5, nini matarajio ya wananchi? Matarajio ya wananchi ni kuona kwamba thamani ya fedha iliyotolewa inafanana au inaenda sambamba na huduma

inayopatikana katika maeneo husika, hilo ndiyo tarajio kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto ambayo inazifanya Halmashauri zetu zishindwe kufikia katika utoaji wa huduma iliyo bora. Mfano, ukienda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Newala, upande wa afya watumishi mahitaji ni 526 waliopo ni 172 upungufu ni 354, hali ambayo inaleta malalamiko kati ya watoa huduma na wahudumiwa, kwa sababu kunakuwa na msuguano wale wahudumiwa wanaona hawafanyiwi ipasavyo lakini wakati mwingine ni kutokana na uchache wa watumishi waliopo, wanashindwa namna ya kujigawa ili waweze kutoa huduma ipasavyo. Kwa hiyo, niombe sana watumishi wa kada ya afya wapelekwe kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Newala ili wakaweze kutoa huduma kwa wananchi kulingana na fedha ambazo Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali imekuwa ikizitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda elimu - Elimu ya msingi upungufu wa walimu ni 327 kwenye uhitaji wa 787. Kwa hiyo, unaona kwamba walimu waliopo msingi wanapata kazi kubwa sana, mzigo ni mkubwa wa ufundishaji na ikumbukwe kwamba mwalimu ili akafundishe lazima aandae somo, sasa Mwalimu huyu anafundisha Darasa la Kwanza, Darasa la Pili mpaka Darasa la Saba anawezaje kuandaa masomo yote, vipindi vyote ili akaweze kufanyakazi inayostahili. Kwa hiyo, tuangalie kwa jicho la pekee namna ambavyo upungufu huu unaathiri utoaji wa elimu iliyo bora kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekondari pia hali ni hiyo hiyo. Mzigo wa walimu ni mkubwa, mwalimu anafundisha *Biology* kuanzia kidato cha kwanza, cha pili, cha tatu cha nne. Fikiria mzigo ambao anaubeba, hajasahihisha bado, ukiacha kuandaa lazima asahihishe aone kazi ambayo imefanywa na mwanafunzi kama inaendana na kile ambacho

amekifundisha, kwa hiyo unakuta mzigo anaobeba ni mkubwa kuliko hali halisi, kuliko uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa fedha zile za elimu bila ada, inapeleka kwa wanafunzi hawa kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita sasa. Lakini kwa sababu ya hali ya upungufu wa walimu uliyopo inalazimika jamii kutafuta walimu wa kwao ili wakawafundishe watoto wao ku - *cover* lile *gap,* lakini wale wanaowafundisha hawatoki mikono mitupu lazima wazazi wachangishane, wawalipe walimu wale. Sasa katika mazingira hayo unakuta wazazi wanalalamika kwamba tunabebeshwa mzigo mkubwa na kwamba ile fedha ambayo tunaipeleka hawaioni ile thamani yake kwa sababu tu ya uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watumishi wa kada ya ualimu wangekuwepo wala hilo *gap* lisingeonekana. Niombe sana tupeleke walimu katika Halmashauri hizi za pembezoni. Pia tunao Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata, Jimbo la Newala Vijijini lina Kata 22 lakini ina Maafisa Maendeleo ya Jamii Wanne tu. Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa ndiyo ambao wanaenda kusimamia zile fedha asilimia 10 inayoenda kwenye Halmashauri, kama hawapo nani atasimamia, matokeo yake fedha zinashindwa kurudishwa kwa sababu hakuna ufatiliaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwa mchango wako.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, wakati huo Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, anajiandaa.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nishukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara yetu ya TAMISEMI. Naomba nimshukuru Mungu ambaye ameendelea kutupa uzima na uhai leo tuko hapa tukichangia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa ajili ya Watanzania. Amefanya kazi kubwa, hivi leo kwa kipindi hiki kifupi katika Jimbo langu nimepokea Bilioni 6.2 kazi kubwa sana, sana, sana. Ninaomba nimpongeze Spika wetu Dkt. Tulia, amefanya kazi kubwa tumeiona kwa macho, maendeleo ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni maendeleo makubwa kuna mabadiliko makubwa. Hongera sana Dkt. Tulia, kwa kazi kubwa ambayo unaifanya katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya kusimamia miradi mbalimbali na maendeleo ya jumla katika Wizara yetu ya TAMISEMI, pia ninaomba nimpongeze kwa kipekee Mkuu wangu wa Mkoa Mwamvua Mlindoko, kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya Mkoa wetu wa Katavi. Anasimamia miradi, anafuatilia, anahakikisha maendeleo yanasonga mbele katika Mkoa wetu wa Katavi, anastahili pongezi Mkuu wetu wa Mkoa wa Katavi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda *TARURA,* ninaomba nichukue fursa hii ya kumpongeza *Chief* anayesimamia

*TARURA*. Anastahili tuzo, anastahili tuzo Mheshimiwa Waziri, tunaomba umpe tuzo. *Chief* wa *TARURA* kwa kazi kubwa nzuri anayoifanya. Leo hii katika maeneo yetu, Majimbo yetu, barabara zinapitika, madaraja yalikuwa hayapitiki watoto walikuwa wanapata shida hawawezi kuvuka kipindi hiki cha masika lakini leo lhii madaraja yamejengwa wananchi wanavuka, watoto wa shule wanavuka, anastahili pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba leo hii *TARURA* waongezewe pesa kwa sababu wanafanya kazi kubwa na vilevile *TARURA* wana mtandao mkubwa wa barabara kuhakikisha vijiji vyetu na vitongoji vyetu uchumi wa wananchi unakua, kwa sababu tumeona kwa kipindi hiki barabara zimefunguka, wananchi wetu wamepata uchumi mkubwa, mazao yote yamebaki shambani, wafanyabiashara wanawafuata wakulima katika maeneo yao sasa tunaomba *TARURA* waongezewe pesa na vilevile madaraja yaendelee kujengwa na wapangiwe bajeti kwa ajili ya matengenezo. *TARURA* hawana bajeti ya matengenezo, lazima wapangiwe bajeti ya matengenezo ili barabara ziweze kuboreshwa siku hadi siku.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi barabara mvua zinanyesha, barabra nyingi zinaharibika, hawana fungu, tunaomba *TARURA* wapewe fungu la matengenezo ili barabara zetu ziweze kupitika mwaka mzima bila tatizo la aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja upande wa elimu ya msingi. Nimepongeza, ninaomba niishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kuhakikisha kuboresha na leo hii tumepata pesa kwa ajili ya kujenga shule mpya, ninaomba nishukuru kwa kupewa pesa hizo, nimepewa pesa kuhakikisha zile shule zote shikizi ambazo tulizijenga wakati uliopita, vyoo vyao vijengwe, tumepokea hizo pesa, ninaomba nishukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima sasa tujiwekeze, walimu walio katika maeneo ya mazingira magumu kama vijijini hawana nyumba, lazima sasa hivi tuweke mikakati kuhakikisha tunawajengea nyumba ili waweze kukaa katika maeneo husika. Tatizo walimu hawakai kwa sababu hawana sehemu ya kuishi katika maeneo yetu ya vijiji. Ninaomba sana, sasa tujiwekeze kuhakikisha tunajenga nyumba ili walimu waweze kukaa katika maeneo safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Serikali imefanya kazi kubwa kupitia vituo vya afya, zahanati zote hizo tumepokea pesa, lakini ninaomba kwenye Jimbo langu, Kituo cha Afya cha Ugala niliahidiwa milioni 800 lakini mpaka sasa hivi nina Milioni 500, Kituo cha Afya cha Itenka niliahidiwa Milioni 800, mpaka sasa hivi nina Milioni 500, ina maana kuwa bado ninadai kuna maeneo ambayo majengo hayajakamilika ninaomba Serikali kupitia Waziri wetu wa TAMISEMI, ni msikivu pamoja na Naibu Mawaziri, tunaomba basi mtumalizie hizo pesa tuweze kumaliza vituo vya afya viweze kukamilika ili wananchi wa Jimbo la Nsimbo waweze kupata huduma safi na salama.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze tumeshaanza kupata vifaatiba vimeshaanza kuwasili na dawa katika Zahanati tulizozijenga na vile ile nilikuwa ninaomba, kuna Zahanati ambayo maboma wananchi wamejenga, zile Zahanati naomba pesa kwa ajili ya umaliziaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika na Serikali ya Mama Samia, kazi kubwa lazima apongezwe Mama huyu amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa inafanywa na Watendaji wa Vijiji lakini ninaomba nishukuru kwa ajira ambazo sasa hivi tumepata ajira 13,000 lakini Watendaji

bado hatuna, ninaomba tufanye ajira ya Watendaji. Watendaji wa Mijini kule Vijijini hawapo, tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaiomba Serikali tunaendelea kuomba kila siku Wenyeviti wa Vijiji tunawapelekea miradi mikubwa wanashika hela nyingi, hebu tuwatazame huko Wenyeviti wa Vijiji, tuwawekee posho *at least* wapate ari ya kufanya kazi. Tunapeleka miradi mikubwa lakini posho yao haijulikani. Ninaomba Wenyeviti wetu sasa hivi wanapokea miradi mikubwa, tunaomba watazamwe kwa jicho la huruma, wapewe chochote ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, wakati huo Mheshimiwa Reuben Kwagilwa pamoja na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, wanajiandaa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa maisha ya Watanzania. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Hakika Mheshimiwa Rais katika wakati wake ameonesha namna nzuri na namna bora ya kuzilea na kuzisaidia Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kuwa Waziri kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kwenye maeneo machache. Eneo la kwanza ni eneo lenyewe la Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 145 (1), inaeleza kuwepo kwa vyombo mbalimbali kwenye maeneo ya Serikali za Mitaa. Vile vile ibara ya 146 (1) inaeleza madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ikiwa ni kurudisha madaraka kwa wananchi na vyombo hivi viweze kuwashirikisha wananchi. Sasa sisi Tanzania kwenye mfumo wa Serikali za Mitaa tume-*buy* mfumo wa wenzetu wa *British mode*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *British mode,* moja ya tabia yake ni kuwa na *double accountability*. Kwa maana watendaji wetu wanakuwa *accountable* kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, lakini *at the same time* wanakuwa *accountable* kwenye Serikali Kuu. Kwenye mazingira ya namna hii, kama kusipokuwa na *proper coordination,* lazima kutakuwa na kigongano kati ya mamlaka hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kwa TAMISEMI, mwaka 2019 tulianza mapitio ya kuboresha sera ya ugatuaji wa madaraka, lakini mpaka leo kumekuwa na ukimya. Mheshimiwa Waziri ukija kwenye majumuisho utuambie, tumefikia wapi kwenye zoezi la kuboresha Sera ya Ugatuaji wa Madaraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, kwa sababu, tayari kuna *double accountability,* ni lazima wenzetu wa Serikali Kuu wakubali kuwa *flexible* ili kuweza kuchukua mawazo ya wananchi katika kutekeleza ile azma ya kurudisha madaraka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wenzetu wa TAMISEMI, mnafanya vitu vizuri, lakini kuna maeneo ambayo hamtutendei haki. Serikali za Mitaa siyo za kupokea tu maelekezo, lazima zishirikishwe; na katika kushirikisha lazima muwe *flexible* kusikiliza na mawazo ya waliokuwa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano wanataka kujenga masoko, unatoa mfumo mmoja wa kujenga masoko nchi nzima. Aliyekwambia Soko la Korogwe linafanana na Soko la Sumbawanga ni nani? Aliyekwambia jiografia ya Korogwe na ya Sumbawanga inafanana ni nani? Haiwezekani, lazima tuangalie mazingira halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, tumemsikia Mheshimiwa Rais akisema mara kadhaa kwamba, kugawa maeneo ya utawala ni gharama kubwa. Nami nakubaliana naye, lakini moja ya chombo muhimu kwenye Serikali za Mitaa ni mamlaka ya kwenye Kijiji kwa maana ya Halmashauri ya Kijiji na Mkutano wa Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaotoka vijijini, vijiji vinakua. Ukiwaona maeneo mawili tofauti kwa vijiji yamekua, yanaanza kuwa na msigano, na shughuli za maendeleo hazifanyiki vizuri. Tunaomba mumshauri Mheshimiwa Rais, kuna gharama kubwa kutangaza mikoa mipya, kutengeneza Halmashauri mpya, lakini hata kutengeneza vijiji! Hakuwezi kuwa na gharama kubwa namna hiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji vimekuwa ni vikubwa, vinahitaji kugawanywa ili wananchi wasogezewe huduma karibu na waweze kufanya shughuli za maendeleo. Kule Korogwe Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja na aliahidi kwamba atatoa vijiji vipya, lakini mpaka leo kumekuwa na ukimya. Tunaomba muishauri mamlaka ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni vituo vya afya. Sera yetu inasema tuwe na vituo vya afya kila Kata, tuwe na zahanati kila Kijiji. Tukaona utekelezaji wake umekuwa mgumu tukasema, tuwe na vituo vya afya vya kimkakati na vya Tarafa. Nimeahidiwa vituo vya kimkakati tangu mwaka 2020 hapa, mpaka leo sijaona hata kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipoingia tu kwenye Wizara ametuita, amekaa vikao na Wabunge, yale tuliyoyasema siyaoni yakiwa *reflected* kwenye bajeti hii. Vituo hivi tunavipata lini? Vinajengwa wakati gani? Tumewaahidi wananchi, tunakwenda kwenye uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye mikopo ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu ya asilimia 10. Ninaungana kabisa na alichokisema Mheshimiwa Rais. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mawazo na maelekezo aliyoyatoa jana. Naomba niwashauri, mnapoenda kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, muongeze. Tukipeleka fedha hizi kwenye mfumo wa kibenki, tutafanikiwa kwenye lengo moja la kuhakikisha tunakuwa na utaratibu mzuri wa utoaji na urejeshaji, lakini bado hatutakuwa na utaratibu mzuri wa kuziwezesha jamii zetu kubaki na matokeo baada ya kumaliza kufanya mrejesho wa hiyo mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya TAMISEMI kutoa maelekezo kuziunganisha idara; Idara ya Maendeleo ya Jamii, Idara ya Kilimo, Idara ya Mifugo, Idara ya Biashara, ili mikopo hii inapotolewa, itolewe kulingana na mazingira halisi ya biashara kwenye maeneo yale, ili baada ya kumaliza kurejesha marejesho ya mkopo huu, wananchi hawa waone biashara hizi zikiendelea, tuone matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotusumbua sasa hivi kwenye kurejesha pia, hakuna mipango mizuri na elimu nzuri ya kuzitumia hizi fedha. Tukiziunganisha idara hizi; Idara ya Kilimo, Idara ya Mifugo, Idara ya Maendeleo ya Jamii, tutafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nikuombe sana Mheshimiwa…

*(Hapa kengele ililia kushiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakuongezea dakika moja umalize jambo la mwisho.

**MHE. TIMOTEHO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naipongeza Serikali kwa ajira ambazo imetangaza. Ukisoma ripoti ya *CAG,* alifanya tathmini kwenye Halmashauri 23 tu, lakini upungufu ulikuwa ni asilimia 35, karibia watumishi 10,000 kwenye Idara ya Elimu peke yake. Hawa walimu 13,000 wanakwenda kuishia kwenye hizo Halmashauri 23 tu. Tuna Halmashauri 184. Tukifanya tathmini kwa nchi nzima, upungufu huu ni mkubwa sana kwa watumishi wa elimu na watumishi wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ajira hizi, bado hazitoshi. Tunaomba wekeni mikakati zaidi ili tupeleke watumishi kwenye maeneo yetu, lakini siyo kuajiri tu wapya, vile vile na mlinganisho na msawazo wa watumishi hasa kati ya Halmashauri za Mijini na Halmashauri za Vijijini. Halmashauri za Vijijini zimechoka kuwa sehemu za watu kupatia ajira na kuondoka kwenda kukaa maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Wakili Timotheo Mnzava. Nilimwita Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, aweze kuchangia.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha, upo mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali, mwaka 2023/2024. Mwongozo huu wenzetu wa TAMISEMI walikutana kati ya tarehe 17 mpaka 21 kuujadili na kuona namna ya kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, wamezigawa Halmashauri zetu katika makundi manne. Kundi la kwanza ni kundi ambalo ziko Halmashauri tisa. Halmashauri hizi tisa zimewekwa kwenye kundi la kupeleka asilimia 70 ya mapato yasiyolindwa kwenye maendeleo. Kundi la pili, lina Halmashauri 17. Kundi hili limepangiwa kupeleka asilimia 60 ya mapato yasiyolindwa kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la tatu lina Halmashauri 102. Kundi hili limepangiwa kupeleka asilimia 40 ya mapato yasiyolindwa kwenye maendeleo na kundi la tatu ambalo ndiyo kundi la Halmashauri ya Handeni Mjini iliyopo, kundi hili lina Halmashauri 56 ikiwemo na Korogwe na Halmashauri nyingine nyingi ambazo ningekuwa na muda ningezitaja. Halmashauri 56 zenyewe zimepangiwa kupeleka asilimia 20 tu ya mapato yasiyolindwa kwenda kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya jambo hili ni nini? Jambo hili linapeleka umasikini kwa wananchi wote waliopo kwenye Halmashauri hizi. Jambo hili, *literally,* halikubaliki! Ukisema kwamba makusanyo yetu ya ndani yasiyolindwa asilimia 20 tu ndiyo iende kwenye maendeleo, tafsiri yake ni kwamba, kwanza tutawa-*discourage* walipa kodi. Mlipa kodi anataka akilipa kodi yake, ushuru ukikusanywa, aone haspitali pale, kituo cha afya kimejengwa, aone madarasa yanajengwa kwa fedha anayokusanya. Sasa tukiwa tunakusanya halafu asilimia 80 yote tunaenda kuinywa chai, tunaenda kuitumia kwenye mafuta kwa ajili ya usimamizi, hii haitakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusababishia matatizo kwa sababu, mbali na kuwa-*discourage* walipa kodi, wanufaika wetu wa asilimia 10 zile tunazokopesha; tulipokuwa tunatenga asilimia 40 tulikuwa tunapeleka asilimia 10 kuwakopesha wananchi, kuwakopesha akinamama, vijana na walemavu, lakini ukitenga asilimia 20 inamaanisha hata hiyo fedha ambayo unawapelekea inapungua,

wanufaika watakuwa wachache. Tafsiri yake ni kwamba, tunatengeneza nchi yenye matabaka makubwa. Wale wenzetu ambao wamepangiwa kupeleka fedha nyingi kwenye maendeleo, ndiyo na fedha zao za kuwawezesha wananchi wao zitakuwa nyingi, lakini na miradi watakayoitekeleza kwenye maendeleo ni mingi kuliko ambavyo sisi tutatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufanya hivi halafu eti wao TAMISEMI wanasema, tukishaondolewa zile asilimia 20 tukabaki kwenye 20 ya fedha za maendeleo, eti watalipa madeni ya watumishi wasiokuwa walimu. Ukimlipa madeni mtumishi, huo ni wajibu wako, na ni jambo zuri kufanya. Wanasema wataleta stahiki kwa Wakuu wa Idara; huo ni wajibu wenu na ni jambo zuri kufanya. Nasema ni wajibu wenu kwa sababu, vyanzo vyote vya mapato kwenye Halmashauri mmevichukua nyie, kwa hiyo, mna wajibu wa kufanya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema mtaongeza *OC proper,* vyote hivyo unavyoviongea vinaenda tu kusaidia uendeshaji wa Halmashauri, lakini ikiwa sisi tulikuwa tunatumia mapato ya ndani kujenga zahanati pale kwenye Zando mwaka juzi, 2021; mwaka jana 2022 tukajenga zahanati Mankinda kwa fedha za ndani, na mwaka huu 2023 tumejenga pale Bangu zahanati kwa fedha za ndani; na tulikuwa tunatarajia kwenye mwaka huu wa fedha tunaopitisha bajeti tukajenge zahanati kule Kwalubaka. Sasa nyie mmechukua fedha zote, tunawaambieni sasa: Je, mtatuletea fedha ili tujenge zahanati hizi ambazo… *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi? Haya Mheshimiwa pale.

**T A A R I F A**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nataka kumwongezea taarifa Mheshimiwa anayezungumza kwamba, TAMISEMI kuzisaidia hizi Halmashauri ambazo amezipunguzia asilimia 40 kwenda asilimia 20, ni kuhakikisha wanapeleka miradi ya kimkakati ili kupandisha mapato kwenye hizi Halmashauri au kama hizo Halmashauri zilishatengewa miradi ya kimkakati, ikamilike ili kuzisaidia kupandisha Halmashauri hizo, siyo kutoa hizo asilimia 40. Tutasaidiaje wananchi wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni taarifa au ni swali?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa nilikuwa namwongezea Mheshimiwa anayeongea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Reuben unaipokea Taarifa?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa ya Mbunge aliyetoka kunipa taarifa ambaye anatokea Momba, na Halmashauri yake ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zimetengwa ili ziingie kwenye asilimia 20 na fedha zote ziende kwenye matumizi ya kawaida badala ya kwenda kwenye matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema aliyenipa taarifa, Halmashauri hizi lazima tuje na mpango wa kuzisaidia. Suala siyo kuzifanya ziwe likizo ya maendeleo. Hatuwezi kuzipa likizo ya maendeleo, eti wawe wanakusanya asilimia 80 yote wanakula, 20 ndiyo inaenda kwenye maendeleo. Hii siyo sawa! Hii haikubaliki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote ya kimkakati mmewapelekea ma-*giants*. Ukija kwenye mradi wa *TACTIC; tier one* ya *TACTIC* iko na ma-*giants,* majiji makubwa. *Tier two* ya *TACTIC* iko na ma-*giants* majiji makubwa, halafu *tier three* ndiyo tuko sisi wachovu ambao ndiyo tena mnatunyang'anya na mapato, halafu na *tier three* yenyewe hamuitekelezi. Hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu mnapanga wapi? Huu ni utafiti wa wapi mmefanya? Nataka niwakumbushe, ukisoma *Five Years Development Plan* tuliyonayo ukurasa wa 12, inasema: *"The aim of the fifth phase Government was to increase development spending to the tune of 30 - 40 percent."* Huu mpango tuliujadili hapa, tukaupitisha hapa, nyie mnawezaje kujifungia chumbani na kubadilisha bila kuja kutuambia hapa? Yaani mnawezaje kufanya hivyo? Yaani Halmashauri zote 56 zi-*paralyze* tu kwa sababu nyie mmeamua? Hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atakapokuja kufanya hitimisho hapa atuambie, sisi wa Handeni, pamoja na Halmashauri nyingine nyingi kama ilivyo Mpumbwe, Kasulu, Handeni *TC,* Nyang'hwale, Nzega, Mpama, Iramba, Ikungi, Longido, Namtumbo na maeneo mengine, mta-*compensate* vipi kwenye hii fedha tuliyokuwa tunapeleka kwenye maendeleo? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Tunakushukuru sana kwa mchango wako.

Nilimwita Mheshimiwa Joseph George Kakunda, wakati huo Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam anajiandaa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa utulivu wake wakati alipokuwa anawasilisha hotuba yake hapa Bungeni asubuhi. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo matatu. Kwanza nitazungumza neno la shukrani; na pili, nitazungumza kidogo maajabu ya Rais Samia, halafu mwisho nitahitimisha na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shukurani kwa niaba ya wananchi wa Sikonge, naomba niwasilishe shukrani zetu za pekee kabisa na za dhati kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo amekuwa akiyasikia maombi yetu na kututekelezea bila kusita. Ametupatia fedha nyingi kwenye sekta za elimu, afya, maji, umeme, miundombinu ya barabara, kilimo cha umwagiliaji, na kadhalika. Kwa hiyo, kwa kweli hapo tunashukuru sana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utufikishie salamu zetu hizi za shukrani kwa Rais ili atambue kwamba tunathamini sana jinsi ambavyo amekuwa na sisi kwa shida na raha muda wote daima. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nieleze kidogo maajabu ya Mheshimiwa Rais. Ajabu la kwanza, tarehe 31/05/2022, saa 3:00 hadi saa 5:00 usiku katika Hoteli ya Serena, ukumbi wa muziki, Mheshimiwa Rais alihudhuria hiyo hafla ambapo miongoni mwa waandaaji alikuwa ni Mheshimiwa Joseph Mbilinyi au Sugu. Hii ilikuwa ni hafla ya muziki wa vijana wa *Hip-hop*. Hakuna Rais yeyote Tanzania aliyewahi kufanya jambo hilo la kutoka Ikulu usiku kwenda kwenye muziki wa vijana. Watanzania walifurahi, lakini dunia ikashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni tarehe 08/03/2023 huko Moshi, Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa Mgeni Rasmi kwenye Kongamano la Siku ya Wanawake Duniani ambalo liliandaliwa na Baraza la Wanawake wa CHADEMA au

BAWACHA. Tukio kama hilo kwa Mwenyekiti wa chama kinachotawala kwenda kuwa mgeni rasmi kwenye kongamano ambalo limeandaliwa na chama cha upinzani halijawahi kutokea, siyo Tanzania tu, bali ni duniani. Kwa hiyo, hayo ni maajabu ambayo Mheshimiwa Rais ameyatumia kuipa elimu dunia kuhusu falsafa zake za kuiongoza nchi hii ambazo ni maridhiano, kustahimiliana, mabadiliko, pamoja na kujenga nchi upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bunge lako Tukufu kwa jinsi ulivyompongeza, inatakiwa tuendelee kumpongeza siku zote kwa jinsi ambavyo ameendelea kuonesha maajabu duniani. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa maajabu yake hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo machache ya ushauri. Eneo la kwanza, Mheshimiwa Waziri na Wabunge wote na Manaibu Mawaziri watakumbuka kwamba, tarehe 04 Aprili, 2023 siku tumeanza Bunge la Bajeti hapa niliandika barua ya wazi, nikaainisha ukubwa wa Jimbo la Sikonge, kilometa za mraba 27,873 linazidi mikoa 11; mikoa kamili. Mkoa wa Kilimanjaro kwa jimbo langu unaingia mara mbili kwa eneo la kijiografia. Kwa hiyo, mtawanyiko wa kata na vijiji ulivyo unaweka changamoto ambazo ndugu zetu hawa wa TAMISEMI wanatakiwa watupe kipaumbele maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niliainisha kwenye barua yangu ile jinsi ambavyo idadi ya watu imeongezeka Sikonge kutoka watu 179,883 mwaka 2012 hadi watu 335,686 ambao ni ongezeko la karibu mara mbili. Katika ongezeko hili asilimia 45 ni watoto ambao wanatakiwa kwenda shuleni. Kwa hiyo, tunahitaji shule mpya zaidi ya 25, tunahitaji madarasa 1,039, tunahitaji madarasa ya kukarabati 90, tunakaribisha maboma 200. Mambo yote haya nimeyaainisha kwenye ile barua yangu ya wazi na Mheshimiwa Waziri ameisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele ambavyo nimevieleza kwenye ile barua yangu ya wazi, naomba sana avikumbuke wakati watakapopata fedha zile ambazo zinakuja nje ya bajeti kwa sababu, haya mengine yapo ndani ya bajeti hii ambayo tutaipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba Serikali ikamilishe na ilete Bungeni Muswada wa Sheria ya Elimu, kutekeleza Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 ambayo ilitoa maelekezo kwamba mtoto asome kuanzia Chekechea mpaka *Form Four* bila kupumzika. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, hata ile Sheria ya Ndoa ambayo ilikuwa inazungumzwa sana kwenye jamii itakuwa haina maana tena kama tutapitisha hiyo Sheria ya Elimu, kwa sababu mtoto atasoma kuanzia Chekechea mpaka Kidato cha Nne bila kupumzika wala kuishia Darasa la Saba wala kuishia wapi. Kwa hiyo, hiyo ndiyo itakuwa suluhisho la matatizo na mjadala kwenye jamii kuhusu mambo ya ndoa. Maana Sheria ya Elimu haitaruhusu mwanafunzi aolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakunda kwa machango wako. Nilimwita Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, wakati huo mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali ombi lako, lakini muda hautoshi. Dakika tano hazinitoshi, samahani sana. Nakushukuru, nitachangia siku nyingine.

**MWENYEKITI:** Nani amekwambia dakika tano Mheshimiwa?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwongozo wako nimeona dakika ambazo zinatumika, saa hiyo hapo na saa nyingine hiyo hapo, mimi naona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani. Nakusihi! *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Changia dakika 10 Mheshimiwa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni dakika kumi…

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia dakika tano.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wote nimeona wanachangia dakika…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, naomba uchangie dakika kumi, Kiti kimetoa mwongozo. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika maeneo mahususi kama matano. Eneo la kwanza ambalo naomba kuelekeza mchango wangu ni miradi inayokuja katika maeneo ya majimbo yetu na miradi inayopelekwa katika halmashauri zetu nchini. Wasimamizi wa miradi hiyo ni Waheshimiwa Madiwani tukiwemo sisi kama sehemu ya Madiwani katika maeneo yale. Lakini pia wasimamizi wengine ni wenyeviti wa serikali za vijiji, na tatu, wapo wenyeviti wa Serikali za Mitaa na vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uwiano wa mapato na matumizi; kinachopelekwa kule katika bajeti zetu unakuta halmashauri inapewa bajeti ya bilioni 42, 46. Lakini wanaokwenda kusimamia bajeti ile ni Waheshimiwa Madiwani ambao wanapewa posho ya shilingi 300,000. Wapo watendaji wa kata wana mishahara zaidi ya shilingi 700,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uwiano kwamba Mwenyekiti na msimamizi wa shughuli za maendeleo za kata ni Mheshimiwa Diwani. Nilikuwa Diwani wa Kata ya Nyampulukano, Sengerema Mjini, najua matatizo wanayopata Waheshimiwa Madiwani katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, suala la Waheshimiwa Madiwani kupewa posho na posho zenyewe zinakuja kwa kuchelewa, jambo ambalo haliwezekani, halikubaliki hata kidogo. Taarifa ya *CAG,* wizi mkubwa unatokea katika halmashauri zetu, wasimamizi wa miradi ile ni Waheshimiwa Madiwani ambao mishahara yao, posho zao haziko katika sehemu ya ajira; haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mafiga matatu tunaachania wapi? Tukienda kutafuta kura tunatafuta kura za Mheshimiwa Rais, tunasema mafiga matatu; tunatafuta kura za Mheshimiwa Mbunge, tunatafuta kura za Mheshimiwa Diwani. Kwenye maslahi tunaachana; haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuwe wakweli; Chama cha Mapinduzi ni chama kikubwa katika Afrika, kina heshima katika Afrika, lakini kinaendesha Serikali ambayo ina matabaka. Kama Mheshimiwa Diwani hataingizwa katika sehemu ya ajira, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, dada yangu, nakupenda lakini safari hii nakamata shilingi kwa mara ya

kwanza. Nimekuwa Mbunge huu mwaka wa pili nakwenda wa tatu, naangalia maslahi ya Madiwani, inashindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida kule kuendesha halmashauri kama Mbunge. Kila tatizo linakuja kwa Mbunge; Diwani kwanza atasafirije, posho ya Diwani ya kikao, vikao vyenyewe vinahesabika. Diwani akiamka asubuhi ana watu kama nane nyumbani kwake; huyu mtoto anaumwa, mwingine anatakiwa kufanyiwa *operation,* nilikuwa Diwani, nilikuwa nayaona haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu huyohuyo Diwani ndio akasimamie madarasa. Sasa kama kuna mifuko kule kumi inatakiwa ijengee akiambiwa miwili Mheshimiwa Diwani na wewe utapata shilingi 20,000, kwa nini asikubali? Naomba sana jambo hili ulifanyie kazi tuone namna gani maslahi ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya wenyeviti wa Serikali za vijiji; mapato yanakusanywa katika halmashauri zetu, ni kutoa mwongozo tu kwamba posho za Waheshimiwa wenyeviti wa Serikali za vijiji zitokane na halmashauri. Wapunguze katika mapato yao, tunapata asilimia 40, hii asilimia 40 iliyopatikana sisi inakwenda katika miradi yetu ya maendeleo. Asilimia 60 inakwenda kutumika kwa watendaji ambao wanaletewa *OC,* wana mishahara, wanaletewa *OC,* wana semina, wana kila kitu. Wapunguze kule wapelekewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina vijiji 71 katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Lakini wenyeviti wangu wa Serikali za vijiji posho watoe kwa Mbunge; hiki kitu hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwa Waheshimiwa wenyeviti na watendaji wa Serikali za Mitaa. Hawa wenyeviti ni kwamba wanapewa mishahara yao ni mihuri, na nilisikia mkuu wa mkoa mmoja anasema anataka kuwanyang’anya

mihuri. Hiyo mihuri inasaidia mtu akienda kuuza mfugo wake katika mnada, Mheshimiwa mwenyekiti wa kitongoji ndiyo anapata 5,000; mtu anakwenda kuweka dhamana anapata shilingi 5,000. Hatuwezi kuwa na tabaka la utawala bora watu wengine wanaishi kwa mhuri halafu wanasimamia mapato ya halmashauri; haiwezekani hata siku moja. Hili ni jambo ambalo siwezi kulikubali mimi kama Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye uchaguzi mwaka kesho. Hawa wenyeviti wa Serikali za vijiji ndio wanakwenda kutoa sura ya nchi hii. Tunaanza nao wao kwenda kuwatafutia kura, tunawatafutia kura wakachaguliwe tu hatutafuti malshi yao; inakuaje Waheshimiwa Wabunge? Hili tunataka lije katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri, wanawekwa namna gani hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya halmashauri; mapato haya yako katika *server* moja katika nchi hii. Kule sisi tunaona kabisa kwamba kwa mfano nina maeneo ya mashine za mpunga zinapakia malori kumi, mtu akichomoa tu kile ki-*server* kinachokaa katika mashine anaanza kutoa risiti zinatoka na unaona kabisa lori moja pale lina shilingi 600,000, unaona hapa kuna milioni sita. Kwa nini wale wasipewe na wao *password* wakurugenzi waone? Sisi Wabunge kuna dhambi gani tukipewa *password* tukaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unaona kabisa kwamba leo yamepakia malori kumi ya mbao, lakini unashangaa linalokwenda kulipiwa ni lori moja; haiwezekani. Mapato yaanaza kupigwa kuanzia huko chini. CAG anakuja kukagua kitu ambacho tayari kimeshaibiwa. Kwa nini msitupe *password* tukaanza kuona sisi hayo mapato? Kuchungulia. Kama tunaweza kuchungulia sisi kwenye *statements* zetu za benki, unaangalia kwenye mfumo leo tumeuzaje. Leo mtu

mmoja tu anaangalia TAMISEMI nchi nzima; upigaji ndio uko kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unamwamini Mkurugenzi kumpa bilioni 42, unashindwa kumuamini mapato ya shilingi bilioni tatu; inawezekana wapi unashindwa kuwapa wao *password* wakaangalie kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya utawala, ametoka kuzungumza kaka yangu hapo; naangalia tu kama mikoa hii, Mkoa wa Tabora, tunaangalia Mkoa wa Morogoro, tuangalie Mkoa wa Geita ulivyo mkubwa, tunaangalia kuna wilaya ziko kubwa; Wilaya ya Kahama; Kiteto, Sengerema. Mimi Wilaya ya Sengerema kata zangu nne, kata moja tu ya Nyamatongo Katunguru, ukichukua Katunguru ukachukua na Ngoma B ukachukua na Chifunfu ni sawasawa na eneo moja tu la Jimbo la Nyamagana; kata nne. Ukichukua kata zangu tano, Igalula, Kagunga, Buyagu na Kishinda ni Jimbo la Nyamagana. Halafu leo hii tunavyozungumza hapa… *(Kicheko)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** …mimi leo Mbunge nina kata 26; haiwezekani maneno kama haya.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kaka yangu, Mheshimiwa Tabasam, tunapozungumza ukubwa wa Jimbo na bajeti, siyo ukubwa wa eneo ni wingi wa idadi ya watu waliopo kwenye eneo husika. Kwa hiyo, atambue kwamba anapoizungumza Nyamagana, anazungumzia Jiji la pili kwa ukubwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake kwa sababu kwanza ninachotaka kukwambia, hiki ninachozungumza mimi ni sehemu ya taarifa ya sensa. Sengerema nina wananchi 500,000…

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** …Ukichukua wananchi wa Jimbo la Buschosa 450,000, ni wilaya ya tatu katika nchi hii kwa idadi ya watu. Haiwezekani kitu kama hiki. Na watu wanaokwenda Nyamagana wanatoka Sengerema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Waendelee kunipa hizo taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Tabasam, kwamba naungana na anachokisema kwa sababu hata ukiangalia kwa mfano Halmashauri ya Mji wa Korogwe ni ndogo kijiografia lakini kwa sensa ni watu 58,000, Korogwe *DC* ni kubwa kijiografia lakini kwa sensa ni watu 200,000 na. Lakini mara nyingi migao inatoka sawasawa.

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa Mheshimiwa Tabasam?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imekaa vizuri. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Serikali za Mitaa kwamba idadi ya wanafunzi wa shule ya msingi kwangu ni 116,000, madarasa niliyonayo ni 950. Upungufu wa madarasa katika Halmshauri ya Wilaya ya Sengerema ni 1,600. Nyumba za walimu ninazo 52 tu, upungufu ni nyumba 600 za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu nilionao hawatoshi kuwafundisha wale wanafunzi. Shule moja ya Chifufu, Shule ya Msingi Bugumbikisa ina wanafunzi 3,700, watoto wa awali 350, wanafunzi 4,000, walimu 22; hawa walimu kweli wako sawa na walimu wa Nyamagana? Shule moja ya Nyamagana ina wanafunzi 2,000 walimu 110; haiwezekani mgao kama huu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza na wewe tunaomba bajeti ya Serikali za Mitaa igawanywe kwa mujibu wa sensa. Mheshimiwa Rais karuhusu pesa, tumetumia zaidi ya bilioni 400 kwa ajili ya kuhesabu watu na makazi. Tuje kwenye bajeti kwa usawa, hakuna maneno haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutakubali, safari hii bajeti hii itakuwa ni ngumu. Dada yangu nakupenda sana, umeangushiwa zigo bovu. Amesema Mheshimiwa Shabiby hapa, gari hili ni jipya lakini lina *engine* ya bajaj. Ninachotaka kukwambia anza kukarabati...

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunisikiliza, Watanzania msikie haya tuliyoyasema. Safari hii mgao ni kwa bajeti, keki ya nchi hii tuipate wote. Hakuna haya maneno watu wengine wapate keki ya nchi hii, watu wengine tuwe wasindikizaji kwenye nchi hii, hapana. Hapana, hatukubali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam.

Nilimwita mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe miongoni mwa wachangiaji. Maana Wizara hii kubwa ya TAMISEMI ndiyo iliyobeba *mabi.. na mabi. na mabi.* ndani yake mkiwa na ma... *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kwamba tunampongeza sana Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia fedha kupitia Wizara hii. Hela nyingi za maendeleo, zinatisha *mabi. na mabi.* hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze sana Waziri, na Naibu Mawaziri wake na wataalam wake wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Moja, Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa wewe ni Waziri ambaye umekuwa akipokea simu na wenzake pamoja na Katibu Mkuu; huu ndiyo ukweli. Kwa hiyo, tunampongeza sana sisi wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzangu wamempongeza kiongozi wa *TARURA; CEO.* Kwenye ukweli lazima tuseme ukweli, *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana, ombi letu sisi kama Wabunge, waongezewe fedha ili kwenye majimbo yetu barabara zinapitika, lakini ziweze kupitika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie ajira. Wabunge wenzangu hapa wamezungumzia ajira; mimi naunga mkono kwa sababu majimbo yote yana wasomi, majimbo yote walimu waliomaliza vyuo wapo. Kwa hiyo, tukuombe Waziri na wataalam wako, uone kila jimbo hatutaki kwamba aajiriwe katika eneo analotoka; hapana. Lakini watolewe angalau kila jimbo ili wazazi hawa tunaowasomesha watoto wetu katika sekondari zetu ambazo hizi zimetolewa hela nyingi kujenga wapate imani ya watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; wakati anawasilisha Waziri hapa nilikuwa namsikiliza kwa makini na Wabunge wenzangu. Rais Dkt. Samia fedha za zahanati peke yake kwa miaka miwili zimeongezeka takribani 1,066; siyo kitu kidogo. Ndani yake na Makambako tumepata zahanati; tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi katika zahanati ambazo wananchi wamejenga, tunaomba zimaliziwe; ni Mkolango, imeisha, Kivavi, Mwembetogwa na Mjimwema. Zahanati hizi wananchi wamejenga kwa kushirikiana na Madiwani na

Mbunge wao, tunaomba zipewe fedha ili ziweze kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vituo vya afya kwa kipindi hiki cha miaka mitatu – nilikuwa nakusikiliza Mheshimiwa Waziri – mama Dkt. Samia ameweza kujenga vituo vya afya 344, ndani yake kuna fedha za tozo vituo 234, kuna fedha za ndani vituo 83, jumla vituo 713; hivi vyote vimebeba maB na maB na maB. Fedha nyingi sana, kwa hiyo, tunakupongeza kwa kusimamia jambo hili ambavyo vituo vya afya viko katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu; kwenye elimu fedha nyingi vilevile wakati unawasilisha hapa zimetolewa za shule za msingi na sekondari. Niombe; kwenye Jimbo la Makambako kuna eneo Kata ya Mjimwema, kata hii ni kubwa, tumeandaa eneo na tumeanza, hatuna sekondari. Kata ya pili ni Kata ya Kitandililo, wananchi wamejenga madarasa matatu, Diwani wao na Mbunge wao nimetia nguvu hapo; tunaomba Serikali iweze kumalizia kuhakikisha Kata hii ya Kitandililo tunatapata sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya sasa nizungumzie siasa; amesema Mbunge mmoja kule, Mheshimiwa Kakunda, kwamba mama aliporuhusu mikutano sisi kama viongozi wa CCM tuliguna kidogo. Lakini imeleta tija sana kwa sababu tulifika mahali Waheshimiwa Wabunge tutakubaliana hapa, sisi sote ni Watanzania – tulianza kuogopana. Leo tumekuwa kitu kimoja, ametuunganisha mama, vyama vyetu sasa tunazungumza lugha moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tumpongeze sana mama kwa jitihada hizi. Mwezi uliopita nimekwenda Unguja, Pemba, Zanzibar, nimekwenda kule nikakutana na wa vyama vingine, tulikaa tunakula chakula pamoja, tunazungumza maendeleo vizuri pamoja, nikasema Rais Dkt. Samia na Rais

Dkt. Mwinyi wanatakiwa kupongezwa sana kwa kutuunganisha Watanzania ambao sasa tunazungumza lugha moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, Mheshimiwa wa Upinzani Mwenyekiti Mbowe, ni lazima naye tumpongeze. Kwa nini nasema tumpongeze; kwa namna maridhiano ambayo wameyafanya. Sasa Mbowe amekuwa naye tunashiriki pamoja, tunaongea pamoja bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mbowe, kwa sababu anataka kuwafanyia maendeleo Watanzania na mama ameshafanya kazi kubwa dunia inamuelewa, 2025 Mbowe tulia muachie mama ili atimize ndoto ya kuwaletea Watanzania maendeleo. Mbowe 2025 shiriki na Madiwani, shiriki na Wabunge, nafasi ya Rais muachie mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile wapo Wabunge wenzetu pale, wale 19, 20 nadhani na yule wa jimbo. Naomba mnisikilize vizuri, na Mbowe anisikilize vizuri, na Mbowe nilikuwa naye kwenye Kamati ya Katiba 2014, tulikuwa Kamati moja na Mbowe, rafiki yangu. Sasa Mbowe na wenzake kwa huruma ya mama amemsamehe kutoka rohoni, mama Dkt. Samia amesema yote yaliyofanyika nafuta, na yeye wale ni wapiganaji wake walikaa mpaka ndani kipindi fulani, awasamehe. Ni wapiganaji wake, awasamehe. *(Makofi/Kigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo gani ambalo mtu huwezi kusamehe kila wakati watoke, watoke; wale ni wapiganaji ambao akina Mheshimiwa Mdee wale walikaa ndani, wakipigana juu ya chama chake, sasa awasamehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi tena kwenye jimbo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la soko, Makambako tunasubiri sana, mlishatueleza mtatujengea stendi ya kisasa, mlishatuambia mtatujengea soko la kisasa. Mheshimiwa Waziri hebu tuma timu ya wataalam, tunasubiri kwa hamu ili tuwaoneshe eneo la kujenga soko na eneo la kujenga stendi ili shughuli za maendeleo katika halmashauri yetu ziweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa kweli ni laizma tumpongeze sana mama kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akifanya, akitupenda Watanzania na dunia imemuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha jioni. Na hapa ninalo tangazo moja ambalo naomba tusikilizane ili niweze kulitangaza. Tangazo limetoka kwa Katibu wa Bunge.

Katibu wa Bunge anasema; naomba uwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba Benki ya *NMB* imeandaa *Iftar* maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. *Iftar* hii itafanyika katika Viwanja vya Bunge leo, Siku ya Ijumaa, tarehe 14, Aprili 2023 kuanzia saa 12.30. Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote wanaalikwa katika *Iftar* hii bila kukosa. Aidha, Wakuu wa mikoa waliopo hapa Dodoma nao wanaalikwa.

Baada ya tangazo hilo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.20 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 17 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*